NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI

### Kikao cha Tatu – Tarehe 1 Februari, 2018

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae, Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Taarifa ya Serikali kuhusu Tathmini ya Hali ya Uchumi na Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Julai – Disemba, 2017 na Mwelekeo hadi Juni, 2018.

**MHE. KHALFAN H. AESHI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2017.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2017.

**MWENYEKITI:** Katibu, tuendelee.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Sasa ni wakati wa maswali, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, swali la Mheshimiwa Omari Kigoda.

Na. 30

### Hitaji la Madaktari na Wauguzi Hospitali ya Wilaya ya Handeni

**MHE. OMARI A. KIGODA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapaleka madaktari na wauguzi katika Hospitali ya Wilaya ya Handeni hasa ikizingatiwa kuwa hali ya hospitali hiyo kwa sasa sio nzuri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea kibali cha ajira mwezi Julai, 2017 Serikali imepanga watumishi

katika maeneo mbalimbali ili kupunguza tatizo la watumishi. Katika mgao huo Halmashauri ya Mji wa Handeni imepokea jumla ya watumishi 10 waliopangiwa vituo vya kazi Novemba, 2017. Watumishi waliopangiwa ni Daktari Daraja la II 1, Tabibu Wasaidizi wawili, Tabibu Meno mmoja, Wauguzi wawili, Afisa Muuguzi Msaidizi mmoja na Wateknolojia Wasaidizi Maabara wawili. Watumishi wote wamesharipoti na wanaendelea na kazi kama walivyopangiwa. Mgawanyo huu umefanyika ili kila eneo lipate wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na watumishi hao wapya, Halmashauri kwa kushirikiana na wadau wa afya inao watumishi 13 wanaofanya kazi kwa mikataba ya muda mfupi ambao wanafanya kazi katika Hospitali ya Wilaya Handeni. Aidha, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri imeomba kibali cha kuajiri watumishi wa kada za afya 182 ili kukamilisha Ikama ya Idara ya Afya ya Halmashauri ya Mji Handeni. Serikali itaendelea kupanga watumishi kadri bajeti ya mishahara itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ambazo zimeathirika kwa kiwango kikubwa kinachoathiri utoaji wa huduma kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kutokana na zoezi la uhakiki wa vyeti *fake* zinaelekezwa kuwasilisha maombi ya ajira mbadala moja kwa moja Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kuweza kutatua changamoto hiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Omari Abdallah Kigoda, swali la nyongeza kama unalo.

**MHE. OMARI A. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina swali, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kapufi.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hospitali ya Manispaa ya Mpanda kwa sasa hivi inafanya kazi kama Hospitali ya Mkoa, imeelemewa kwa kiasi kikubwa na wangonjwa wanaotoka katika Halmashauri

mbalimbali. Wakati tukisubiri mipango ya Serikali ya kutujengea Hospitali ya Mkoa, ni lini Serikali itatusaidia kuongeza waganga pamoja na wauguzi? Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuna upungufu wa wauguzi pamoja na madakatari. Nizitake Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda pamoja na Halmashauri zingine waige mfano mzuri ambao umefanywa na Halmashauri ya Handeni kwa kutumia *own source* ili kuweza kuwaajiri wale watumishi ambao ni muhimu sana kwa kipindi hiki wakati wanasubiri wale ambao wataajiriwa na Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tatizo lililopo Handeni linafanana kabisa na tatizo lililopo katika Hospitali ya Mkoa wa Tabora ya Kitete, ina upungufu mkubwa wa madaktari na wauguzi. Je, ni lini Serikali itapeleka madaktari na wauguzi katika Hospitali ya Mkoa ambayo inategemewa na mkoa mzima?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la swali la msingi, ni kweli tunatambua kuna upungufu mkubwa wa wauguzi pamoja na madaktari na hasa katika Hospitali ya Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, kwa kadri ambavyo ikama inahitajika kutokana na bajeti, ni vizuri basi niwatake Mkoa wa Tabora kwa ujumla wake waanze kwa haraka kuiga mfano mzuri wa Handeni kwa kutumia *own source* za kwao ili kuweza kuziba hilo pengo lililopo wakati

tunasubiri bajeti iruhusu kwa ajili ya kuajiri hao wengine ambao watatoka Serikali Kuu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Martha Umbulla.

Na. 31

**Changamoto Katika Hospitali ya Rufaa Ngazi ya Mkoa ya Haydom**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA** aliuliza:-

Hospitali ya Rufaa ngazi ya Mkoa ya Haydom inahudumia wananchi wengi lakini inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa watumishi, madaktari wakiwemo Madaktari Bingwa pamoja na ukosefu wa maji.

(a) Je, Serikali itachukua hatua gani za dharura kutatua changamoto hizo?

(b) Kwa kuwa watumishi hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu, je, ni kwa nini Serikali isiondoe kodi kwenye posho zao kama vile *on-call allowance, hardship allowance* na *food allowance?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Haydom inayomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ina jumla ya watumishi 680 ambapo kati yao watumishi wa Serikali ni 156. Serikali imekuwa ikiisaidia hospitali kupitia Sera

ya Ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi *(PPP)* ambapo mpaka sasa imepeleka watumishi 156 wa kada mbalimbali wakiwepo madaktari 10 ambapo saba ni Madaktari Bingwa na watatu ni Madaktari wa Kawaida. Mbali na watumishi, Hospitali ya Haydom inapata ruzuku ya dawa kupitia *MSD* na ruzuku ya fedha za *Busket Funds* kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu. Hata hivyo, Serikali itaendelea kupeleka watumishi hasa madaktari na wauguzi kadri vibali vya ajira vitakavyokuwa vinapatikana.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Haydom inapata maji kutoka chanzo cha maji kilichopo umbali wa kilometa 20 katika Kijiji cha Binja, Kata ya Endamilay, Wilaya ya Mbulu. Hospitali hiyo inajitosheleza kabisa kwa maji hayo. Hata hivyo, maji haya yanapatikana kwa gharama kubwa kutokana na kukosekana kwa nishati ya umeme katika eneo husika, hivyo hospitali kulazimika kusukuma maji kwa kutumia mitambo ya dizeli (jenereta) inayotumia jumla ya lita 2,800 kwa mwezi sawa na shilingi 6,020,000/= ambayo ni sawa na shilingi 72,240,000/= kwa mwaka.

Kwa kuwa hivi sasa kupitia Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini *(REA)* inasambaza umeme katika maeneo mbalimbali yakiwapo ya Haydom inatarajiwa kuwa umeme huo utasaidia mradi wa maji wa Hospitali ya Haydom kupata huduma ya umeme na hivyo kupunguza gharama za uendeshaji wa kutumia dizeli.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Haydom ina makundi mawili ya waajiriwa kama ifuatavyo; kundi la kwanza ni waajiriwa walioajiriwa na Hospitali ya Haydom moja kwa moja na hukatwa kodi ya mapato kama sheria inavyoelekeza; kundi la pili ni la waajiriwa waliajiriwa na Serikali lakini wanafanyakazi Hospitali ya Kilutheri Haydom, watumishi hawa wanalipwa posho ya kuitwa kazini baada ya masaa ya kazi *(on-call allowance)* na Hospitali ya Haydom na hii ndiyo sababu inayopelekea wakatwe kodi katika posho hiyo. Makato hayo yanatokana na Sheria ya Kodi ya Mapato *(Income Tax)* ya mwaka 1973.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha Umbulla, una swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza naomba nimpongeze sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kuridhisha. Pia nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali yetu kwa kuipandisha hadhi Hospitali ya Haydom kuwa Hospitali ya Rufaa Ngazi ya Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na upandishwaji hadhi huko, ni kwa nini Serikali yetu isione umuhimu wa kuhakikisha kwamba inajenga miundombinu ya hospitali hii muhimu inayohudumia mikoa zaidi ya mitatu hasa katika suala la upatikanaji wa maji, jambo ambalo ni muhimu sana? Amekiri mwenyewe kwamba *source* ya maji sasa hivi ni umbali wa kilometa 25 kutoka hospitali kwa kutumia jenereta ambayo inakabiliwa na uharibifu wa mara kwa mara. Suala la *REA* Awamu ya Tatu linachukua muda mrefu, tungeomba Serikali ifikirie kupeleka umeme katika hospitali hii muhimu kabla ya hata *REA* kufikia eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, suala la *income tax* kwenye posho za watumishi wa Hospitali ya Haydom tayari ameshaonyesha kwamba kuna tabaka mbili ya watumishi katika hospitali hiyo, lakini ukweli na utafiti unaonyesha kwamba baadhi ya watumishi katika Hospitali za Wilaya na kwingineko katika nchi yetu hawakatwi kodi kwenye *on-call allowances* lakini hawa watumishi wa Haydom wanakatwa na hasa tukizingatia kwamba wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Tunaomba Serikali itoe kauli katika hilo?

**MWENYEKITI:** Tafadhali naomba maswali ya nyongeza yawe mafupi. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Umbulla, naomba kwa moyo wa dhati kabisa nimpongeze kwa jinsi ambavyo amekuwa akipigania

wananchi wa mkoa wake lakini bila kusahau hata Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo jinsi ambavyo wamekuwa wakiipigania hospitali yao hii ya Haydom. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maswali yake ya nyongeza anasema kwamba ufanyike utaratibu wa haraka ili kuwezesha kupatikana umeme kabla ya *REA.*

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, utaratibu wa haraka kabisa na chanzo cha uhakika ni kwa kutumia *REA* Awamu ya Tatu, nadhani ndiyo njia sahihi. Kwa taarifa tulizonazo Serikalini ni kwamba tayari mkandarasi yupo kule. Kwa hiyo, tuvute subira, kama mmesubiri muda wa kutosha, kipindi kilichobaki ni kifupi na tatizo hili litakuwa limeondoka*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na watumishi ambao wameajiriwa na Hospitali hii ya Haydom kukatwa *on-call allowance. On-call allowance* inakatwa kwa sababu wao katika malipo ambayo wanafanya, wanajumuisha pamoja na mshahara wao na ukisoma ile Sheria ya *Income Tax,* unapotaka kukata kodi lazima utizame vyanzo vyote, ni tofauti na hawa wa Serikalini ambao *allowance* hizi huwa zinalipwa dirishani, hazisubiri mpaka kipindi cha kuja kulipa mshahara wa mwisho. Kwa hiyo, ni namna tu watakavyojipanga wakaji-*adjust* inawezekana kabisa wasikatwe hicho wanachokatwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara na Mheshimiwa Nchambi.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Waziri ana jambo anataka kusema.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** *Okay.*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona na namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa majibu yake kwa maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni vizuri tuweke rekodi sawasawa. Bunge hili kupitia *Finance Act* ya mwaka 2011 liliongeza misamaha kwa posho mbalimbali. Katika vitu vilivyoongezwa kwamba vitasamehewa kodi ya mapato ni *allowance payable to an employee who offers intramural private services to patients in a public hospital and housing allowance, transport allowance, responsibility allowance, extra duty allowance and honoraria payable to an employee of the Government or its institution whose budget is fully or substantially paid out of Government budget subvention. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *allowances* hizi ndizo zilizosamehewa kodi kwa mujibu wa sheria na *TRA* hiki ndicho wanachofanya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waitara tuendelee.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tunapozungumza Hospitali ya Amana imepelekwa katika Wizara ya Afya na kwa maana hiyo Manispaa ya Ilala haina Hospitali ya Wilaya. Bahati nzuri katika Jimbo la Ukonga, Kata ya Kivule kuna eneo la ekari 45, Manispaa ya Ilala imeshaanza kuweka msingi.

Je, ili kupata huduma ya afya katika Manispaa ya Ilala kwa kuwa na Hospitali ya Wilaya, nini kauli ya Serikali katika jambo hili? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Hospitali ya Amana imechukuliwa na hivyo kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge hawana hospitali. Pia ni ukweli usiopingika kwamba jana nilipata fursa ya kuteta na Mheshimiwa Mbunge akaniambia katika *own source* yao walikuwa wametenga shilingi bilioni moja kwa ajili la kuanza ujenzi wa hospitali yao. Kwa hiyo, ninachowaomba, zile jitihada ambazo walishazianzisha za kuanza kujenga hospitali ya kwao ya Wilaya zisisimame, ni lazima zitiwe msukumo tuhakikishe kwamba wananchi wetu wanapata maeneo mengi ya kujitibia. Nikitoka hapa nitafanya kila jitihada niwasiliane na Mkurugenzi ili nimuelekeze hicho kiasi cha pesa ambacho kimetengwa kifanye kazi iliyokusudiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *wabheja* sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Jimbo la Kishapu lina zahanati 45 zilizokamilika na zinafanya kazi, vituo vya afya vinne vimekamilika vinafanya kazi na viwili tayari tunasubiri vianze kufanya kazi hivi karibuni na tuna hospitali kubwa ya kisasa ambayo inafanya kazi vizuri. Kwa kuwa tumekwishaleta maombi ya upungufu wa baadhi ya madaktari, wauguzi na watumishi wa kada ya afya, je, Mheshimiwa Naibu Waziri, uko tayari kukaa na mimi hata leo tupitie maombi hayo uone namna ambavyo utasaidia jitihada za watu wa Kishapu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *wabheja* sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla ya kujibu kama niko tayari au siko tayari, naomba niwapongeze kwa jitihada ambazo

zimefanyika za kuweza kuhakikisha kwamba huduma za afya zinapatikana kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niko tayari kabisa, kabisa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Massay swali kwa ufupi halafu wa mwisho Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa muda wa kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali hii ya Haydom kwenye swali la msingi iko katika jimbo langu na inaihudumia Mikoa ya Arusha, Manyara, Mara, Singida na Shinyanga. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu alishafika na kutuahidi kwamba atatupatia watumishi zaidi na Mheshimiwa Ummy amefika kwenye hospitali hiyo. Je, lini sasa Serikali inatimiza ile ahadi yake ya kutupatia watumishi katika hospitali hii ambayo inahudumia mikoa mingi niliyoisema?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali ilishatoa ahadi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tatizo la watumishi linaweza kutatuliwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mbunge ni shahidi, jana alikuwepo, Mheshimiwa Waziri wa Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora alitoa majibu kwamba kwa zile Halmashauri na maeneo ambayo tunahitaji kuweza kuziba pengo hilo kwa haraka ni vizuri barua zikaandikwa. Pia tunakiri kabisa juu ya kujengea uwezo Hospitali ya Haydom kwa sababu inahudumia wagonjwa wengi, naomba tufuate *procedures* za kawaida ili jambo hili liweze kutatuliwa kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nitoe shukrani kwa Serikali, wanasema kwamba usiposhukuru kwa kidogo basi hata kikubwa hutaweza kupata, kwa sababu nililalamika hapa sina hata kituo cha afya kimoja, lakini sasa hivi nimepewa pesa kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya cha pili na pesa za kuboresha kile kituo cha afya cha zamani ambacho nilisema ni mfu, kwa hiyo nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado Hospitali ya Wilaya ya Liwale ina tatizo la *nursing officers* na mpiga picha wa *x-ray.* Ni lini Serikali itaweza kutupatia watumishi hawa wa kada mbili; mpiga picha wa *x-ray* na *nursing officers?* Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Liwale, ambalo kimsingi amekuwa akipigania sana wananchi wake na mimi najua na jana alikuwepo na majibu yaliyokuwa yametolewa aliyasikia. Kwa msisitizo na nimejibu katika swali kutoka kwa Mheshimiwa Kigoda kwamba ni vizuri tukaweza kutumia *own source* kama ambavyo wao wamefanya na katika maeneo ambayo wameajiri ni pamoja na hawa wataalam wa picha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, inawezekana, kama wenzetu wa Handeni wamefanya, Liwale tunaweza. Bahati nzuri kule sasa hivi hali ya kipato inakwenda juu kabisa. Kwa hiyo, ni namna tu ya kupanga kitu gani ni kipaumbele kwa ajili ya wananchi kupata huduma. Ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba kwa kupitia bajeti yake ikiruhusu tutaweza kuajiri na kupeleka watumishi wa kada ya afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega sasa aulize swali lake.

Na. 32

**Kutokamilika kwa Mradi wa Maji Mto Ibofwe - Kalenga**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Upembuzi yakinifu wa kutumia chanzo cha maji cha Mto Ibofwe ili kumaliza tatizo la maji katika Kata za Magulilwa, Luhota, Mseke, Ifunda, Mgama na Maboga ulifanyika kati ya mwaka 1995 – 2000 chini ya usimamizi wa Mbunge wakati huo, Mheshimiwa George Mlawa na bajeti ya utekelezaji wake kupitishwa na Bunge hili ili uwe katika kipindi cha mwaka 2000-2005/2005-2010.

Je, ni tatizo gani lililofanya mradi huo usikamilike na kuwaacha wananchi wakiendelea kuteseka wakati Bunge lilikwishapitisha bajeti ya mradi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji wa kutumia chanzo cha Mto Ibofwe ulifanyiwa usanifu wa awali miaka ya 1990 lakini haukufanyiwa usanifu wa kina *(detailed design)* ambao ungebaini mahitaji na gharama halisi za kutengeneza mradi huo ndiyo maana haukutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwapatia huduma ya maji wananchi wa Kata za Maboga, Lumuli, Isupilo na Itengulinyi, Serikali inatekeleza mradi mkubwa wa maji

unaogharimu shilingi bilioni 2.18 utakaonufaisha wakazi 6,914 katika maeneo hayo. Mradi huo ulioanza kutekelezwa mwaka 2013/2014 ulisimama utekelezaji wake mwaka 2015 kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 umetengewa shilingi milioni 800 na unatarajiwa kukamilika Desemba, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kati ya Julai 2016 na Desemba 2017, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imechimba visima sita katika Kata za Magulilo kisima kimoja, Luhota visima vitatu, Maboga kisima kimoja na Mgama kisima kimoja vinavyohudumia wananchi 1,600. Idadi ya visima kwenye kata hizo tangu miaka ya 1990 hadi sasa imefikia visima 41 vinavyohudumia wakazi 8,200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mwaka huu 2017/2018, jumla ya shilingi 410,000,000 zimetengwa kutekeleza miradi ya maji ya Izazi - Mnadani, Migoli - Mtera, Malinzanga, Isupilo – Lumweli – Itengulinyi - Magunga na Mfyome. Mpango wa muda mrefu wa Serikali ni kufanya usanifu wa kina *(detailed design)* ili hatimaye tutumie chanzo cha Mto Ibofwe kumaliza kabisa matatizo ya maji kwenye maeneo hayo. Usanifu wa kina utafanyika mwaka 2018/2019 kwa gharama ya shilingi milioni 49.56 ambazo ziko kwenye mapendekezo ya bajeti ya mwaka 2018/2019 endapo Bunge litaridhia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Victor una swali la nyongeza?

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nitoe masikitiko makubwa sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, ambapo tarehe 8 Juni, 2016 niliuliza swali kuhusu vijiji na kata hizo hizo na aliyekuwa Naibu Waziri na sasa ni Waziri mwenye dhamana TAMISEMI alinipa majibu ambayo yalikuwa yanaeleza kwamba vijiji hivyo vimetengewa bajeti ya shilingi milioni 49.5 ambayo itatekelezwa mwaka 2016/2017. Mpaka sasa hivi hakuna kinachoendelea, ni Bunge hili hili ambalo linatoa majibu hayo na leo tena nimepewa asilimia hiyohiyo 49.5 kwamba itatekelezwa 2018/2019. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu, ni lini Serikali itapeleka pesa kwa wananchi hawa, toka mwaka 1995 mpaka leo ni upembuzi yakinifu unafanyika, ni lini hawa wananchi watapata maji? *(Makofi)*

MheshimiwaMwenyekiti, swali la pili, ni kwa nini hawakufanya upembuzi wa kina wakati bajeti ilitengwa? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi, ni kweli kwamba usanifu wa kina haukufanyika ule wa zamani, lakini kwa sasa tunatarajia usanifu kina utafanyika mwaka 2018/2019 kwa ajili ya utekelezaji wa kumaliza kabisa matatizo ya maji kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ambalo lilikuwa ndiyo la kwanza, ni kwamba kazi ambazo zimefanyika kuanzia 2016 mpaka Desemba, 2017 nimesema hapa kwamba tumejenga visima sita katika Kata za Magulilwa, Luhota, Maboga na Mgama. Hii kazi imefanyika na taarifa hizi zimetoka kule kule kwenye Halmashauri yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, taarifa za kina zaidi namuomba sana tushirikiane naye baada ya kikao hiki ili tuweze kushauriana vizuri namna bora ya kuhakikisha kwamba tunamaliza matatizo ya wananchi kwenye maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Arusha una majimbo ambayo kijiografia yana mazingira magumu sana,

hasa Jimbo la Ngorongoro na mara nyingi Mawaziri mmekuwa mkifika pale mmeona mazingira yale na kumekuwa na tatizo kubwa sana la upatikanaji wa maji kwenye vijiji vilivyoko katika Jimbo la Ngorongoro.

Je, Serikali sasa ina mkakati gani wa haraka wa kuhakikisha Jimbo la Ngorongoro linatizamwa kwa upekee na wananchi wake wanaweza kupata maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali ambalo limeelekezwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhusiana na utekelezaji wa miradi ya maji katika Halmashauri ya Ngorongoro kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Januari, tumesaini mkataba wa milioni 270 kwa ajili ya mradi wa maji katika Halmashauri ya Mji wa Ngorongoro, sasa hivi tunafanya *design* ambapo tunatarajia mwezi Aprili, tutasaini mkataba mkubwa ambapo tutapeleka maji zaidi ya vijiji tisa likiwemo eneo la Mageli. Kwa hiyo, suala la maji upande wa Ngorongoro linashughulikiwa na tutahakikisha kwamba asilimia 85 itakapofika 2020 inafikiwa pia katika Halmashauri ya Ngorongoro. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na swali la Mheshimiwa Vedasto Ngombale.

Na. 33

**Kuwawezesha Wavuvi Wadogowadogo Wilayani Kilwa**

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE** aliuliza:-

Sekta ya Uvuvi ni moja ya maeneo ambayo Serikali ya Awamu ya Tano inayaona kuwa yanaweza kukuza uchumi kwa kuongeza Pato la Taifa, kupunguza umaskini na tatizo la ajira.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo Wilayani Kilwa kwa kuwapatia zana za kisasa za uvuvi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati yenye lengo la kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuwawezesha wavuvi wadogowadogo wakiwemo wa Wilaya ya Kilwa kupata zana za uvuvi kwa bei nafuu ili kufanya uvuvi endelevu na wenye tija. Miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kuondoa kodi kwa zana na malighafi za uvuvi zikiwemo *engine* za kupachika, nyuzi za kushonea, nyavu na vifungashio kupitia Sheria ya *VAT* ya mwaka 2007.

Vilevile kupitia Chapisho la Pamoja la kodi la Afrika Mashariki *engine* za uvuvi na malighafi zinazotumika kutengeneza zana mbalimbali za uvuvi na viambata vyake zimepewa punguzo la kodi ili kuwawezesha wavuvi kumudu bei za vifaa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Programu ya Kutoa Ruzuku kwa Wavuvi, Serikali katika Awamu ya Kwanza ilinunua *engine* 73 na hadi sasa *engine* 49 zimelipiwa na kuchukuliwa na vikundi vya wavuvi vilivyokidhi vigezo vikiwemo vikundi 27 kutoka Ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kuomba Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kuhamasisha wavuvi kujiunga kwenye Vyama vya Ushirika vya Msingi ili waweze kunufaika na fursa hii kama wavuvi wengine katika ukanda huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali imeanzisha Benki ya Kilimo ambayo pamoja na masuala mengine inaweza kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa wavuvi ili kuboresha shughuli zao za kimaendeleo. Kutokana na kuwepo kwa benki hii na taasisi nyingine za kifedha, Serikali inaendelea kuhamasisha wavuvi kote nchini kujiunga katika Vyama vya Ushirika wa Wavuvi ili waweze kukopesheka na kuweza kununua zana za kisasa za uvuvi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vedasto una swali la nyongeza?

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejikita kwenye kutoa misaada midogomidogo kwa wavuvi kama vile *engine* na nyuzi za kushonea nyavu za wavuvi. Je, Serikali iko tayari kuwakopesha wavuvi wa Kilwa zana za kisasa kama vile boti kwa ajili ya vikundi hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, Serikali au majibu ya Waziri yameshindwa kuthibitisha kama yamewasaidia wavuvi wa Kilwa kupata zana hizo za kisasa na inawezekana kabisa wavuvi wa Kilwa hawana taarifa yoyote kuhusiana na utaratibu huu. Sasa Serikali au Waziri anaweza kunithibitishia kwamba katika hizo mashine zilizobaki wavuvi wa Kilwa wanakopeshwa mashine hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ipo tayari kuwawezesha wavuvi wa Kilwa? Ndiyo, Serikali ipo tayari kuwawezesha wavuvi wa Kilwa kupitia vikundi vyao. Tena na hapa naomba nimuelekeze tu kwamba vikundi hivyo vinaweza vikatumika hata vile vya *BMU (Beach Management Unit)* na mashine hizi bado zipo, tunawakaribisha Waheshimiwa Wabunge

wote ambao watahitaji mashine hizi wafuate utaratibu kupitia kwa Maafisa Uvuvi wetu ambapo watapeleka kwa Mkurugenzi na baadae maombi yale yatafika Wizarani katika Idara yetu ya Mafunzo na Elimu ya *FETA* kwa ajili ya kuweza kuwapatia wavuvi wetu ili waweze kufanya uvuvi wenye tija.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula na Mheshimiwa Yussuf.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na mikakati mizuri ya Serikali katika kusaidia wavuvi kuwawezesha kwa namna mbalimbali kwa mikopo na vifaa, kwa Kanda ya Ziwa na Ziwa Victoria kwa sasa hali imekuwa tofauti. Hivi tunavyozungumza wananchi wavuvi wa Kanda ya Ziwa, Mikoa ya Ziwa Victoria wanapata taabu kutokana na zana zao, nyavu, mitumbwi kuchomwa moto na faini zisizokuwa rafiki kwa maisha yao halisi na kazi wanayoifanya.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupambana na suala hili la uvuvi haramu kutokufika kwenye kiwango cha kumuumiza mvuvi ambaye tunataka tumsaidie afike mbali zaidi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na mipango yake ya kuhakikisha kwamba inawawezesha wavuvi wadogo wadogo kote nchini ikiwemo wavuvi wa Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mabula amezungumzia juu ya mkakati wa Serikali wa kuhakikisha tunapambana na uvuvi haramu. Ni kweli Serikali inaendelea na kazi ya kupambana na uvuvi haramu kwa kuzingatia Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya mwaka 2014 na Kanuni yake ya

mwaka 2009 ambayo kwa pamoja na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 tumeendelea kuhakikisha kwamba tunafanya kazi kubwa ya kudhibiti uvuvi haramu kwa ajili ya ulinzi wa rasilimali za nchi yetu. Naomba niwahakikishie wavuvi wa Kanda ya Ziwa kwamba zoezi hili ni kwa manufaa ya Taifa letu na vizazi vyetu vya leo na vya miaka ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nyavu mbalimbali ambazo anazisema Mheshimiwa Mabula, tayari tumepata maombi ya kutoka kwa wadau mbalimbali ya kuhakikisha kwamba wanaagiza nyavu zilizo na viwango kwa mujibu wa sheria ili ziweze kusambazwa katika maduka ili wananchi wa kule Kanda ya Ziwa waweze kununua na kuweza kuendelea na shughuli zao za uvuvi bila ya kuvunja sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf na wa mwisho Mheshimiwa Zitto.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la mahitaji ya samaki limekuwa kubwa sana kwa sababu idadi ya Watanzania imekuwa na hata watoto wangu Wasukuma sasa wanajua utamu wa samaki wa baharini.

Mheshimiwa Waziri tatizo sio nyavu, sio ndoana wala sio nyuzi bali ni namna ya kuwafikia wale samaki, uvuvi wa kisasa unahitaji kuwa na *gas cylinders* na *mask* na vitu kama hivyo uzamie ufike kule, samaki sasa wanapatikana katika kina kikubwa cha maji. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kwa wavuvi wetu na vifaa vya kisasa ambavyo vitawasaidia wavuvi wetu kuweza kuwafikia samaki huko waliko na sio nyavu, nyuzi na ndoana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa swali la nyongeza la

Mheshimiwa Salim alilouliza kwamba Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wavuvi hawa kuweza kupata fursa ya kwenda katika maeneo yenye samaki kwa urahisi. Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika hatua za awali za kuhakikisha kwamba tunakwenda sambamba na ongezeko la mahitaji ya samaki, tumeingia mkataba na nchi ya Maldives ambapo hivi sasa tunakwenda katika kuboresha teknolojia yetu. Mvuvi anapotoka mwaloni au anapotoka pwani anapokwenda kuvua tayari patakuwa na vyombo vya *satellite* katika vituo rasmi kumwezesha kujua wapi samaki waliko kwa maana ya *distance* gani katika eneo la bahari au la ziwa. Teknolojia hii itamsaidia anapotoka pale kuwa na uhakika kwamba atakapokwenda pale atapata mazao hayo ya bahari na maziwa kwa urahisi na itamsaidia kutumia rasilimali kidogo ya mafuta na muda mchache lakini akiwa amepata mazao ya kutosha.

**MWENYEKITI:** Mheshiwa Zitto wa mwisho.

**MHE. KABWE Z.R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunavyozungumza wavuvi wa Kanda ya Ziwa hasa Soko la Mwaloni Mwanza hawana uwezo wa kuuza mazao yao ya samaki popote pale Tanzania. Akitaka kupeleka Mtwara, Kigoma, Morogoro, Dodoma, Serikali inamtaka alipe *export royalty* pale Mwanza kwa mazao ambayo anayauza ndani ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Wizara ya Mifugo na Uvuvi inanyanyasa wavuvi wa Kanda ya Ziwa na sasa nasikia kwamba wataelekea mpaka wavuvi wa Kigoma na Mbeya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ya Awamu ya Tano, haina nia ya kumnyanyasa mvuvi wa Tanzania. Nia yetu ni katika kuhakikisha kwamba mosi, tunalinda rasilimali za nchi yetu. Tunahakikisha kwamba mianya yote ya upotevu wa mapato yatokanayo na rasilimali za nchi yetu, ni lazima tudhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wetu umetuonesha, anayoyasema Mheshimiwa Zitto ni mazao ya samaki kule Kanda ya Ziwa maarufu kama *kayabo.* Utafiti wetu *kayabo* kwa kiasi kikubwa haziliwi Tanzania, Kanda ya Ziwa yote hakuna walaji wakubwa wa *kayabo.* Imethibitishika kupitia tafiti zetu *kayabo* inaliwa zaidi nje ya mipaka ya nchi yetu na kwa kiasi kidogo sana katika Mikoa ya pembezoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi nia yetu sio kuwanyima wafanyabiashara na wadau wa uvuvi kufanya shughuli za uvuvi bali ni kuhakikisha mapato yetu hayawezi kupotea. Ndiyo maana tumewaomba wahakikishe kwamba wanalipia *export royalty* kwa sababu tulikwenda katika mipaka ya Ngara na kwingineko ambapo wananchi wenyewe kwa utafiti mdogo tulioufanya wametuthibitishia kwamba pale Ngara mathalani ulaji wa *kayabo* ni mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, samaki wale wengi wanakwenda nje ya mipaka yetu. Wavuvi wale na wafanyabiashara wasio kuwa na nia njema na mapato ya nchi yetu wanatumia fursa hiyo kudanganya kwamba wanapeleka Ngara, Songwe Tunduma na kwingineko mipakani mwetu, hali ikiwa si hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote tuungane mkono katika wakati huu ambapo tunajaribu kuhakikisha kwamba rasilimali za nchi yetu zinainufaisha nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa samaki mchango wake kwa Wizara, Halmashauri na Serikali Kuu haizidi shilingi bilioni 10 kwa mwaka, sisi tunataka tutoke katika shilingi bilioni 10 twende kwenye shilingi bilioni 200. Uwezo huo tunao, sababu hizo tunazo, tunaomba mtuunge mkono ili tuweze kufika mahala hapo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni sasa aulize swali lake.

Na. 34

**Utendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

**MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

Katiba ya Jamhuri ya Muungano inatambua uwepo wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

(a)Je, kwa nini ripoti za Tume hiyo hazitolewi kwa muda muafaka kila mwaka kama masharti ya Katiba yanavyosema?

(b)Je, ripoti ya mwisho ya Tume hiyo ilitolewa mwaka gani na lini imewasilishwa Bungeni?

(c)Je, kwa nini harakati za Tume hiyo katika kushughulikia migogoro ya ardhi, ukaguzi wa vituo vya polisi, magereza pamoja na matukio ya uvunjaji wa haki za binadamu umezorota kinyume na miaka ya nyuma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 131(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaelekeza Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kuwasilisha taarifa zake kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya haki za binadamu ambaye hutakiwa kuwasilisha taarifa hizo nbele ya Bunge mapema iwezekanavyo. Taarifa hizo ni muhtasari wa masuala yote yaliyofanyika katika mwaka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa huko nyuma taarifa za Tume zilikuwa zikichelewa kuwasilishwa Bungeni

kwa wakati. Hata hivyo, mwezi Desemba, 2017, Tume imewasilisha taarifa zake za nyuma hadi mwaka 2014/2015 kwa Waziri mwenye dhamana ili aziwasilishe Bungeni. Taarifa ya mwaka 2015/2016 ipo katika hatua ya mwisho ya uchapaji na itakapokuwa tayari itawasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana. Taarifa ya mwaka 2016/2017 ipo katika maandalizi na inasubiri kukamilika kwa taarifa ya ukaguzi wa hesabu za Tume.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya mwisho iliyotolewa na kuwasilishwa Bungeni ilikuwa ya kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo, kweli kwamba utendaji wa Tume umezorota, Tume imeendelea kufanya kazi zake kama zilivyoainishwa katika Katiba na Sheria. Aidha, Tume imekuwa ikiongeza jitihada kila mwaka kukagua vituo vya polisi, magereza, vituo vya mafunzo kwa upande wa Zanzabar, kufuatilia migogoro ya ardhi na kufuatilia utekelezaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwa ujumla. Lengo kuu la ukaguzi na ufuatiliaji huu ni kutathmini hali ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora na kutoa mapendekezo kwa taasisi husika. Vilevile Tume imekuwa ikifuatilia utekelezaji wa haki za makundi mbalimbali ambayo ni pamoja na watoto hususani watoto walio katika mkinzano na sheria, wanawake na watu wenye ulemavu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ussi Pondeza una swali la nyongeza?

**MHE.USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo ninalo. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri ni tatizo gani lililopelekea ripoti zenye umuhimu mkubwa kama huu wa haki za binadamu zisichapishwe kwa wakati ili Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla wakaweza kujua hali za haki za binadamu katika nchi yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Wabunge kwa upande wa Zanzibar hawapati fursa ya kukagua vituo vya polisi wala vyuo vya mafunzo ili kuwatembelea waliozuiliwa

na waliofungwa kujua kama utekekelezaji wa haki za binadamu unafanyika kwa kiwango ambacho kinatakiwa. Je, Serikali iko tayari kuwatengenezea Wabunge wa Zanzibar utaratibu wa kuweza kuvikagua vituo vya polisi na vyuo vya mafunzo ili kuona haki ya binadamu inatendeka kwa kiasi gani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Pondeza kwa maswali mafupi ya Kibunge, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza amezungumzia kuhusu uchapishwaji wa hizi ripoti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi ni kwamba, ni kweli taarifa hizi zinapaswa kuwasilishwa Bungeni kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameuliza na ndiyo maana tumetoa maelezo yetu kama Serikali kwamba ziko ambazo zimekamilika lakini ziko ambazo zinasubiri ukaguzi wa mahesabu ndipo ziweze kuchapwa na kuletwa Bungeni kwa sababu ndiyo itakuwa taarifa kamili.

Kwa hiyo, nimuondoe hofu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafahamu umuhimu wa taarifa hizi kuwasilishwa mbele ya Bunge na ndiyo maana Tume inaendelea kufanya kazi hiyo kuhakikisha kwamba taarifa hizi zinafika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la nyongeza la pili ameulizia kuhusu kuwashirikisha Wabunge wa Zanzibar. Kwa mujibu wa Ibara ya 130(1) na kifungu cha 6 cha Sheria Namba 7 ya Tume ya mwaka 2001, Tume imepewa majukumu kufanya kazi hiyo ya kwenda kufanya ukaguzi yenyewe. Kwa hiyo, kazi hii kimsingi ni kazi ya Tume, lakini ambacho tunaweza tukakifanya kwa sababu ya kuombwa ushiriki wa Waheshimiwa Wabunge katika jambo hili na sisi pia tuko tayari kushirikiana nao ili wapate fursa kufahamu hali zilizoko katika maeneo ya magereza na vituo vya polisi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peter Msigwa na Mheshimiwa Jaku.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini katika ukiukwaji wa haki za binadamu katika nchi yetu katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Tano umeongezeka sana.

Je, ni lini Tume hii itatoa ripoti kwa sababu polisi wamekuwa wakikaa na watu mahabusu zaidi ya saa 24 kinyume cha sheria kitu ambacho kinakiuka haki za binadamu. Mimi binafsi nasema haya kwa uzoefu nilionao, mara nyingi nimekuwa nakwenda kwenye *custody* nayaona haya na naongea kama Mbunge kwamba kuna ukiukwaji wa haki za binadamu, kuna watu wanakaa zaidi ya miezi miwili katika vituo vya poilisi wanakuwa *tortured,* wanapigwa na wanaumizwa.

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na tatizo hili ambapo kumekuwa na ukiukwaji wa haki za binadamu katika vituo vya polisi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la msingi la Mhehimiwa Msigwa hapa imebeba hoja, ni lini Tume italeta taarifa kuhusiana na vitendo ambavyo vinavyanywa na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwneyekiti, kazi ya Tume hii inajikita katika maeneo tofauti tofauti, ukiacha masuala ambayo yanahusisha polisi, lakini Tume hii ina kazi nyingi za kufanya kwa maana ya kutoa elimu lakini vilevile kwenda kutembelea katika shule za maadilisho, mahabusu za watoto na kila Tume inapokwenda kufanya kazi hiyo imekuwa ikiandaa taarifa na kuziwasilisha katika taasisi husika na mojawapo ikiwa ni kutoa maangalizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa tu ya Mheshimiwa Mbunge, Tume imekuwa ikifanya kazi hii. Kwa mfano, kipindi cha mwaka jana ilitolewa kauli moja kutoka kule Zanzibar na Jeshi la Polisi la kuzuia baadhi ya wafuasi wasiwakilishwe mahakamani na Tume ilitoa maelekezo na kulionya Jeshi la Polisi kwamba hizo ni haki za kimsingi kwa sababu ukisoma kwenye Sheria ya Mwenedo wa Makosa ya Jinai, kifungu cha 40 kinaelekeza kabisa kwamba kila mtu ana haki ya kuwasilishwa katika kesi za jinai.

Kwa hiyo, Tume imefanya kazi yake kuhakikisha kwamba likitokea jambo lolote lile kuhusu taasisi mbalimbali za Serikali au binafsi ambazo zinaonekana kama zinakiuka haki basi wamekuwa kwakitoa taarifa zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa kumalizia ni kwamba pamoja na ukaguzi unaofanyika taarifa hizi zimekuwa zikiandaliwa na wahusika wamekuwa wakiwasilishiwa na hapa Bungeni taarifa itakuja rasmi kwa sababu ya ile taarifa ambayo tunaitegemea ya Tume ambayo itawasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU H. AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi alisema Tume imekuwa ikiongeza jitihada kila mwaka kukagua vituo vya polisi na magereza. Je, katika kukagua vituo hivyo hasa vya polisi wameona makosa gani na hatua gani zimechukuliwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili Kikatiba wanafunzi walioko magerezani...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku unatakiwa ulize swali moja tu la nyongeza. Mheshimiwa Waziri naomba majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jaku anataka kufahamu baada ya kaguzi hizi ni makosa gani yameonekana. Nirudie tu majibu yangu ya msingi niliyoyasema kwamba ripoti hii ikikamilika itawasilishwa. Nachelea kusema moja kwa moja kwa sababu iko ndani ya ripoti na ripoti hii itawasilishwa. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge avute subira ripoti hii ikiwasilishwa ataona ukaguzi uliofanyika na matokeo ya ukaguzi huo.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalumu sasa aulize swali lake.

Na. 35

**Hitaji la Mahakama ya Mkoa - Katavi**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Mkoa wa Katavi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejiwekea mpango mkakati wa kujenga Mahakama katika Mikoa na Wilaya zote nchini kwa awamu. Katika mpango huu, Mahakama ya Mkoa wa Katavi ambalo jengo lake litakuwa pia ni Mahakama ya Wilaya ya Mpanda lilipangwa kujengwa katka mwaka wa fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari ujenzi umekwishakuanza na unatarajia kukamilika kabla ya Juni 2018. Aidha, huu ni moja ya miradi ya ujenzi wa Mahakama inayotekelezwa nchini kwa kutumia teknolojia rahisi na ya kisasa ya moladi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lupembe, majibu hayajajitosheleza una swali lingine?

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niipongeze Serikali kwa kazi nzuri na juhudi zinazoendelea kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunashukuru kweli tunajengewa Mahakama ya Mkoa pamoja na Wilaya katika jengo moja. Lile jengo limejengwa vyumba vinne tu na Mahakimu wa Mkoa wanahitajika wawili na Mahakimu wa Wilaya wanahitajika wawili. Jaji akija hana ofisi ya kukaa na hakuna sehemu nyingine ya huduma mbalimbali za kiofisi.

Je, Serikali haioni kwamba hilo jengo ni la muda tu siyo la muda mrefu? Serikali haioni kama itapata hasara kujenga sasa hivi na wakati mwingine wajenge tena. Lini sasa Serikali itaongeza lilelile jengo liwe kubwa na la kutosheleza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, ndani ya Mkoa wetu wa Katavi Mahakimu ni wachache sana, je, Serikali itaongeza lini Mahakimu ndani ya Mkoa wetu wa Katavi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza anazungumza kuhusu jengo hili kuwa na vyumba ambavyo havitoshi na kama Serikali itaingia hasara kwa sababu baadae tena itahitajika kujenga jengo lingine. Nianze kwa kusema jengo hili la

Mahakama ya Mkoa linajengwa katika eneo moja ambalo linaitwa Ilembo, Manispaa ya Mpanda. Tumempeleka mkandarasi ambaye anaitwa *Moladi Tanzania* yuko pale anafanya kazi hiyo, kilichojitokeza ni kwamba baada ya mvua kubwa kunyesha na udongo wa pale Ilembo ni mfinyanzi mkandarasi na *consultant* wameshauriana tumebadilisha michoro tena ambayo inachorwa upya na lengo hapa ni kuhakikisha tunajenga jengo lenye ubora wa juu ili shughuli za Mahakama ziendelee katika eneo hilo la Ilembo katika Manispaa ya Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hatua ya kwanza ambayo Serikali imefanya. Mheshimiwa Mbunge naomba ukubaliane kwamba ni hatua kubwa sana ya ujenzi wa vyumba hivyo ambavyo vitawaweka Mahakimu wa Mkoa pamoja na Mahakimu wa Wilaya. Yako bado maeneo mengi nchi nzima ambayo yana mahitaji ya Mahakama. Kwa hiyo, kwa kuanza pale Ilembo ni fursa ya kipekee kwa Mkoa na tushukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo msemo mmoja wanasema ndege mmoja wa mkononi ana thamani kuliko wawili wa shambani. Sasa tayari pale Mpanda wameshapata majengo haya, waishukuru Serikali ikitotokea bajeti nyingine tutaona namna ya kufanya lakini mahitaji ni makubwa sana kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, amezungumza kuhusu Mahakimu wachache, hii ni changamoto si tu katika Mkoa wa Katavi lakini katika Mikoa mingi sana ndani ya nchi yetu. Pindi pale bajeti itakaporuhusu ya kuwaajiri watumishi wengine, Mkoa wa Katavi pia na wenyewe tutauangalia ili kuondoa changamoto ya ukosefu wa Mahakimu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Ttunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto, Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo, sasa aulize swali lake.

Na. 36

## Utumiaji wa Vipodozi Visivyokuwa na Viwango

**MHE. MATTAR ALI SALUM** aliuliza:-

Wananchi wengi hapa nchini hasa wanawake hutumia vipodozi ambavyo havina viwango vinavyofaa kwa matumizi ya binadamu. Pamoja na jitihada za Serikali kuzuia bidhaa hizo lakini bado vinaingizwa nchini na kutumika.

(a) Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kuzuia uingizwaji na utumiaji wa vipodozi hivi?

(b) Je, Serikali inaweza kutumia fedha kiasi gani kuzuia bidhaa hiyo kuingia nchini?

(c) Je, adhabu gani inatolewa kwa yeyote atakayekamatwa akiingiza nchini vipodozi visivyofaa kwa matumizi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo, lenye sehemu (a) (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, *TFDA* imekuwa ikichukua hatua zifuatazo kudhibiti uingizwaji na utumiaji wa vipodozi. Vipodozi vyote hutakiwa kusajiliwa kabla ya kibali cha kuingiza nchi kutolewa. Mpaka sasa *TFDA* imesajili jumla ya vipodozi 3,179 ambavyo ndivyo vinavyorushusiwa kuingizwa na kutumika nchini. *TFDA* imefungua Ofisi saba za Kanda katika Mikoa ya Arusha kwa maana ya Kanda ya Kaskazini, Dar es Salaam - Kanda ya Mashariki, Dodoma - Kanda ya Kati, Mbeya - Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mtwara - Kanda

ya Kusini, Mwanza - Kanda ya Ziwa na Tabora - Kanda ya Magharibi kwa lengo la kuimarisha ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 maeneo 3,648 yalikaguliwa ambapo kati ya hayo maeneo 120 yalikutwa na vipodozi ambavyo havina viwango vinavyofaa kwa matumizi kwa binadamu na wahusika kuchukuliwa hatua za kisheria. Vilevile jumla ya tani 407.82 za vipodozi vilivyopigwa marufuku vyenye thamani ya shilingi za Kitanzania bilioni 1.36 ziliteketezwa na *TFDA* na kesi 52 zilifunguliwa Mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sanjari na hilo, wakaguzi wa *TFDA* wamewekwa katika vituo vya forodha kwenye mipaka ya Namanga, Holili, Horohoro, Tunduma, Sirari, Kasumulu, Mutukula, Rusumo, Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Mwanza, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa JK Nyerere na vituo vingine vya forodha vilivyoko katika Mkoa wa Da es Salaam kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa bidhaa ikiwa ni pamoja na vipodozi vinavyoingizwa nchini.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 *TFDA* ilitenga na kutumia jumla ya shilingi milioni 154.8 kwa ajili ya *operation* maalum ya ukaguzi wa bidhaa ikiwa ni pamoja na vipodozi. Aidha, katika mwaka 2017/2018, mamlaka imetenga fedha jumla ya shilingi milioni 132.16 ambazo zimekuwa zikitumika katika *operation* za kubaini na kukamata vipodozi haramu.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 91(b) cha Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura ya 129 kinatoa adhabu isiyopungua miezi mitatu au kulipa faini isiyopungua shilingi 500,000 au adhabu zote mbili kwa pamoja kwa yeyote atakayekamatwa akiingiza vipodozi visivyofaa kwa matumizi ya binadamu. Sambamba na adhabu hii, vilevile mtuhumiwa anapaswa kugharamia uteketezaji wa vipodozi vyote vilivyokamatwa na wakaguzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Mattar una swali la nyongeza?

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake ambayo yanaridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wako wafanyabiashara wanaendelea kuingiza na kufanyabiashara ya vipodozi hivi ndani ya nchi na vipodozi hivi vinawapatia madhara wananchi wetu kwa kiwango kikubwa sana, wanapata maradhi makubwa kutokana na vipodozi hivyo. Je, Serikali yako inatoa kauli gani iliyokuwa kali kuhakikisha hawa wafanyabiashara hawatoingiza wala hawafanyi tena biashara ya vipodozi hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali ina mkakati gani wa kuwasidia wale watumiaji ambao wametumia vipodozi hivi bila kuvitambua kurudi katika hali yao ya kawaida? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo. Niendelee tu kusisitiza kwamba Serikali inaendelea kuimarisha ukaguzi katika vituo vyake kama nilivyoainisha hapo awali, tunaendelea kuboresha maabara zetu, lakini vilevile sasa hivi nimezungumzia kifungu cha adhabu tunafikiria kukiboresha zaidi ili kutoa adhabu kali kwa wale ambao wanaingiza vipodozi haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili lilikuwa linauliza je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wahanga wa vipodozi vilivyo chini ya viwango. Kwa sasa hivi Serikali hatuna mkakati wowote wa kuwasidia wale wahanga, lakini tunachokifanya ni kutoa elimu ya kutotumia vipodozi ambavyo havijasajiliwa nchini. Vilevile tunashirikiana na mamlaka mbalimbali ikiwa ni pamoja na *TFDA,* Polisi na Halmashauri kubaini vipodozi ambavyo vimeingia nchini

kinyume cha taratibu na kuvikamata na kuchukua hatua stahiki kwa wale ambao wanahusika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Susan Lyimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Abdallah Juma.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sambamba na vipodozi hivyo, pia kumekuwepo na wimbi la baadhi ya akina dada na akina mama kutumia sindano za kuongeza sehemu za maumbile yao kama vile makalio na maziwa. Je, nyongeza hizi za maumbile yao zina athari yoyote kiafya na kama zinayo Serikali inatoa tamko gani? *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Susan. Mheshimiwa Naibu Waziri kama unaweza kulijibu swali hilo. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu alituumba kila mtu kwa aina yake, kwa rangi yake na maumbile yake. Nyongeza hizi kitaalam zina madhara kama vilivyo vipodozi haramu. Ngozi ina matumizi yake, Mwenyezi Mungu hakuiweka pale kwa makosa, inatusaidia sisi kwanza kujikinga na mionzi na magonjwa. Kwa hiyo, matumizi ya vipodozi moja, yanaleta madhara katika ngozi lakini pili yanaweza kupelekea mtu kupata saratani sambamba na hizi sindano na dawa nyingine za kuongeza maumbile zina madhara makubwa kwenye mwili. Kauli yangu kwa wananchi, tuache kutumia vipodozi na madawa haya, Mwenyezi Mungu alituumba na makusudio yake tuendelee kuishi kwa maumbile na rangi zetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya kitaalam. Mheshimiwa Asha Abdullah Juma. *(Makofi)*

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa mashaka na madhila yatokanayo na matumizi ya vipodozi hatarishi yanazidi kuwaathiri wananchi wetu waliokuwa wengi, japokuwa

Mheshimiwa Waziri umegusia kama mtatoa elimu, lakini nataka kujua kuna mkakati gani madhubuti kwa elimu hii ya umma ili wananchi hawa wafahamu na wasiweze kutumia vipodozi hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali iwe na mkakati wa kuwawajibisha na kuwalazimisha kulipa gharama za tiba kwa maradhi yanayosababishwa na matumizi ya vipodozi hivi kwa vile kila siku tunaambiwa tusitumie na wao hawasikii. Kwa hiyo, sehemu ile ya tiba walipe wale kwa sababu Serikali ina maradhi mengi sana ya kushughulikia, lakini bado...

**MBUNGE FULANI:** Hilo swali au nini?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** ...inashughulikia maradhi ya makusudi ya kutafuta weupe. Kwa hivyo, Serikali ina kauli juu ya hilo?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa ushauri na swali. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Asha Mshua, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumeanza mkakati wa kutoa taarifa na elimu katika vyombo vya habari, mihadhara, matangazo ya redio, mafunzo kwa njia ya mada, maonyesho pamoja na huduma kwa wateja.

Katika mwaka wa fedha 2016/2017 tumeweza kutoa elimu kwa wanafuzi 73,323 katika vyuo saba na shule za sekondari 170 katika mikoa yote 21 nchini. Nitaendelea kusisitiza kwamba tunapokea ushauri wako Bi. Mshua na tutajaribu kuzingatia wakati tunafikiria kuongeza adhabu zinazohusiana na uingizaji na matumizi ya vipodozi haramu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 37

### Ongezeko la Watoto wa Mitaani

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza:-

Kumekuwa na wimbi kubwa la ongezeko la watoto wa mtaani katika miji na majiji mengi hapa nchini.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na sheria zitakazoibana jamii kuwa na wajibu wa kulea watoto hawa badala ya kuwaachia majukumu Mashirika yasiyo ya Kiserikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna ongezeko la watoto wa mitaani katika miji na majiji mengi hapa nchini. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inatekeleza Sheria ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009 ambayo inabainisha majukumu ya familia, jamii pamoja na Halmashauri za Miji na Majiji hapa nchini katika kutekeleza wajibu wa matunzo na malezi ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi wakiwemo watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 95(1) cha Sheria ya Mtoto kinaelekeza na naomba kunukuu; *"Ni jukumu la kila mwanajamii ambaye atakuwa na ushahidi au taarifa ya kuwa haki za mtoto zinavunjwa na wazazi, walezi au ndugu ambao wana jukumu la kumlea mtoto lakini wameshindwa kufanya hivyo au wameacha kwa makusudi kutoa huduma za chakula, malazi, haki ya kucheza au kupumzika, mavazi, haki ya matibabu na elimu atatakiwa kutoa taarifa kwa uongozi wa Halmashauri husika."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 95(2), kinamuelekeza Afisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri husika kupokea taarifa ya malalamiko na kumwita mlalamikiwa ili kujadili tatizo hilo. Maamuzi yatatolewa na Afisa Ustawi wa Jamii kwa kuzingatia maslahi mazima ya mtoto husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo mlalamikiwa atapuuza maamuzi yalyotolewa na Afisa Ustawi wa Jamii, shauri hilo litafikishwa Mahakamani kwa mujibu wa kifungu cha 95(5) ambacho kinaelekeza na naomba kunukuu; *"Mtu yeyote atakayekiuka kifungu cha 95(1) atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani atahukumiwa kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini za Kitanzania au kifungo cha miezi mitatu jela au vyote viwili"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuzielekeza Halmashauri zote nchini kutunga Sheria Ndogo zitakazodhibiti watu wanaosababisha watoto kuishi na kufanya kazi mitaani. Aidha, Waheshimiwa Wabunge na sisi tutoe elimu ya uwepo wa sheria hii kwa wapiga kura wetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Hawa Subira una swali la nyongeza?

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tabia sugu ya wazazi hasa wababa kutelekeza watoto na kuwaachia akina mama walee watoto hao peke yao.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudumu wa kuyapa nguvu Madawati ya Jinsia na Mabaraza ya Usuluhishi katika kata zetu ili waweze kuweka sheria ngumu ambayo itawafanya wababa hawa wasiweze kutelekeza watoto wao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali ina mpango gani wa kuzileta Bungeni Sheria za Ustawi wa Jamii ili tuweze kuzibadilisha kama siyo kuziondoa zile za zamani ili ziweze kuendana na hali ya maisha ya sasa? Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga kwa maswali yake mazuri, lakini vilevile kuwa mtetezi mzuri wa haki za watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba Serikali imeandaa na kuzindua Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili wa Jinsia dhidi ya akina Mama na Watoto wa mwaka 2017/2018 na utaisha mwaka 2020/2021. Sambamba na hilo, utekelezaji wake umeshaanza kwani hivi tunavyoongea sasa hivi tumezindua madawati 417 katika vituo vyetu vyote vya polisi ambavyo vinasimamia masuala yote yanayohusiana na ukatili wa kijinsia kwa akina mama na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, sasa tunakwenda mbali zaidi na kwamba tunaanzisha Kamati za Ulinzi wa wanawake na watoto ambapo Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa Maendeleo ya Jamii na Wajumbe wa Mabaraza watakuwa ni sehemu ya mkakati huo, kuwajengea uwezo, kuwapa elimu kusimamia haki za wanawake na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri katika swali lako la pili kwamba viwango vya sasa haviendani na hali halisi, sasa hivi tu katika mchakato wa kuandaa Sheria mpya ya Ustawi wa Jamii ambayo itazingatia hali ya sasa.

**MWENYEKITI:** Naomba maswali mafupi sana ya nyongeza, Mheshimiwa Khatib, Mheshimiwa Maryam Msabaha na Mheshimiwa Halima Bulembo.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa hakuna shaka yoyote chanzo kikuu cha ongezeko la watoto hawa ni kutokana na wanaume wanaoshindwa kutimiza wajibu wao na kuwaachia ulezi wanawake peke yao. Katika Bunge lililopita nilishuhudia binafsi hapa Bungeni wanawake wakileta watoto waliotelekezwa na Waheshimiwa Wabunge. *(Kicheko/ Makofi/Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Kweli, kweli.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kupitia Waziri wa Afya, yuko tayari kutoa wito kwa wanawake wote waliotelekezewa watoto na Waheshimiwa Wabunge wawalete hapa na wakabidhiwe majukumu yao? *(Kicheko/ Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shida siyo kuzaa, shida ni matunzo na kulea na mimi nitoe rai kwa wanaume wote pamoja na sisi Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha kwamba tunashiriki kikamilifu katika matunzo na malezi ya watoto. Hata hivyo, nataka tujielekeze zaidi katika mfumo wa sheria na kutengeneza mfumo endelevu. Sheria yetu inatutaka twende katika Ofisi za Ustawi wa Jamii katika Halmashauri zetu badala ya kuwaleta watoto hawa wote hapa Bungeni. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Maryam Msabaha.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi nipate kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kumekuwa na tatizo la watoto wa mitaani hasa kwenye miji mikubwa kwa mfano, Arusha, Mwanza, Dar es Salaam na kadhalika na watoto hawa wamekuwa wakitumiwa kwenye masuala ya uhalifu kama madawa ya kulevya na kadhalika. Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha watoto hawa wanarudi shuleni na kupata angalau malezi bora? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali tunakiri tumekuwa na tatizo hilo na moja ya jambo ambalo tumelifanya kwanza ni kubaini idadi ya watoto katika hii miji mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika takwimu tulizokuwa nazo sasa hivi katika Mikoa ya Mwanza, Dar es Salaam, Iringa, Mbeya, Dodoma na Arusha tuliweza kubaini watoto 7,748 ambapo 6,365 walibainika kwamba wanashinda mitaani na kurudi nyumbani na watoto 1,383 hushinda na kulala mitaani. Pamoja na juhudi hizo, Serikali kati ya mwezi Julai, 2017 mpaka Novemba, 2017 tuliweza kuwaunganisha watoto 952 na kuwarejesha katika familia zao.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Halima Bulembo, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Malembeka na

Mheshimiwa Ritta Kabati. Natoa nafasi zaidi kwa wanawake kwa sababu linawagusa. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 8 Septemba, 2016 niliuliza swali kama hili na nikatoa utafiti nikampa Naibu Waziri ambao ulionesha Serikali ya Tanzania haijui tatizo la watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Baada ya kusikiliza majibu ya Serikali, nalazimika kusema kwamba bado Serikali haijalijua kwa undani suala la watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Je, ni lini sasa Serikali itaamua kufanya utafiti na kuja kutupa namba sahihi ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu nchini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema kwamba Serikali haijui takwimu sahihi na hapa katika majibu yangu ya swali la nyongeza ambalo lilikuwa limeulizwa na Mheshimiwa Maryam Msabaha nimetoa takwimu naomba nizirudie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mikoa sita ambayo tumefanya ukaguzi kwa maana ya Mkoa wa Mwanza, Dar es Salaam, Iringa, Mbeya, Dodoma na Arusha tumebaini watoto 7,748 kati yao 6,365 walikuwa wanashinda mitaani na kurudi majumbani na watoto wengine 1,383 hushinda na kulala mitaani.

Katika hawa watoto Mheshimiwa Halima Bulembo 952 tumeweza kuwarudisha na kuwaunganisha na familia zao. Kwa hiyo, naomba nimalizie kwa kusema kwamba Serikali inatambua tatizo hilo na imeshachukua hatua.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya ukatili na unyanyasaji mkubwa wa watoto wa kike ni wa kuwanyima fursa ya kurudi shuleni pale ambapo wanapata ujauzito kwa kuzingatia mazingira mbalimbali ambayo yanapelekea watoto wetu wa kike kupata mimba wakiwa watoto wadogo. Sasa ninatambua kwamba kipindi cha Serikali ya Awamu ya Nne ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na *cabinet* yake, kuna *initiative* mbalimbali walizozifanya hali iliyopelekea kuanza utekelezaji wa *re-entry policy*, kwamba mtoto anapata mimba, anapata fursa ya kurudi shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitaka tu Serikali iniambie, kwa kuzingatia kwamba kama viongozi, tuna wajibu wa kujali mustakabali wa mtoto wa kike; na kwa kuzingatia kwamba katika nchi yetu kuna mazingira mengi ambayo nikiyataja hapa siwezi kuyamaliza, yanayopelekea mtoto huyu kushindwa kusoma na kushindwa kuzuia hivyo vishawishi ama kushindwa kukabiliana na nguvu kubwa za nje ambazo zinamzidi uwezo wake wa akili; ni lini sasa Serikali itafanya utekelezaji wa ile kazi kubwa ambayo mlifanya katika kipindi cha miaka 10 iliyopita mpaka kipindi cha awamu ya Mheshimiwa Jakaya kilipoisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitaji kujua utekelezaji tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kulikuwa na maandalizi ya *re-entry policy* lakini utekelezaji wake sasa umepitwa na wakati kutokana na maagizo ambayo yametolewa na Serikali kwamba mtoto ambaye amepata ujauzito hataruhusiwa kurudi tena katika shule ambayo alikuwa anasoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maagizo haya hayajamzuia mtoto wa kike ambaye amepata ujauzito kutoendelea na

masomo. Naomba tuelewane vizuri, imezuia mtoto wa kike kurudi shule ambayo alikuwa anasoma, lakini haijazuia mtoto wa kike kuendelea na masomo. Kwa hiyo, ndani ya Serikali tunajaribu njia mbadala ya kuhakikisha kwamba watoto hawa ambao wamepata ujauzito wanaendelea na masomo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu, karibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maelezo yake mazuri kuhusiana na suala la watoto ambao wanapata ujauzito kurudi shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema ni kwamba Serikali imekwishaeleza kwamba mwanafunzi anayepata ujauzito hawezi kurudi shuleni, lakini mwanafunzi huyo anaweza akaendelea na masomo kwa kupitia njia mbadala ambazo tuna vituo vya elimu, zipo Taasisi zetu za Elimu ya Watu Wazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, msimamo wa Serikali ni kwamba mwanafunzi hawezi kurudi shuleni lakini anaweza akapata masomo kupitia njia mbalimbali ambazo Serikali inazitoa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Malembeka halafu Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala la kutelekezwa kwa watoto ni jambo ambalo wanawake/ Wabunge hatuwezi kulifumbia macho; ili kupata uhakika na ukweli kuhusu watoto wanaotelekezwa na Waheshimiwa Wabunge wanaume, kwa nini tusifungue Kituo cha Ustawi wa Jamii hapa ili kuweka mambo sawa? Ahsante. *(Kicheko/ Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Malembeka. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana suala la utelekezaji wa watoto hapa Bungeni ni changamoto kubwa sana. Naomba nirudie majibu yangu ya msingi kwamba sheria ya mtoto imeweka utaratibu mzuri tu wa kushughulikia mashauri ambayo yanahusu utelekezwaji ama watoto kutopata matunzo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusisitiza kwamba madawati yetu ya Halmashauri katika ngazi ya Halmashauri yatumike katika masuala haya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwani kuna tatizo kufungua dawati Bungeni? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. RITTA A. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa na mimi nafasi kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna baadhi ya wazazi au walezi hasa katika Majiji kwa mfano Jiji la Dar es Salaam wamekuwa wakiwatumia watoto wadogo kuomba omba hata kule kwenye magari, tumekuwa tukishuhudia na nimeona katika jibu la msingi Mheshimiwa Waziri amesema kwamba wazazi kama hao wanatakiwa wachukuliwe sheria/ hatua, kwa sababu watoto hawa wanakosa haki yao ya msingi na wakati elimu ni bila malipo.

Je, ni nani sasa anawachukulia hatua wale wazazi au walezi ambao wanawatumia watoto katika kuomba omba kwenye magari?

**MWENYEKITI:** Mhehimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto ya mwaka 2008 mtoto hana haki zake kama tano. Mtoto ana haki ya kuishi, kuendelezwa, kulindwa, kushirikishwa na pia mtoto hana haki ya kutobaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba mtoto kama nilivyoainisha katika haki zake za msingi, ni jukumu la kwetu sisi wazazi, walezi, jamii na Serikali katika ngazi ya Mitaa na Serikali Kuu kuhakikisha kwamba mtoto anapata haki zake zote hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kabati alikuwa ameelekeza swali lake katika Mkoa wa Dar es Salaam, tuna mikakati mbalimbali ambayo tunaendelea nayo kuhakikisha kwamba watoto wale wa mitaani wanapata haki zao stahili pamoja na kuondolewa katika mitaa.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Kikwembe, tumalizie wa mwisho.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilitaka kufahamu kutokana na maswali yaliyokuwa yanaulizwa, Mheshimiwa Mbunge aliyeketi muda siyo mrefu ameongea kuhusu Waheshimiwa Wabunge kutelekeza watoto. Sasa nilitaka kuuliza, Waheshimiwa Wabunge hawa wanatelekeza watoto kwa Waheshimiwa Wabunge wenzao ama nje ya Wabunge? *(Kicheko)*

**MWENYEKITI**: Mhehimiwa Naibu Waziri, majibu kwa hilo swali. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Kumekucha! *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Au haliwezekani kujibiwa? Kama huwezi, basi unaweza kuliacha.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

inaonekana suala la kutelekeza watoto katika Bunge limekuwa ni kubwa sana. Hili nalirudisha katika kiti chako sasa uweze kuangalia utaratibu mzuri wa kuweza kulishighulikia. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Basi limefika hapa, litafanyiwa kazi yake ipasavyo. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, sasa Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mbunge wa Bariadi sasa aulize swali lake.

Na. 38

**Barabara ya Bariadi Hadi Daraja la Mto Sibiti**

**MHE. ANDREW J. CHENGE** aliuliza:-

Sera ya Serikali ni kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa kwa barabara za kiwango cha lami. Mkoa wa Simiyu haujaunganishwa na mikoa jirani ya Singida na Arusha.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara ya Bariadi – Kisesa – Mwanhuzi hadi Daraja la Mto Sibiti na hatimaye ijengwe kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Andrew Chenge, Mbunge wa Bariadi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshaanza juhudi za kuunganisha Mkoa wa Simiyu na Mikoa jirani ya Singida na Arusha kwa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mchepuo wa kusini wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti *(Serengeti Southern Bypass).* Upembuzi yakinifu unajumuisha barabara ya Karatu – Sibiti kupitia Mbulu na Karatu kupitia Ziwa Eyasi hadi Sibiti – Mwanhuzi – Lalago hadi

Maswa. Matokeo ya mapendekezo ya njia ipi ya kupita yatapatikana kazi hii itakapokamilika katika mwaka wa 2018. Kazi hii inafadhiliwa na Serikali ya Ujerumani kupitia Benki yake ya Maendeleo (*KfW*).

Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara ya Kolandoto *Junction* – Lalago – Mwanhuzi – Sibiti – Oldean *Junction* (kilometa 328) umekamilika ikiwemo sehemu ya barabara kuu ya Ng'oboko – Mwanhuzi hadi daraja la Sibiti. Kazi hii imegharamiwa na Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Bariadi – Kisesa – Mwanhuzi hadi daraja la Sibiti imegawanyika katika sehemu mbili kama ifuatavyo: sehemu ya kwanza ni barabara ya Mkoa wa Baliadi - Kisesa – Mwandoya hadi Ng'oboko yenye urefu wa kilometa 100.71 inavyoungana na barabara kuu ya Kolandoto – Lalago – Mwanhuzi hadi Daraja la Sibiti. Sehemu ya pili ni sehemu ya barabara kuu kuanzia Ng'oboko – Mwanhuzi hadi daraja la Sibiti yenye urefu wa kilometa 79.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa ujenzi wa daraja la mto Sibiti lenye urefu wa mita 82 pamoja na barabara unganishi (kilometa 25) unaendelea na unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Bariadi – Kisesa – Mwandoya – Ng'oboko (kilometa 105) pamoja na Sibiti – Mkalama – Nduguti – Iguguno hadi Singida (kilometa 103.54) ziko kwenye mpango mkakati wa miaka mitano kwa ajili ya kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hizo tajwa za usanifu zikikamilika, Serikali itatafuta fedha za kujenga barabara zote kwa kiwango cha lami kwa awamu na kulingana na upatikanaji wa fedha. Hivyo, Makao Makuu ya Mikoa ya Simiyu, Arusha na Singida yatakuwa yameunganishwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Andrew Chenge, una swali la nyongeza?

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Natambua juhudi za Serikali zinazofanyika kwa kuunganisha Mkoa wa Simiyu na Mikoa jirani ya Singida na Arusha. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza ningependa kufahamu kama huo mpango mkakati wa miaka mitano alioutaja Mheshimiwa Waziri, unashabihiana vipi na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 na 2020?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kwenye bajeti ya mwaka 2018/2019 kuingiza sehemu ya barabara hiyo ya Moboko – Mwandoya – Kisesa - Bariadi kwa upande wa Mkoa wa Simiyu; na mto Sibiti – Mkalama – Nguguti - Iguguno na Singida ili sehemu hizi mbili za barabara hii muhimu ziweze kufanyiwa kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Chenge. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Chenge kwa namna ambavyo anapigania hii barabara iweze kujengwa, lakini kwa maendeleo kwa ujumla katika Mkoa huu wa Simiyu.

Vilevile niseme kwamba barabara hii ambayo anaizungumza Mheshimiwa Chenge ni muhimu sana kwa mikoa mingi ikiwemo Kagera, Mwanza, Shinyanga, Mara kwa sababu barabara hii itakapojengwa itawezesha watu wote katika mikoa hii ninayoitaja kupita na kupunguza umbali katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kama alivyosema katika swali lake la kwanza, kwamba katika

mpango wa miaka mitano, tunashughulikia hii kwa sababu imetajwa pia katika ilani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba Mheshimiwa Andrew Chenge mwenyewe anafahamu kwamba tumeshaanza ujenzi katika Mto Sibiti na kazi hii itakamilika mwishoni mwa mwaka huu na ule utaratibu wa uratibu wa usanifu wa barabara hii, fedha nyingi sana zimetengwa. Zimetengwa *Euro* milioni 2.8 ili kuweza kukamilisha kazi hii. Niseme tu kwamba ili kazi ikamilike kuendana na kipindi hiki cha miaka mitano na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, ziko *consultancy* nne ambazo zimeungana pamoja ili kuhakikisha kazi inakamilika kwa haraka. Kwa hiyo, utekelezaji wa Ilani utakwenda sambamba na kazi kubwa sana ambayo inaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu kuingiza hii sehemu kwenye usanifu katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha, ushauri wako huu muhimu nauchukua ili wakati wa *process* ya bajeti hii inaendelea, tulifanyie kazi itakapowezekana, tutaweka fedha ili kuanza usanifu wa vipande hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande hiki cha barabara kutoka Mkalama kwenda Singida, iko barabara nyingine ambayo inatoka upande wa Sibiti, inapita Msingi kwenda Ulemo hii pia itawezesha watu wa maeneo yale waweze kupita kiurahisi wakitokea Mkoa wa Simiyu.

Mhesimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwa wananchi wa Meatu, Simiyu watakuwa na *access* nzuri kwenda kutibiwa Haydom. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tunatambua umuhimu wa barabara hii na ndiyo maana tumeiweka katika ilani na tutaitekeleza ili wananchi waweze kupata manufaa makubwa zaidi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu kwa leo wa maswali tumeishia saa 4.30 lakini kuna swali moja itabidi nilimalizie, nalo ni swali la Mheshimiwa Rashid Akbar Shangazi, Mbunge wa Newala Vijiji, sasa aulize swali lake.

**MHE. RASHID A. AJALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sio Shangazi. Shangazi ni *partner* wangu. Mimi ni Rashid Akbar Ajali. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Sawa Mheshimiwa Akbar, tuendelee.

Na. 39

**Upanuzi wa Barabara ya Kuelekea Chitandi – Masasi**

**MHE. AJALI R. AKBAR** aliuliza:-

Wilaya ya Newala ni Wilaya kongwe ambayo hata utawala wa Wajerumani ulizingatia mpango bora wa matumizi ya ardhi ambao Wilaya hiyo imepangwa tangu enzi lakini hivi karibuni *TANROADS* wamefanya upanuzi wa barabara ulioelekea hadi Chitandi – Masasi.

Je, kwa nini Serikali kupitia *TANROADS* Mtwara isifanye tathmini ya nyumba za wakazi hao na kuwalipa fidia?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ajali Rashid Akbar, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mbuyuni – Makong'onda – Newala sehemu ya Chitandi – Masasi yenye urefu wa kilometa 41.55 ni barabara ya mkoa inayoungana na barabara ya Mkoa ya Mtwara – Newala – Masasi yenye urefu wa kilometa 221. Barabara hii ina upana wa eneo la Hifadhi ya Barabara ya mita 60. Kabla ya marekebisho kupitia Sheria ya Barabara ya mwaka 2007 upana wa eneo la hifadhi ulikuwa mita 45, yaani mita 22.5 kutoka katikati ya kila upande wa barabara. Sehemu ya barabara hii inapita katika milima mikali ya Makong'onda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, katika bajeti ya mwaka 2016/2017 ilitenga shilingi milioni 581.586 na mwaka 2017/2018 ilitenga shilingi milioni 396.437 kwa ajili ya kuboresha ahadi ya barabara kufikia kiwango cha lami katika milima ya Makong'onda na kupunguza ajali kwenye sehemu ya miteremko mikali. Jumla ya kilometa mbili za barabara katika milima Makong'onda zimejengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na utekelezaji wa upanuzi wa barabara unaoendelea, Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* ilitoa notisi kwa wananchi wanaomiliki mali ndani ya mita 22.5 za eneo la hifadhi ya barabara ili waondoe mali zao na kuacha wazi eneo hilo kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Barabara Namba 13 ya Mwaka 2007 na kanuni za mwaka 2009.

Aidha, kwa walio ndani ya mita 7.5 ambazo ni kutoka zinapoishia mita 22.5 za eneo la hifadhi ya barabara na mita 30 zilizoainishwa katika Sheria ya Barabara Namba 13 ya mwaka 2007, tathmini ya mali zao itafanyika pindi Serikali itakapohitaji maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutolewa notisi hizo, baadhi ya wananchi walipeleka malalamiko yao katika Mahakama ya Ardhi ya Kanda ya Mtwara kupinga kuondoa mali hizo ambapo hadi sasa shauri hilo bado liko Mahakamani. Taratibu za Kimahakama zitakapokamilika, Serikali itachukua hatua stahiki kwa kuzingatia uamuzi wa Mahakama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Akbar, una swali la nyongeza?

**MHE. AJALI R. AKBAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo kuhusu barabara hii kupitia kwenye milima, tatizo langu ni uwepo wa sheria kwamba kama nilivyozungumza kwenye swali langu la

msingi, mji huu wa Newala upo tangu mwaka 1800; kama wakati ule ilikuwa inaitwa *Dutch East Africa*. Hii sheria ya mwaka 2007 imekuta wananchi wale wakiwa na taasisi zile katika uwepo halali. Kuna polisi, mabenki na wananchi, maana yake walikuwepo kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake wanachopinga wao ni kwamba hii sheria imewakuta wao wakiwepo kisheria. Kwa hiyo, swali langu la msingi, je, ni lini *TANROADS* watafanya mazungumzo na wananchi hawa wa Newala ili tukaondoe kesi ile Mahakamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kutokana na ufinyu wa Mji wa Newala, je, sasa *TANROADS* wako tayari badala ya kupitisha ile barabara Newala Mjini, wapitishe Kiduni hadi Nambunga kwa Mheshimiwa Mkuchika ili kuepuka mrundikano wa barabara katika ya mji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge, anafuatilia sana maendeleo ya Newala na anajua eneo hili ambalo analizungumza pia ni maarufu sana kwa uzalishaji wa korosho.

Kwa hiyo, namuahidi kwamba sisi Serikali tuko tayari kwenda kufanya mazungumzo na ninampongeza sana kwa nia yake thabiti ya kuhakikisha kwamba kama shauri hii tunalimaliza, itaharakisha pia ujenzi wa barabara. Kwa hiyo, tuko tayari kuzungumza ili tulimalize ili wananchi hawa waweze kupata haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa ule utaratibu ambao wanafikiria, na mimi eneo lile nilitembelea, ni kwamba tukiweza kupitisha *bypass* kwenye eneo hilo, tutaweza pia kuufanya mji upendeze lakini pia kupanua huduma, kwa hiyo,

tutakuwa tuko tayari kuhakikisha kwamba tunarekebisha michoro na saa nyingine wananchi waweze kupata haki zao. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa leo muda wetu wa maswali umeishia hapo.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya muda wetu wa maswali kuisha, tuna matangazo. Tangazo la kwanza, ni wageni ambao wapo katika Bunge letu asubuhi hii ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, wako wageni wa aina mbili, kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao wa kwanza ni wageni wanne wangu mwenyewe, Mwenyekiti Najma Murtaza Giga, ambao ni Wajumbe wa Umoja wa Wazazi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Mkoa wa Katavi, wakiongozwa na Katibu wa Wazazi wa Mkoa, Ndugu Mwasiti Mohamed. Karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wawili wa Mheshimiwa Joseph Mhagama, ambao ni viongozi wa Shule ya Sekondari ya Wilima kutoka Madaba Mkoa wa Ruvuma ambao ni Mwenyekiti wa Bodi ya shule hiyo, Ndugu Richard Mwaseba pamoja na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Mwalimu Christopher Mng'ong'o. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Mhagama. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo wako wanafunzi 70 kutoka Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini Mkoa wa Dodoma. Wanafunzi wetu karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wengine ni wanafunzi 75 na walimu 15 kutoka Shule ya Msingi St. Monica ya Jijini Arusha. Karibuni sana wanafunzi wetu katika Bunge letu.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Haya nipeni majina.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Jesca Kishoa.

**MWENYEKITI:** Mhesimiwa Jesca.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Flatei Massay

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Kanyasu.

**MWENYEKITI:** Tumemaliza? Tuanze na Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekit, ahsante. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7) kuhusiana na Mheshimiwa Waziri ambaye amehitimisha kwa wakati huu, Mheshimiwa Kwandikwa, wakati akijibu swali la Mheshimiwa Chenge na wengine waliofuata, hakuwa akisikika vizuri kwenye *microphone* na hii ni kwa sababu yeye kuwa ha-*focus,* anakuwa anageuka kulia, kushoto, nyuma geuka. Sasa nilikuwa naomba Mwongozo wako, kwa sababu kama hawa Mawaziri hawajapatiwa semina ya namna ya kuzungumza wanapokuwa humu Bungeni, kwa sababu majibu ya Serikali hayakusikika. Kwa vyovyote vile tunaweza kuja kuuliza swali lile lile na akatoa majibu yale yale pasipo sisi kumsikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba mwongozo wako kuhusiana na suala hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nasimama kwa Kanuni ya 68(7). Ninaomba Mwongozo wako, wakati Bunge linaendelea hapa, Mheshimiwa Msigwa aliuliza swali hapa na kuonesha kwamba Serikali au Polisi wanakamata kamata watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona nimepata wasiwasi kidogo. Naomba Mwongozo wako ili nijue hili, ili kama jambo hili lipo, basi Serikali iseme habari ya kukamata kamata watu, maana naona kama vile Mheshimiwa Msigwa alipoliuliza ni kama vile anaonewa au kuna uonevu wa namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTATINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Kwanza naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uvuvi na Mifugo kwa majibu yake mazuri ambayo ameyajibu leo asubuhi na pia naomba kuipongeza Serikali kwa utekelezaji wa ulinzi wa maliasili zetu za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaotoka katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa tunashuhudia operesheni kubwa inayoendelea ya Maafisa wa Uvuvi pamoja na Polisi ambayo inasababisha ukamataji wa nyavu, mitumbwi na watu na kuwaweka ndani kwa zaidi ya siku nne mpaka tano kwa kisingizio cha kusubiri faini ya papo kwa hapo ambayo ni zaidi ya mamilioni ya shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, jana Diwani wa Kata ya Kisesa, Ndugu John Bunyanya alikamatwa nyumbani kwake saa kumi jioni na kuamuliwa kupigwa faini ya shilingi milioni 40. Alipokosa pesa, alipelekwa polisi na kuwekwa ndani na limekuwa likifanyika hivyo kwa muda mrefu.

**MBUNGE FULANI:** Yesu wangu!

**MHE. CONSTATINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako, kisingizio cha maamuzi haya ni matumizi ya Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2004, Kanuni ya 2009 na Sheria ya Mazingira ambayo wanaziunganisha pamoja Maafisa hawa na kupata mamlaka ya kukamata, kupiga faini na kuweka watu ndani. Ni nini Mwongozo wa Serikali juu ya jambo hili? Kwa nini wananchi hawa ambao tayari wametii Sheria ya Serikali ya kukata nyavu hizi, wanakamatwa wakiwa wanakata nyavu nyumbani na siyo ziwani na kuwekwa ndani na sasa hivi kila askari barabarani ni Afisa Uvuvi, kila mtu anakamatwa hovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako ili wananchi hawa waache kuteseka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Miongozo niliyopokea ni mitatu.

Mwongozo wa kwanza ni wa Mheshimiwa Jesca kuhusiana na suala la Waziri kutosikika vizuri na kuzungukazunguka. Ni kwamba suala la kuzungukazunguka sifikiri kama linaathiri sana kwa vile kila mtu ana namna yake ya kuzungumza. Kwa hiyo, hilo Mwongozo wake ni huo, lakini suala la kutosikika vizuri, mimi sijaliona. Kwa hiyo, kama kutakuwa na hitilafu hiyo basi naomba lipelekwe mbele zaidi. *(Makofi)*

Tukija kwa Mheshimiwa Flatei kuhusu suala alilozungumzia, hilo naiomba au naitaka Serikali itoe maelezo kuhusiana na hilo ili tujue nini kinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kutoa ufafanuzi kuhusiana na mwongozo ambao umetolewa na Mheshimiwa Flatei Massay uliotokana na swali la nyongeza lililoulizwa na

Mheshimiwa Msigwa kuhusiana na tuhuma dhidi ya Jeshi la Polisi la kukamata watu na kuweka ndani zaidi ya saa 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa niliomba kusimama pale wakati maswali yanajibiwa vizuri kabisa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, hukuniona, lakini ni kwamba ni kweli dhamana ni haki ya kila raia na inataka mtu akae ndani kwa saa zisiyozidi 24. Kwa mujibu wa sheria hiyo hiyo, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai pamoja na Sheria ya Polisi na Polisi Wasaidizi imeweka masharti na utaratibu wa dhamana hiyo.

Sasa inawezekana tu pengine Mheshimiwa Msigwa labda tu ni kutokuielewa hii sheria, lakini kimsingi nadhani ni kifungu cha 148, kinaainisha juu ya aina ya makosa ama sababu ambazo zinasababisha na kupelekea mtu kuweza kukaa zaidi ya saa 24 katika Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mambo ambayo yameainishwa katika sheria hiyo, naomba niyataje machache. Kwanza, Polisi inaweza kuomba kibali kutoka Mahakama ikiwa haijakamilisha upelelezi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna aina ya makosa ambayo hayapaswi kupewa dhamana, kwa mfano masuala ya kuua kwa kukusudia, ubakaji, ujambazi, ugaidi na kadhalika. Pia mtu ambaye amekiuka dhamana/ameruka dhamana, ameshawahi kupewa dhamana akaikiuka, mtu huyo anakiuka masharti ya upewaji dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ikiwa Polisi itajiridhisha kwamba kumpatia dhamana mtuhumiwa huyo kutakuwa kunahatarisha maisha yake na maisha ya jamii ambayo inawazunguka, basi mtu huyo anaweza akawekwa ndani zaidi ya saa 24. Sasa inawezekana pengine, mifano ya aina ya watuhumiwa ambao amewazungumzia Mheshimiwa Msigwa ilikuwa inagusia watu wa aina kama hiyo na ndiyo maana akaona kwamba kuna watu wamekaa zaidi ya saa 24 katika vituo vya polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa kama kuna mtu ambaye amekaa zaidi ya masaa 24 kinyume na hao ambao nimewataja au ambao wameainishwa katika sheria hiyo ya Makosa ya Jinai, kifungu 148 basi taarifa hizo tuletewe ili tuweze kuchukua hatua, kitu ambacho sikifikirii. Kwa sababu katika jambo ambalo Jeshi la Polisi linajitahidi sana sasa katika Serikali ya Awamu ya Tano ni kuhakikisha kwamba Jeshi letu la Polisi linaendelea kufanya kazi zake kwa weledi na kwa kufuata sheria na kwa uadilifu. Katika jambo hilo tumefanikiwa katika kiwango kikubwa sana na hata malalamiko mengi ya wananchi sasa yamepungua kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo ufafanuzi wa Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, ahsante. Maelezo hayo ya Serikali ndiyo Mwongozo wangu katika suala la Mheshimiwa Flatei.

Kuhusu suala la Mheshimiwa Kanyasu kwa vile linataka ufuatiliaji na kufanyiwa kazi sasa naiagiza Serikali kwenye suala hilo waweze kulifanyia kazi bila kuchelewa. *(Makofi)*

Katibu, tuendelee.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

### Hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali na Hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa

**MWENYEKITI:** Hoja za Kamati, namkaribisha sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali aje kuwasilisha hoja yao. Karibu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kuwasilisha Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* kwa mwaka 2017. Inatolewa chini ya Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa hii yote ya *PAC* iingie kwenye *Hansard.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya Kamati ya *PAC*, kuhusu shughuli zilizotekelezwa kwa mwaka 2017 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2017 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali ilipokea na kujadili Taarifa ya *CAG* kuhusu ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2016. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa maelezo yanayotolewa katika taarifa hii yanatokana na hesabu zilizokaguliwa kama ilivyowasilishwa katika Taarifa hiyo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali zilizingatia majukumu yake yaliyoainishwa katika kifungu cha 14 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa majukumu hayo unatokana na taarifa ya hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyobainishwa katika kifungu cha 16 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za Kamati kwa mwaka 2017 zililenga kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali kama yalivyobainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa

fedha unaoshia tarehe 30 Juni, 2016. Aidha, Shughuli hizo zilikusudia kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali wakati wa kupitia na kujadili taarifa za Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali iliyowasilishwa Bungeni mwezi Januari, 2016 jumla ya mapendekezo 14 ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali yaliridhiwa na kuwa Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya shughuli hiyo kwa ujumla yalionesha kuwa maazimio nane kati ya maazimio 14 ambayo ni sawa na asilimia 64.2 yalikuwa yametekelezwa au yalikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, maeneo sita ambayo ni sawa na asilimia 35.8 yalikuwa hayajatekelezwa hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mafungu mahususi ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma ulibainisha mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, dosari katika mkataba wa *Mlimani City* na Chuo Kikuu. Kutokana na mkataba wa makubaliano ya ujenzi wa Mradi wa *Mlimani City* ambao ulianza tarehe 01 Oktoba, 2004 na ukitakiwa kukamilika tarehe 01 Septemba, 2006 kwa makubaliano ya mkodishwaji na mkodishaji yaani Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na *Mlimani Holding,* mradi huu haujakamilika mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya *CAG* pamoja na mahojiano na uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, umebaini dosari kubwa katika usimamizi na uendeshaji wa mradi huo hali ambayo inaipatia Serikali hasara. Dosari hizo ni kama zifuatazo:-

(a) Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 inaelekeza kuwa ili kibali cha uwekezaji kitolewe, lazima mwekezaji alete ushahidi wa kuwa na mtaji wa kutosha. Hivyo dola za Marekani 75 ambazo ni sawa na shilingi za Kitanzania 160,000 kwa *exchange rate* ya sasa zilizooneshwa kama mtaji kwenye hesabu za *Mlimani Holdings* ni kinyume cha sheria hiyo ya *TIC* inayohusu uwekezaji;

(b) *Turnstar Holding Ltd* ni miongoni mwa mwanahisa wa *Mlimani Holding,* anayemiliki hisa moja tu. *Turnstar Holding* ametoa mikopo kwa *Mlimani City* jumla ya dola za Marekani 49,027,840. Kamati ilipata mashaka kuhusu nia ya mbia huyu kwa kuwa *Mlimani Holding* ana hisa 900 ambazo hazijauzwa hivyo angeweza kununua badala ya kukopesha. Kamati inaona mbia huyu lengo lake ni kujinufaisha zaidi kwa kutoa mikopo kwa vile riba anayolipwa itatolewa kwenye mapato ghafi kabla ya kugawana faida;

(c) Kwa zaidi ya miaka 13 tangu mkataba uingiwe, mradi wa ujenzi wa hoteli ya nyota tatu yenye vyumba 100, bado haujaanza kinyume na makubaliano, hivyo kuongeza gharama za kumalizika mradi na *botanical garden;*

(d) Kumekuwepo ukiukwaji mkubwa wa malipo ya pango la ardhi ya Chuo Kikuu kama ilivyooneshwa katika kifungu 1.1(j) na 10.1 cha mkataba kinaeleza kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kitapata asilimia 10 ya pango ya mapato ghafi.

Hata hivyo, Kampuni ya *Mlimani Holdings* imekuwa ikifanya malipo ya pango kwa Chuo kwa asilimia 10 ya mapato baada ya kutoa gharama za uendeshaji, hivyo, kuikosesha Serikali mapato stahiki kinyume na mkataba;

(e) Ukiukwaji wa kifungu cha 11.2(1) cha hati ya makubaliano ya mpangaji kinachomtaka *Mlimani Holdings* kutopangisha mtu yeyote ambaye hajathibitishwa na Mpangishaji, yaani Chuo Kikuu. Hata hivyo, ukaguzi umethibitisha kuwa *Mlimani Holding* amekuwa akipangisha wapangaji wengine bila kupata kibali cha Chuo Kikuu cha

Dar es Salaam, hivyo kusababisha Chuo kukosa taarifa sahihi za mapato ya kodi kutoka kwa wapangaji wake;

(f) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati haijarishishwa na mazungumzo yanayoendelea kati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mwekezaji wa *Mlimani City.* Mwekezaji huyo amekuwa akiyakataa mapendekezo yote ambayo yangekuwa na maslahi kwa pande zote mbili, badala yake amekuwa akishikilia mapendekezo yenye maslahi kwake tu. Wakati huo huo ameweza kuongeza eneo la maduka na maegesho ya magari ambavyo havikuwemo katika mkataba. Kama hiyo haitoshi, mwekezaji ameshindwa kuanza utekelezaji wa ujenzi wa hotel na bustani; na

(g) Mapitio ya Mkataba yamebainisha kuwa mkataba huo hauelezi hali halisi ya ugawaji wa mali pindi mkataba utakapoisha (miaka 50 au 85). Hakuna makubaliano rasmi yanayoeleza mgawanyo wa mali na miundombinu itakayokuwepo pindi mkataba utakapoisha. Athari ya jambo hili ni kuwa kuna uwezekano wa kutokea mvutano wa kisheria pindi mkataba huu utakapofika ukomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dosari nyingine ni kuhusu ushiriki wa Serikali kupitia Kituo cha *TIC* ambapo *TIC* na *Mlimani City Holdings* wamekuwa wakibadilisha muda wa utekelezaji wa mradi mara kwa mara kwa kumwongezea mwekezaji muda wa kukamilisha mradi bila kuhusisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa mfano, mkataba wa kwanza ulisainiwa tarehe 27 Februari, 2006 na kumwongezea mwekezaji kipindi cha utekelezaji wa mradi hadi tarehe 30 Oktoba, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba wa pili ulisainiwa tarehe 13 Julai, kabla ule wa pili haujaisha hapo 2007 kwa kuongeza muda wa utekelezaji hadi tarehe 30 Novemba, 2013; na mkataba wa tatu ulisainiwa tarehe 10 Decemba, 2014 ambao uliongeza muda wa utekelezaji wa mradi huo hadi 31 Desemba, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mkataba unaonesha kuwa ilitakiwa kujengwa nyumba 50 za kuishi *(housing estate/*

*villas).* Kamati ilipotembelea mradi huu zilionekana nyumba 45 tu na nyumba moja yenye vyumba viwili vilivyotenganishwa na milango miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na dosari hizo zilizofafanuliwa katika aya (a) hadi (i) hapo juu, ni dhahiri mradi wa *Mlimani City* una dosari kubwa hivyo kuinyima Serikali mapato stahiki. Hivyo mradi huu unatakiwa uangaliwe kwa kina kuanzia mkataba wa kwanza hadi hapo ulipofikia sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kusimama muda mrefu kwa Mradi wa Dege, Kigamboni unaotekelezwa na *NSSF.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *Dege Eco Village*, Kigamboni ni wa ubia kati ya Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii pamoja na Kampuni ya *Azimio Housing Limited* ambapo katika mradi huo, Azimio ana hisa asilimia 55 na *NSSF* asilimia 45 kwa makubaliano ya uchangiaji wa ardhi na fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia ukaguzi uliofanywa na *CAG* na baada ya uchambuzi wa Taarifa ya Hesabu za *NSSF* zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2016, Kamati imebaini kuwa mradi huo ulisimamishwa na Serikali tangu mwezi Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mradi huo unasimama, jumla ya shilingi bilioni 219 mali ya wanachama wa *NSSF* zilikuwa zimetumika katika mradi huo. Mnamo tarehe 9 Novemba, 2016 Kamati ya *PAC* iliunda Kamati ndogo kwa ajili ya kushughulikia kwa kina hoja ya mradi wa Dege. Kamati hiyo ilitekeleza kazi zake na kuwasilisha taarifa ya uchambuzi na mapendekezo ikapelekwa kwa Mheshimiwa Spika tarehe 13 Februari, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mnamo tarehe 20 Januari, 2018 Kamati ilitembelea mradi huu wa Dege na kujionea hali halisi ya ghorofa 156 zenye nyumba 3,700 *(units)* ambazo hakuna hata moja iliyokamilika na kuuzwa. Kamati

ilipata wasiwasi juu ya usalama wa fedha za wanachama kiasi cha shilingi bilioni 219 ambazo zimeshawekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mradi huu limechukua muda mrefu kukamilika. Kamati inaisisitiza Serikali kufanya kila liwezekanalo kuepusha upotevu wa fedha za umma zilizowekezwa hapo kwa kuzingatia ukweli kuwa mradi ule kuendelea kusimamama unapungua thamani *(depreciation),* kunakuwa na ongezeko la gharama za ujenzi, uharibifu wa miundombinu na hapo Serikali inaendelea kupata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, madeni ambayo Serikali inadaiwa na mifuko ya hifadhi ya jamii ni kiasi cha shilingi trilioni 1.6

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Kamati iliripoti mwaka 2017 katika taarifa yake ya mwaka hapa Bungeni, Serikali imeendelea kulimbikiza deni inalodaiwa na mifuko mbalimbali ya hifadhi ya jamii. Hadi kufikia Juni 30, 2016 deni la mifuko ya hifadhi ya jamiiambalo muda wake wa kulipwa ulikuwa umepita lilifikia shilingi trilioni 1.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokulipwa kwa madeni hayo yaliyochambuliwa katika Jedwali hapo juu kunaathiri uwezo wa kifedha na kiutendaji wa taasisi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne ni kuhusu udhaifu katika ukusanyaji wa madeni, usimamizi na utoaji wa zabuni katika Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hairidhishwi na kasi ndogo ya Serikali na taasisi zake katika ulipaji wa madeni yake kwa *TANESCO* ambapo imepelekea deni hilo kuongezeka toka shilingi 129,298,000,000 tarehe 30 Juni, 2016 hadi kufikia shilingi bilioni 189.8 hapo 30 Juni, 2017. Hali hii inatokana na baadhi ya Wizara na Taasisi kutolipa ama kupunguza madeni yao kwa wakati na kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Wizara na Taasisi zinazobeba deni kubwa ni Hospitali ya Muhimbili, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, *DAWASCO*, Magereza na nyinginezo ambazo kwa pamoja zinachangia karibu nusu ya deni hilo kwa kiasi cha shilingi bilioni105.28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha zaidi kwani kati ya taasisi za Serikali zinazodaiwa na *TANESCO* ni Wizara yenyewe, Wizara mama ya Nishati kwa kutolipa kodi ya pango ya Jengo la *TANESCO* ambalo Wizara imekodisha. Deni hilo ni shilingi bilioni 1.6. Kamati inaishauri Serikali kulipa madeni yake kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa ya *CAG* zipo dosari katika manunuzi ya Umma kama vile:-

(i) Mikataba mingi kusainiwa baada ya kazi kutolewa kinyume na taratibu;

(ii) Mchakato wa zabuni kuchukua muda mrefu kuliko uliowekwa na sheria;

(iii) Zabuni kwenye kanda kutolewa katika kiwango cha juu kuliko kilichowekwa kisheria;

(iv) Kutoa mafungu manne *(lots)* badala ya mawili kwa mwombaji mmoja kinyume na kanuni za manunuzi; na

(v) Kukosekana kwa mpango madhubuti wa manunuzi hivyo kusababisha uwepo wa manunuzi ya dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba tano ni dosari za kimfumo katika Mamlaka ya Bandari Tanzania. Katika taarifa yake ya mwaka hapa Bungeni, mwezi Januari, 2016, Kamati ilibainisha dosari za kimfumo katika Mamlaka ya Bandari Tanzania ambazo zinasababisha upotevu mkubwa wa mapato ya Serikali. Kamati ilitegemea kuwa suala hilo lingekuwa limeshughulikiwa kwa ukamilifu katika mwaka wa fedha 2016/ 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, dosari za mfumo wa *COBOL* unaotumiwa na *TPA* umeendelea kuwa na changamoto za kuwasiliana na mifumo tanzu kama vile *Harbor View Plus, Cargo Management System* na *Tanzania Customs Intergrated System.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dosari hizo zimeendelea kuipotezea Serikali mapato kutokana na baadhi ya meli taarifa zake kutorekodiwa ipasavyo. Aidha, *TPA* wamekuwa wakishindwa kuhakiki taarifa za moja kwa moja za meli na mizigo inayohudumiwa na kitengo cha kuhudumia makontena *(TICTS),* hivyo kutokuwa na uhakika wa taarifa za fedha wanazolipwa na *TICTS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya *TPA* kwa Kamati ni kuwa wanafunga mfumo mpya wa *ERP (SAP)* na ununuzi wa mfumo wa *Port Operations Sytem (POS)* ambayo itawezesha kuunganisha mtiririko wa utoaji wa ankara, ukusanyaji mapato na kuviunganisha moja kwa moja kwenye kumbukumbu za hesabu *(general ledger)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *TPA* kutoa ahadi ya kuwa mifumo hiyo itakamilika na kuanza kufanya kazi kati ya Novemba, 2017 na Januari, 2018, bado Kamati ina mashaka makubwa na uhakika wa mifumo hiyo na udhibiti wa mapato ya Serikali katika *TPA*, ikizingatiwa kuwa mifumo hiyo inanunuliwa kwa gharama kubwa ya fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba sita, ununuzi wa magari ya polisi yenye thamani ya dola za Marekani 29,606,100 bila ya kuwepo mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya *CAG* inabainisha kuwa mnamo tarehe 05 Septemba, 2013 Jeshi la Polisi liliingia makubaliano na Kampuni ya Ashok Leyland ya nchini India kwa ajili ya ununuzi wa magari 777 yenye thamani ya dola za Marekani 29,606,100. Magari hayo yalipangwa kununuliwa kwa mkopo *(Credit facility)* kutoka Benki ya uagizaji na uingizaji bidhaa ya Exim ya India *(Export – Import Bank of India)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya *CAG* imebainisha dosari katika mchakato wa ununuzi wa magari hayo kama ifuatavyo:-

(a) Mkataba kati ya Jeshi la Polisi na Kampuni ya Ashok Leyland uliingiwa tarehe 05 Septemba, 2017 wakati Mkataba wa mkopo wa manunuzi ya magari husika kati ya Serikali na Benki ya Exim ya India ulisainiwa tarehe 19 Juni, 2015. Kwa msingi huo na kwa kuzingatia masharti ya kipengele 9.1 cha mkataba wa mkopo kati ya Serikali na Benki ya Exim ya India. Makubaliano hayo yalikuwa batili kwa sababu mkataba kati ya Jeshi la Polisi na Kampuni ya Ashok Leyland ulikwisha muda wake tangu mwezi Oktoba, 2014. Makubaliano ya Mkopo kati ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Exim ya India hayakwenda sambamba na Mkataba wa ununuzi wa magari. Hivyo ununuzi wa magari hayo una utata mkubwa sana.

(b) Gharama halisi za ununuzi wa magari hayo pia una dosari. Uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya *CAG* umebaini kuwa sehemu ya mkataba inafafanua kuwa gharama za dola za Marekani 29,606,100 zinahusu ununuzi wa magari na usafiri wakati gharama za bima zingelipwa na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kipengele cha 3 cha makubaliano ya mkopo kinabainisha kuwa gharama za dola za Marekani 29,606,100 zinahusu ununuzi wa magari, usafiri na bima. Kwa msingi huo, gharama halisi za mkataba huo bado zina utata.

(c) Pamoja na dosari hizo, *CAG* amebaini kuwa Jeshi la Polisi lilipokea magari 181 kutoka Kampuni ya Ashok mwezi Oktoba, 2015 kwa masharti ya mkataba uliomalizika muda wake tangu mwezi Oktoba, 2014.

(d) Katika mahojiano kati ya Afisa Masuuli na Kamati alikiri kwamba fedha kiasi cha dola za Marekani 10,000,000 zililipwa kwa *Ashok Leyland Limited* kama malipo ya awali kabla ya mkataba kusainiwa.

(e) Kamati haikuridhishwa na bei za baadhi ya magari kuwa juu pamoja na kwamba kuna baadhi ya magari yameshatumika *(used cars).*

(f) Kamati haikupata mkataba ili kujiridhisha kuhusu muda uliokubaliwa kwa magari hayo kupokelewa na aina ya magari yaliyoagizwa, kwa kuwa orodha ilionesha aina mbalimbali za magari.

(g) Jumla ya magari yaliyoagizwa yalikuwa 777, yaliyopokelewa ni magari 181; idadi hii inafanya magari ambayo bado hayajapokelewa kuwa 596. Fedha iliyolipwa ni sawa na asilimia 40 na magari yaliyokuja ni sawa na asilimia 20 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyofafanuliwa hapo awali, mazingira na mchakato mzima wa ununuzi wa magari husika ulikuwa na utata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na dosari hizo, mnamo mwezi Novemba, 2017 kulibainika uwepo wa baadhi ya magari hayo katika Bandari ya Dar es Salaam bila kuwepo maelezo ya kutosha kutoka Jeshi la Polisi, jambo linalothibitisha hoja ya *CAG* na ya Kamati kuwa mchakato wa manunuzi ulifanywa bila kuzingatia sheria na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa baadhi ya magari yaliyoletwa kwa mujibu wa Mkataba husika ni mabovu na yanaonekana yamekwishatumika hivyo kuendelea kuthibitisha mapungufu katika mchakato wa manunuzi husika. Kamati ina maoni kuwa fedha za Umma hazikutumika ipasavyo katika manunuzi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba saba, madeni yasiyokusanywa katika Shirika la Uzalishaji Mali, Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2016, Shirika la uzalishaji mali la Jeshi la kujenga Taifa (SUMA –

JKT) lilikuwa linadai madeni mbalimbali yanayofikia shilingi 60,952,565,232.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu kubwa ya deni ambalo SUMA JKT inadai, lipo katika Mradi wa Matrekta ambalo ni takriban kiasi cha shilingi 49,223,329,000 na hivyo kuwa asilimia 80.7 ya deni lote ambalo shirika linadai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa mradi mzima wa matrekta uliotekelezwa na SUMA JKT haukandaliwa, kusimamiwa wala kutekelezwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nane ni kutokuwepo na Ufanisi kwa Benki ya Kilimo Tanzania. Benki ya Kilimo Tanzania ilianzishwa chini ya Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002 na kupewa cheti cha usajili chenye namba 94075 mnamo tarehe 26 Septemba, 2011. Lengo la kuanzishwa kwa benki hii lilikuwa ni kutoa huduma za kifedha za muda mfupi, wa kati na mrefu kwa shughuli za Kilimo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umethibitisha kuwa Benki hii haijatimiza malengo ya kuanzishwa kwake na badala yake imetumia sehemu ya gharama na kuwa *cost centre.* Sababu za Kamati kuwa na maoni hayo ni kwa kuzingatia kwamba:-

(a) Kiasi kidogo cha mtaji kilichotolewa mara moja tu tangu benki hiyo ilipoanzishwa kwa shilingi bilioni 60 ikilinganishwa na ahadi ya shilingi bilioni 800 zilizotakiwa kutolewa, hivyo kukwamisha ufanisi wa benki; na

(b) Matumizi ya kawaida ya benki yapo juu ikilinganishwa na kazi iliyofanyika hadi sasa. Kwa mfano, kiasi cha mikopo kilichotolewa kwa wakulima hadi tarehe 30 Juni, 2016 ni shilingi 2,234,266,673 tu ikilinganishwa na matumizi ya shilingi 2,719,092,314 tangu Benki hiyo ianzishwe;

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia uchambuzi huo wa Kamati, ni bayana kuwa Benki ya Kilimo Tanzania

haijatimiza kwa ufanisi malengo yake. Serikali inapaswa kutoa fedha iliyoahidi kwa *TADB* ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi kwa kuwa kiasi kilichotolewa ni kidogo ikilinganishwa na mahitaji yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo ya maendeleo ya utalii ya shilingi 6,357,529,854 kutowasilishwa Wizara ya Maliasili na Utalii kutoka Hazina. Kifungu cha 5(4) ya Kanuni za Maendeleo ya Utalii za mwaka 2012 kinaanzisha tozo ya maendeleo ya utalii ambayo Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* inatakiwa kukusanya kutoka kwenye tozo ya kitanda *(the bed night levy)* na kisha kuirejesha kwa Mkurugenzi wa Utalii. Malengo ya tozo hiyo ni kusaidia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya Hesabu za Fungu 69 Wizara ya Maliasili na Utalii ya mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2016 umebaini kuwa Wizara Fedha haijaresha fedha zilizokusanywa na *TRA* kwa niaba ya Wizara ya Maliasili na Utalii za jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 6.35 kwa ajili ya tozo ya maendeleo ya utalii. Jambo hili ni kinyume na Sheria ya Bajeti na linapunguza nidhamu ya matumizi ya fedha za umma. Jambo hili ni kinyume na Sheria ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza Wizara ya Fedha na *TRA* wazingatie sheria na kanuni zinazohusu marejesho ya fedha wanazokusanya kwa niaba ya taasisi mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu kutotekelezwa kwa mapendekezo ya *CAG* kuhusu umiliki wa Benki ya Azania. Benki ya Azania ambayo hapo awali ilijulikana kama *1st Adili Bancorp Limited* ni benki iliyoanzishwa mnamo mwaka 1995. Wanahisa wake ni Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (36%); Mfuko wa *PPF* (30%); Mfuko wa *PSPF* (12%); Mfuko wa *LAPF* (14%); Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki (2.3%); wafanyakazi wa Benki ya Azania na wanahisa wengine (1.4%).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko ya Pensheni kwa pamoja inamiliki asilimia 92 ya benki hiyo. Hata hivyo, pamoja na umiliki huo, Serikali kupitia kwa *CAG* haijawahi kukagua hesabu za Benki hiyo kinyume kabisa na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria, Azania Benki inatakiwa kuwa chini ya Msajili wa Hazina *(TR),* hivyo kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na kifungu cha 9(a)(iii) na (iv) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya mwaka 2008 kinaitaka Benki ya Azania kuwasilisha Hesabu kwa *CAG* kwa ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, fedha za umma zilizowekezwa katika Benki ya Azania zinakosa usimamizi wa moja kwa moja wa umma kupitia kwa *CAG* na pia kupitia kwa Bunge. Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni mali ya Serikali na kwa kuwa mifuko hiyo ndiyo inamiliki Benki ya Azania kwa asilimia 92, ni dhahiri benki hiyo ni mali ya Serikali na hivyo ni sharti taratibu za kuwajibika za Serikali zikazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya umiliki wa Taasisi ya Ukuzaji Maendeleo Vijijini *(Pride Tanzania Limited)* ilitolewa na *CAG* kwa mwaka wa fedha 2012/2013 lakini utekelezaji wake haujakamilika, hivyo Kamati kuendelea kufuatilia hoja husika, kwani inahusisha maslahi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Pride Tanzania Limited* ilianzishwa mnamo tarehe 05 Mei, 1993 chini ya Sheria ya Makampuni *(CAP 212)* kwa madhumuni ya kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo. Kwa rejea ya taarifa za Msajili wa Hazina hadi mwaka 2008 ilibainisha kuwa taasisi hiyo ilikuwa inamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100. Taasisi hii ilianzishwa kwa mtaji wa dola za Marekani milioni 4.7 ikiwa ni msaada toka Serikali ya Norway.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ilipofika mwaka 2012, taasisi hii iliondolewa katika orodha ya Msajili wa Hazina katika mazingira yenye utata mkubwa. Kuondolewa kwa

taasisi hii katika orodha ya Msajili wa Hazina, kunaweza kupelekea kubadilishwa kwa umiliki wa Taasisi na kuiweka katika mikono ya watu binafsi na hivyo kuinyima Serikali fursa ya kiusimamizi katika taasisi hii ambayo historia ya uanzishwaji wake inathibitisha kuwa ilianzishwa kwa fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi mabaya ya shilingi 523,929,646.06 katika Shirikisho la Serikali za Mitaa *(ALAT).* Uchambuzi wa Kamati ulibaini matumizi yasiofaa ya shilingi 523,929,646.06 ya fedha za Umma katika Shirikisho la Serikali za Mitaa *(ALAT).* Fedha hizo zilikuwa zimepangwa kutumika kwa ajili ya kujenga Kitega Uchumi cha Shirikisho Mkoani Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lengo la kufanikisha ujenzi huo, wanachama wa *ALAT* walitakiwa kuchangia kiasi cha shilingi milioni 600.5 kwa kipindi cha miaka mitatu. Taarifa ya *CAG* ilibaini kuwa hadi tarehe 29 Januari, 2016 wanachama walikuwa wamechangia jumla ya shilingi milioni 525.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kati ya tarehe 16 Juni, 2012 hadi tarehe 22 Machi, 2013 Menejimenti ya *ALAT* bila idhini ya Mkutano Mkuu, ilibadilisha matumizi ya fedha hizo ambapo walitumia shilingi milioni 76 kwa matumizi ya kawaida ya kila siku ya ofisi, shilingi milioni 80 ziliwekwa kama akiba ya muda maalum katika benki ya *ABC* na shilingi 367.8 hazikuwa na nyaraka zimetumikaje. Hadi kufikia tarehe 11 Machi, 2016, akaunti ya Shirikisho ilibakiwa na shilingi milioni 1.78 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni matumizi mabaya ya fedha za umma na ukiukwaji mkubwa wa sheria za fedha. Aidha, kubadili matumizi ya fedha kwa malengo yasiyokusudiwa na bila idhini ya mamlaka husika ni ukiukwaji wa Sheria ya Bajeti. Hivyo ni muhimu hatua stahiki zikachukuliwa kwa wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu ya tatu ni maoni na mapendekezo. Kamati ina maoni kuwa, kumeendelea kuwepo na maeneo yenye matumizi mabaya

ya fedha za Umma katika Wizara na Mashirika ya Umma hasa katika maeneo ya usimamizi wa mikataba na ununuzi. Maeneo haya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uhitimishe.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *okay.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongelea upungufu wa mkataba wa *Mlimani City* na tumeomba kufanywe *Forensic Performance Audit* ili ijulikane hatma ya *Mlimani City. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Dege, Kigamboni, tumesema taarifa iliyopelekwa kwa Mheshimiwa Spika, ifanyiwe kazi haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu urejeshaji wa Mifuko ya Jamii, tumesema kwamba Serikali iingie mikataba. Kwanza, kwa vile madeni hayo hayamo kwenye orodha ya Deni la Taifa, Serikali iwasilishe Bungeni taarifa rasmi kuhusu mpango wa ulipaji wa madeni hayo na Serikali iingie mkataba rasmi na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili ijulikane kwamba mifuko hiyo inadai nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ununuzi wa magari yenye thamani ya dola milioni 29, Kamati inapendekeza kwamba ifanyike *Forensic and Performance Audit* ili ijulikane mkataba huu ulivyoingiwa na hapo ilipofikia, ili kutakapoonekana kuna ukiukwaji wa taratibu za fedha za Serikali, basi hatua stahiki zichukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TPA* tumesisitiza kwamba wafunge huo mfumo haraka sana.

Kuhusu madeni ya JKT tumependekeza kwamba, Serikali ichukue hatua stahiki kurekebisha dosari za utoaji wa mikopo, kutokana na kwamba mengine hawajulikani ni nani walikopa matrekta hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, urejeshaji wa fedha zilizokusanywa na *TRA* kwa niaba ya taasisi mbalimbali; Kamati imesema kwamba Serikali na *TRA* kurejesha kwenye taasisi husika kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanisi mdogo wa Benki ya Kilimo *(TADB);* dosari hizo zimesababisha malengo kutofikiwa. Kwa hiyo, basi Bunge liazimie kwamba, Serikali itimize ahadi zake za kutoa hizo shilingi bilioni 100 kila mwaka ili benki hiyo iweze kufanya kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana na *ALAT,* Bunge liazimie kwamba, Serikali ichukue hatua za kisheria na kinidhamu kwa watumishi wote wa *ALAT* waliohusika na matumizi haya ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taasisi ya Benki ya Azania na Taasisi ya *Pride;* tumeomba Serikali ifanye uchambuzi yakinifu ili ijulikane hizo pesa zimekwenda wapi na nani walikuwa wanahusika na ubadhirifu wa pesa hizo za *Pride.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunashukuru sana uongozi wote kuanzia Spika na uongozi wote wa Bunge na Wenyeviti wote pamoja na Kamati yangu yote kwa vile imefanya kazi nzuri. Simsahau Makamu Mwenyekiti wangu na Wanakamati wote. Majina yao yote tunaomba yaingie pia kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda pia kuwashukuru Makatibu wote wa Bunge na Wakurugenzi. Mwisho Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa tuliopata kutoka Taasisi ya Ukaguzi ya *CAG* chini ya Profesa Mussa Asad, Mhasibu Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Msajili Hazina. *(Makofi)*

Pia tunashukuru Kurugenzi ya Usimamizi wa Mali za Serikali kwa kuendelea kuisaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. KHALFANI H. AESHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

## TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC) KWA MWAKA 2017 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

*(Inatolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016)*

### SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 MAELEZO YA JUMLA

**1.1 Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), kuhusu Shughuli zilizotekelezwa kwa mwaka 2017 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili inavyostahili.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2017, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ilipokea na kujadili Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2016, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa maelezo yanayotolewa katika Taarifa hii yanatokana na Hesabu zilizokaguliwa kama zilivyowasilishwa katika Taarifa hiyo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

## 1.2 Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali zilizingatia majukumu yake yaliyoainishwa katika kifungu cha 14 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Majukumu hayo ni:-

a) Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za Umma katika Wizara za Serikali yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

b) Kufuatilia utekelezaji wa Mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati hiyo yenye lengo la kuondoa matatizo hayo; na

c) Kutoa Mapendekezo na Ushauri kwa Wizara za Serikali kuhusu matumizi mazuri ya fedha za Umma ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa majukumu hayo unatokana na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyobainishwa katika kifungu cha 16 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Utaratibu wa kutekeleza majukumu ya Kamati kwa kipindi chote ulizingatia masharti ya Kanuni ya 117 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016. Miongoni mwa Masharti hayo ni kuzingatia Bajeti ya Kamati iliyoidhinishwa kwa mwaka na kukutana pale ilipoitishwa na Spika, Naibu Spika au Mwenyekiti wa Kamati baada ya kupata idhini ya Spika.

## 1.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli za Kamati kwa mwaka 2017, zililenga kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za Umma katika Wizara za Serikali

kama yalivyobainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa fedha unaoshia tarehe 30 Juni, 2016. Aidha, Shughuli hizo zilikusudia kufuatilia utekelezaji wa Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali wakati wa kupitia na kujadili Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa kwa Mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2015.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2016 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alifanya Ukaguzi wa jumla ya Taasisi 122 za Serikali Kuu ikijumuisha Wizara na Idara zinazojitegemea 62, Wakala 37, Mifuko maalum 18, Sekretarieti za Mikoa 26, Taasisi nyingine 42, Vyama vya Siasa 19, Bodi za Mabonde ya Maji 13 na Balozi 34.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mashirika ya Umma, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alikaguwa na kutoa Taarifa ya jumla ya Mashirika ya Umma 150 kati ya 200 yaliyotakiwa kukaguliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Katika ngazi ya Kamati, Kamati ilifanikiwa kuchambua na kujadili Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za jumla ya Mafungu ya Serikali Kuu 34 na yale ya Mashirika ya Umma 38. Aidha, Kamati ilipata fursa ya kutembelea baadhi Miradi ya Maendeleo ikiwamo ya barabara, umeme, ukarabati wa shule na vyuo na uwekezaji katika Miradi ya ujenzi wa nyumba.

**Mheshimiwa Spika,** Awali naomba kulijulisha Bunge hili kwa muhtasari Matokeo ya Shughuli za Kamati wa Mwaka 2016 kama ifuatavyo: -

### 1.3.1 Maeneo yenye Matatizo ya Matumizi yasiofaa ya Fedha za Umma

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kubaini maeneo yenye matatizo ya

matumizi mabaya ya fedha za Umma. Kutokana na Shughuli hiyo Kamati ilibaini baadhi ya maeneo hayo kuwa ni pamoja na haya yafuatayo: -

a) Utekelezaji wa Miradi uliofanywa na baadhi ya Mashirika ya Umma bila kuwa na tija hivyo kuisababishia Serikali hasara;

b) Dosari katika usimamizi wa Miradi inayotekelezwa na Wizara mbalimbali hivyo kupoteza fedha za Serikali;

c) Kutokuwepo kwa nyaraka za Malipo kwa baadhi ya Taasisi za Wizara, Idara, Wakala na Mashirika ya Umma;

d) Kutozingatiwa ipaswavyo kwa Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake;

e) Dosari katika usimamizi wa Mikataba;

f) Ufanisi mdogo wa Benki za Umma;

g) Kutozingatiwa kwa Sheria ya Bajeti, Sheria ya Fedha za Umma na Kanuni mbalimbali; na

h) Kutorejeshwa kwa wakati kwa Mikopo iliyotolewa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa Serikali.


### 1.3.2 Utekelezaji wa Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Hesabu za Serikali kipindi kilichopita

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali iliyowasilishwa Bungeni mwezi Januari, 2016 jumla ya Mapendekezo 14 ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali yaliridhiwa na kuwa Maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa kipindi kilichopita, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa za Maafisa Masuuli mbalimbali sambamba na uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi

Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2015.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya Shughuli hiyo kwa ujumla yalionesha kuwa Maazimio 8 kati ya Maazimio 14 ambayo ni sawa asilimia 64.2 yalikuwa yametekelezwa au yalikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, Maeneo 6 ambayo ni sawa na asilimia 35.8 yalikuwa hayajatekelezwa hadi sasa. Hali ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge imefafanuliwa katika chati ifuatayo: -




**Chati Namba 1: Hali ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge**

**Mheshimiwa Spika,** Kama ilivyofafanuliwa katika chati Namba 1 hapo juu, na kwa lengo la kulipa Bunge lako mwendelezo wa majadiliano *(Coherent discussion)* naomba kuyataja Maeneo ambayo hadi sasa hayajatekelezwa kikamilifu kwa muhtasari kama ifuatavyo: -

a) Kutokulipwa kwa wakati madeni ambayo Serikali inadaiwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;

b) Kutoanzishwa kwa mfuko wa uwekezaji wa Umma *(Public investment fund)*;

c) Hali ya kifedha ya Mfuko wa PSPF kutoimarika ipasavyo;

d) Usimamizi duni wa Mikataba katika Wizara na Mashirika ya Umma;

e) Kutokamilika kwa uzingatiaji wa Mfumo kihasibu wa "*IPSAS Accrual basis* "kwa Taasisi za Serikali Kuu; na

f) Baadhi ya Taasisi za Umma kuendelea kutozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI

### 2.1 Maelezo ya Jumla kuhusu Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Ili kubainisha maeneo yenye matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za Umma na kwa kuzingatia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Kaguzi mahususi za Mafungu ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma, Vigezo vya msingi vilitumika kuainisha maeneo hayo ikiwa ni pamoja na: -

a) Thamani ya pesa iliyotumika katika matumizi yaliyoripotiwa na kukaguliwa *(Value for money criteria);*

b) Madhumuni ya Bajeti na matumizi yaliyofanyika *(Misappropriation criteria)* na iwapo Vigezo vya msingi katika matumizi ya fedha za Umma vilizingatiwa *(Criteria)*;

c) Kiasi cha matumizi ikilinganishwa na mahitaji halisi *(Extravagance);*

d) Matokeo ya Taarifa za Kaguzi Maalum *(Special audit)* zilizofanyika hivi karibuni;

e) Umakini katika matumizi yaliyoripotiwa na kukaguliwa;

f) Kujirudia mara kwa mara kwa hoja husika ya ukaguzi *(frequency of reoccurrence)*;

g) Uzingatiaji wa Mamlaka halali za kuidhinisha matumizi ya fedha *(Abuse of established control)*;

h) Uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na taratibu za matumizi ya fedha za Umma *(Compliance criteria)*; na

i) Kuwepo kwa Kumbukumbu na nyaraka zinazopaswa kutunzwa kwa ushahidi wa matumizi kama zilivyohitajiwa na CAG na mambo mengine ya ujumla ikiwa ni pamoja na hali ya matumizi ya fedha za Umma iliyoripotiwa (*Condition*), sababu za hali ya matatizo yaliyopo (*Possible cause*) na athari inayoweza kupatikana kwa matatizo hayo (*Impact*).

## 2.2 Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia Vigezo na mambo ya msingi niliyoyataja hapo awali, Uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mafungu mahususi ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma ulibainisha mambo yafuatayo:-

### 2.2.1 Dosari katika Mkataba wa Mlimani City (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam)

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na Mkataba wa makubaliano ya Ujenzi wa Mradi wa Mlimani City ambao ulianza tarehe 01 Oktoba, 2004 na ukitakiwa kukamilika tarehe 01 Septemba, 2006 kwa makubaliano ya mkodishwaji na mkodishaji kwa maana ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Kampuni ya Mlimani Holding Limited (MHL), Mradi huu haujakamilika mpaka sasa.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya CAG pamoja na mahojiano na uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, umebaini dosari kubwa katika usimamizi na uendeshaji wa Mradi huo hali ambayo inaipatia Serikali hasara. Dosari hizo ni kama zifuatavyo: -

a) Sheria ya uwekezaji ya mwaka 1997 inaelekeza ili kibali cha uwekezaji kitolewe lazima muwekezaji alete ushahidi wa kuwa na mtaji wa kutosha hivyo Dola za Marekeani 75 zilizooneshwa kama mtaji kwenye hesabu za MHL ni kinyume cha sheria hiyo ya TIC inayohusu uwekezaji;

*b) Turnstar Holding Ltd* ni miongoni mwa Mwanahisa wa MHL anaemiliki hisa moja. *Turnstar Holding Ltd* ametoa mikopo kwa MHL jumla ya Dola za Marekani 49,027,840. Kamati ilipata mashaka kuhusu nia ya mbia huyu kwa kuwa MHL ana hisa 900 ambazo hazijauzwa hivyo angeweza kununua badala ya kukopesha. Kamati inaona mbia huyu lengo lake ni kujinufaisha zaidi kwa kutoa mikopo kwa vile riba anayolipwa inatolewa kwenye mapato ghafi kabla ya kugawana faida;

c) Kwa zaidi ya miaka 13 tangu Mkataba uingiwe, Mradi wa ujenzi wa hoteli ya nyota 3 yenye vyumba 100 bado haujaanza kinyume na makubaliano hivyo kuongeza gharama za kumalizika Mradi na Botanical Garden na pia haijatengenezwa;

d) Kumekuwepo ukiukwaji mkubwa wa malipo ya pango la ardhi (rent) ya Chuo Kikuu ambapo kifungu 1.1(j) na kifungu 10.1 cha Mkataba kinaeleza kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kitapata asilimia 10 ya pango ya mapato ghafi. Hata hivyo, Kampuni ya Mlimani Holding Limited (MHL) imekuwa ikifanya malipo ya pango kwa Chuo kwa asilimia 10 ya mapato baada ya kutoa gharama za uendeshaji hivyo kuikosesha Serikali mapato stahiki kinyume na Mkataba;

e) Kukiukwa kifungu cha 11.2(l) cha hati ya makubaliano ya mpangaji kinachomtaka MHL kutopangisha mtu yeyote ambaye hajathibitishwa na Mapangishaji (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam). Hata hivyo, ukaguzi umethibitisha kuwa MHL amekuwa akipangisha wapangaji wengine bila kupata kibali cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hivyo kupelekea Chuo kukosa taarifa sahihi za mapato ya kodi kutoka kwa wapangaji wake;

f) Kamati hairidhishwi na mazungumzo yanayoendelea kati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mwekezaji wa Mlimani City (MHL). Mwekezaji huyo amekuwa akiyakataa mapendekezo yote ambayo yangekuwa na maslahi kwa pande zote mbili badala yake amekuwa akishikiria mapendekezo yenye maslahi kwake tu. Wakati huo ameweza kuongeza eneo la maduka na maegesho ya magari ambavyo havikuwemo katika Mkataba. Kama hiyo haitoshi, Mwekezaji ameshindwa kuanza utekelezaji wa Ujenzi wa Hotel na bustani ya wanyama na mimea (Botanic Garden) ambavyo vipo kwa mujibu wa Mkataba.

g) Mapitio ya Mkataba yamebainisha kuwa Mkataba huo hauelezi hali halisi ya ugawanaji mali pindi Mkataba utakapoisha (Miaka 50 au 85). Hakuna makubaliano rasmi yanayoeleza mgawanyo wa mali na miundo mbinu itakayokuwepo pindi Mkataba utakapoisha. Athari ya jambo hili ni kuwa kuna uwezekano wa kutokea mvutano wa kisheria pindi Mkataba huu utakapofika ukomo;

h) Dosari nyingine ni kuhusu ushiriki wa Serikali kupitia kituo cha Uwekezaji (TIC) ambapo TIC na Mlimani City Holdings (MHL) wamekuwa wakibadilisha muda wa Utekelezaji wa Mradi mara kwa mara kwa kumuongezea muwekezaji muda wa kukamilisha Mradi bila ya kuhusisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa mfano, Mkataba wa kwanza ulisainiwa tarehe 27 Februari, 2006 na kumuongezea Mwekezaji kipindi cha Utekelezaji wa Mradi hadi tarehe 30 Oktoba, 2009. Mkataba wa pili ulisainiwa tarehe 13 Julai, 2007 kwa kuongeza muda wa Utekelezaji hadi tarehe 30 Novemba, 2013 na Mkataba wa tatu ulisainiwa tarehe 10 Decemba, 2014 ambao uliongeza muda wa utekelezaji wa Mradi huo hadi 31Decemba, 2019; na

i) Mkataba unaonesha kuwa ilitakiwa kujengwa nyumba 50 za kuishi (housing estate/Villas). Kamati ilipotembelea Mradi huu zilionekana nyumba 45 tu na nyumba moja yenye vyumba viwili vilivyotenganishwa na milango miwili.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na dosari zilizofafanuliwa katika aya (a) hadi (i) hapo juu, ni dhahiri, Mradi wa Mlimani City una dosari kubwa hivyo kuinyima Serikali mapato stahiki. Hivyo Mradi huu unatakiwa uangaliwe kwa kina kuanzia Mkataba wa Kwanza hadi hapo ulipofikia sasa.

### 2.2.2 Kusimama muda mrefu kwa Mradi wa Dege, Kigamboni unaotekelezwa na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF)

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Dege Eco Village, Kigamboni ni wa ubia kati ya Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Kampuni ya Azimio Housing Limited (AHEL) ambapo katika Mradi huo, AHEL ana hisa asilimia 55 na NSSF asilimia 45 kwa makubaliano ya uchangiaji wa ardhi na fedha taslim.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia Ukaguzi uliofanywa na CAG na baada ya Uchambuzi wa Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za NSSF kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2016, Kamati imebaini kuwa Mradi huo ulisimamishwa na Serikali tangu mwezi Januari, 2016[1].

**Mheshimiwa Spika,** Hadi Mradi huo unasimama jumla ya Shilingi bilioni 219 mali ya Wanachama wa NSSF zilikuwa zimetumika katika Mradi huo. Mnamo tarehe 09 Novemba, 2016 Kamati ya PAC iliunda Kamati ndogo kwajili ya kushughulikia kwa kina hoja ya Mradi wa Dege. Kamati hiyo ilitekeleza kazi zake na kuwasilisha taarifa ya uchambuzi na mapendekezo kwa Mheshimiwa Spika tarehe 13 Februari, 2017.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, mnamo tarehe 20 Januari, 2018 Kamati ilitembelea Mradi huu wa Dege na kujionea hali halisi ya ghorofa 156 zenye nyumba 3,700 (Units) ambazo hakuna hata moja iliyokwisha kamilika na kuuzwa. Kamati ilipata wasiwasi juu ya usalama wa fedha za wanachama kiasi cha shilingi Bilioni 219 ambazo zimekwisha wekezwa.

---

[1]Rejea Ukurasa wa 24 wa “Key Audit Matters” kwa Taarifa ya Hesabu za NSSF kwa Mwaka wa fedha 2015/2016

**Mheshimiwa Spika,** Suala la Mradi huu limechukua muda mrefu kukamilika. Kamati inasisitiza Serikali kufanya kila liwezekanalo kuepusha upotevu wa fedha za Umma zilizokwisha wekezwa hapo kwa kuzingatia ukweli kuwa Mradi huu kuendelea kusimamama unapungua thamani *(Depreciation[2]),* ongezeko la gharama za ujenzi na uharibifu wa miundo mbinu unaoendelea.

### 2.2.3 Madeni ambayo Serikali inadaiwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kiasi cha Shilingi trilioni 1.6

**Mheshimiwa Spika,** Kama ambavyo Kamati ili ripoti mwaka jana katika taarifa yake ya mwaka hapa Bungeni, Serikali imeendelea kulimbikiza deni inalodaiwa na Mifuko mbalimbali ya Hifadhi ya Jamii. Hadi kufikia Juni 30, 2016 deni la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambalo muda wake wakulipwa ulikuwa umepita lilifikia Shilingi trilioni 1.6.

**Mheshimiwa Spika,** Madeni haya yanatokana na Mikopo ya moja kwa moja iliyochukuliwa na Serikali, dhamana ambazo Serikali ilitoa na michango ambayo haikuwasilishwa kulingana na matakwa ya kisheria. Aidha, CAG amebainisha kuwa madeni hayo yamevuka muda wake wa kulipwa kwa mujibu wa makubaliano. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama unavyoonekana katika jedwali lifuatalo: -

**Jedwali Namba 2.1: Madeni ambayo Serikali inadaiwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | LAPF | 243.43 |
| 2. | WCF | 26.6 |
| 3. | PPF | 139.55 |
| 4. | NHIF | 43.8 |
| 5. | PSPF | 623.93 |
| 6. | NSSF | 519.05 |
| | **JUMLA** | **1,596.36** |

***Chanzo: Taarifa ya CAG kuhusu Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha 2015/2016***

[2]International Audit Standard (IAS 16)

**Mheshimiwa Spika,** Kutokulipwa kwa madeni hayo yaliyochambuliwa katika Jedwali hapo juu kunaathiri uwezo wa kifedha na kiutendaji wa taasisi husika. Hoja ya Kamati katika eneo hili ni kuishauri Serikali kutimiza ahadi yake iliyoitoa kwa Kamati na kwa Bunge kwa kuanza kulipa madeni hayo kupitia hati fungani *(None cash bond)* na njia nyinginezo ili kuokoa baadhi ya Mifuko ambayo kwa kiasi fulani imeanza kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na ukamilifu.

### 2.2.4 Udhaifu katika ukusanyaji wa madeni, usimamizi na utoaji wa Zabuni katika Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

#### a) Ukusanyaji wa Madeni

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hairidhishwi na kasi ndogo ya Serikali na Taasisi zake katika ulipaji wa madeni yake kwa Tanesco ambapo imepelekea deni hilo kuongezeka toka shilingi bilioni 129.298 30 Juni, 2016 hadi kufikia shilingi 189,806,872,396.96 30 Juni, 2017. Hali hii inatokana na baadhi ya Wizara na Taasisi kutokulipa ama kupunguza madeni yao kwa wakati na kikamilifu. Baadhi ya Wizara na Taasisi zinazobeba deni kubwa ni Hospitali ya Muhimbili, Wizara ya Maji naUmwagiliaji, DAWASCO, Magereza na nyinginezo ambazo kwa pamoja zinachangia karibu ya deni kwa kiasi cha shilingi 105,288,757,564.70.

**Mheshimiwa Spika,** inasikitisha zaidi kwani kati ya Taasisi za Serikali zinazodaiwa na Tanesco ni Wizara ya Nishati kwa kutolipa kodi ya pango ya Jengo la Tanesco ambapo Wizara imekodisha kiasi cha shilingi bilioni 1.6. Kamati inashauri Serikali kulipa madeni yake kwa wakati.

#### b) Usimamizi na Utoaji wa Zabuni

**Mheshimiwa Spika**, katika taarifa ya CAG zipo dosari katika manunuzi ya Umma kama vile:

i. Mikataba mingi kusainiwa baada ya kazi kutolewa kinyume na taratibu;

ii. Mchakato wa Zabuni kuchukua muda mrefu kuliko uliowekwa na Sheria;

iii. Zabuni kwenye kanda kutolewa katika kiwango cha juu kuliko kilichowekwa kisheria;

iv. Kutoa Mafungu manne (4 lots) kwa muombaji mmoja kinyume na kanuni za manunuzi haziruhusu mzabuni kupewa zaidi ya mafungu 2 *(lots);* na

v. Kukosekana kwa mpango madhubuti wa manunuzi hivyo kusababisha uwepo wa manunuzi ya dhalura.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza Tanesco kuzingatia Sheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma.

### 2.2.5 Dosari za Kimfumo katika Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)

**Mheshimiwa Spika,** Katika Taarifa yake ya mwaka hapa Bungeni, mwezi Januari, 2016, Kamati ilibainisha dosari za kimfumo katika Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) ambazo zinasababisha upotevu mkubwa wa mapato ya Serikali. Kamati ilitegemea kuwa suala hilo lingekuwa limeshughulikiwa kwa ukamilifu katika mwaka wa fedha 2016/ 2017.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo dosari hizo za kimfumo zimeendelea katika TPA. Dosari za mfumo wa COBOL unaotumiwa na TPA umeendelea kuwa na changamoto za kuwasiliana na mifumo tanzu kama vile Harbor View Plus (HVP), Cargo Management System (CMS) na Tanzania Customs Intergrated System (TANSIS).

**Mheshimiwa Spika,** Dosari hizo zimeendelea kuipotezea Serikali mapato kutokana na baadhi ya meli taarifa zake kutorekodiwa ipasavyo. Aidha, TPA wamekuwa wakishindwa kuhakiki taarifa za moja kwa moja za meli na mizigo inayohudumiwa na kitengo cha kuhudumia makontena cha

TICTS hivyo kutokuwa na uhakika wa taarifa za fedha wanazolipwa na TICTS.

**Mheshimiwa Spika,** Maelezo ya TPA kwa Kamati ni kuwa wanafunga mfumo mpya wa ERP (SAP) na Ununuzi wa mfumo wa Port Operations Sytem (POS) ambayo itawezesha kuunganisha mtiririko wa utoaji ankara, ukusanyaji mapato na kuviunganisha moja kwa moja kwenye kumbukumbu za Hesabu *(General ledger)*.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na TPA kutoa ahadi ya kuwa mifumo hiyo itakamilika na kuanza kufanya kazi kati ya Novemba 2017 na Januari, 2018, bado Kamati ina mashaka makubwa na uhakika wa mifumo hiyo na udhibiti wa mapato ya Serikali katika TPA, ikizingatiwa kuwa mifumo hiyo inanunuliwa kwa gharama kubwa ya fedha za Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Itakumbukwa kuwa, mapema mwezi Novemba, 2017 Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa nyakati tofauti walibaini mapungufu makubwa ya mfumo wa uondoshaji mizigo katika Bandari yetu. Hii inadhihirisha kuwa endapo hatua madhubuti hazitachukuliwa kwa haraka, basi upotevu wa mapato ya Serikali utaendelea na ufanisi wa Bandari utashuka.

### 2.2.6 Ununuzi wa Magari ya Polisi yenye Thamani ya Dola za Marekani 29,606,100 bila ya Kuwepo Mkataba

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya CAG inabainisha kuwa mnamo tarehe 05 Septemba, 2013 Jeshi la Polisi liliingia makubaliano na Kampuni ya Ashok Leyland ya nchini India kwa ajili ya ununuzi wa magari 777 yenye thamani ya Dola za Marekani 29,606,100. Magari hayo yalipangwa kununuliwa kwa mkopo *(Credit facility)* kutoka Benki ya uagizaji na uingizaji bidhaa ya Exim ya India *(Export – Import Bank of India)*.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya CAG imebainisha dosari katika mchakato wa ununuzi wa magari hayo kama ifuatavyo: -

(a) Mkataba kati ya Jeshi la Polisi na Kampuni ya Ashok Leyland uliingiwa tarehe 05 Septemba, 2017 wakati Mkataba wa mkopo wa manunuzi ya magari husika kati ya Serikali na Benki ya Exim ya India ulisainiwa tarehe 19 Juni, 2015. Kwa msingi huo na kwa kuzingatia masharti ya kipengele 9.1 cha Mkataba wa mkopo kati ya Serikali na Benki ya Exim ya India, makubaliano hayo yalikuwa batili kwa sababu Mkataba kati ya Jeshi la Polisi na Kampuni ya Ashok Leyland ulikwisha muda wake tangu mwezi Oktoba, 2014. Makubaliano ya Mkopo kati ya Serikali ya Tanzania na Exim benki India hayakwenda sambamba na Mkataba wa ununuzi wa magari. Hivyo ununuzi wa magari hayo una utata mkubwa;

(b) Gharama halisi za ununuzi wa magari hayo pia una dosari. Uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya CAG umebaini kuwa sehemu ya Mkataba inafafanua kuwa gharama za Dola za Marekani 29,606,100 zinahusu ununuzi wa magari na usafiri wakati gharama za bima zingelipwa na Jeshi la Polisi. Hata hivyo, kipengele cha 3 cha makubaliano ya mkopo kinabainisha kuwa gharama za Dola za Marekani 29,606,100 zinahusu ununuzi wa magari, usafiri na bima. Kwa msingi huo gharama halisi za Mkataba huo bado zina utata;

(c) Pamoja na dosari hizo, CAG amebaini kuwa Jeshi la Polisi lilipokea magari 181 kutoka Kampuni ya Ashok mwezi Oktoba, 2015 kwa masharti ya Mkataba uliomalizika muda wake tangu mwezi Oktoba 2014;

(d) Katika mahojiano kati ya Afisa Masuuli na Kamati alikiri kwamba fedha kiasi cha Dola za Marekani 10,000,000 zililipwa kwa Ashok Leyland Limited kama malipo ya awali (advance payment) kabla ya Mkataba kusainiwa;

(e) Kamati haikuridhishwa na bei za baadhi ya magari kuwa juu pamoja na kwamba kuna baadhi ya magari yamekwisha tumika (used cars);

(f) Kamati haikupata Mkataba ili kujiridhisha kuhusu muda uliokubaliwa kwa magari hayo kupokelewa na aina

ya magari yaliyoagizwa, kwa kuwa orodha ilionesha aina mbalimbali za magari;

(g) Jumla ya magari yaliyoagizwa yalikuwa 777 yaliyopokelewa ni magari 181 idadi hii inafanya magari ambayo bado hayajapokelewa kuwa 596. Fedha iliyolipwa ni sawa na asilimia 40 na magari yaliyokuja ni sawa na asilimia 20 tu.

**Mheshimiwa Spika,** Kama ilivyofafanuliwa hapo awali, mazingira na mchakato mzima wa ununuzi wa magari husika ulikuwa na utata. Kamati imebaini kuwa Mkataba wa mwisho wa manunuzi ya magari hayo umesainiwa [3]tarehe 15 Februari, 2017 hivyo kuibua hoja ni kwa nini magari yalipokelewa bila ya kuwepo Mkataba.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na dosari hizo, mnamo mwezi Novemba, 2017 kulibainika uwepo wa baadhi ya magari hayo katika Bandari ya Dar es Salaam bila ya kuwepo maelezo ya kutosha kutoka Jeshi la Polisi, jambo linalothibitisha hoja ya CAG na ya Kamati kuwa mchakato wa manunuzi ulifanywa bila kuzingatia sheria na taratibu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa baadhi ya magari yaliyoletwa kwa mujibu wa Mkataba husika ni mabovu na yanaonekana yamekwishatumika hivyo kuendelea kuthibitisha mapungufu katika mchakato wa manunuzi husika. Kamati ina maoni kuwa fedha za Umma hazikutumika ipasavyo katika manunuzi haya.

### 2.2.7 Madeni yasiokusanywa katika Shirika la uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT)

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2016, Shirika la uzalishaji mali la Jeshi la kujenga Taifa (SUMA – JKT) lilikuwa linadai madeni mbalimbali yanayofikia Shilingi 60,952,565,232.

---

[3]Rejea Ukurasa wa 39 wa Majibu ya Hoja za Ukaguzi ya Afisa Masuuli wa Fungu -28

Madeni hayo yamegawanyika katika makundi makuu matano kama yanavyochambuliwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Namba 2.2: Mchanganuo wa Madeni inayodai SUMA - JKT**

| Na. | Maelezo ya Deni | Kiasi "Shilingi" |
|---|---|---|
| 1. | SUMA MAKAO MAKUU | 1,066,054,000.00 |
| 2. | MRADI WA MATREKTA | 49,223,329,000.00 |
| 3. | IDARA YA KILIMO NA VIWANDA | 1,421,737,000.00 |
| 4. | IDARA YA UJENZI | 5,184,520,000.00 |
| 5. | SUMA JKT GUARD LTD | 4,056,925,232.00 |
| | **JUMLA** | **60,952,565,232.00** |

***Chanzo: Taarifa ya Hesabu Jumuifu za SUMA – JKT kwa mwaka wa fedha 2015/2016***

**Mheshimiwa Spika,** Kama inavyoonekana katika jedwali hapo juu, sehemu kubwa ya deni ambalo SUMA JKT inadai lipo katika Mradi wa Matrekta ambalo ni takribani kiasi cha Shilingi 49,223,329,000 na hivyo kuwa asilimia 80.7 ya deni lote ambalo Shirika linadai.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa Mradi mzima wa Matrekta uliotekelezwa na SUMA JKT haukandaliwa, kusimamiwa na kutekelezwa ipasavyo. Kamati imethibitisha kuwa hapakuwekwa taratibu madhubuti za kuhakikisha watu waliokopeshwa matrekta hayo wanarejesha fedha husika.Ni kwa msingi huo, fedha za Umma zilizowekezwa katika Mradi huo zina viasharia ya kutumika isivyofaa na hivyo kuikosesha Serikali manufaa.

### 2.2.8 Kutokuwepo na Ufanisi kwa Benki ya Kilimo Tanzania (TADB)

**Mheshimiwa Spika,** Benki ya Kilimo Tanzania ilianzishwa chini ya Sheria ya Makampuni ya mwaka[4] 2002 na kupewa cheti cha usajili chenye namba 94075 mnamo tarehe 26 Septemba, 2011.Lengo la kuanzishwa kwa Benki hii lilikuwa kutoa huduma za kifedha za muda mfupi, kati na mrefu kwa shughuli za Kilimo hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umethibitisha kuwa Benki hii haijatimiza malengo ya kuanzishwa kwake na badala yake imekuwa sehemu ya gharama kwa Serikali *(Cost Centre).* Sababu za Kamati kuwa na maoni hayo ni kwa kuzingatia: -

a) Kiasi kidogo cha mtaji kilichotolewa mara moja tu tangu benki hiyo kuanzishwa cha shilingi bilioni 60 ikilinganishwa na ahadi ya shilingi bilioni 800 zilizotakiwa kutolewa, hivyo kukwamisha ufanisi wa Benki;

b) Matumizi ya kawaida ya Benki yapo juu ikilinganishwa na kazi iliyofanyika hadi sasa. Kwa mfano kiasicha mikopo kilichotolewa kwa wakulima hadi tarehe 30 Juni, 2016 ni shilingi 2,234,266,673.00 tu ikilinganishwa na matumizi ya Shilingi 2,719,092,314.00 tangu Benki hiyo ianzishwe;

c) Hivyo basi Kamati inaitaka Serikali itekeleze ahadi yake ya kutoa shilingi Bilioni 100 kila mwaka ili kuweza kukamilisha kiasi kilicho bakia.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia uchambuzi huo wa Kamati, ni bayana kuwa Benki ya Kilimo Tanzania haijatimiza kwa ufanisi malengo yake. Serikali inapaswa kutoa fedha iliyoahidi kwa TADB ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi kwa kuwakiasi kilichotolewa ni kidogo ikilinganishwa na mahitaji yaliyopo.

---

[4] Companies Act no. 2 of 2002

**Mheshimiwa Spika,** Kwa lengo hilo hilo, Serikali inashauriwa kuangalia upya uhalisia wa uwepo wa TADB na wakati huo huo kuna Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB) ambayo imekuwa ikijishughulisha na utoaji wa Mikopo ya kilimo. Benki hizi zote mbili zina malengo yanayofanana ya kuwa vyombo vya Umma vya kugharamia shughuli za maendeleo kama kilimo, *State – owned development finance institutions (DFIs).*

### 2.2.9 Tozo ya Maendeleo ya Utalii ya Shilingi 6,357,529,854 kutowasilishwa Wizara ya Maliasili na Utalii kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 5(4) ya Kanuni za Maendeleo ya utalii za mwaka 2012 kinaanzisha tozo ya Maendeleo ya utalii ambayo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inatakiwa kukusanya kutoka kwenye tozo ya kitanda *(The bed night levy)* na kisha kuirejesha kwa Mkurugenzi wa utalii. Malengo ya tozo hiyo ni kusaidia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za utalii.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya Hesabu za fungu 69 Wizara ya Maliasili na utalii kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2016 umebaini kuwa Wizara fedha (Hazina) hijaresha fedha zilizokusanywa na TRA kwa niaba ya Wizara ya Maliasili na utalii za jumla ya kiasi cha Shilingi 6,357,529,454 kwa ajili ya tozo ya maendeleo ya utalii.

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto ya kutotekeleza Sheria na Kanuni zinazohusiana na urejeshaji wa mapato yanayokusanywa na TRA kwa niaba ya Taasisi mbalimbali za Serikali imebainika katika maeneo mengi. Mwenendo huo wa kutorejesha mapato yanayokasimiwa kukusanywa na TRA unaathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa mipango inayotakiwa kutekelezwa na Taasisi husika.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo hili ni kinyume na Sheria ya Bajeti na linapunguza nidhamu ya matumizi ya fedha za Umma. Kamati inasisitiza Wizara ya fedha na TRA wazingatie Sheria na Kanuni zinazohusu marejesho ya fedha wanazokusanya kwa niaba ya Taasisi mbalimbali za Serikali.

### 2.2.10 Kutotekelezwa kwa Mapendekezo ya CAG kuhusu Umiliki wa Benki ya Azania

**Mheshimiwa Spika,** Benki ya Azania ambayo hapo awali ilijulikana kama *1st Adili Bancorp Limited* ni Benki iliyoanzishwa mnamo mwaka 1995. Wanahisa wake ni Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii, NSSF (36%), Mfuko wa PPF (30%) Mfuko wa PSPF (12%) Mfuko wa LAPF (14%), Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki (2.3%), Wafanyakazi wa Benki ya Azania na Wanahisa Wengine (1.4%).

**Mheshimiwa Spika,** Mifuko ya Pensheni kwa pamoja inamiliki asilimia 92 ya Benki hiyo. Hata hivyo, pamoja na umiliki huo Serikali kupitia kwa CAG haijawahi kukagua Hesabu za Benki hiyo kinyume kabisa na Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Sheria, Azania Benki inatakiwa kuwa chini ya Msajili wa Hazina (TR), hivyo kwa mujibu wa ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na kifungu cha 9(a) iii na iv cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 kinaitaka Benki ya Azania kuwasilisha Hesabu kwa CAG kwa ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa muktadha huo, fedha za Umma zilizowekezwa katika Benki ya Azania zinakosa usimamizi wa moja kwa moja wa Umma kupitia kwa CAG na pia kupitia kwa Bunge. Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni mali ya Serikali na kwa kuwa Mifuko hiyo ndiyo inamiliki Benki ya Azania kwa asilimia 92, ni dhahiri Benki hiyo ni mali ya Serikali hivyo ni sharti taratibu za kuwajibikaji za Serikali zikazingatiwa.

### 2.2.11 Umiliki wa Taasisi ya Ukuzaji Maendeleo Vijijini *(Pride Tanzania Limited)*

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya umiliki wa Taasisi ya Ukuzaji Maendeleo Vijijini *(Pride Tanzania Limited)* ilitolewa na CAG kwa mwaka wa fedha 2012/ 2013 lakini utekelezaji wake haujakamilika hivyo Kamati kuendelea kufuatilia hoja husika kwani inahusisha maslahi ya fedha za Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Pride Tanzania Limited ilianzishwa mnamo tarehe 05 Mei, 1993 chini ya Sheria ya Makampuni (CAP 212) kwa dhamana kwa madhumuni ya kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo. Kwa rejea ya taarifa za Msajili wa Hazina za hadi mwaka 2008, ilibainishwa kuwa Taasisi hiyo ilikuwa inamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100. Taasisi hii ilianzishwa kwa Mtaji wa Dola za Marekani 4,701,800 ikiwa ni msaada toka Serikali ya Norway.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo ilipofika mwaka 2012, Taasisi hii iliondolewa katika orodha ya Msajili wa Hazina katika mazingira yenye utata mkubwa. CAG anafafanua kuwa uhalali wa kuondolewa kwa Taasisi hiyo katika orodha ya Msajili wa Hazina haukuwekwa wazi. Pamoja na hilo, Taasisi hii ambayo ilianzishwa kwa fedha zilizochukuliwa chini ya dhamana ya Serikali haijawahi kuwasilisha Taarifa ya Hesabu zake kwa CAG kwa ajili ya [5]ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kuondolewa kwa Taasisi hii katika orodha ya Msajili wa Hazina kunaweza kupelekeakubadilishwa kwa umiliki wa Taasisi na kuiweka katika mikono ya watu binafsi na hivyo kuinyima Serikali fursa ya kiusimamizi katika Taasisi ambayo historia ya uanzishwaji wake inathibitisha kuwa ilianzishwa kwa fedha za Umma.

### 2.2.12 Matumizi Mabaya ya Shilingi 523,929,646.06 katika Shirikisho la Serikali za Mitaa (ALAT)

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati ulibaini matumizi yasiofaa ya shilingi 523,929,646.06 ya fedha za Umma katika Shirikisho la Serikali za Mitaa (ALAT). Fedha hizo zilikuwa zimepangwa kutumika kwa ajili ya kujenga kitega Uchumi cha Shirikisho Mkoani Dodoma.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa lengo la kufanikisha ujenzi huo, Wanachama wa ALAT walitakiwa kuchangia kiasi cha shilingi 6,500,000,000 kwa kipindi cha miaka 3. Taarifa ya CAG ilibaini kuwa hadi tarehe 29 Januari, 2016 Wanachama walikuwa wamechangia jumla ya shilingi 525,717,522.

---

[5] Masharti ya kifungu cha 31 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kati ya tarehe 16 Juni, 2012 hadi tarehe 22 Machi, 2013 Menejimenti ya ALAT bila idhini ya Mkutano Mkuu ilibadilisha matumizi ya fedha hizo ambapo walitumia shilingi 76,000,400 kwa matumizi ya kawaida ya kila siku ya ofisi, shilingi 80,000,000 ziliwekwa kama akiba ya muda maalum katika Benki ya ABC na shilingi 367,929,276.06 hazikuwa na nyaraka zimetumikaje. Hadi kufikia tarehe 11 Machi, 2016, akaunti ya Shirikisho ilibakiwa na shilingi 1,787,845.94 tu.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo hili ni matumizi mabaya ya fedha za Umma na ukiukwaji mkubwa wa sheria za fedha. Aidha, kubadili matumizi ya fedha kwa malengo yasiokusudiwa na bila idhini ya Mamlaka husika ni ukiukwaji wa sheria ya bajeti hivyo ni muhimu hatua stahiki zikachukuliwa kwa wahusika.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maelezo ya jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa Hesabu kwa mwaka wa fedha uanoishia tarehe 30 Juni, 2016, Kamati ina Maoni na Mapendekezo kama ifuatavyo: -

### 3.2 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, Maoni ya Kamati yanazingatia azma ya Bunge kuwa na Kamati mahsusi inayohusika na usimamizi wa matumizi ya fedha za Umma. Msingi wa Maoni hayo ni nia ya kuepusha matumizi mabaya ya fedha za Umma katika Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kama kanuni za Bunge zinavyofafanua. Kwa mantiki hiyo, Kamati ina Maoni yafuatayo:-

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa kumeendelea kuwepo na maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za

Umma katika Wizara na Mashirika ya Umma hasa katika maeneo ya usimamizi wa mikataba na manunuzi. Maeneo haya mawili yanahitaji usimamizi wa karibu wa Serikali na Bunge. Pamoja na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali, ni muhimu ushauri na mapendekezo ya Kamati, CAG na PPRA yakazingatiwa na Serikali ili kuondoa mianya ya upotevu wa fedha za Umma katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusu utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati yenye lengo la Kuondoa matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za Umma, Kamati ina maoni kuwa eneo hili bado lina changamoto ya utekelezaji na ufuatiliaji. Kamati inaitaka Serikali kutekeleza kwa uhalisia mapendekezo na maazimio ya Bunge. Aidha, Kamati ina maoni kuwa ni muhimu kukaanzishwa utaratibu rasmi wa kikanuni wa kufuatilia utekelezwaji wa mapendekezo ya Kamati za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ujenzi wa Tanzania ya viwanda utaenda sambamba na kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za Umma katika Wizara, Idara, Wakala, Balozi na Mashirika ya Umma. Ni sharti muhimu Taasisi za kiuwajibikaji kama Bunge, NAOT, TAKUKURU, DCI, DPP na Mahakama zikaendelea kujengewa uwezo na kupewa rasilimali za kutosha kutekeleza majukumu ya kiusimamizi ili kuhakikisha fedha za Umma zinalindwa ipasavyo.

## 3.3 Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Kamati yamejengwa kwa kuzingatia ukubwa wa athari ya hoja inayohusika, matokeo yenye kuambatana na hoja husika, uwezekano wa hoja kujirudia na hatua zinazotakiwa kuchukuliwa kushughulikia hoja husika [6]*(Risk levels)*.

---

[6] Grouping of different risks according to their estimated cost of likely impact, likelihood of occurrence and countermeasures required

**Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Kamati ni yale yanayolenga hoja zenye athari ya juu *(High risk issues)* na hivyo kuhitaji utekelezaji wa haraka ili Kuondoa matumizi yasiofaa ya fedha za Umma katika Taasisi za Serikali.

### 3.3.1 Mapungufu ya Mkataba wa Mradi wa "Mlimani City"

**KWA KUWA,** Kamati imebaini dosari kubwa katika mkataba na uendeshaji wa Mradi wa Mlimani City;

**NA KWA KUWA,** Mapungufu hayo yanainyima Serikali mapato stahiki na hivyo kuwa eneo mojawapo lenye matumizi mabaya ya fedha za Umma;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaishauri Serikali kwamba: -

CAG aombwe kufanya ukaguzi wa kiuchunguzi na kiufanisi (Forensic and Performance Audit) katika mchakato mzima wa Mikataba yote inayohusu Mradi wa Mlimani City na kuwasilisha taarifa ya ukaguzi huo Bungeni.

### 3.3.2 Kutokamilika kwa Mradi wa Dege, Kigamboni

**KWA KUWA,** Mradi wa ujenzi wa Dege Eco Village unaotekelezwa na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) umekwama kukamilika kwa wakati na unakabiliwa na changamoto kubwa;

**NA KWA KUWA,** Kutokamilika kwa Mradi huo kunaweza kusababisha upotevu mkubwa wa fedha za Umma;

**KWA HIYO BASI,** Kamati inaendelea kusisitiza kwamba Serikali itekeleze mapendekezo ya Kamati yanayohusu Mradi wa Dege mapema iwezekanavyo ili kuokoa fedha za Umma zilizowekezwa katika Mradi huo.

### 3.3.3 Urejeshaji wa Mikopo ambayo Serikali inadaiwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

**KWA KUWA,** Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inaidai Serikali fedha kiasi kikubwa na deni limeendelea kuongezeka;

**NA KWA KUWA,** Madeni hayo yanapunguza uwezo wa Mifuko husika kutekeleza majukumu yake ya kisheria kwa ufanisi unaotakiwa;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaishauri Serikali kwamba:-

a) Kwa kuzingatia kwamba madeni hayo hayamo kwenye orodha ya deni la Taifa, Serikali iwasilishe Bungeni Taarifa rasmi kuhusu mpango wa ulipaji wa Madeni hayo ikizingatiwa kuwa madeni hayo hayaoneshwi kwenye deni la Taifa; na

b) Serikali iingie mikataba rasmi na Mifuko ya Hifadhi Jamii kuhusu Mikopo iliyochukuliwa kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sahihi za madeni husika.

### 3.3.4 Ununuzi wa Magari yenye Thamani ya Dola za Marekani 29,606,100 uliofanywa na Jeshi la Polisi bila ya Uwepo wa Mkataba

**KWA KUWA,** Taarifa ya CAG imebainisha dosari kubwa katika mchakato wa manunuzi wa magari 777 uliofanywa na Jeshi la Polisi ikiwa ni pamoja na manunuzi kufanyika bila ya uwepo wa Mkataba na mkanganyiko katika gharama halisi za manunuzi hayo;

**NA KWA KUWA,** Manunuzi hayo yana viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za Umma na ukiukwaji wa Sheria za Manunuzi na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaishauri Serikali kwamba: -

a) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aombwe kufanya ukaguzi maalum utakaohusisha ukaguzi wa kiuchunguzi na kiufanisi *(Forensic and performance audit)* katika mchakato mzima wa manunuzi ya magari husika ili

kubaini iwapo Sheria husika zilizingatiwa na iwapo manunuzi hayo yalikuwa na tija kwa Serikali; na

b) Endapo itadhihirika kwamba kulikuwa na ukiukwaji wa taratibu za manunuzi hatua za kisheria na kinidhamu zichukuliwe kwa watu wote waliohusika katika mchakato wa manunuzi wa Magari hayo.

### 3.3.5 Mapungufu katika Mfumo wa usimamizi wa mapato ya Bandari (TPA)

**KWA KUWA,** Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) imeendelea kutumia mfumo wa kizamani wa COBOL ambao hauna uwezo wa kuunganisha mifumo mingine ya shughuli za Bandari;

**NA KWA KUWA,** Matumizi ya mifumo hiyo imekuwa ikisababisha upotevu mkubwa wa mapato ya Serikali na kupunguza ufanisi wa Bandari yetu;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaishauri Serikali kwamba;

TPA ihakikishe inakamilisha mfumo wa *Enterprises Resource Planning* (ERP) na kutimiza ahadi yake kuwa mfumo huo ungefanya kazi kwa awamu kuanzia Novemba, 2017 na kukamilika Januari, 2018 ili dosari za usimamizi wa mapato zilizobainika zisijirudie tena.

### 3.3.6 Madeni ambayo SUMA JKT inadai kwa watu na Taasisi mbalimbali

**KWA KUWA,** Kumekuwa na malimbikizo makubwa ya deni lisilokusanywa na SUMA JKT kutoka kwa watu na Taasisi mbalimbali hususan deni linalotokana na Mradi wa Matrekta;

**NA KWA KUWA;** Kutokukusanywa kwa deni hilo kumeenda kinyume na Mikataba na hivyo kuisababishia Serikali hasara kubwa;

**KWA HIYO BASI;** Bunge linaishauri Serikali kwamba:-

a) Serikali ifanye uchunguzi wa kina ili kubaini taratibu zilizotumika katika utoaji wa Mikopo ya matrekta kwa watu na Taasisi mbalimbali;

b) Serikali ichukue hatua stahiki kwa mujibu wa mikataba ya ukopeshaji matrekta kurejesha fedha za Serikali ambazo hazijakusanywa; na

c) Serikali ichukue hatua stahiki za kurekebisha dosari za utoaji wa Mikopo ya matrekta na kuchukua hatua kwa watu watakaothibitika walikiuka taratibu katika utoaji wa Mikopo husika.

### 3.3.7 Urejeshaji wa fedha zinazokusanywa na TRA kwa niaba ya Taasisi mbalimbali za Serikali

**KWA KUWA,** Imebanikia kuwa kumekuwepo na ucheleweshaji wa kurejesha fedha zinazokusanywa na TRA kwa niaba ya Taasisi mbalimbali za Serikali kwa mujibu wa Sheria na Kanuni;

**NA KWA KUWA,** Kutorejeshwa kwa fedha hizo kunaathiri mipango na utekelezaji wa Taasisi husika na ni kinyume na masharti ya Sheria ya Bajeti;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali kupitia Wizara ya fedha itekeleze kwa ukamilimu masharti ya Sheria na Kanuni zinazohusu makusanyo kufanywa na TRA na kisha kurejesha kwenye Taasisi husika kwa muda mwafaka.

### 3.3.8 Ufanisi mdogo wa Benki ya Kilimo (TADB)

**KWA KUWA,** Uchambuzi wa Kamati umebainisha kuwa Benki ya Kilimo Tanzania (TADB) imekuwa ikiendeshwa kwa ufanisi usioridhisha kunakotokana na dosari za kiutendaji na uwezo mdogo wa mtaji;

**NA KWA KUWA,** Dosari hizo zimesababisha malengo ya kuanzishwa kwa Benki hiyo kutofikiwa na hivyo manufaa tarajiwa kutoonekana bayana;

**KWA HIYO BASI;** Bunge linaishauri Serikali yafuatayo: -

a) Serikali ifanye mapitio ya utendaji wa Benki ya Kilimo Tanzania ili kubaini iwapo kwa mazingira ya sasa itaweza kujiendesha kwa kuwa na tawi moja tu Dar es Salaam;

b) Serikali iwe na mpango mkakati madhubuti wa kuwa na Taasisi imara za fedha za Umma *(State owned financial institutions)* za kugharamia shughuli za uwekezaji katika Kilimo, Viwanda na uwezeshaji wa makundi maalum; na

c) Serikali itimize ahadi yake ya kutoa shilingi bilioni 100 kila mwaka, kwa miaka 8 ili benki hii iweze kujiendesha kwa ufanisi.

### 3.3.9 Matumizi mabaya ya Fedha za Umma katika Jumuia ya Serikali za Mitaa (ALAT)

**KWA KUWA,** Kamati kupitia uchambuzi wa Taarifa ya CAG, imebainisha matumizi ya shilingi 523,929,646.06 bila kuidhinishwa na Bodi ya ALAT na kutumika kinyume na malengo kusudiwa;

**NA KWA KUWA,** Matumizi hayo yamevunja Sheria ya Bajeti na Sheria ya usimamizi wa fedha za Umma;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaishauri Serikali kwamba ichukue hatua za kisheria na kinidhamu kwa watumishi wote wa ALAT waliohusika na matumizi hayo ya fedha za Umma.

### 3.3.10 Umiliki wa Benki ya Azania na Taasisi ya Pride

**KWA KUWA,** Taarifa ya CAG imeibua utata mkubwa kuhusu umiliki na uendeshaji wa Benki ya Azania na Taasisi ya kifedha ya Pride;

**NA KWA KUWA,** Utata wa umiliki katika Taasisi hizo umesababisha kutokuwepo kwa mfumo rasmi wa uwajibikaji

na usimamizi wa Serikali na Bunge hivyo kuathiri usimamizi wa fedha za Umma zilizowekwa kwenye Taasisi hizo 2;

**KWA HIYO BASI;** Bunge linaishauri Serikali kwamba ichukue hatua za kurekebisha dosari za umiliki na uendeshaji wa Benki ya Azania. Vilevile Serikali ichukue hatua kwa kuirejesha Taasisi ya Pride Serikalini kutoka kwenye umiliki binafsi na kuwachukulia hatua za kisheria watakaobainika kushiriki katika kujimilikisha Taasisi hiyo.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukurani

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Kamati imeeleza kwa kina mapungufu mbalimbali yaliyojitokeza katika Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016 na kutoa mapendekezo ya namna ya kuondoa mapungufu hayo kwa lengo la kuhimiza uwajibikaji katika matumizi ya fedha za Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako makini ambao umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo kwa kutoa maelekezo na miongozo thabiti pale Kamati ilipohitaji msaada wako. Aidha, namshukuru Naibu Spika Dr. Tulia Ackson pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kukusaidia kuongoza Bunge letu kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha, nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati na kunipa heshima ya kuiwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Aeshi Khalfan Hilary, Mb **- M/Mkiti**
3. Mhe. Felister Aloyce Bura, Mb
4. Mhe. Dkt. Shukuru Kawambwa, Mb
5. Mhe. Shally Joseph Raymond, Mb
6. Mhe. Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mb
7. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb
8. Mhe. Musa Bakari Mbarouk, Mb
9. Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula, Mb
10. Mhe. Jamal Kassim Ali, Mb
11. Mhe. Tunza Issa Malapo, Mb
12. Mhe. Ali Salim Khamisi, Mb
13. Mhe. Omar Mohamed Kigua, Mb
14. Mhe. Khadija Nassir Ali, Mb
15. Mhe. Esther Lukago Midimu, Mb
16. Mhe. Fakharia Shomari Khamis, Mb
17. Mhe. Yosefa Ferdinand Komba, Mb
18. Mhe. Munde A. Tambwe, Mb
19. Mhe. Josephine Ngezabuke, Mb
20. Mhe. Ezekiel Magolyo Maige, Mb
21. Mhe. Allan Joseph Kiula, Mb
22. Mhe. Omary Tebweta Mgumba, Mb
23. Mhe. Rhoda Edward Kunchela, Mb
24. Mhe. Catherine Ruge, Mb
25. Mhe. Abdallah Haji Ali, Mb
26. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushauri wake kwa Kamati pale alipotakiwa kufanya hivyo. Natoa Shukurani kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu shughuli za Kamati, kupitia kwa Mkurugenzi Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto, Sekretarieti ya Kamati ikijumuisha Ndugu Erick Maseke, Wilfred Magova, Mwajuma Ramadhani, Asmini Kihemba na Msaidizi wa Huduma za Kamati Bi. Modesta Kipiko.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi chini ya CAG Profesa Mussa Assad, Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali (AcGen) chini ya Ndugu Francis Mwakapalila na Ofisi ya Msajili wa Hazina (TR) chini ya Dr. Oswald Mashindano. Aidha naishukuru Kurugenzi ya Usimamizi wa mali za Serikali (DGAM) kwa kuendelea kuisadia Kamati katika utekelezaji wa shughuli zake kwa weledi na ufanisi.

### 4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika,** Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Naomba kutoa Hoja.

Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC)**

1 Februari, 2018

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kaboyoka, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa taarifa yako. Sasa tunamkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Karibu sana. *(Makofi)*

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* Kuhusu Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma katika Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha Unaoishia tarehe 30 Juni, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu

ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu usimamizi wa matumizi ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoisha tarehe 30 Juni, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika Kipindi cha mwaka 2017, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* ilipokea na kujadili Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kuhusu Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2016, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa maelezo yaliyotolewa katika taarifa hii yanatokana na hesabu zilizokaguliwa kama zilivyowasilishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kipindi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majukumu ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

(i) Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za Serikali za Mitaa yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

(ii) Kufuatilia utekelezaji wa Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hii, ili kuondoa matatizo hayo; na

(iii) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Serikali za Mitaa kuhusu matumizi mazuri ya fedha ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutekeleza majukumu hayo, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117(8) yanayohusu ruhusa kwa Kamati kujiwekea utaratibu wa kutekeleza majukumu yake. Njia kuu tatu zilitumika kukamilisha kazi hizo:-

(i) Kufanya rejea ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* na taarifa za awali za Kamati;

(ii) Mahojiano na Menejimenti za Halmashauri kwa lengo la kupata maelezo yao kuhusu hoja zilizoibuliwa katika Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG);* na

(iii) Kufanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwenye Halmashauri kuhusu matumizi ya fedha za umma kwa nia ya kujiridhisha na muonekano wa thamani halisi *(value for money)* ikilinganishwa na kiasi cha matumizi kilichoripotiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2015/2016 yalilenga kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa kama yalivyobainishwa katika Taarifa ya Ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu muhtasari wa uchambuzi wa matokeo hayo. Maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi yasiyofaa ya fedha za umma. Matatizo ya Matumizi ya Fedha za Serikali za Mitaa ni mkusanyiko na mwenendo usioridhisha na unaojirudiarudia katika matumizi ya fedha na ambao hauzingatii sheria, kanuni na taratibu za matumizi ya fedha za umma na mwenendo huo hauna tija kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi ya fedha za Serikali za Mitaa yaliyobainishwa katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ni kama ifuatavyo:-

(i) Ununuzi wa huduma, vifaa na kuingia mikataba pasipo kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 *(Public Procurement Act)*;

(ii) Usimamizi wa matumizi ya fedha za umma usiozingatia sheria, kanuni na taratibu;

(iii) Usimamizi usio na tija wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo unaosababisha kuwepo kwa miradi ya maendeleo isiyo kamilika kwa muda mrefu, miradi iliyokamilika lakini haitumiki kama ilivyokusudiwa kinyume na masharti ya mkataba na baadhi ya miradi kukamilika ikiwa katika ubora wa hali ya chini; *(Makofi)*

(iv) Uzembe katika kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri, upotevu wa rasilimali usio na maelezo ya kuridhisha wa vitabu vya wazi vya kukusanyia mapato;

(v) Kutokutekeleza maagizo ya Kamati kwa kipindi cha nyuma na kutokujibu hoja za ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa wakati;

(vi) Kutochangia kikamilifu na kwa wakati fedha asilimia 10 kutoka katika mapato ya vyanzo vya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana na kutotenga na kuwasilisha kikamilifu asilimia 20 ya ruzuku inayopokelewa kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya mamlaka ya chini ya Vijiji na Serikali za Mitaa; na

(vii) Wakuu wa Idara na Vitengo kukaimu nafasi zao kwa muda mrefu bila kuthibitishwa jambo ambalo linakwamisha ufanisi wa utekelezaji majukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya Kamati inaonesha kuwa pamoja na jitihada zilizofanywa na Serikali na majibu yaliyowasilishwa na Serikali, bado Kamati haijaridhishwa kwani kuna maeneo bado hayajafanyiwa kazi na mengine utekelezaji wake haujakamilika. Baadhi ya maeneo ambayo utekelezaji wake siyo wa kuridhisha ni:-

(a) Fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kuchelewa kutolewa na pengine kutotolewa kabisa na Hazina; *(Makofi)*

(b) Kutotenga na kupeleka asilimia 20 ya ruzuku ya fidia kutoka Serikali Kuu *(General Purpose Grant - GPG)* kwa

ajili ya mamlaka za chini kufuatia Serikali Kuu kufuta kodi zenye kero kwa wananchi; *(Makofi)*

(c) Kuchangia asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana;

(d) Kuendelea kufunga Hesabu za mwisho wa mwaka *(final accounts)* katika Halmashauri nje ya Mfumo wa Hesabu *(Epicor 9.05 system)*; na

(e) Utekelezaji usioridhisha wa miradi ya maendeleo hususan miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha utendaji wa Halmashauri, Kamati inaendelea kutoa wito kwa Halmashauri kutekeleza mapendekezo yake kwa ukamilifu na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla kuhusu matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati; Kamati ilikumbwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kushindwa kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo ili kuhakiki thamani ya miradi, kutathmini hali ya sasa ya miradi na changamoto zake katika kutoa huduma kwa wananchi. Kamati inaona kwa kufanya mahojiano ya mezani pekee, haitoshi kutoa taswira ya uhalisia na uhalali wa matumizi ya fedha za umma.

Sehemu ya pili ni uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji; katika mwaka wa fedha 2015/2016, jumla ya Halmashauri 171 zilikaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kupatiwa Hati ya Ukaguzi *(Audit Opinion)* kulingana na matokeo ya ukaguzi huo. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 4.2 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2014/2015 ambapo jumla ya Halmashauri zilizokaguliwa na kupatiwa hati za ukaguzi zilikuwa 164.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jedwali Namba 2 linaonesha mwenendo wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kipindi cha miaka minne mfululizo (2012/2013 hadi 2015/2016).

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna uwezekano wa Halmashauri hizo kuwa na makosa kadhaa ambayo kwa mujibu wa viwango vya Ukaguzi wa Kimataifa *(ISSAI),* makosa hayo hayazuii mkaguzi kufanya ukaguzi kwa mawanda yanayotakiwa na kuathiri taarifa ya fedha. Aidha, Halmashauri zilizopata hati zisiyoridhisha zilikuwa na dosari mbalimbali za kihesabu zikiwemo:-

(a) Baadhi ya mali za kudumu kutoonyeshwa katika taarifa ya fedha;
(b) Kutenganisha thamani ya ardhi na majengo kwa kufuata viwango vya kihasibu vya kimataifa *(IPSAs 17)*;
(c) Kuondoa thamani ya baadhi ya mali za Halmashauri bila kufuata taratibu za fedha
(d) Makosa katika kiasi cha bakaa kati ya taarifa ya fedha na fedha taslimu;
(e) Kiasi cha fedha cha ruzuku ya matumizi ya kawaida kuripotiwa pungufu;
(f) Baadhi ya malipo kufanyika bila vielelezo; na
(g) Kukosekana kwa vielelezo vya kiasi cha fedha kilichofutwa kwenye vitabu kabla ya kuingia benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka miwili mfululizo baadhi ya Halmashauri zimeendelea kupatiwa Hati yenye Shaka kufuatia upungufu na dosari katika taarifa zao za fedha. Baadhi ya dosari hizo zilikuwa ni kama ifuatavyo:-

(a) Deni halisi la Halmashauri halikuonyeshwa katika kitabu cha *LAAC*;

(b) Uthibitisho wa wadaiwa na wadai wa Halmashauri haukuwasilishwa kwa *CAG* kwa ajili ya uhakiki wa uhalali wake;

(c) Malipo ya fidia ya ardhi yalifanyika lakini Halmashauri zilishindwa kuwasilisha mchanganuo wa uthibitisho wa malipo hayo kwa *CAG* kwa uhakiki;

(d) Malipo ya posho kwa watumishi kufanyika mara mbili *(double payments)*;

(e) Kukosekana kwa vielelezo vya uhalali wa malipo ya asilimia kumi ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana;

(f) Mkanganyiko *(confusion)* katika taarifa ya hesabu za mradi na kusababisha bakaa kutojulikana zilipo; na

(g) Kutotangaza maoni ya taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* katika magazeti yanayosomwa zaidi na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutokana na Taarifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa na maelezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mahojiano baina ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Halmashauri 42 zilizoitwa kuja mbele ya Kamati, Kamati haijaridhika na utendaji wa Halmashauri 14 zifuatazo:-

Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma, Halmashauri ya Wilaya ya Korongwe, Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Halmashauri ya Wilaya ya Hanang, Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, Halmashauri ya Wilaya ya Longido na Halmashauri ya Mji, Geita kwa kupata Hati za Ukaguzi zenye mashaka kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia vigezo na mambo ya msingi yaliyoyatajwa hapo awali, uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ulibainisha mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, usimamizi wa mikataba na manunuzi usiozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma. Kamati imebaini kuwa jumla ya Halmashauri 171 sawa na asilimia 92 zilifanya ununuzi wa thamani ya shilingi bilioni

11.5 nje ya bajeti ya mwaka. Vilevile Halmashauri hizo zilitumia jumla ya shilingi bilioni 1.49 kulipa madeni ya miaka ya nyuma licha ya kuwa madeni hayo hayakuwepo katika taarifa za fedha za miaka hiyo. Ulipaji huo wa madeni ulifanyika nje ya bajeti za Halmashauri hizo kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtindo huu siyo tu unaashiria hatari ya upotevu wa Fedha za Umma, bali pia unaathiri ufanikishaji wa malengo ya bajeti yalikusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Kamati katika tatizo la kutofuata sheria na taratibu za manunuzi ya umma, ni kuwa matumizi hayo ni ufujaji wa fedha za Umma na hayana tija na hivyo, Serikali inaendelea kupoteza fedha nyingi ambazo zingeweza kutumika kutatua matatizo ya wananchi katika maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo namba 8(2)(c) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa la mwaka 2009 linazitaka Halmashauri kudhibiti na kutunza nyaraka zote za malipo. Nyaraka za malipo huthibitisha uhalali wa malipo kwa huduma au kwa bidhaa zilizonunuliwa. Katika mwaka 2015/2016 jumla ya Halmashauri 109 sawa na asilimia 59 zilifanya malipo yenye thamani ya shilingi bilioni 9.8 bila kuwa na nyaraka muhimu kama vile hati ya madai, hati ya kukiri kupokea malipo na taarifa ya shughuli zilizolipwa. Ufafanuzi halisi unaonekana katika Jedwali Namba tatu (3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitaka kujua sababu ya kufanya malipo hayo bila kuwa na nyaraka na kubaini kuwa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani *(Pre-Audit Section)* hakikufanyi kazi yake ipasavyo katika Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo, ni dhahiri matumizi hayo ya fedha za umma yamekiuka misingi na taratibu, jambo ambalo linahatarisha manufaa yaliyokusudiwa kwa Halmashauri na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limebainika pia, tatizo lingine kubwa la Halmashauri kushindwa kusimamia ipasavyo akaunti za amana kutokana na kutokuwepo kwa utunzaji mzuri wa rejista za amana. Akaunti ya Amana isipotumiwa vizuri huweza kutumika katika kugharamia matumizi mbalimbali bila kuonyesha akisi yake kuwa fedha hizo ziliingizwa katika akaunti hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016 matumizi mbalimbali yenye thamani ya shilingi bilioni 13.8 yamefanyika bila kuonesha kama kiasi hicho kilikuwa kimepokelewa katika akaunti za amana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili limesababishwa na udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani (*weak internal control system*). Kadhalika, matumizi hayo mabaya ya akaunti ya amana yanafanyika kwa visingizo vifuatavyo:-

(a) Maagizo kutoka ngazi za juu.

(b) Fedha kuingizwa kwenye akaunti hiyo bila kuwepo mwongozo wa matumizi.

(c) Kufanya matumizi bila idhini ya mamlaka husika na hivyo kuathiri kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri nne (4) zilizoonekana kuwa na kiasi kikubwa cha matumizi yasiyothibitika kutoka katika akaunti ya amana ambazo ni Halmashauri ya Meatu, Halmashauri ya Nkasi, Halmashauri ya Wanging'ombe na Halmashauri ya Handeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hoja ya Kamati ni kuwa Maafisa Masuuli wanazembea katika kusimamia mifumo ya ndani ya udhibiti wa mapato na matumizi, hali ambayo huchangia matumizi mabaya ya fedha za umma na kuathiri hali ya upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi usio na tija wa mikataba na utekelezaji wa miradi ya maendeleo; katika

mahojiano na Halmashauri 42 katika kipindi hiki, Kamati imebaini udhaifu katika usimamizi wa utekelezaji wa mikataba na usimamizi wa miradi ya maendeleo hali inayoathiri moja kwa moja utoaji wa huduma kwa wananchi. Mathalani, katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, miradi mitano yenye thamani ya shilingi bilioni 4.2 haijakamilika kwa muda mrefu kutokana na udhaifu katika usimamizi wa mikataba**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhaifu huo unasababisha baadhi ya Miradi ya Maendeleo katika Halmashauri nchini kuchukua muda mrefu kukamilika, au kukamilika kwa wakati lakini kwa kiwango cha chini tofauti na makubaliano. Aidha, dosari hii imesababisha miradi mingine kutokamilika kabisa, na mingine kutotekelezwa. Vilevile, kuna baadhi ya Miradi imekamilika lakini haitumiki kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** tarehe 25 Mei, 2012 Halmashauri ya Manispaa Ilala iliingia mkataba na Kampuni ya *Remix Centre Limited* kwa ajili ya kupima viwanja vya wananchi katika baadhi ya maeneo ya Kata ya Chanika na Msongola. Tarehe Mosi Desemba, 2014, wakati utekelezaji wa mkataba huo ukiendelea, yalifanyika makubaliano ya mkataba huo ambayo havikuwa na vielelezo vya uhalali wala chanzo chake lakini yalikubaliwa na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni hii ilipewa kipindi cha miaka mitatu kupima jumla ya viwanja 30,000 lakini hadi kufikia tarehe 6 Januari, 2016 kampuni hii ilikuwa imepima viwanja 870 tu sawa na asilimia tatu ya viwanja vyote. Pamoja na kusuasua kwa utekelezaji wa mradi huu halmashauri haikuweza kujitoa katika mradi huu. Kadhalika halmashauri haikuweza kutoa hati za viwanja vilivyopimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *Remix Centre Limited* ililipwa kiasi cha shilingi milioni 715.27 kwa ajili ya mauzo ya viwanja 84 lakini pia kampuni hiyo ililipwa kiasi cha shilingi bilioni 3.6 bilioni na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (*TAA)* kama mauzo ya viwanja 800. Ingawa fedha hizo zimetokana na mradi huo chini ya usimamizi wa pamoja

na halmashauri, hakuna fedha yeyote iliyowasilishwa kwa Halmashauri. Kampuni hiyo imeshindwa kuonesha kwa uwazi jumla na uhalali wa gharama zilizotumika katika mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kufanya mahojiano na Halmashauri 42, Kamati ilifanya ziara katika Halmashauri saba zifuatazo: Halmashauri Jiji la Mbeya, Halmashauri ya Jiji la Tanga, Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma, Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe na Halmashauri ya Wilaya ya Kyela. Katika ziara hiyo Kamati iliweza kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kumi na tisa na yafuatayo ni matokeo yaliyobainishwa katika baadhi ya miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Wilaya Rungwe, Kamati ilifanya ukaguzi wa mradi wa maji Masoko. Kama ilibaini kasoro ya mradi kutokamilika kwa wakati kwani utekelezaji wa mradi huo ulianza mwaka 2009 na hadi sasa bado haujakamilika. Halmashauri ya Rungwe iliamua kuvunja Mkataba na Mkandarasi mwaka 2012 kutokana na Mkandarasi kuchelewesha mradi na kushindwa kuwasilisha hati ya dhamana *(performance bond)*. Wakati wa kuvunja Mkataba huo mkandarasi alikuwa ameshalipwa kiasi cha shilingi bilioni 1.263 na Mkandarasi Mshauri *(project consultant)* alilipwa kiasi cha shilingi milioni 675.19 nje ya utaratibu kwa kigezo cha muda *(time based contract).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Halmashauri haikuzingatia maoni na ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali juu ya ongezeko la kiasi cha shilingi milioni 549.78 sawa na asilimia 37 ya gharama ya kazi iliyoongezeka nje ya Mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati ilikagua mradi wa Soko la Mwanjelwa lililopo katika Jiji la Mbeya. Kamati ilibaini upungufu mkubwa katika ujenzi na uendeshaji wa mradi huo. Soko hilo limekamilika lakini vyumba na vizimba vingi havitumiki kama ilivyokusudiwa, baadhi ya

wafanyabiashara ndogondogo walio nje ya soko hawalipi kodi, msimamizi au mkusanya ushuru katika soko hilo *M/S Prolat Consultant* aliyewekwa na Benki ya *CRDB* anakusanya mapato ya soko hilo bila Halmashauri ya Jiji kufahamu kiasi kinachokusanywa kutokana na mkataba uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika Halmashauri ya Jiji ina mzigo mkubwa wa kulipa deni la Benki lililotokana na ujenzi wa soko hilo kiasi cha shilingi bilioni 63 pamoja na riba ifikapo mwaka 2031. Deni ambalo ukokotoaji wake umetiliwa shaka. Halmashauri ya Jiji la Mbeya haina uwezo wa kulipa deni hilo kutokana na upungufu uliopo katika uendeshaji wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ilitoa maelezo kuwa palikuwa na mawasiliano baina ya Kamati ya Watumiaji Maji (*COWSO)* na Manispaa kutaka mwongozo wa ukabidhishaji wa mradi huo kwa mtu binafsi lakini Manispaa haikutoa ushirikiano. Kimsingi mradi huo haukabidhiwa kwa mtu binafsi kuuendesha ni kinyume na taratibu na hivyo kwa namna yoyote Mkataba uliopo baina ya Halmashauri na mwendeshaji huyo ni batili na unapaswa kuvunjwa mara moja. Huu ni mfano wa namna Halmashauri zinavyoshindwa kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa manufaa ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Kamati ni kwamba, kumebainika kutokuwa na maendeleo katika halmashauri nyingi hali ambayo, imechangiwa na uzembe na baadhi ya watumishi, uchache wa wataalam kwenye halmashauri, usanifu hafifu wa miradi, kutokushirikishwa kwa wananchi kikamilifu na utaratibu mbovu wa utoaji zabuni kwa Wakandarasi. Hivyo, wananchi wameendelea kukosa huduma tarajiwa licha ya Serikali kuendelea kutenga fedha nyingi kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhaifu katika kusimamia ukusanyaji wa mapato, kumeendelea kuwepo na udhaifu katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato bila ya hatua stahiki kuchukuliwa mapema hali hii imesabisha kiasi kikubwa

cha fedha kutokusanywa kwa wakati, upotevu wa vitabu vya kukusanyia mapato na kutowasilishwa na Halmashauri kushindwa kukusanya kabisa mapato yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutotekeleza Maagizo ya Kamati na kutojibu Hoja za Ukaguzi; Kifungu cha 15(a) hadi (c) cha Nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kinaitaka Kamati kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati awali. Kumbukumbu zinaonesha kuwa Kamati ilizitaka Halmashauri nchini kuzingatia masharti ya kifungu cha 40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 (*Public Audit Act*) ya mwaka 2008. Kifungu hicho kinawapa Maafisa Masuuli wajibu wa kujibu hoja zinazotolewa katika Taarifa za kila mwaka za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG*). Hata hivyo, Kamati imebaini kuwepo na Maafisa Masuuli katika Halmashauri nchini wanaozembea kujibu Hoja za ukaguzi kinyume na masharti ya sheria**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini udhaifu uliopo katika dhana ya uwajibikaji hasa inapotokea maagizo ya Kamati na hoja za ukaguzi kuvuka mwaka mmoja wa fedha kwenda mwingine au Kamati kuvunjika kufuatia Bunge kumaliza uhai wake na hasa dhana ya maagizo ya Kamati kutotekelezwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kuweka wazi kuwa hakuna sababu za msingi zilizotolewa na Halmashauri yeyote za kushindwa kujibu hoja za ukaguzi na kutekeleza maagizo ya Kamati. Hii inaonesha kuwa utekelezaji wa matakwa haya unafanywa kwa mazoea. Mathalani, Halmashauri ya Wilaya ya Rombo ilishindwa kabisa kujibu hoja za ukaguzi na kutekeleza maagizo ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutotenga mchango wa asilimia 10 ya mapato kutoka vyanzo vya ndani kwa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana na asilimia 20 za ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Halmashauri zote 42 zilizohojiwa na Kamati kwa mwaka huu

zipo zilizotenga kiasi kidogo na nyingine hazikutenga kabisa wala kuwasilisha marejesho ya fedha za Mfuko huu. Aidha, Kamati imebaini kiasi cha shilingi bilioni 4.1 ziko mikononi wa vikundi na hakuna mfumo madhubuti wa kuzirejesha wakati Mfuko huu unaendeshwa kwa kuweka fedha na kukusanya marejesho ili vikundi vingine pia vipate fursa ya kukopa. Kamati imebaini kuwa matumizi ya Mfuko huu huishia kwenye gharama za uendeshaji semina na uchapishaji vipeperushi kwa Watendaji badala ya walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Kamati ni kwamba, uwepo wa Mfuko huo unaongeza kasi ya maendeleo katika ngazi za chini, je, Serikali haioni sasa kuwa umefika wakati muafaka wa kuunda Sheria maalum ya kusimamia Mfuko huu ili kuongeza uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, upelekaji wa fedha za fidia ya vyanzo vya mapato vilivyofutwa, asilimia ishirini 20 ya *GPG* kwenda kwa mamlaka za Serikali za mitaa na vijiji, kushindwa kutimiza majukumu yake kikamilifu kwa kukosa fedha za kujiendesha. Katika halmashauri zote 42 zilizohojiwa hapakuwa na halmashauri hata moja iliyotenga na kupeleka mchango huu kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ilikuwa na kiasi kikubwa zaidi cha ruzuku iliyotakiwa kupeleka katika Serikali na vijiji ambako kiasi cha shilingi milioni 720.04 hazikupelekwa. Aidha, halmashauri nyingine ambazo hazikupeleka ruzuku katika Serikali za mitaa na vijiji kwa miaka miwili mfululizo ni pamoja na Halmashauri ya Karagwe, Halmashauri ya Muleba na Halmashauri ya Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika baadhi halmashauri fedha zilizopelekwa kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ruzuku ya vijiji na mitaa zimeonekana kuchanganywa kimakosa na mapato ya ndani kabla ya kutenga asilimia 20 hali hii haitoi picha kiasi halisi kinachotakiwa na kuwasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wa Idara na Vitengo kukaimu nafasi zao kwa zaidi ya miezi sita bila kuthibitishwa na watumishi kukaa muda mrefu kituoni. Kwa mujibu ya taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali imebainika kuwa Wakuu wa Idara na Vitengo 373 katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa wamekaimu nafasi zao kwa zaidi ya miezi sita bila kuthibitishwa. Pia, Halmashauri mpya na zilizo pembezoni zinaongoza kuwa na Idadi kubwa ya Wakuu wa Idara na Vitengo ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba uitimishe.

**MHE. VEDASTUS E. NGOMBALE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya Tatu maoni na Mapendekezo ya Kamati. Naomba sasa nitoe mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Manunuzi yasiyozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma:-

KWAK UWA imebainika kwamba halmashauri hazifuati Sheria ya Manunuzi ya Umma katika manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali;

NA KWA KUWA manunuzi hayo hayana tija zaidi ya kuzitia hasara Halmashauri na kupunguza kiwango cha huduma kwa wananchi;

KWA HIYO BASI Kamati inaliomba Bunge liazimie kuwa:-

(a) Serikali iweke utaratibu wa kutoa Taarifa za tathimini ya manunuzi za *PPRA (Public Procurement Regulatory Authority)* inayohusu Serikali za Mitaa sambamba na taarifa ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG).* Kwa kufanya hivyo kutalipa Bunge fursa ya kushauri katika utekelezaji wa maeneo ya umma, kwani fedha nyingi za umma zinatumika katika manunuzi ya taasisi hizo;na

(b) Serikali iweke Mpango Mkakati unaotekelezeka, katika kuhakikisha halmashauri zinazingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usimamizi wa matumizi usiozingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Fedha za Umma.

KWA KUWA imebainika kuwepo na upungufu katika kusimamia matumizi na ukiukwaji wa mifumo ya udhibiti wa ndani ikiwa pamoja na kupitisha na kuidhinisha malipo, malipo kukosa viambatisho, malipo kufanyika kwenye vifungu vya matumizi visivyo sahihi na kukosekana kwa hati za malipo hayo;

NA KWA KUWA kuna kulegalega katika kuzingatia sheria, kanuni na miongozo inayosimamia shughuli za Halmashauri;

KWA HIYO BASI Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa:-

(a) Serikali ihimarishe ufuatiliaji na uimarishaji wa mifumo ya kudhibiti wa malipo ikiwa pamoja na uimarishaji wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani; na

(b) Serikali iwachukulie hatua za kinidhamu watendaji wote wanaohusika na upotevu wa nyaraka mbalimbali za malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhaifu katika kusimamia mapato kutoka katika vyanzo vya ndani.

KWA KUWA mapato kutoka vyanzo vya ndani hulenga kupunguza utegemezi wa halmashauri wa ruzuku kutoka Serikali Kuu katika kutekeleza majukumu yake;

NA KWA KUWA Halmashauri nyingi zimeonesha udhaifu na kutoweka jitihada katika kuhakikisha kuwa tathmini ya vyanzo hivyo inafanyika ili kuongeza wigo wa

makusanyo na kuweka mikakati katika usimamizi wa mapato hayo;

KWA HIYO BASI Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa:-

(a) Serikali itoe maelezo ya Mpango Mkakati uliopo katika kuhakikisha kuwa tathmini ya vyanzo inafanyika katika Halmashauri zote, kuondoa udhaifu katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato hayo na kueleza ni hatua gani zitachukuliwa kwa halmashauri itakayoonekana dhahiri kuzembea usimamizi wa makusanyo kutoka vyanzo vya ndani

(b) Ofisi ya Rais, TAMISEMI itoe muda maalum kwa kila halmashauri kuhakikisha inasimika na kuanza kutumia mfumo wa kieletroniki wa ukusanyaji mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi kukaimu nafasi zao kwa zaidi ya miezi sita bila kuthibitishwa:-

KWA KUWA imebainika kuwa idadi kubwa ya Wakuu wa Idara na Vitengo katika Halmashauri wanakaimu nafasi zao kwa kipindi kirefu bila kuthibitishwa;

NA KWA KUWA kuthibitishwa katika nafasi inayokaimiwa ni suala la kisheria na haki ya mtumishi husika na kwamba kunaongeza hali na uwezo wa kutoa maamuzi ya kiutendaji;

KWA HIYO BASI Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa, Serikali ihakikishe inawathibitisha Watumishi wanaokaimu nafasi hizo kwa zaidi ya miezi sita na kuweka mpango wa kuhakikisha tatizo hili linamalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yote ya Kamati iingizwe katika *Hansard*.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ngombale Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu ya Serikali za mitaa kwa taarifa hiyo.

# TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC) KUHUSU USIMAMIZI WA MATUMIZI YA FEDHA ZA UMMA KATIKA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2016 – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

(*Inatolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016*)

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu usimamizi wa matumizi ya Fedha za Umma katika Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoisha tarehe 30 Juni, 2016.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuliwezesha Bunge lako tukufu kutekeleza vema majukumu yake katika eneo la kusimamia matumizi ya fedha za umma, Kamati ilizingatia masharti ya Kifungu cha 15 (a)-(c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kinachoweka msingi wa kazi za Kamati hii. Naomba kutambulisha Sura ya Taarifa ninayowasilisha ambayo imegawanyika katika sehemu nne. Sehemu ya kwanza inahusu maelezo ya jumla na sehemu ya pili inahusu matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya tatu inaonyesha Maoni ya Kamati kuhusu mambo yaliyobainika wakati wa uchambuzi pamoja na mapendekezo yanayotokana na maoni hayo. Na sehemu ya nne inahitimisha Taarifa hii na kutoa hoja kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 123 ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa katika Kipindi cha mwaka 2017, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) ilipokea na kujadili Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2016. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa maelezo yanayotolewa katika Taarifa hii yanatokana na hesabu zilizokaguliwa kama zilivyo wasilishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kipindi hicho.

## 1.2 Majukumu ya Kamati:

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa kazi za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa unatokana na Taarifa ya Ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ambapo Utekelezaji wa majukumu ya Kamati hii unatokana na Kifungu cha 15 (a)-(c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, ambayo kwa Kamati hii ni Hadidu za Rejea. Majukumu hayo ni:-

i. Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za Serikali za Mitaa yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;
ii. Kufuatilia utekelezaji wa Mapendekezo yaliyokwisha tolewa na Kamati ili kuondoa matatizo hayo; na

iii. Kutoa Mapendekezo na ushauri kwa Serikali za Mitaa kuhusu matumizi mazuri ya fedha ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kutekeleza majukumu hayo, Kamati ilizingatia masharti ya kanuni ya 117 (8) yanayohusu ruhusa kwa Kamati kujiwekea utaratibu wa kutekeleza majukumu yake. Njia kuu tatu (3) zilizotumika kukamilisha kazi hiyo nazo ni:-

i. Kufanya rejea ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na Taarifa za awali za Kamati.
ii. Mahojiano na Menejimenti za Halmashauri kwa lengo la kupata maelezo yao kuhusu hoja zilizoibuliwa katika Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).
iii. Kufanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwenye Halmashauri kuhusu matumizi ya fedha za Umma kwa nia ya kujiridhisha na muonekano wa thamani halisi (value for money) ikilinganishwa na kiasi cha matumizi kilichoripotiwa.

**Mheshimiwa Spika,** njia zote hizo zilitumika kwa kuhusisha Kamati na wakati mwingine kwa kujigawa katika Kamati ndogo kama ilivyoruhusiwa Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (18) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Uamuzi wote wa Kamati ulifikiwa kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

## 1.3 Muhtasari wa Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu ya Kamati kwa mwaka 2015/2016 yalilenga kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika serikali za mitaa kama yalivyo bainishwa katika Taarifa ya ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016.

**Muheshimiwa Spika,** Naomba kulijulisha Bunge kwa muhtasari matokeo ya uchambuzi kama ifuatavyo:-

### 1.3.1 Maeneo yenye Matatizo Sugu ya Matumizi yasiyofaa ya Fedha za Umma;

**Mheshimiwa Spika,** Matatizo ya Matumizi ya Fedha za Serikali za Mitaa ni mkusanyiko wa mwenendo usioridhisha na unao jirudiarudia katika matumizi ya fedha na ambao hauzingatii Sheria, Kanuni na Taratibu za Matumizi ya Fedha za Umma na Mwenendo huo hauna tija kwa Umma. Baadhi ya maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi ya fedha za

Serikali za Mitaa yaliyobainishwa katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/16 ni kama ifuatavyo:-

a) Ununuzi wa huduma, Vifaa na kuingia Mkataba pasipo kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011(Public Procurement Act);
b) Usimamizi wa matumizi ya fedha za umma usiozingatia Sheria, kanuni na Taratibu;
c) Usimamizi usio na tija wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo unaosababisha kuwepo kwa Miradi ya Maendeleo isiyo kamilika kwa muda mrefu, miradi inayokamilika lakini haitumiki kama ilivyokusudiwa kinyume na masharti ya mkataba na baadhi ya miradi kukamilika ikiwa katika ubora wa hali ya chini; na
d) Uzembe katika kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri na upotevu wa rasilimali usio na maelezo ya kuridhisha wa Vitabu vya wazi vya kukusanyia mapato;
e) Kutokutekeleza Maagizo ya Kamati kwa kipindi cha nyuma na kutokujibu hoja za ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa wakati;
f) Kutochangia kikamilifu na kwa wakati fedha asilimia kumi (10%) kutoka katika mapato ya vyanzo vya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana na kutotenga na kuwasilisha kikamilifu asilimia ishirini (20%) ya ruzuku inayopokelewa kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya Mamlaka za Chini (Vijiji na Serikali za Mitaa); na
g) Wakuu wa idara na vitengo kukaimu nafasi zao kwa muda mrefu bila kuthibitishwa jambo ambalo linakwamisha ufanisi wa kutekeleza majukumu.

### 1.3.2 Utekelezaji wa Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa katika taarifa yake kwa mwaka wa fedha 2013/14 na 2014/15.

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 9 Novemba 2016 Kamati iliwasilisha taarifa Bungeni iliyohusu usimamizi wa matumizi ya fedha za Umma katika Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2013/14 na 2014/15. Taarifa hiyo ilikuwa na

mapendekezo tisa (9) yaliyopitishwa kama maazimio ya Bunge na hivyo kuhitaji utekelezaji. Kwa sababu hiyo Kamati ilifuatilia ili kujua hatua iliyofikiwa kuhusu utekelezaji wa maazimio hayo. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuhusu hatua iliyofikiwa na Serikali katika kutekeleza Maazimio hayo ya Bunge kama inavyoonesha kwenye Jedwali Na. 1 linatoa Muhutasari wa hatua ya utekelezaji iliyofikiwa

**Jedwari Na. 1:** Muhtasari wa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati katika taarifa yake kwa hesabu za serikali za mitaa kwa mwaka wa fedha 2013/14 na 2014/15 na utekelezaji wa Serikali.

| Na | Muhtasari wa mapendekezo ya Kamati | Muhtasari wa utekelezaji wa Serikali |
|---|---|---|
| 1 | Manunuzi yasiyozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011. | a) Watumishi kuchukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kutengua uteuzi wa wakurugenzi wa Halmashauri za Manispaa Kinondoni, Kigoma, Mpanda, Gairo, Nzega na Halmashauri ya Mji Tunduma.<br>b) Marekebisho ya Sheria ya Manunuzi ya Umma namba 7 ya mwaka 2011 na kanuni zake yaliyoweka sharti la mapitio ya mikataba yenye thamani kuanzia TZS 1 bilioni ipitiwe kwanza na Mwanasheria Mkuu wa Serikari kabla ya kusainiwa.<br>c) Uundwaji wa dawati maalum la wataalam katika Halmashauri kwa ajili ya kuratibu masuala ya kitaalam katika makubaliano ya uwekezaji wa miradi mikubwa. |
| 2 | Usimamizi wa mikataba na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. | a) Serikali imeimarisha sehemu ya ufuatiliaji na tathmini katika Ofisi ya Rais TAMISEMI.<br>b) Uimarishaji wa Sekretarieti za mikoa kwa kutoa fedha kwa ajili ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo. |
| 3 | Kutekeleza maagizo ya Kamati na kujibu Hoja za Ukaguzi. | a) Serikali imeimarisha sehemu ya ufuatiliaji na tathmini katika Ofisi ya Rais TAMISEMI.<br>b) Wakuu wa mikoa wameelekezwa kuhudhuria vikao vya mabaraza ya madiwani yanapokuwa yanajadili taarifa ya CAG ili kuelewa undani wa hoja na mikakati ya kuzijibu.<br>c) Utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati na taarifa ya CAG vitatumika kupima utendaji wa wakurugenzi na Waweka Hazina katika Halmashauri. |
| 4 | Halmashauri kutenga Mchango wa Asilimia Kumi (10%) ya Mapato kutoka vyanzo vya ndani kwa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana. | a) Serikali inaendelea kufanya tathmini ili kupata uwiano ulio sahihi wa matumizi ya fedha za mapato ya ndani.<br>b) Ofisi ya Rais TAMISEMI imetoa agizo kwa Makatibu Tawala kusimamia utekelezaji wa agizo hili. |
| 5 | Kutenga na kupeleka ruzuku ya asilimia ishirini (20%) kwa ajili ya Serikali za Mitaa na Vijiji. | Ofisi ya Rais TAMISEMI imetoa agizo kwa Makatibu Tawala kusimamia utekelezaji wa agizo hili. |

| | | |
|---|---|---|
| 6 | Ukusanyaji wa Mapato kutoka vyanzo vya ndani. | a) Kuanzisha mfumo wa kukusanya mapato wa kielektroniki – LGRCIS.<br>b) Manunuzi ya vifaa vya kukusanyia mapato (point of sales) badala ya kutoa stakabadhi zinazoandikwa kwa mkono.<br>c) Kufanya tathmini ya vyanzo vya mapato vitakavyotakiwa kukusanywa na mawakala. |
| 7 | Uboreshaji wa mfumo wa udhibiti wa ndani (internal control system). | a) Halmashauri zote kuhamia katika mfumo wa kielektroniki katika usimamizi wa mapato na matumizi.<br>b) Kutumia teknolojia ya mkongo wa Taifa wa mawasiliano (optic fiber) ili kuongeza kasi ya Utendaji kazi wa mfumo wa Epicor.<br>c) Maboresho katika mfumo wa Epicor 9.05 bado yanaendelea<br>d) Maboresho ya utendaji kazi wa kitengo cha ukaguzi wa ndani katika Halmashauri. |
| 8 | Wakuu wa Idara na Vitengo kukaimu nafasi zao bila kuthibitishwa kwa muda mrefu na baadhi ya wakuu wa idara kutokuwa na uwezo. | a) Jumla ya nafasi 2,021 za wakuu wa idara zimejazwa.<br>b) Nafasi 802 zinakaimiwa na watumishi ambao wako katika hatua ya upekuzi. |
| 9 | Fedha za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kuchelewa kutolewa au kutotolewa kabisa na Hazina. | Serikali inaendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato na usimamizi. |

***Chanzo:** Uchambuzi wa Kamati kufuatia taarifa ya Ofisi ya Rais TAMISEMI ya mwezi Januari 2017 kuhusu utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati.*

**Mheshimiwa Spika**, Tathmini ya Kamati inaonesha kuwa pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali na majibu yaliyowasilishwa na Serikali, bado Kamati haijaridhishwa kwani kuna maeneo bado hayajafanyiwa kazi na mengine utekelezaji wake haujakamilika. Baadhi ya maeneo ambayo utekelezaji wake sio wa kuridhisha ni:-

a) Fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kuchelewa kutolewa nap engine kuto kutolewa kabisa na Hazina.

b) Kutotenga na kupeleka Asilimia Ishirini (20%) ya ruzuku ya fidia kutoka Serikali Kuu (General Purpose Grant - GPG) kwa ajili ya Mamlaka za Chini kufuatia Serikali Kuu kufuta kodi zente kero kwa Wananchi.

c) Kuchangia 10% ya mapato ya ndani kwa mfuko wa maendeleo wa wanawake na vijana.
d) Kuendelea kufunga Hesabu za mwisho wa mwaka (final accounts) katika Halmashauri nje ya Mfumo wa Hesabu (Epicor 9.05 system).
e) Utekelezaji usioridhisha wa miradi ya maendeleo hususani miradi ya maji.

Ili kuboresha utendaji wa Halmashauri, Kamati inaendelea kutoa wito kwa Halmashauri kutekeleza mapendekezo yake kwa ukamilifu na kwa wakati.

### 1.4 Maoni ya Jumla kuhusu Matokeo ya Utekelezaji wa shughuli za Kamati;

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri zimeendelea kuwa na dosari katika taarifa zake kuhusu Hesabu zilizokaguliwa. Kamati imeendelea kuhimiza uboreshaji wa utendaji kazi ili kuongeza tija. Kwa kuwa ushauri wa Kamati hauzingatiwi na utekelezaji wa maagizo yake haupewi kipaumbele hivyo Halmashauri zimeendelea kuwa na mapungufu na dosari zisizo za lazima.

Kamati ilikumbwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kushindwa kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo ili kuhakiki thamani ya miradi, kutathmini hali ya sasa ya miradi na changamoto zake katika kutoa huduma kwa wananchi. Kamati inaona kuwa Kufanya mahojiano ya mezani pekee haitoshi kutoa taswira ya uhalisia na uhalali wa matumizi ya fedha za umma.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI

### 2.1 Maelezo ya Jumla kuhusu Uchambuzi;

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2015/16 jumla ya Halmashauri 171 zilikaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi

Mkuu wa Hesabu za Serikali na kupatiwa Hati ya Ukaguzi (Audit Opinion) kulingana matokeo ya ukaguzi huo. Hii ni sawa na ongezeko la 4.2% ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2014/15 ambapo jumla ya Halmashauri zilizokaguliwa na kupatiwa hati za ukaguzi zilikuwa 164.

**Jedwari Na. 2**: Mwenendo wa hati za Ukaguzi zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kipindi cha miaka minne mfululizo (2012/13 hadi 2015/16).

| Mwaka | Hati Zinazoridhisha | Hati Zenye Shaka | Hati Zisizoridhisha | Hati Mbaya |
|---|---|---|---|---|
| 2015/2016 | 138 | 32 | 1 | 0 |
| 2014/2015 | 47 | 113 | 3 | 1 |
| 2013/2014 | 150 | 13 | 0 | 0 |
| 2012/2013 | 112 | 27 | 1 | 0 |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Ukaguzi ya CAG kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2015/16*

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla ongezeko hili limetokana na utendaji wa Halmashauri nchini umeendelea kuboreshwa na hivyo kubadili aina ya hati zilizotolewa. Idadi ya Hati zinazoridhisha imeongezeka kutoka 47 katika mwaka 2014/15 hadi kufikia hati 138 katika mwaka wa fedha 2015/16. Kadhalika, hati zenye shaka zimepungua kutoka hati 113 katika mwaka wa fedha 2014/15 hadi kufikia hati 32 katika mwaka wa fedha 2015/16. Hivyo katika mwaka wa fedha 2015/16 ni asilimia 18% ya Halmashauri ndizo zilizopewa hati yenye shaka.

**Mheshimiwa Spika,** Ingawa taarifa ya ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonyesha kuwa Halmashauri nyingi zimeimarika katika kufuata taratibu za fedha na kupatiwa hati inayoridhisha, bado kuna uwezekano wa Halmashauri hizo kuwa na makosa kadhaa ambayo kwa mujibu wa viwango vya Ukaguzi wa Kimataifa (ISSAI) makosa hayo hayazuii mkaguzi kufanya ukaguzi kwa mawanda yanayotakiwa na kutoathiri taarifa ya fedha. Aidha, Halmashauri zilizopata hati isiyoridhisha zilikutwa na dosari mbalimbali za kihesabu zikiwemo:-

a) Baadhi ya mali za kudumu kutoonyeshwa katika taarifa za fedha;
b) Kutotenganisha thamani ya ardhi na majengo kwa kufuata viwango vya kihasibu vya Kimataifa (IPSAs 17);
c) Kuondoa thamani ya baadhi ya mali za Halmashauri bila kufuata taratibu za fedha;
d) Makosa katika kiasi cha bakaa kati ya taarifa ya fedha na fedha taslimu;
e) Kiasi cha fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida kuripotiwa pungufu;
f) Baadhi ya malipo kufanyika bila vielelezo; na
g) Kukosekana kwa vielelezo vya kiasi cha fedha kilichofutwa kwenye vitabu kabla ya kuingia benki.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa miaka miwili mfululizo baadhi ya Halmashauri zimeendelea kupatiwa hati yenye shaka kufuatia upungufu na dosari katika taarifa zao za fedha. Miongoni mwa dosari hizo ni kutojibu hoja za ukaguzi na maandalizi ya kitabu cha LAAC kufanyika bila kufuata utaratibu wa kawaida. Mathalani, Halmashauri hazikuandaa juzuu za viambatisho vya majibu ya hoja za ukaguzi na maagizo ya Kamati jambo lililozuia mawanda ya Kamati kufanya uhakiki. Mfano wa baadhi ya dosari hizo ni kama ifuatavyo;

a) Deni halisi la Halmashauri halikuonyeshwa katika kitabu cha LAAC;

b) Uthibitisho wa wadaiwa na wadai wa Halmashauri haukuwasilishwa kwa CAG kwa ajili ya uhakiki wa uhalali wake;

c) Malipo ya fidia ya ardhi yaliyofanyika lakini Halmashauri zilishindwa kuwasilisha mchanganuo na uthibitisho wa malipo hayo kwa CAG kwa uhakiki;

d) Malipo ya posho kwa watumishi kufanyika mara mbili (double payments);

e) Kukosekana kwa vielelezo vya uhalali wa malipo ya Asilimia Kumi (10%) ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana;

f) Mkanganyiko (confusion) katika taarifa ya hesabu za mradi na kusababisha bakaa kutojulikana zilipo; na

g) Kutotangaza maoni (opinion) na taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika magazeti yanayosomwa zaidi na wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na Taarifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa na maelezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, na Mahojiano baina ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Halmashauri 42 zilizoitwa kuja mbele ya Kamati; Kamati haijaridhika na utendaji wa Halmashauri 14 zifuatazo:-H/M Sumbawanga, H/M Shinyanga, H/M Dodoma, H/W Korongwe, H/W Ukerewe, H/W Sengerema, H/W Morogoro, H/W Hanang, H/W Rombo, H/W Kibondo, H/W Kasulu ,H/W Ngara, H/W Longido na H/Mj Geita kupata Hati za Ukaguzi zenye mashaka kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo.

## 2.2 Uchambuzi kwa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2015/16

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia vigezo na mambo ya msingi niliyoyatajwa hapo awali, Uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ulibainisha mambo yafuatayo:-

### 2.2.1 Usimamizi wa Mikataba na Manunuzi yasiyozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma (*Sura ya 9 ukurasa wa 89 hadi 152 wa taarifa ya ukaguzi ya CAG*)

**Mheshimiwa Spika,** Yapo manunuzi ya bidhaa na huduma yaliyofanyika nje ya Bajeti ya mwaka husika (kinyume na utaratibu unaotaka manunuzi yote kufanyika kulingana na bajeti iliyoidhinishwa), manunuzi kufanyika kwa fedha

taslimu kinyume na Sheria ya Manunuzi ya Umma, Manunuzi kufanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni, Fedha kulipwa kwa manunuzi ambayo hayakufanyika,na Utekelezaji wa shughuli za Miradi ambayo haipo kwenye Mpango wa Manunuzi wa Mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni,2016 imeonesha kuwa jumla ya Halmashauri 50 nchini sawa na asilimia 29 Zilikuwa na tatizo la ununuzi usiozingatia taratibu za ununuzi zilizowekwa na Sheria ya ununuzi wa Umma. Miongoni mwa mambo yaliyokiuka taratibu za ununuzi (Procurement Practises and Procedures) ni kununua bidhaa na Huduma nje ya bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka huo. Kamati ilibaini kuwa jumla ya Halmashauri 171 sawa na asilimia 92 zilifanya ununuzi wa thamani ya TZS 11.5 bilioni nje ya Bajeti ya mwaka. Vilevile Halmashauri hizo jumla ya TZS 1.49 bilioni kulipa madeni ya miaka ya nyuma licha ya kuwa madeni hayo hayakuwepo katika Taarifa za Fedha za miaka hiyo. Ulipaji huo wa madeni ulifanyika nje ya bajeti za Halmashauri hizo kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016. Mtindo huo sio tu unaashiria hatari ya upotevu wa fedha za umma, bali pia unaathiri ufanikishaji wa malengo ya bajeti yalikusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2015/16 kati ya Halmashauri 171 zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Halmashauri 50 sawa na 29% hazikufuata Sheria ya Manunuzi ya Umma katika kufanya manunuzi mbalimbali ya huduma na bidhaa. Halmashauri hizo ni pamoja na H/Jiji Dar es Salaam, H/Jiji Mbeya, H/M Musoma, H/W Arusha, H/W Chunya, H/W Iringa, H/W Nkasi, H/W Sumbawanga, H/W Tabora.

**Mheshimiwa Spika, Hoja ya Kamati katika tatizo la kutofuata sheria na taratibu za manunuzi ya umma, ni kuwa matumizi hayo ni ufujaji wa fedha za umma na hayana tija. Na hivyo, Serikali inaendelea kupoteza fedha nyingi, ambazo zingeweza kutumika kutatua matatizo ya Wananchi katika maeneo mengine.**

### 2.2.2 Usimamizi wa matumizi ya fedha za umma usiozingatia Sheria, kanuni na Taratibu *(Sura ya 10 ukurasa wa 153 hadi 173 wa taarifa ya ukaguzi ya CAG)*

**Mheshimiwa Spika,** Agizo Namba 8(2) (c) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa la mwaka 2009 linazitaka Halmashauri kudhibiti na kutunza nyaraka zote za malipo. Nyaraka za malipo huthibitisha uhalali wa malipo kwa huduma au bidhaa iliyonunuliwa. Katika mwaka 2015/16 jumla ya Halmashauri 109 sawa na asilimia 59 zilifanya malipo yenye thamani ya TZS 9.8 bilioni bila kuwa na nyaraka muhimu kama vile hati ya madai, hati ya kukiri kupokea malipo na taarifa ya shughuli za zilizolipwa ufafanuzi halisi unaonekana katika Jedwali na.3

**Jedwari Na. 3:** Muhtasari wa kiasi cha malipo yaliyofanyika kwa nyaraka pungufu kwa miaka minne (4) mfululizo.


| Na | Mwaka wa fedha | Kiasi cha Malipo (TZS) | Jumla ya Halmashauri zilizofanya malipo hayo |
|---|---|---|---|
| 1 | 2015/2016 | 9,818,166,618.00 | 109 |
| 2 | 2014/2015 | 10,031,058,789.00 | 82 |
| 3 | 2013/2014 | 3,878,602,680.00 | 80 |
| 4 | 2012/2013 | 3,514,703,776.00 | 67 |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Ukaguzi ya CAG kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2015/16*

Kamati ilitaka kujua sababu ya kufanya malipo bila kuwa na nyaraka na kubaini kuwa kitengo cha ukaguzi wa awali (pre- audit section) hakifanyi kazi yake ipasavyo katika Halmashauri. Kwa maelezo hayo, ni dhahiri matumizi hayo ya Fedha za umma yamekiuka misingi na taratibu jambo ambalo linahatarisha manufaa yaliyokusudiawa kwa Halmashauri na wananchi kwa ujumla.

**Mheshimiw Spika,** ili kuliwezesha bunge lako tukufu kupata mwenendo wa malipo yasiyokuwa na nyaraka za uthibitisho kwa miaka minne, Grafu Na. 1 linaonesha hali ilivyo.

Grafu Namba 1: Mwenendo wa Malipo kwa nyaraka pungufu kwa miaka minne (4) mfululizo




***Chanzo:** Taarifa ya Ukaguzi ya CAG kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2015/16*

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mantiki hiyo malipo hayo hayakuthibitisha uhalali wake. Uchambuzi unaonyesha kuwa tatizo la malipo kufanyika pasipo kuwa na nyaraka limekuwa likiongezeka mwaka hadi mwaka, hali hii, ni dalili ya kushindwa kupata suluhisho la kudumu katika tatizo hili sugu la matumizi ya fedha za Umma. Kukosekana kwa nyaraka muhimu za kuthibitisha uhalali wa malipo ni kiashiria kikubwa cha wizi.

**Mheshimiwa Spika,** Limebainika pia, tatizo lingine kubwa kwa Halmashauri kushindwa kusimamia ipasavyo akaunti za amana kutokana na kutokuwepo kwa utunzaji mzuri wa rejista za amana. Akaunti ya amana isiposimamiwa vizuri huweza kutumika katika kugharamia matumizi mbalimbali bila kuonyesha akisi yake kuwa fedha hizo ziliingizwa katika akaunti hizo. Katika mwaka 2015/16 matumizi mbalimbali yenye thamani ya TZS 13.8 bilioni yalifanyika bila kuonesha kama kiasi hicho kilikuwa kimepokelewa katika akaunti za amana. Tatizo hili linasababishwa na udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani (weak internal control system).

Kadhalika, Matumizi hayo mabaya ya akaunti ya amana yanafanyika kwa visingizo vifuatavyo:-

Maagizo kutoka ngazi za juu, Fedha kuingizwa kwenye akaunti hiyo bila kuwepo muongozo wa matumizi, Kufanya matumizi bila idhini ya mamlaka husika na hivyo kuathiri kazi zilizokusudiwa. Halmashauri nne (4) zilizoonekana kuwa na kiasi kikubwa cha matumizi yasiyodhibitiwa kutoka katika akaunti ya amana ni H/W Meatu (TZS 3.05 bilioni), H/W Nkasi (TZS 718.5 milioni), H/W Wanging'ombe (TZS 561.3 milioni) na H/W Handeni (TZS 460.6 milioni).

**Mheshimiwa Spika, Hoja ya Kamati ni kuwa Maafisa Masuuli wanazembea katika kusimamia mifumo ya ndani ya udhibiti wa mapato na matumizi, hali ambayo huchangia matumizi mabaya ya fedha za umma na kuathiri hali ya upatikanaji wa huduma bora kwa Wananchi.**

### 2.2.3 Usimamizi usio na tija wa mikataba na utekelezaji wa miradi ya maendeleo (*sura ya 8 na 9 ya ukurasa wa 78 hadi 152 wa taarifa ya ukaguzi ya CAG* )

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu kubwa ya fedha zinazotengwa na serikali katika bajeti kila mwaka na kupelekwa katika Halmashauri hutumika katika manunuzi ya bidhaa na huduma. Kwa hali hiyo, mchakato unaohusisha matumizi hayo unapaswa kuwa madhubuti ili kudhibiti ufujaji wa fedha za umma. Lakini pia, fedha nyingine kama vile mapato kutoka katika vyanzo vya ndani na fedha za wafadhili kwa kiasi kikubwa hutumika katika manunuzi ya bidhaa na huduma.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mahojiano na Halmashauri 42 katika kipindi hiki, Kamati imebaini udhaifu katika usimamizi wa utekelezaji wa mikataba na usimamizi wa miradi ya maendeleo hali inayoathiri moja kwa moja utoaji wa huduma kwa Wananchi. Mathalani, katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, miradi mitano (5) yenye thamani ya TZS 4.2 bilioni haijakamilika kwa muda mrefu kutokana na udhaifu katika usimamizi wa mikataba.Udhaifu huo unasababisha baadhi

ya Miradi ya Maendeleo katika Halmashauri nchini kuchukua muda mrefu kukamilika, au kukamilika kwa wakati lakini kwa kiwango cha chini tofauti na makubaliano. Aidha, dosari hii imesababisha miradi mingine kutokamilika kabisa, na mingine kutotekelezwa. Vilevile, kuna baadhi ya Miradi imekamilika lakini haitumiki kama ilivyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Baadhi ya Halmashauri zimeendelea kuonyesha udhaifu katika usimamizi wa utekelezaji wa kandarasi mbalimbali. Mathalani Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ilitoa zabuni zenye thamani ya TZS 2.02 bilioni kwa Wazabuni mbalimbali lakini Wazabuni hao walishindwa kumaliza kandarasi kwa wakati, vilevile lipo tatizo la wazabuni na wakandarasi kushindwa kuwasilisha mpango wa kazi hata baada ya kupewa muda wa ziada (extension), kutowasilisha hati ya dhamana ya utekelezaji miradi (performance bond) kwa Halmashauri, na kutowasilisha hati ya ulipaji wa kodi (tax clearance certificate).

**Mheshimiwa Spika,** Tarehe 25 Mei 2012 Halmashauri ya Manispaa Ilala iliingia mkataba na Kampuni ya Remix Centre Ltd kwa ajili ya kupima viwanja vya wananchi katika baadhi ya maeneo ya kata ya Chanika na Msongola. Tarehe 1 Desemba 2014, wakati utekelezaji wa mkataba huo ukiendelea, yalifanyika mabadiliko ya mkataba huo ambayo hayakuwa na vielelezo vya uhalali wala chanzo chake lakini yalikubaliwa na Halmashauri. Kampuni hii ilipewa kipindi cha miaka mitatu (3) kupima jumla ya viwanja 30,000 lakini hadi kufikia tarehe 6 Januari 2016 kampuni hii ilikuwa imepima viwanja 870 tu sawa na asilimia 3% ya viwanja vyote. Pamoja na kusuasua kwa utekelezaji wa mradi huu Halmashauri haikuweza kujitoa katika mradi huu. Kadhalika Halmashauri haikuweza kutoa hati za viwanja vilivyopimwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Remix Centre Ltd ililipwa kiasi cha TZS 715.27 milioni kwa ajili ya mauzo ya viwanja 84 lakini pia kampuni hiyo ililipwa kiasi cha TZS 3.6 bilioni na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) kama mauzo ya viwanja 800. Ingawa fedha hizo zimetokana na mradi huo chini ya usimamizi wa pamoja na Halmashauri,

hakuna fedha yeyote iliyowasilishwa kwa Halmashauri. Kampuni hiyo imeshindwa kuonyesha kwa uwazi jumla na uhalali wa gharama zilizotumika katika mradi.

**Mheshimiwa Spika**, sambamba na kufanya mahojiano na Halmashauri 42 Kamati ilifanya ziara katika Halmashauri saba (7) zifuatazo ; H/Jiji Tanga, H/ Jiji Mbeya, H/M Dodoma, H/W Korogwe, H/W Kilindi, H/W Rungwe na H/W Kyela. Katika ziara hizo Kamati iliweza kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kumi na tisa (19) na yafuatayo ni matokeo yaliyobainishwa katika baadhi ya miradi.

**Mheshimiwa Spika,** Halmashauri ya Korogwe ilidhinishiwa fedha kiasi cha TZS 314 milioni kwa ajili ya mradi wa maji wa Changalikwa. Mkandarasi Cosmos Engineering Co ltd aliingia mkataba namba (LGA/125/2012- 2013/W/55/ LOT 3) Agosti, 2013 wa kujenga miundombinu ya maji katika kata ya Changalikwa. Kamati ilibaini mapungufu kadhaa kama vile; Mtandao wa mabomba wenye mita 300 kati ya mita 7,040 yamepasuka na kukatika sehemu mbali mbali. Mita (Consumer Meter) za mradi hazifanyi kazi japo kuwa huduma maji inaendelea, Hodhi la kunyweshea mifugo maji (Cattle Trough) limejengwa chini ya kiwango na kushindwa kutumika, gharama kubwa ya huduma ya maji kutokana na matumizi ya jenereta. Kamati imebaini pia kuwepo kwa mazingira ya viashiria vya rushwa, kwani licha ya mradi huo kutekelezwa kwa kiwango cha chini Msimamizi mshauri (project consultant) ameendelea kupewa kazi katika mradi huo. Kadhalika, Halmashauri hiyo imeshindwa kutoa vielelezo vya matumizi ya fedha kiashi cha TZS 20 milioni zilizotumika katika Mradi huo.

**Mheshimiwa Spika**, katika Halmashauri ya Wilaya Rungwe, Kamati ilifanya ukaguzi wa Mradi wa maji Masoko. Kama ilibaini kasoro za mradi kutokamilika kwa wakati kwani utekelezaji wa mradi huo ulianza mwaka 2009 na hadi sasa bado haujakamilika. Halmashauri ya Rungwe iliamua kuvunja Mkataba na Mkandarasi mwaka 2012 kutokana na Mkandarasi kuchelewesha mradi na kushindwa kuwasilisha hati ya dhamana (performance bond). Wakati wa kuvunja

Mkataba huo mkandarasi alikuwa ameshalipwa kiasi cha TZS 1.263 bilioni na Mkandarasi Mshauri (project consultant) alilipwa kiasi cha TZS 675.19 milioni nje ya utaratibu kwa kigezo cha muda (time based contract). Aidha, Halmashauri haukuzingatia maoni na ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali juu ya ongezeko la kiasi cha TZS 549.78 sawa na Asilimia 37 ya gharama ya kazi iliyoongezeka nje ya Mkataba wa mwanzo.

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile Kamati ilikagua mradi wa Soko la Mwanjelwa lililopo katika Jiji la Mbeya. Kamati ilibaini mapungufu makubwa katika ujenzi na uendeshaji wa mradi huo. Soko hilo limekamilika lakini vyumba na vizimba vingi havitumiki kama ilivyokusudiwa, baadhi ya Wafanyabiashara ndogondogo walio nje ya soko hawalipi kodi, Msimamizi au Mkusanya ushuru katika soko hilo M/S **Prolat Consultant** aliyewekwa na Benki ya CRDB anakusanya mapato ya soko hilo bila Halmashauri ya Jiji kufahamu kiasi kinachokusanywa kutokana na mkataba uliopo. Kadhalika Halmashauri ya Jiji ina mzigo mkubwa wa kulipa deni la Benki lilitokana na ujenzi wa soko hilo kiasi cha TZS 63 Bilioni pamoja na riba ifikapo mwaka 2031, deni ambalo ukokotoaji wake umetiliwa mashaka. Halmashauri ya Jiji la Mbeya haina uwezo wa kulipa deni hilo kutokana na mapungufu yaliyopo katika uendeshaji wa mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Kupitia mradi wa LSP II unaoratibiwa na Ofisi ya Bunge, Kamati ilifanya ukaguzi wa thamani katika mradi wa maji wa Mkonze katika Manispaa ya Dodoma. Mradi huu ulikuwa na thamani ya TZS 497.1 milioni na ulianza kutekelezwa tarehe 27 Septemba 2012 na kukamilika tarehe 22 Machi 2014 ikiwa ni mwaka mzima tangu tarehe rasmi ya kumaliza ujenzi kupita. Mradi huu ulipangwa kuwa na vituo vya kutolea huduma ya maji (Water Delivery Points) 15 na kunufaisha wananchi 8,570 katika kata ya Mkonze. Mwaka 2015 Kamati ya Maendeleo ya Kata ya Mkonze iliamua kumkabidhi mradi huo Ndg. Yasin Ally ili auendeshe kwa kuwa Kamati haikuwa na fedha ya kununua pampu ya kuvutia maji (Water Pump) iliyokuwa imeungua.

**Mheshimiwa Spika,** Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ilitoa maelezo kuwa palikuwa na mawasiliano baina ya Kamati ya Watumiaji Maji (COWSO) hiyo na Manispaa kutaka mwongozo wa ukabidhishaji wa mradi huo kwa mtu binafsi lakini Manispaa haikutoa ushirikiano. Kimsingi mradi huo kukabidhiwa kwa mtu binafsi kuundesha ni kinyume na taratibu na hivyo kwa nanmna yeyote Mkataba uliopo baina ya Halmashauri na mwendeshaji huyo ni batili na unapaswa kuvunjwa mara moja. Huu ni mfano wa namna Halmashauri zinavyoshindwa kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa manufaa ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika, Hoja ya Kamati ni kwamba, kumebainika kuwepo kwa kasoro nyingi za usimamizi, ufuatiliaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika halmashauri Nchini. Hali ambayo, imechangiwa na uzembe wa baadhi ya Watumishi, uchache wa wataalamu kwenye Halmashauri, Usanifu hafifu wa miradi, kutokushirikishwa kwa Wananchi kikamilifu na utaratibu mbovu wa utoaji zabuni kwa Wakandarasi. Na hivyo, Wananchi wameendelea kukosa huduma tarajiwa licha ya Serikali kuendelea kutenga fedha nyingi kwa ajili ya miradi ya maendeleo husika.**

### 2.2.4 Udhaifu katika kusimamia ukusanyaji wa Mapato ya Ndani (*sura ya 11 ukurasa wa 204)*

**Mheshimiwa Spika,** kumeendelea kuwepo na udhaifu katika usimamizi wa ukusanyaji wa Mapato kutoka Vyanzo vya Ndani unaofanywa na Halmashauri kwa Mawakala wa Mapato bila hatua stahiki kuchukuliwa mapema. Hali hii imesababisha kiasi kikubwa cha fedha kutokusanywa kwa wakati, upotevu wa vitabu vya kukusanyia mapato na kutowasilishwa na Halmashauri kushindwa kukusanya kabisa mapato yake.

Ili kuondokana na utegemezi wa ruzuku kutoka serikali kuu Halmashauri zimekuwa zikihimizwa kuongeza wigo wa vyanzo mapato kwa kufanya tathmini ya vyanzo vilivyopo na kuongeza vingine. Halmashauri inaposuasua katika kukusanya mapato sio tu kwamba inaonyesha kutozingatia


ushauri wa Kamati bali pia huendelea kuwa tegemezi kwa ruzuku kutoka Serikali Kuu na hivyo kushindwa kutoa huduma kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Agizo la 38 (3) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa la 2009, linazitaka Halmashauri kumtaka wakala wa kukusanya mapato kuweka dhamana yenye thamani ya malipo ya miezi mitatu, ili kuikinga Halmashauri hiyo na hasara zinazoweza kutokea iwapo wakala atashindwa kukusanya na kuwasilisha mapato kutoka vyanzo vya ndani. Lakini kwa kukosekana kwa mbinu, mkakati na jitihada katika kusimamia kwa ukamilifu ukusanyaji wa mapato kumepelekea Halmashauri nyingi kushindwa kukusanya mapato hayo. Mathalani, katika mwaka wa fedha 2015/16 jumla ya Halmashauri 80 hazikukusanya mapato kutoka kwa mawakala kiasi cha TZS 6.03 bilioni. Sambamba na hilo, jumla ya Halmashauri 91 zilishindwa kukusanya mapato kutoka katika vyanzo vyake vya ndani kiasi cha TZS 21.03 bilioni pamoja na ukweli kwamba Halmashauri zinao uwezo wa kutunga au kurekebisha sheria ndogo ili kuongeza vyanzo vya mapato.

**Jedwali Na. 4 :** Muhtasari wa makusanyo kutoka vyanzo vya ndani kwa baadhi ya Halmashauri zilizoshindwa kufikia malengo kwa mwaka wa fedha 2015/16.

| Na. | Jina la Halmashauri | Bajeti iliyoidhinishwa | Makusanyo halisi |
|---|---|---|---|
| 1 | H/Mji Babati | 6,044,154,000.00 | 2,243,110,445.00 |
| 2 | H/W Buhigwe | 638,895,000.00 | 127,587,000.00 |
| 3 | H/W Gairo | 889,565,800.00 | 238,919,208.00 |
| 4 | H/W Kigoma | 477,607,000.00 | 214,852,032.00 |
| 5 | H/W Mbogwe | 1,130,281,000.00 | 526,532,190.00 |
| 6 | H/W Morogoro | 1,891,754,500.00 | 569,119,112.00 |
| 7 | H/W Ngorongoro | 4,527,363,584.00 | 1,535,621,971.00 |
| 8 | H/W Siha | 1,705,516,770.00 | 758,444,735.00 |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi ya CAG kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2015/16*




***Chanzo:*** *Taarifa ya Ukaguzi ya CAG kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2015/16*

**Mheshimiwa Spika,** Grafu namba 2 linaonesha kuwa Halmashauri zote 8 hazikuweza kukusanya zaidi ya nusu ya bajeti iliyoidhinishwa. Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe inaonekana kuwa na makusanyo pungufu zaidi kwa kulinganisha na Halmashauri nyingine. Kadhalika, Halmashauri ya Mji Babati, Morogoro na Ngorongoro zinaonekana kuwa na makisio makubwa ambayo hayana uhalisia ikilinganishwa na kiasi kilichokusanywa. Makusanyo halisi yangeweza kuongezeka iwapo Halmashauri zingekuwa na utaratibu wa kufanya tathmini ya vyanzo vya mapato ya ndani.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, kumeendelea kuwa na udhaifu katika kuhakikisha kuwa vitabu vya kukusanyia mapato vinawasilishwa kwa Afisa Masuuli kila mwezi kama taratibu za fedha zinavyoelekeza. Kushindwa kuwasilisha vitabu vya kukusanyia mapato kunasababisha upotevu wa mapato na ubadhilifu wa fedha za umma. Kadhalika, Halmashauri hushindwa kujua kwa usahihi kiasi kilichokusanywa na hivyo kupunguza kiwango cha makusanyo. Katika mwaka wa fedha 2014/15 jumla ya vitabu 814 havikuwasilishwa wakati wa ukaguzi na katika mwaka 2015/16 jumla ya vitabu 817

havikuwasilishwa. Kamati inaona kuwa hili ni tatizo sugu na kuzitaka Menejimenti za Halmashauri nchini kuimarisha Mfumo wa udhibiti wa ukusanyaji mapato ya ndani.

**Mheshimiwa Spika, Hoja ya Kamati ni kwamba, Halmashauri zimekosa ufanisi katika usimamizi na udhibiti wa ukusanyaji mapato kutoka vyanzo vya ndani. Pamoja na udhaifu wa kusimamia, Halmashauri zimeendelea kukosa mapato kutoka vyanzo vya ndani , na hivyo kuwa tegemezi kwa Serikali Kuu.**

### 2.2.5 Kutotekeleza Maagizo ya Kamati na kutojibu Hoja za Ukaguzi (*sura ya 3 ukurasa wa 17 wa taarifa ya CAG)*

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 15 (a)-(c) cha Nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kinaitaka Kamati kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwisha tolewa na Kamati awali. Kumbukumbu zinaonesha kuwa Kamati ili zitaka Halmashauri nchini kuzingatia masharti ya kifungu cha 40 cha sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 (Public Audit Act) ya mwaka 2008. Kifungu hicho kinawapa Maafisa Masuuli wajibu wa kujibu hoja zinazotolewa katika Taarifa za kila mwaka za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Hata hivyo, Kamati imebaini uwepo wa Maafisa Masuuli katika Halmashauri nchini zembea kujibu Hoja za ukaguzi kinyume na masharti ya sheria.

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha kwa kuwapa nafasi ya kusikilizwa Maafisa hao (Rihght to be heard), Kamati ilipanga Vikao vya mahojiano na kupokea maelezo kutoka kwa Menejimenti za Halmashauri nchini zilizoainishwa kuwa na hoja. Wakati wa Mahojiano Kamati ilibaini kuwa Maafisa Masuuli walishindwa kutoa maelezo yenye mantiki kuhusu sababu za kutojibu hoja. Aidha, wapo baadhi yao walishindwa kujibu hoja kwa wakati na wengine kushindwa kujibu hoja kwa ukamilifu. Mambo yaliyosababisha Halmashauri nyingi nchini kuendelea kuwa na hoja nyingi za ukaguzi zisizojibiwa. Kwa bahati mbaya tatizo hili la kutojibu

hoja za ukaguzi limekuwa likijirudia mara nyingi jambo linalotosha kuainisha suala hili katika orodha ya matatizo sugu

**Mheshimiwa Spika,** hoja za ukaguzi ni kiashiria cha kuwepo kwa matumizi mabaya ya Fedha za Umma. Kwa msingi huo, Kamati ilitoa mapendekezo maalum kuhusu tatizo hilo ili kurekebisha dosari hiyo. Ni jambo linaloleta wasiwasi kwa Mapendekezo ya Kamati kuhusu matumizi ya fedha za Umma kutozingatiwa kama inavyoonyeshwa kwenye jedwari lifuatalo kwa muda miaka mitatu.

**Jedwali Na. 4:** Muhtasari wa utekelezaji wa Maagizo ya Kamati na Hoja za Ukaguzi katika Halmashauri nchini kwa mwaka wa fedha 2015/16

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Halmashauri | Jumla ya Mapendekezo | Yaliyotekelezwa | Yanayoendelea kutekelezwa | Yasiyotekelezwa |
|---|---|---|---|---|---|
| **2014/15** | **164** | **1094** | **433** | **231** | **430** |
| Asilimia ya utekelezaji | - | 100 | 40 | 21 | 39 |
| **2013/14** | **118** | **900** | **408** | **201** | **291** |
| Asilimia ya utekelezaji | - | 100 | 45 | 22 | 33 |
| **2012/13** | **123** | **1146** | **536** | **240** | **370** |
| Asilimia ya utekelezaji | - | 100 | 47 | 21 | 32 |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Ukaguzi ya CAG kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2015/16*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini udhaifu uliopo katika dhana ya uwajibikaji hasa inapotokea maagizo ya Kamati na hoja za ukaguzi kuvuka mwaka mmoja wa fedha kwenda mwingine au Kamati kuvunjika kufuatia Bunge kumaliza uhai wake na hasa dhana ya maagizo ya Kamati kutotekeleza kabisa. Halmashauri zinapaswa kuwa na Mpango Mkakati wa Muda Maalum wa kutekeleza maagizo ya Kamati na kujibu hoja za ukaguzi ambao utaonyesha muda, namna ya utekelezaji, na muhusika hivyo kutoa nafasi ya uwajibikaji pale uzembe unapobainika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kuweka wazi kuwa hakuna sababu zamsingi zilizotolewa na Halmashauri

yeyote za kushindwa kujibu hoja za ukaguzi na kutekeleza maagizo ya Kamati. Hii inaonyesha kuwa utekelezaji wa matakwa haya unafanywa kwa mazoea.Mathalani, Halmashauri ya Wilaya ya Rombo ilishindwa kabisa kujibu hoja za ukaguzi na kutekeleza maagizo ya Kamati

**Hoja ya Kamati ni Kuwa, Maagizo ya Kamati hutokana na mahojiano baina ya Kamati na Halmashauri kufuatia Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, nini Tamko la Ofisi ya Rais – TAMISEMI juu ya uzembe wa kutotekeleza maagizo ya Kamati na kutojibu hoja za Ukaguzi kwa ukamilifu na kwa wakati?**

### 2.2.6 Kutotenga mchango wa Asilimia Kumi (10%) ya Mapato kutoka vyanzo vya ndani kwa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana na Asilimia Ishirini (20%) ya ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Vijiji (*sura ya 13 ukurasa wa 254 wa taarifa ya CAG)*

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuongeza kasi ya shughuli za maendeleo katika Halmashauri nchini, Halmashauri hutakiwa kuchangia asilimia 10% ya mapato yake ya ndani katika mfuko wa maendeleo wa wanawake na vijana. Mfuko huu hujiendesha kwa kukopa na kujizungusha (loan revolving fund) na fedha hukopeshwa kwa vikundi vinavyojihusisha na shughuli za maendeleo kwa makundi ya wanawake na vijana chini ya usimamizi na uratibu wa Halmashauri yenyewe. Ingawa Kamati imekuwa ikisisitiza Halmashauri kutenga asilimia 10% na kuwasilisha katika mfuko huo, lakini imekuwa ni vigumu kwa Halmashauri kutekeleza suala hilo kwa ukamilifu.

Halmashauri zote 42 zilizohojiwa na Kamati kwa mwaka huu zipo zilizotenga kiasi kidogo na nyingine hazikutenga kabisa wala kuwasilisha marejesho ya fedha za Mfuko huu. Aidha, Kamati imebaini kiasi cha TZS 4.1 Bilioni ziko mikononi wa vikundi na hakuna mfumo madhubuti wa kuzirejesha wakati Mfuko huu unaendeshwa kwa kuweka fedha na kukusanya marejesho ili vikundi vingine pia vipate fursa ya kukopa

(Revolving Fund). Kamati imebaini kuwa matumizi ya Mfuko huu uishia kwenye gharama za uendeshaji semina na uchapishaji vipeperushi kwa Watendaji badala ya walengwa.

**Mheshimiwa Spika,** Halmashauri zote zimekuwa zikitoa sababu ya kuwa na mzigo mkubwa wa gharama za uendeshaji hivyo kushindwa kutenga na kuwasilisha mchango huo. Maoni ya Kamati ni kuwa, kutopeleka michango katika Mfuko huo kunapunguza tija ya mfuko huo kwa kutotoa fursa kwa wajasiriamali kunufaika na mikopo. Ukweli ni kwamba wajasiriamali wengi wanaweza kunufaika na mikopo kupitia mfuko huu kwa kuwa masharti ya ukopaji ni machache na yanayoweza kutimizwa, riba inayotozwa ni nafuu kulinganisha na riba zinazotozwa na mabenki ya biashara na taasisi nyingine za fedha, na pia mchakato wa utoaji mkopo kupitia mfuko huu ni mfupi.

**Mheshimiwa Spika,** Maagizo yanayotolewa na Kamati ya LAAC hayana nguvu kisheria na hivyo utekelezaji wake unaweza kuchukuliwa kuwa wa hiari na hivyo kusababisha ugumu wa kushitaki na kupata ufumbuzi kwa kutumia sheria. Mathalani, Halmashauri ya Jiji Mwanza katika mwaka 2015/16 haikutenga jumla ya TZS 1.03 bilioni kwa mfuko huu, Halmashauri ya Manispaa Ilala kiasi cha TZS 2.35 bilioni na Halmashauri ya Manispaa Kinondoni TZS 5.1 bilioni. Hata hivyo, kwa mujibu wa mwongozo wa mfuko huu, zilitakiwa kutenga na kuwasilisha mchango huo lakini hazikutekeleza hivyo.

**Hoja ya Kamati ni kwamba, uwepo wa Mfuko huo unaongeza kasi ya maendeleo katika ngazi za chini, Je Serikali haioni sasa kuwa umefika wakati muafaka wa kuunda Sheria maalum ya kusimamia Mfuko huu ili kuongeza uwajibikaji?**

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile, upelekaji wa fedha za fidia ya vyanzo vya mapato vilivyofutwa, asilimia ishirini (20%) ya GPG kwenda kwa mamlaka za serikali za mitaa na vijiji, haufanyiki kama ilivyoagizwa. Hali hii inasababisha serikali za mitaa na vijiji kushindwa kutimiza majukumu yake kikamilifu kwa kukosa

fedha za kujiendesha. Katika Halmashauri zote 42 zilizohojiwa hapakuwa na Halmashauri hata moja iliyotenga na kupeleka mchango huu kwa ukamilifu. Katika mwaka wa fedha 2015/16 Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ilikuwa na kiasi kikubwa zaidi cha ruzuku iliyotakiwa kupelekwa katika serikali za mitaa na vijiji, ambako kiasi cha TZS 720.04 milioni hazikupelekwa. Aidha, Halmashauri nyingine ambazo hazikupeleka ruzuku katika serikali za mitaa na vijiji kwa miaka miwili (2) mfululizo (2014/15 na 2015/16) ni pamoja na H/W Karagwe, H/W Muleba na H/M Dodoma.

Katika baadhi ya Halmashauri, Fedha zilizopokelewa kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ruzuku ya vijiji na mitaa zimeonekana kuchanganywa kimakosa na mapato ya ndani kabla ya kutenga asilimia ishirini (20%). Hali hii haitoi picha ya kiasi halisi kinachotakiwa kutengwa na kuwasilishwa.

**Hoja ya Kamati ni kwamba, asilimia ishirini (20%) ya fedha za ruzuku kutoka Serikali Kuu kwenda kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Vijiji ililenga kuvipatia fedha Vijiji na Mitaa kufuatia kufutwa kwa vyanzo vya mapato vilivyokuwa na kero. Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka kukata fedha hizi kabla ya kuwasilisha katika Halmashauri na ili kuondoa mapungufu haya mara moja?**

### 2.2.7 Wakuu wa Idara na Vitengo kukaimu Nafasi zao kwa zaidi ya miezi sita (6) bila kuthibitishwa na Watumishi kukaa muda mrefu kituoni. (*sura ya 7 ukurasa wa 67 wa taarifa ya CAG)*

**Mheshimiwa Spika,** Agizo D 24(3) la Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 linaweka wazi kuwa mtumishi yeyote hatatakiwa kukaimu nafasi za ukuu wa idara au vitengo kwa zaidi ya miezi sita (6). Kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) imebainisha kuwa Wakuu wa Idara na Vitengo 373 katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa wanakaimu nafasi zao kwa zaidi ya miezi sita (6) bila kuthibitishwa. Na pia, Halmashauri mpya na zilizo pembezoni zinaongoza kuwa na Idadi kubwa ya

Wakuu wa Idara na Vitengo wanaokaimu kwa muda mrefu kama vile Itigi, Msalala, Chemba, Ukerewe na Nkasi.

**Mheshimiwa Spika,** Halmashauri kama mamlaka ya ajira kwa watumishi wake inao wajibu wa kuhakikisha kuwa agizo hili linatekelezwa kikamilifu kwa kuanza mchakato wa kuwathibitisha watumishi wote wanaokaimu nafasi zao ili kuongeza tija katika utendaji wa kazi na kutoa haki kwa watumishi wanaokaimu nafasi kwa kipindi kirefu. Kamati inaamini kwamba Watumishi wanaokaimu nafasi zao hushindwa kufanya maamuzi ya kiutendaji kwa maslahi ya Halmashauri zao na badala yake huishia kuegemea kwenye kivuli cha kukaimu Nafasi hizo na kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa kiwango kinachotakiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Halmashauri zilikokuwa na idadi kubwa ya watumishi wanaokaimu nafasi za ukuu wa idara na vitengo zimekuwa na dosari kubwa katika taarifa zake zilizowasilishwa mbele ya Kamati (hususani maandalizi ya kitabu cha LAAC). Mathalani, Halmashauri ya Korogwe, ambayo Kamati ilifanya ziara na kubaini Wakuu wa Idara kumi na moja (11) kwenye Halmashauri hiyo wamekuwa wakikaimu nafasi hizo kwa zaidi ya kipindi cha mwaka mmoja, jambo ambalo limechangia utendaji na uwajibikaji kuwa wachini pamoja na Halmashauri hiyo kuwa na dosari na matatizo mengi katika usimamizi wa fedha za umma kwa miaka mitatu (3) mfululizo.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, kuna upungufu mkubwa wa Watumishi katika Halmashauri nchini, ambao umeendelea kuathiri utendaji kazi, na upatikanaji wa huduma bora kwa Wananchi. Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika Halmashauri 126 umeonesha kuna mahitaji mapya ya Watumishi 243,548 ikilinganishwa na idadi ya Watumishi 349,974 waliopo. Sekta ambazo zimeathiriwa kwa kiasi kikubwa ni Afya, Elimu na Kilimo, ambazo kwa kiasi kikubwa ndizo zinagusa maslahi ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, kutokana na upungufu wa rasilimali watu katika Halmashauri, Kamati iliweza kubaini tatizo la baadhi ya Watumishi kukaa katika kituo kimoja cha kazi kwa muda mrefu bila kuhamishwa, hali hii inaendelea kuathiri utekelezaji wa majukumu na kujenga utamaduni wa kufanya kazi kwa mazoea katika Halmashauri nchini. Katika mahojiano na menejimenti za Halmashauri Kamati ilibaini tatizo hili katika H/W Kibondo,H/W Bariadi, H/W Nkasi na H/W Liwale ambazo baadhi ya Watumishi wamekaa kwa muda mrefu sana.

**Mheshimiwa Spika, Hoja ya Kamati ni kuwa mchakato wa kuwathibitisha Wakuu wa Idara na Vitengo wanaokaimu nafasi zao kwa muda mrefu, umekuwa na urasimu mwingi, sambamba na hilo kumekuwa na upungufu wa Watumishi katika maeneo mengine hivyo kuathiri utendaji katika Halmashauri nchini.**

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.0 Maelezo ya jumla;

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kutoa maelezo ya kina kuhusu yajitokeza katika mijadala na Halmashauri 42 zilizoitwa mbele ya Kamati, Sehemu hii ya tatu ya Taarifa itatoa Maoni na Mapendekezo Saba (7) kwa ajili ya kuliomba Bunge lako Tukufu liyajadili na kuyaafiki ili yawe Maazimio ya Bunge kwa ajili ya kuchochea Nidhamu ya Matumizi ya Fedha za Umma katika Serikali za Mitaa.
Mapendekezo haya yanatolewa kwa kuzingatia maeneo yenye Matatizo Sugu ya matumizi mabaya ya Fedha za Umma katika Serikali za Mitaa.

### 3.1 Maoni (*Opinion*);

**Mheshimiwa Spika**, Maoni ya Kamati yanazingatia azma ya Bunge kuwa na Kamati mahsusi inayohusika na usimamizi wa matumizi ya fedha za Umma. Msingi wa maoni

hayo ni nia ya kuepusha matumizi mabaya ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa.

### 3.2 Mapendekezo (*Recommendations*);

**Mheshimiwa Spika,** Naomba sasa nitoe mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo;

### 3.2.1 Manunuzi yasiyozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma;

**Kwa kuwa** imebainika kwamba Halmashauri hazifuati Sheria ya Manunuzi ya Umma katika manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali,

**Na kwa kuwa** Manunuzi hayo hayana tija zaidi ya kuzitia hasara Halmashauri na kupunguza kiwango cha huduma kwa Wananchi,

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaliomba Bunge liazimie kuwa:-

(a) Serikali iweke utaratibu wa kutoa Taarifa za tathimini ya manunuzi za PPRA (Public Procurement Regulatory Authority) inayohusu serikali za mitaa sambamba na taarifa ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Kwa kufanya hivyo kutalipa Bunge fursa ya kushauri katika utekelezaji wa eneo la manunuzi ya umma, kwani fedha nyingi za umma zinatumika katika manunuzi ya taasisi hizo;na

(b) Serikali iweke Mpango Mkakati unaotekelezeka, katika kuhakikisha Halmashauri zinazingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma

### 3.2.2 Usimamizi wa matumizi usiozingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Fedha za Umma

**Kwa kuwa** Imebainika kuwepo na mapungufu katika kusimamia matumizi na ukiukwaji wa mifumo ya udhibiti wa ndani ikiwa pamoja na kupitisha na kuidhinisha malipo,

malipo kukosa viambatisho, malipo kufanyika kwenye vifungu vya matumizi visivyo sahihi na kukosekana kwa hati za malipo hayo;

**Na kwa kuwa** kuna kulegalega katika kuzingatia sheria, kanuni na miongozo inayosimamia shughuli za Halmashauri;

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa:-

a) Serikali ihimarishe ufuatiliaji na uimarishaji wa mifumo ya kudhibiti wa malipo ikiwa pamoja na uhimarishaji wa kitengo cha ukaguzi wa ndani;na

b) Serikali iwachukulie hatua za kinidhamu watendaji wote wanaohusika na upotevu wa nyaraka mbalimbali za malipo.

### 3.2.3 Usimamizi usio na tija wa utekelezaji wa mikataba na miradi ya maendeleo

**Kwa kuwa** Imebainika kuwepo na udhaifu katika usimamizi wa mikataba, usanifu wa miradi kuwa chini ya kiwango na kutozingatia mipango endelevu (sustainable plans) katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo hususani miradi ya maji. Hali hii, imeendelea kuathiri kwa kiasi kikubwa utoaji wa huduma kwa Wananchi kama ilivyokusudiwa. Aidha, mchakato wa upatikanaji wa fedha kwa wakati kutoka Hazina umeendelea kuwa ni changamoto kubwa. Na hivyo kusababisha kwa miradi kuchukua muda mrefu kukamilika, na baadhi ya miradi kutotekelezwa kabisa;

**Na kwa kuwa** fedha nyingi za umma zimeelekezwa kwenye miradi, na hadi sasa miradi hiyo haitoi huduma kama ilivyo kusudiwa. Pamoja na kuwepo kwa kasoro nyingi ambazo zinaonyesha wazi wazi matumizi mabaya ya fedha za umma sambamba na viashiria vingi vya kuwepo kwa vitendo vya rushwa;

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa:-

a) Serikali itoe maelezo ya kina na sababu za kushindwa kukamilika kwa Miradi mbalimbali ya Maendeleo;

b) Serikali ilifanyie kazi sula la Mradi wa soko la mwanjelwa lililopo katika jiji la mbeya pamoja na kuchukua hatua za haraka na za makusudi kuhakikisha kuwa inamaliza changamoto za mradi wa soko hilo. Hazina inapaswa kuaangalia njia bora ya kupitia upya ukokotoaji wa deni la Benki ya CRDB la zaidi ya TZS 63 bilioni ambazo zitatakiwa kulipwa ifikapo mwaka 2031, kwani Halmashauri ya jiji la Mbeya haina uwezo wa kulilipa deni hilo;na

c) Kuazimia kuunda Kamati maalum ya Bunge itakayochunguza sababu na chanzo cha tatizo la miradi ya maji kutekelezwa chini ya kiwango au kutotekelezwa kabisa. Kamati iweze kutoa ushauri utakaosaidia Serikali katika utekelezaji bora wa miradi ya maji nchini kwani miradi ya maji inawagusa wanachi wengi.

### 3.2.4 Udhaifu katika kusimamia mapato kutoka katika vyanzo vya ndani

**Kwa kuwa** Mapato kutoka vyanzo vya ndani hulenga kupunguza utegemezi wa Halmashauri wa ruzuku kutoka Serikali Kuu katika kutekeleza majukumu yake;

**Na kwa kuwa** Halmashauri nyingi zimeonyesha udhaifu na kutoweka jitihada katika kuhakikisha kuwa tathmini ya vyanzo hivyo inafanyika ili kuongeza wigo wa makusanyo na kuweka mikakati katika usimamizi wa mapato hayo;

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa;

(a) Serikali itoe maelezo ya Mpango Mkakati uliopo katika kuhakikisha kuwa tathmini ya vyanzo inafanyika katika Halmashauri zote, kuondoa udhaifu katika usimamizi wa

ukusanyaji wa mapato hayo, na kueleza ni hatua gani zitachukuliwa kwa Halmashauri itakayoonekana dhahiri kuzembea usimamizi wa Makusanyo kutoka vyanzo vya ndani;na

(b) Ofisi ya Rais, TAMISEMI itoe muda maalum kwa kila Halmashauri kuhakikisha inasimika na kuanza kutumia mfumo wa kieletroniki wa ukusanyaji mapato.

### 3.2.5 Kutotekeleza Maagizo ya Kamati na kutojibu Hoja za Ukaguzi;

**Kwa kuwa** Hoja za ukaguzi zinazotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Halmashauri na Maagizo ya Kamati ya LAAC hulenga kuzisaidia Halmashauri kuondoa mapungufu ili kuongeza tija;

**Na kwa kuwa** Halmashauri zimeshindwa kujibu hoja hizo kwa wakati na kutekeleza maagizo ya Kamati kwa kipindi kirefu sasa na hivyo kubaki kuwa na mapungufu katika utendaji kazi;

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaliomba Bunge lako liazimie kuwa:-

a) Serikali itoe maelezo ya kushindwa kujibu hoja kwa wakati na kutotekeleza maagizo ya Kamati hali inayoongeza mrundikano wa maagizo na hoja zisizo fanyiwa kazi;na

b) Serikali ieleze njia mbadala na hatua ya kuzibana Halmashauri zinazoshindwa kujibu hoja za ukaguzi na kutekeleza maagizo ya Kamati kwa wakati.

### 3.2.6 Kutotenga mchango wa Asilimia Kumi (10%) ya Mapato kutoka vyanzo vya ndani kwa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana na asilimia ishirini (20%) ya ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Vijiji;

**Kwa kuwa** Imedhihirika wazi kuwa uwasilishaji wa michango hii haipewi kipaumbele hali inayosababisha Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana kutojiendesha kwa

tija na kuwa fedha za ruzuku kwa Mamlaka za serikali za mitaa na vijiji haziwasilishwi ili kuziwezesha mamlaka hizo kuwahudumia Wananchi ipasavyo;

**Na kwa kuwa** Hakuna sheria inayohusu mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana. Kadhalika, upelekajii wa fedha katika mamlaka za serikali za mitaa na vijiji kukosa usimamizi na uwajibikaji;

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa:-

a) Serikali iandae Sheria itakayotoa mwongozo wa uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana kama ilivyoazimiwa na Bunge katika Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa mwaka jana;na

b) Kuhakikisha Serikali ina andaa utaratibu madhubuti wa upelekaji wa fedha katika mamlaka ya serikali za mitaa na vijiji moja kwa moja badala ya kuzitegemea Halmashauri ambazo zimeonyesha kushindwa kufanya hivyo.

### 3.2.7 Watumishi kukaimu Nafasi zao kwa zaidi ya miezi sita (6) bila kuthibitishwa;

**Kwa kuwa** Imebainika kuwa idadi kubwa ya Wakuu wa Idara na Vitengo katika Halmashauri wanakaimu nafasi zao kwa kipindi kirefu bila kuthibitishwa na sababu kubwa ikiwa ni mlolongo mrefu wa taratibu za upekuzi;

**Na kwa kuwa** Kuthibitishwa katika nafasi inayokaimiwa ni suala la kisheria na haki ya Mtumishi husika na kwamba kunaongeza hali na uwezo wa kutoa maamuzi ya kiutendaji;

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa:-

a) Serikali ihakikishe inawathibitisha Watumishi wanaokaimu nafasi hizo kwa zaidi ya miezi sita (6), na kuweka mpango wa kuhakikisha tatizo hili linamalizika;

b) Serikali ihakikishe inaweka mkakati wa kuwa hamisha watumishi wale ambao wamekaa kwenye kituo kimoja cha kazi kwa muda mrefu , ili kuondoa hali ya ufanyaji kazi kwa mazoea ;na

c) Ofisi ya Rais TAMISEMI inatakiwa kupanga watumishi kulingana na mahitaji hususani katika Halmashauri mpya na zilizo pembezoni.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukurani;

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukua fursa hii tena kutoa Shukrani zangu za dhati kwako kwa namna ambavyo umekuwa ukitoa Miongozo mbalimbali ya kusaidia ufanisi katika utendaji wa Kamati ya LAAC. Nachukua fursa hii pia kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati yangu kwa kutekeleza vyema na kwa ustadi mkubwa Majukumu yao bila kuchoka. Aidha, Nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano mkubwa walio uonyesha katika kipindi cha Majadiliano baina ya Kamati na Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Ndg. Steven Kagaigai kwa kuteuliwa kuwa Katibu wa Bunge la Tanzania. Namkaribisha na mhakikishia ushirikiano wa kila hali katika kufanikisha utendaji wa Kamati hii na Bunge kwa ujumla. Napenda pia kutoa shukrani zangu kwa Ndg. Athuman Hussein Mkurugenzi wa Kamati za Bunge na Ndg. Michael Chikokoto Mkurugenzi Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge. Aidha, Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Watumishi wote wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Taarifa ya Ukaguzi na ufafanuzi wa kina tulioupata katika kipindi chote cha Mahojiano na Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika,** Nachukua nafasi hii pia kumpongeza Mhe. Suleiman Jafo aliyeteuliwa kuwa Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI na kumshukuru kwa ushirikiano mkubwa

wakati wote wa vikao vya Kamati. Lakini pia, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipo wapongeza Mhe. Josephat Sinkamba Kandege na Mhe. Joseph George Kakunda kwa kuteuliwa kuwa Manaibu Waziri kwenye Ofisi ya Rais TAMISEMI. Kadhalika, nimshukuru Mhandisi Musa Iyombe Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja na watumishi wote katika Ofisi hii, hasa Watumishi kutoka kitengo cha usimamizi na ufuatiliji wa Fedha katika serikali za mitaa kwa ushirikiano wao wakati wote wa shughuli za Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa niaba ya Kamati yangu, nachukua fursa hii kuwapongeza Makatibu wa Kamati hii Ndg. Dismas Muyanja, Ndg. Godfrey Kassanga na Ndg. Victor Mhagama wakisaidiwa na Ndg. Waziri Kizingiti pamoja na Watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano wao wakati wote ambao Kamati yangu iliwahitaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) ambayo leo hii inawasilisha Taarifa hii katika Bunge lako Tukufu, inaundwa na Wajumbe 25 wafuatao:

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Vedasto Edgar Ngombale,Mb | **Mwenyekiti** |
| 2. Mhe. Abdallah Dadi Chikota, Mb | **Makamu Mwenyekiti** |
| 3. Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mb | Mjumbe |
| 4. Mhe. Rose Kamili Sukum, Mb | Mjumbe |
| 5.Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| 6. Mhe. Amina Nassoro Makilagi, Mb | Mjumbe |
| 7. Mhe. Lucy Mayenga, Mb | Mjumbe |
| 8. Mhe. Godfrey William Mgimwa, Mb | Mjumbe |
| 9. Mhe. Nimrod Mkono, Mb | Mjumbe |
| 10. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb | Mjumbe |
| 11. Mhe. Ignas Aloyce Malocha, Mb | Mjumbe |
| 12. Mhe. Aysharose Ndogholi Matembe, Mb | Mjumbe |
| 13.Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb | Mjumbe |
| 14. Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza, Mb | Mjumbe |
| 15. Mhe. Mangungu Ali Issa, Mb | Mjumbe |
| 16. Mhe. Martin Mtonda Msuha, Mb | Mjumbe |
| 17. Mhe. Edward Franz Mwalongo, Mb | Mjumbe |
| 18. Mhe. Alex Raphael Gashaza, Mb | Mjumbe |

| | |
|---|---|
| 19. Mhe. Joseph Roman Selasini, Mb | Mjumbe |
| 20. Mhe. Jackline Ngonyani Msongozi, Mb | Mjumbe |
| 21. Mhe. Richard Philip Mbogo, Mb | Mjumbe |
| 22. Mhe. John Peter Kadutu, Mb | Mjumbe |
| 23. Mhe. Anastazia James Wambura, Mb | Mjumbe |
| 24. Mhe. Mgeni Jadi Kadika, Mb | Mjumbe, na |
| 25. Mhe. Azza Hamad Hillal, Mb | Mjumbe. |

**4.2 Hoja;**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu imebainisha Matatizo Sugu katika Matumizi ya Fedha za Umma katika Halmashauri zetu katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2015/16. Aidha, Kamati imetoa Mapendekezo dhidi ya matatizo hayo kama suluhisho. Kwa maana hiyo sasa, ni Wajibu wa Serikali katika kujipanga vema kutekeleza ushauri huo bila kutegemea usimamizi wa karibu wa Kibunge. Baada ya kufanya uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Ukaguzi, ni rai ya Kamati kwa Halmashauri kujitathmini na kutambua nafasi zao katika ujenzi wa Uchumi na Maendeleo kwa ujumla katika Taifa letu. Ni imani ya Kamati kuwa Halmashauri zetu zitatimiza wajibu wao ipasavyo.

..............................................

Mhe. Vedasto Edgar Ngombale Mwiru, Mb.
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC)**
Februari, 2018

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge sasa tunaingia kwenye mjadala wa pamoja na tutaanza na Mheshimiwa Allan Kiula baadaye Mheshimiwa Munde Tambwe na atafuatiwa na Mheshimiwa Hamidu Bobali. Mheshimiwa Allan Kiula.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nami kuweza kupata nafasi ya kuchangia katika

mawasilisho ambayo yamewasilishwa na Wenyeviti wa Kamati. Ningependa kujikita kwenye wasilisho la Kamati ya *PAC,* yapo mambo ambayo yanabidi yatolewe uamuzi na Bunge ili yajadiliwe kwa kina ili kuweza kuweka mambo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia suala la Mlimani City, Mlimani City limeelezwa kwenye taarifa ya *PAC* na tumeweza kuona ambavyo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hakinufaiki Mkataba wa Mlimani City. Ukisoma kwa kituo, *paragraph* hiyo, utaona jinsi mwekezaji alipokuja na jinsi mtaji wake alivyoutoa na baadaye akatengeneza madeni, akaenda *TIC* akaweza kunufaika na msamaha wa uwekezaji.

Mheshimiwa mwenyekiti, pia tumeona uendelezaji, tulitembelea Mlimani City pale katika maeneo ambayo yanatakiwa yaendelezwe, kimkataba kama walivyokubaliana hayaendelezwi, kuna hoteli ya nyota tatu haijajengwa, lakini pia kuna *botanic garden* haijafanyiwa kazi na ukiangalia kwenye maelezo yao kuna mahali wale watu wanagawana *dividend*, kwa maana kuwa mradi huo una faida, lakini pia hawalipi kodi stahiki kama walivyokubaliana kwenye mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifanya mahojiano na wenzetu wa Chuo Kikuu, ikaonekana wanaendelea na mazungumzo, lakini mazungumzo hayo wanayofanya, eneo lolote lile ambalo, lina manufaa kwa Chuo Kikuu yule mwekezaji, halitaki, isipokuwa anataka maeneo ambayo wao wanaona kwamba wanaweza kunufaika nayo, ndipo hapo mabadiliko yafanyike, wa-*review* ule mkataba, ukiwemo muda wa mkataba ambao ni muda mrefu sana, lakini pia wameendeleza wamefanya *extension* pale, hiyo *extension* iliyofanyika, imefanyika haikuwemo kwenye mkataba na wameendeleza maeneo ambayo wanapata pesa. Kwa hiyo suala zima la Mlimani City, inabidi liangaliwe kwa macho mawili na Bunge hili lazima liazimie, mkataba huo upitiwe upya na *TIC* watoe maelezo ya kutosha ili tuweze kuona chuo kikuu kinanufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo zima la ukopeshaji wa matrekta Suma *JKT*. Bunge lililopita tulizungumza kwamba bado yapo madeni makubwa watu hawajalipa matrekta, kwa hiyo, matrekta yanakuwa kama vile yalitolewa zawadi, Kamati imeshindwa kuona kwamba kwa nini madeni haya hayalipwi. Kama trekta ni rasilimali linafanya kazi, linalima na wengine wanakodisha ina maana watu wote waliokopa matrekta wanatakiwa wayalipe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulizungumza, mwaka mzima sasa umepita hapa, hatuoni juhudi zozote. Kwa hiyo tulishawishi bunge liazimie kwamba hawa Suma JKT na wenyewe ambao hawasimamii ukusanyaji wa madeni waweze kuchukuliwa hatua na pesa za Serikali zisipotee. Hilo ni jambo muhimu sana kwa sababu uzoefu unaonesha kwamba mali ya umma inapotea hivi hivi kienyeji, lakini hiyo ni pesa ya Serikali na ni pesa ambayo inatakiwa irudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia iliweza kupitia, utendaji kazi katika mashirika mbalimbali na Wizara mbalimbali. Ukiangalia ukurasa wa 25 wa kitabu cha wasilisho la *PAC* kipengele 2.2.6 ambacho kinazungumza ununuzi wa magari ya polisi yenye thamani ya dola za Marekani milioni 29. Jambo hili lina lenyewe lina utata mkubwa sana na utata wake ni kwamba pamoja na nia njema ya jeshi la polisi, lakini mkataba huo hauna maelezo yakinifu kuonesha kwamba uliingiwaje, ulifanyikaje na huo mkataba utamalizika lini, yaani hayo magari mengine, yatakuja lini. Kwa sababu ukisoma pale utaona idadi ya magari yaliyoletwa ni kidogo kulingana na yaliyohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mkataba huo wa E*xim* Bank ya India ambao uliingia ulifikia mahali ukawa ume-*expire,* hiyo *credit facility* ikawa ikawa ime-*expire* kabla ya utekelezaji wake kukamilika. Kwa hiyo sisi tunahoji tija ya mkataba huo na namna ulivyoingia na tunashauri kwamba lazima lifanyike jambo kubwa au maamuzi mazito kuhakikisha kwamba mkataba huo unakamilika na pesa za Serikali kuna mahali zilitolewa dola milioni 10 kama *advance* zijulikane ziko

wapi. Kwa maana hiyo sisi tunaishauri Bunge tuweke azimio kuwe na *reviw due deligency* ya jambo hilo lote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ukienda ukurasa 21, suala la *TANESCO, TANESCO* inawadai watu wengi madeni. Mashirika mengi yanadaiwa, tulizungumza tena hili jambo lishazungumzwa na linarudi tena kuzungumzwa na *TANESCO* hawa, wanaonekana wanahangaika sana lakini pesa ziko kwa wateja, sasa tunashindwa kuelewa kwamba tatizo ni nini na kwa nini hatua hazichukuliwi. Kamati ilipata mashaka sana, nami napata mashaka sana, kwa sababu mashirika mengi ofisi nyingi zinahamia Dodoma Makao Makuu na madeni yako Dar es Salaam, sasa wanahamia Makao Makuu huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaona ule msukumo wa kulipa madeni utakuwa ni mdogo, pamoja na kwamba, Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli alisema kama ni umeme kata sasa watakatiwa Dar es Salaam wanakuja kuanzia maisha huku upya, sasa jambo hilo na lenyewe inabidi liangaliwe ili liweze kuwa kuwa na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba, jana tumepitisha hapa Sheria ya kuunganisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, lakini ukiangalia ukurasa wa 20 utaona madeni ambayo Serikali inadaiwa na mifuko ya jamii. Jambo hilo ni muhimu kwa afya ya Mifuko. Kwa hiyo, bado tunalishawishi Bunge liazimie kuona kwamba Serikali inalipa hayo madeni kikamilifu. Ukiona hilo jedwali linaonesha Mifuko na madeni na kiasi kinachodaiwa. Kwa hiyo, tunashawishi jambo hilo lifanyike kwa nguvu zote na Bunge liazimie kuona kwamba madeni haya yanalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Mifuko hii wanasema ifanyiwe *actuarial valuation,* inakwisha sijui mwaka gani, yaani maisha yake bado inaonesha yana uhai, lakini Kamati inapata mashaka kama pesa hizi bado ziko Serikalini, sasa hata hiyo *actuarial valuation* inakuwa pia ina mashaka kidogo. Kwa hiyo, tunalishauri Bunge lione umuhimu lione umuhimu wa kuhakikisha kwamba madeni yanalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda ukurasa wa 37 umiliki wa taasisi ya ukuzaji maendeleo *Pride Tanzania Limited,* hapa Kamati kwa kauli moja inasema tu *Pride Tanzania,* irudi Serikalini kwa sababu ndiyo iliyotoa mtaji mkubwa, lakini baadaye ikahamishwa inaendeleshwa na utaratibu na watu wengine. Kwa hiyo, tunasema *pride* irudi kwa sababu mtaji ulitoka Serikalini. Kwa hiyo, tunaomba Bunge na Wabunge wenzetu tutakapofika kwenye maazimio, tuone umuhimu wa *pride* kurudi Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho katika kuchangia leo nataka nizungumze kidogo kuhusu bandari, na *TRA* uhusiano wake wa kutokurejeshwa kwa mapato ya *wharfage.* Jambo hilo ni muhimu sana kwa sababu bandari zetu zinaendelezwa kwa hizo pesa, ambazo pesa hizo kimsingi zinakusanywa na *TRA,* lakini tunatambua kwamba *TRA* ni wakala tu na pesa zinakwenda moja Benki Kuu, Hazina wanatakiwa warudishe hizo pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tungependa labda Waziri mhusika atakapojibu hoja aseme kwamba kwa nini pesa hizi hazirudishwi, kwa sababu tunatambua kwamba kuna pesa nyingi hazijarudishwa ambazo zingetumika kwa maendeleo ya bandari zetu.

Mhemishiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na naomba Bunge likisoma maazimio tuyapokee maazimio yote kwa pamoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Allan. Tunaendelea na Mheshimiwa Munde Tambwe na baadaye Mheshimiwa Hamidu Bobali na Mheshimiwa George Lubeleje, wajiandae.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii niweze kuchangia hotuba ya *CAG* na *PAC* na hotuba ya *LAAC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kuipongeza ofisi ya *CAG* kazi nzuri walioifanya, lakini niipongeze Kamati

yangu ya *PAC* kwa kazi kubwa walioifanya katika kupitia vitu hivi. Nianze moja kwa moja na mambo ya TANESCO, kwa sababu nchi yetu iko kwenye Sera ya Viwanda, hatuwezi kuwa na viwanda bila kuwa na umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi za Serikali zinadaiwa pesa nyingi, ukiangalia ukurasa wa 21 mwaka 2016 tulikuwa tunadaiwa shilingi bilioni mia moja ishirini na tisa. Kufikia sasa ukiangalia ukurasa wa 22 tunadaiwa shilingi bilioni mia moja themanini na tisa. Niiombe sasa Ofisi ya ya Waziri wa Fedha, Hazina, ifanye mkakati wa makusudi mazima, kuzikata fedha taasisi hizi zinazodaiwa, kutokana na bajeti zao za umeme kila wanapoleta bajeti zao, huwa kuna bajeti za umeme, tunaomba bajeti hizi za umeme zikatwe moja kwa moja na zipelekwe *TANESCO* ili tuweze kuwa na umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linawezekana, *Local Government* walikuwa wanakatwa hela za *LAPF*, hazipelekwi kwenye mifuko yao, lakini Serikali ikaamua kukata moja kwa moja kupitia Hazina na kupeleka kwenye mifuko yao na sasa hivi pesa zinakwenda. Tunaomba sasa kwa umuhimu wa *TANESCO,* ili tuweze kuenda na sera ya viwanda, Serikali ikate pesa hizo za Taasisi moja kwa moja na kuzipeleka kwenye sehemu husika ambayo ni *TANESCO*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumuunge mkono mkono Rais katika suala hili la umeme, Rais amehangaika sana, kwanza kabisa, ameanza kuvunja mikataba mibovu ya umeme, amevunja mikataba ya *Symbion*, lakini, amevunja mkataba mkubwa wa kifisadi wa *IPTL* ambao ulikuwa unachukua karibu milioni thelathini, kila mwezi, kuwapa kununua mafuta mazito ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais anafanya kazi sana, anastahili pongezi na anastahili kuungwa mkono kwa vitendo. Niwaombe sana Hazina wahakikishe fedha hizi zinarudi *TANESCO* kupitia Taasisi zinazohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, ameweka nguvu kubwa Kinyerezi *one (*I), lakini ameweka nguvu kubwa

Kinyerezi II. Yote hiyo ni kuhakikisha umeme unapatikana. Kuna watu waliokuwa na wasiwasi sana na *Stieglers Gorge*, kwamba haiwezi kufanikiwa, lakini kwa jambo la kushangaza Mheshimiwa Rais na Serikali yake wameshatangaza tenda, kwa ajili ya kujenga huo mgodi wa umeme na umeme huo nadhani muda sio mrefu mwaka 2021 tutaanza kupata *megawatts* 2000 kutoka huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Mheshimiwa Rais anapojituma niwaombe Mawaziri wanaohusika nao wajitume, tuone tunamuunga mkono kiasi gani, ili kupata umeme wa kutosha na viwanda vyetu tunavyovijenga kwa kasi viweze kufanya kazi kutokana na umeme huo tutakaoupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nampongeza sana Mheshimiwa Rais na nimwambie tu kwamba hizi ni *legacy* anazoziacha, hatutakaa tumsahau kwa kazi kubwa anazozifanya na ataweza tu, ameweza *standard gauge*, barabara, *Flyovers,* ameweza elimu bure, naamini ataweza na *Stieglers Gorge* itajengwa na itatoa umeme na watu tutafaidika*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa nikachangie kuhusu *NSSF, k*wanza nianze kupongeza, miradi mizuri ya majengo ya *NSSF,* mradi mzuri wa Twangoma tumeenda kukagua zile nyumba ni nzuri, tumekagua nyumba za Kijichi ni nzuri, lakini naamini na nyumba za Dege zitakapokwisha zitakuwa nzuri. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ahsante.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munde taarifa, Mheshimiwa Sophia Taarifa!

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:**Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji anayeongea, kwanza, namshukuru anavyomshukuru Rais

wake wa sasa lakini yeye alikuwa Mjumbe wa Bodi kwa Rais aliyepita. Kwa hiyo tunafikiri Rais wa sasa anasaidia kunyoosha wale waliofanya vibaya akiwemo na yeye Mjumbe wa Bodi ya *TANESCO* kwa Serikali iliyopita. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munde.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti kwanza naomba unitunzie muda, lakini nisimlaumu sana Mheshimiwa Sophia ni njuka, haelewi chochote, sijawahi kuwa Mjumbe wa Bodi ya *TANESCO*. Kama ana uhakika alete uthibitisho Bungeni kwamba niliwahi kuwa Mjumbe wa Bodi ya *TANESCO,* mwambie atulie, huo unjuka usimsumbue sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kuendelea. *NSSF,* ina mradi wa Dege ambao tumeenda kuutembelea mradi ule umechukua pesa nyingi za umma karibu bilioni mia mbili na *point*. Tunaiomba sana Serikali aidha iongeze mbia mwingine mradi ule uishe au itumie mbinu mbadala yoyote kuhakikisha mradi ule unakwisha ili mradi ule ufanye kazi pesa za umma zirejee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiombe pia Serikali, miundombinu ya barabara ya kwenda Kijichi na Tuangoma, kwa kweli hairidhishi hata mtu anakwenda kupanga akianza kupelekwa anaweza kuona huko anapokwenda hapafai. Kwa hiyo, tunaomba sana mradi wa miundo ya barabara itengenezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii Watanzania hizi nyumba za *NSSF*, zinakopesheka, kwa sababu ukienda leo kununua nyumba ya milioni themanini, unaambiwa ulipe asilimia 10. Ukilipa asilimia 10 zinazobaki zinagawiwa kwa miaka 15. Unaingia ndani na unalipa polepole, tofauti na mashirika mengine unatakiwa ulipe hela *cash* ndiyo uingie ndani. Aidha, ukakope Benki na Benki tunajua kwamba watu wengi hawakopesheki hasa sisi wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawapongeza sana *NSSF* kwa kazi nzuri wanaifanya. Napongeza pia uongozi mpya kwa Mkurugenzi wa *NSSF*, naye ni Mkurugenzi mzuri sana anajitahidi tunamwombea kila la kheri aweze kupata mwekezaji mwingine amalizane na huu mradi uliopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongee sasa kuhusu Mlimani City, ulipata bahati ya kwenda kutembelea mradi wa Mlimani City, kwa kweli tunaomba Serikali ifuatilie mradi huu kwa makini zaidi. Inasikitisha sana mkataba huu ni mbovu kupita kiasi, watu hawa kwenye mkataba walikubaliana walipe 10 *percent ya gross* ya mapato ya Milimani City, lakini mpaka leo hii, watu wao wanalipa *net* ya *ten percent* sio *gross.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipouliza Mlimani City Uongozi wa Chuo cha *UDSM* kwa nini watu wao hawalipwi *gross* wanalipwa *net*, wanasema mgogoro unaendelea. Sasa hivi wana miaka 13, ni jambo la kushangaza kusikia bado mgogoro unaendelea, haujatatuka kwa maiaka 13, tunamnufaisha mwekezaji ambaye alikuja bila mtaji na dola 75 kama shilingi laki moja na nusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuamini, sasa hivi pale Dar es Salaam wameanzisha Milimani City mradi wa *parking* za magari, hakuna mfumo wowote, unawaonyesha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwamba *parking* zile zinaingiza shilingi ngapi kwa siku, kwa wiki, wala kwa mwezi. Ni mwekezaji anakuja ku-*declare* kwamba kwa mwezi huu, nimeingiza milioni tatu wanakubali bila kujua chochote, ni vitu vinasikitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti kuna ukumbi pale Mlimani City, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hawajui ukiwauliza ukumbi ule unaingiza shilingi ngapi kwa mwezi au kwa wiki, ni mwekezaji anakuja ku-*declare*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkaguzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, haruhusiwi kwenda kukagua Mlimani City, anakatiliwa na mwekezaji, hivi ni vitu ambayo nimwombe

sana Waziri wa Fedha, aunde Tume ya haraka iwezekanavyo na Waziri Mkuu, wakakague upya ule mradi ufanyiwe uchunguzi wa kina. Mtu huyu amepewa mkataba wa miaka 85, inatia shaka. Niiombe sana Serikali yangu ifanye pale kazi mpya iende ikaague, tukae tena mezani Mkataba ufumuliwe na uwekwe mkataba vizuri. Kuna vitu vinasikitisha sana huwezi kuona majengo yote haya yale hatuingizi pesa yoyote kwenye Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo kuhusu *Pride*, kwa sababu ni mama, sisi akinamama ndiyo tunaokopa *Pride* ni jambo linalosikitisha sana kuona kwamba kuna watu wamezihodhi pesa za *Pride,* niiombe Serikali sasa ichukue hatua za makusudi mazima kuhakikisha wale wote waliohusika kwenye masuala mazima ya *Pride*, wanachukuliwa hatua za kisheria. Tunaamini Serikali ya Awamu ya Tano ina uwezo huo mkubwa na tunaamini watajulikana na pesa zetu zitapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Munde. Tunaendelea na Mheshimiwa Hamidu Bobali na baadaye Mheshimiwa George Lubeleje ajiandae.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kwa mwaka huu naomba niwatakie Waheshimiwa wote heri ya mwaka mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na suala la Halmashauri na Uongozi kwenye halmashauri na kikubwa nitaomba, usikivu wa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, kwamba kama kuna changamoto kubwa ambazo taarifa ya Kamati imeziainisha, kukusanya mapato madogo, kutopeleka fedha za asilimia 10 na mengine. Changamoto kubwa tuliyonayo ni aina ya Wakurugenzi tulionao kwenye Halmashauri zetu. Uwezo na utendaji kazi wa Wakurugenzi wa nchi hii kwa sasa ni kikwazo kikubwa sana kwa maendeleo ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kama utaamua kufanya *assessment* ya kupima *performance* ya Wakurugenzi wako ni sehemu kubwa ya watu wanaokuangusha wewe na wanaoingusha Serikali kwa sababu ya uwezo wao. Hii imetokana na namna walivyopatikana, kama ingekuwa Wakurugenzi walipatikana kwenye mfumo ule wa kawaida wa Watumishi wa Umma huu upungufu mwingine usingekuwepo leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo ambalo nataka niliseme kama kuna jambo ambalo nilifikiria ningeliona kwenye taarifa ya Kamati na hii ni *challenge* kwa Kamati *ya LAAC* kwamba Kamati ingekuja na mapendekezo ya kushauri Bunge, liishauri Serikali namna ya upatikanaji wa Wakurugenzi, Wakurugenzi walioteuliwa na Mheshimiwa Rais wengi uwezo wao wa ufanyaji kazi ni mdogo hauendani na majukumu yaliyopo kwenye Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda ukamhoji Mkurugenzi namna anavyofanya kazi wewe mwenyewe unajiuliza kwamba huyu hivi tangu lini amekuwa Mtumishi wa Umma. Huko kwenye Halmashauri kuna migogoro mikubwa kati ya Wakurugenzi na Wakuu wa Idara kwa sababu Wakuu wa Idara wana-*perform* vizuri kuliko Wakurugenzi. Haya wote mnayashuhudia kama Waheshimiwa Wabunge mnashiriki kwenye vikao vya Halmashauri vya Madiwani kwenye Mabaraza kule wote mtakuwa mashahidi. Aina ya Wakurugenzi wetu ni wana-*perform* vibaya mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulitakiwa tuanzie hapa, siku moja nilipokuwa namsikia Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI anasema tutajenga viwanda 100 kwenye kila Mkoa nilikuwa najiuliza kwamba hao watu wenyewe wa kusimamia wako wapi. Yaani jambo moja ambalo lili-*click* kwenye kichwa changu hao watu wenyewe wa kusimamia wako wapi. Pale kwangu kuna watu wametaka kuja kuanzisha viwanda tangu mwaka jana mwezi wa Tisa mpaka leo kupewa ardhi tu ile watu watatu, wanataka kuja kuanzisha viwanda vya kuchakata muhogo mpaka leo watu watatu Mkurugenzi ukimuuliza anasema sijui kitu gani hakijakamilika

najua ni kwa sababu ya *performance* uwezo walionao ni mdogo kweli. Hilo jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu suala la miradi ya maji hususani ile ya vijiji 10 kwenye kila Halmashauri pamoja na miradi ya umwagiliaji. Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kama kuna jambo ambalo nchi hii Serikali imepata hasara kubwa ni kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji kwenye Halmashauri na nafikiri *more than 70%* ya ile miundombinu sasa haifanyi kazi. Kamati ilitakiwa ije na ripoti ituambie kila halmashauri ni halmashauri gani angalau imefikia *50%* hakuna, angalau kama kuna miradi ilianzishwa vijiji 10 ya maji ambayo imeweza kuitekelezeka kwa asilimia 50 kwenye Halmashauri hakuna. Huu ni uthibitisho kwamba kuna fedha zimetumika vibaya na kuna fedha zililiwa vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni la msingi sana kwenye Halmashauri na hili nilivyokuwa nalifikiria nikaona kwamba, kama kuna uwezekano labda wale Wakuu wa Idara ya Maji labda waondoke kuwa *monitored* na TAMISEMI ili wawe moja kwa moja kwenye Wizara ya Maji ama watoke Wizara ya Maji waende moja kwa moja TAMISEMI. Hapa naona kuna-*contradiction* namna mnavyofanya kazi, inawezekana namna ya upelekaji wa maagizo yanakwenda yanawachanga wale watu, kwamba Wizara ya Maji wanaweza kusema hivi TAMISEMI ikasema, ikapelekea kukawa na shida kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, naamini kuna miradi mingi ya maji ilianzishwa tena kwa lengo jema na Serikali kule kwenye halmashauri miradi ile haifanyi kazi. Halafu hakuna *continuation* hakuna mwendelezo leo unaweza ukakuta limeanzishwa hili kesho lile halijakamilika linaenda kuanzishwa lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mradi pale ulijengwa na TAMISEMI tena lambo la kunyweshea mifugo, ulijengwa uligharimu karibu milioni mia mbili haujakamilika, haufanyi kazi tumeenda mwaka huu kwenye bajeti ya halmashauri

unaenda kuanzishwa tena mradi mwingine ambapo hata huu wa kwanza haujakamilika. Sijui kama TAMISEMI wanajua, sijui hiyo Wizara yenyewe ya Mifugo inajua kwa sababu naona kama mambo yanajichanganya changanya tu. Hilo jambo lingine ambalo ni la msingi sana nilitaka nilizungumzie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu katika ukurasa wa 65 wa kitabu cha *LAAC* Kamati inaomba Bunge kuazimia kuunda Kamati Maalum ya Bunge itakayochunguza sababu na chanzo cha tatizo la miradi ya maji kutotekelezwa. Ndiyo hili nilikuwa nalisema kwamba, kama Bunge litaona inafaa naunga mkono hoja hii kwamba Bunge liunde Kamati ipitie kwenye kila Halmashauri, ikachunguze ni miradi mingapi ya maji ilianzishwa ile ya vijiji 10 pamoja na umwagiliaji iliyoanzishwa na TAMISEMI, tuone mingapi inafanya kazi na mingapi haifanyi kazi. Katika hii tutagundua madudu mengi kweli kweli kwa sababu Halmashauri nyingi hazijatekeleza vizuri hili suala. Kwa hiyo, naomba niunge mkono hili suala la kuunda Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Halmashauri kutokupewa pesa kwa wakati, wakati mwingine haya yote tunayasema kwamba Wakurugenzi hawafanyi kazi, uwezo wao mdogo ni kweli, lakini jambo lingine kwamba hizo fedha zenyewe za kufanyia kazi wanazipata wapi. Unakwenda kwenye halmashauri leo mwezi huu tupo karibu kwenye *quarter* ya tatu unakuta fedha za *development* kutoka kwenye Serikali Kuu labda wamepata asilimia 15, asilimia 20 unajiuliza sasa huyu Mkurugenzi hapa anafanya kazi gani kwa sababu upatikanaji wa fedha kutoka Serikali Kuu ni kikwazo na Mheshimiwa Waziri wa Fedha bahati yupo hapa alieleze Bunge tatizo ni nini. Leo kwenye Halmashauri tunapitisha bajeti kwa ajili ya Mwaka wa Fedha 2018/2019, fedha za mwaka 2017/2018 hazipo, fedha za maendeleo hazipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine linalokwamisha maendeleo kwenye Halmashauri zetu ni Serikali Kuu kutopeleka fedha kwenye halmashauri zetu.

Jambo hili ni hatari linaua moja kwa moja Halmashauri ya Wilaya. Leo tunalaumu fedha za asilimia 10 haziendi, halmashauri inapewa maagizo ya kutumia fedha hizi za ndani kwenye kuajiri watumishi. Nimesikia hapa leo mmoja wa Waziri anajibu kwamba halmashauri itumie fedha za ndani kuajiri watumishi. Fedha hizi ambazo zingepaswa kupelekwa kule kwa vijana zile asilimia 10 kwa wanawake na walemavu, leo Waziri anakuja kusimama anatolea agizo waajiri watumishi

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo lingine ambalo linakwamisha ni suala la fedha kutoka Serikalini ziende kwenye halmashauri na jambo hili pia linapelekea halmashauri kuwa na mzigo mkubwa kwa sababu hata yale mapato yetu ya ndani ambayo asilimia 60 tumepanga kupeleka kwenye maendeleo, tunaondosha tunapeleka kwenye maeneo ambayo yalipaswa yagharamiwe na fedha za Serikali Kuu. Kwa hiyo, hili ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nilimalizie ni kuhusu suala la Halmashauri kukosa mapato ya ndani kadri tulivyopanga. Unakuta tumepanga tukusanye labda milioni 300 kutoka kwenye mazao ya wakulima kwa mfano mbaazi. Halmashauri yetu sisi ambayo mbaazi ni chanzo kikubwa cha mapato tunashindwa kukusanya ule ushuru kwa sababu mbaazi imekosa soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama kuna jambo ambalo lingine ni la msingi sana ni Serikali kujielekeza katika kutafuta masoko ya mazao ya wakulima kwa sababu mazao yakikosa soko halmashauri hazipati pesa za kujiendesha. Kwa hiyo, leo mbaazi inauzwa mpaka Sh.150, Sh.200 halmashauri hii itatoza ushuru wa shilingi ngapi kwa mkulima ili ipate mapato yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo la Serikali kutafuta masoko sio jambo la blaa blaa linalohitaji majibu mepesi ni jambo la lazima kwa sababu Serikali ipo kwa ajili ya wananchi na wananchi lazima watafutiwe masoko na Serikali iwahudumie wananchi wake, lisiwe jambo sasa la kuja

hapa fulani amesema hivi, hili Lindi hawataki, tunahitaji majibu ya kweli kwamba mtu akilima mbaazi zake apate soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bobali. Tunaendelea na Mheshimiwa Lubeleje na baadaye Mheshimiwa Catherine Ruge ajiandae.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja hii ya Kamati hizi mbili. Kwanza nizipongeze sana hizi Kamati mbili kwa kazi nzuri wanazozifanya lakini tatizo lipo, hawapewi fedha za kwenda kukagua miradi, wanakagua makaratasi tu. Sasa bila kwenda kuona miradi ile *value for money* kwa kweli inakuwa ni kazi bure tu. Unaweza kukuta shule imejengwa lakini kama haikukaguliwa madirisha mabovu, kuna nyufa na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuchelewa kwa fedha za miradi ya maendeleo. Bunge kama Bunge sisi ndio tunaopitisha bajeti hapa. Bajeti za Halmashauri za Wilaya pamoja na bajeti ya Serikali Kuu, lakini jambo la kusikitisha fedha hazifiki kwa wakati. Hakuna Halmashauri hata moja hapa ambayo imeshapata fedha za ruzuku zaidi ya asilimia 40 hakuna. Sasa nauliza huko Hazina kuna nini, kama *TRA* wanakusanya kila mwezi hela za kutosha kwa nini fedha hizi zisipelekwe Wilayani. *(Makofi)*

Mheshiniwa Mwenyekiti, miradi ya maji kuchelewa, nina masikitiko makubwa sana kuna visima sita vimechimbwa Wilaya ya Mpwapwa tangu Agosti, 2016, lakini mpaka leo hakuna *pump*, hakuna bomba wala hakuna nini. Kwa hiyo, visima vile vimechimbwa vimekuwa kama ni *white elephant* wananchi wanaangalia tu. Sasa namshukuru sana Waziri wa TAMISEMI, MheshimiwaJafo anajitahidi sana kutembelea miradi hii, tulifika naye Kijiji cha Mima akaona huu mradi maji, akaona ujenzi wa kituo cha afya kinavyoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mawaziri mtembelee miradi hii, bila kutembelea ndugu zangu, msikae maofisini mkadhani kwamba miradi inakwenda vizuri, kumbe miradi imekwama. Hata hivyo, awamu hii niwapongeze Mawaziri wanajitahidi kutembelea miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri nyingi zilikuwa zinapata hati chafu, lakini baada ya kuunda hii Kamati ya *LAAC* imefanya kazi nzuri sana, sasa hivi ukifanya utafiti ni Halmashauri chache tu wanapata hati chafu, kwa hiyo, niwashukururu sana lakini kama nilivyosema wapewe fedha kwa ajili ya kwenda kuona ile miradi *value for money* sio kukagua makaratasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kodi ya majengo bado tunasistiza sisi Wabunge kodi ya majengo irudishwe kwenye halmashauri zenyewe sasa kodi ya majengo (*property tax)* wanakusanya *TRA* ni kweli wanakusanya lakini wanakusanya mwaka mzima ndiyo waanze kugawa kwenye Halmashauri miradi hiyo si imekwama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri zilikuwa zinakusanya *property tax* kila *quarterly* wanaanza kutumia zile fedha. Kwa hiyo, nashauri kwamba kwa sababu ni chanzo kimojawapo cha mapato ya halmashauri kwa sababu halmashauri nyingi hazina vyanzo vya mapato kwa hiyo kodi ya majengo ndio kilikuwa chanzo kimojawapo. Kwa hiyo, ombi langu chanzo hiki cha mapato kirudishwe Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watumishi kukaimu muda mrefu katika Halmashauri; ni kweli wanakaimu muda mrefu sana. Ukienda kila Halmashauri ukimuliza huyu, mimi ni Afisa Elimu Kaimu, mimi ni Mhandisi wa Maji Kaimu, mimi sijui nani Kaimu. Sasa nashauri Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kama hawa watu wana ujuzi wa kutosha wana-*qualification* za kupandishwa vyeo kwa nini wasithibitishwe kushika nafasi hizo. Waendelee kukaimu miaka miwili, miaka mitatu hapana. Kwa hiyo, wasikaimu muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro kati ya Madiwani na Watendaji wa Halmashauri; bahati nzuri nilikuwa Diwani, Mwenyekiti wa Halmashauri na Mbunge nimejifunza mambo mengi sana. Sisi ndiyo tumeanzisha Halmashauri ya Wilaya mwaka 1984, kulikuwa na matatizo makubwa sana, lakini sasa yanaanza kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, semina au mafunzo kwa Madiwani ni muhimu. Sisi tulikuwa tunakwenda mafunzo Hombolo tunapewa mafunzo ili kupunguza migogoro kati ya Watendaji na Madiwani. Utakuta Madiwani wanamkataa Mkurugenzi inawezekana hakuna sababu zozote za msingi au Madiwani kuingilia utendaji, hilo nalo ni tatizo, lakini Madiwani wakipewa mafunzo nina hakika kabisa hii migogoro itapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache naunga mkono hoja hizi zote mbili za Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* pamoja na Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lubeleje. Tunaendelea na Mheshimiwa Catherine Ruge.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia hoja zilizopo mbele yetu. Nitajikita kwenye taarifa ya Kamati ya *PAC* ambayo ni mjumbe. Kwanza kabisa nitumie fursa hii kuipongeza Kamati ya *PAC* kwa taarifa nzuri, lakini nimpongeze Mwenyekiti wangu mama Kaboyoka kwa uongozi wake na ujasiri mkubwa aliouonesha wakati wa kipindi chote cha kuongoza na kuandaa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nitaomba kujikita kwenye maeneo machache katika taarifa hii *PAC*. Kwa kuanza nitaomba kuchangia kwenye mradi wa *Mlimani City* na kabla sijaanza kuchangia naomba ku-*declare interest kwamba* nilisoma Chuo Kikuu cha *Dar es*

*Salaam, Focus of Commerce* ambayo sasa *UDBS (University of Dar es Salaam Business School)* nilipata *degee ya Accounts, Bachelor of Commerce in Accounting.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *Mlimani City* una maajabu, una maajabu mengi lakini naomba nizungumzie maajabu saba ya Mradi wa *Mlimani City*. Ajabu namba moja mtaji ambao uliowekezwa kwenye mradi huu wa *Mlimani City*. Tangu mradi huu umeanzishwa Mwekezaji ameweza ku-*issue shares* 100 tu kati ya *shares* 1,000 ambazo ziko *authorized* kwenye mtaji wa hiyo kampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *share* hiyo kwa miaka hiyo iliuzwa Dola 0.75, kwa hiyo mtaji mzima wa *Mlimani City* ulikuwa ni Dola 75 kwa sasa hivi ni 150,000 au 160,000 sikumbuki *by then 2004 exchange rate* ilikuwa ngapi ambao mnakumbuka mnaweza mka-*calculate* na mkajua ni kwa kiasi gani mradi mkubwa kama wa *Mlimani City* uliweza kuwekezwa kwa mtaji kiasi kidogo namna hiyo. Mpaka leo zaidi ya miaka 10 *share* 900 kwenye kampuni hiyo bado hazijauzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajabu namba mbili, ni mbia mwenye *share* moja anaitwa *Transtor,* huu mradi una Wabia wawili *Highland View* na *Transtor* ameweza kukopesha Kampuni ya *Mlimani City* dola za Kimarekani 40,000 wakati yeye ana *share* moja badala ya kuwekeza kwenye ile Kampuni kwa kununua zile *share* ambazo mpaka leo hazijauzwa tangu kampuni hiyo imeanzishwa ambayo ina *share* 900 mpaka sasa hivi haziko *issued*. Hiyo ni ajabu namba mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini unajiuliza ni sababu gani labda ameamua kukopesha badala ya kununua *shares*. Wahasibu wenzangu sababu ni mbili tu. Sababu ya kwanza ni yeye kuendelea kupata riba au *interest income* kutokana na pesa anayoikopesha *Mlimani City*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili kwa sababu *interest expense* inapunguza faida kabla ya kupata *net*

*income,* kwa hiyo *automatically* faida ya *Mlimani City* inapungua na mwishoni kabisa na pesa inayolipwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazo hesabu za Mlimani *City Holdings* hapa zinaonesha kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 mwaka mmoja tu *financial charges* kwa maana *interest expenses* zilikuwa 1.9 Milioni US *Dollars*, kwa maana hiyo kwa mwaka mmoja tu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimepoteza mapato karibu Dola za Kimarekani Milioni 2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajabu namba tatu ya mradi huu wa Mlimani *City*, ni uwiano uliopo kati ya gawio la faida na *rental income* au kodi ya pango ambayo wanalipwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Yaani haya ni maajabu na yanaweza kutokea Tanzania tu. Ukiangalia mapato ambayo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeanza kulipwa kuanzia Mwaka 2006 mpaka Mwaka 2017, wamelipwa Dola za Kimarekani Milioni 7.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hawa Wabia, *actually* Mbia ni mmoja kwa sababu ana *shares* 99 na ile moja unaweza ukairudisha ni *redeemable anytime* unaweza ukai-*redeem* kurudi kwenye Kampuni. Kwa hiyo, Mbia ni mmoja, huyu Mbia ameweza kujilipa *dividend* au gawio la faida la 3.8 milion *dollars*. Hiyo ni nusu ya pesa iliyolipwa kwa Mlimani *City* kama *Rental Income* au Kodi ya Pango kwa miaka, kuanzia Mwaka 2006 mpaka leo; miaka 11. *It's can only happening in* Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajabu namba nne, ya Mkataba huu wa Mlimani *City* na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni kukiukwa kwa masharti ya Mkataba kwa zaidi ya miaka 10 na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimekaa kimya. Kinachonishangaza ni kwamba hiki Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ndiyo kinazalisha Wanasheria wabobezi, wakiwepo baba yangu Profesa Kabudi, dada yangu Dkt. Tulia, lakini hawakuuona huu upungufu wote mkubwa uliopo kwenye mradi mpaka CAG alivyoenda kufanya *Special Audit* mwaka

jana mwezi wa Nne na akaibua hiyo hoja na wao kuanzia mwezi wa Tano wakaanza kumwandikia mwekezaji kuwa anakiuka masharti. Hiyo ni ajabu namba nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajabu tano, Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba Makamu Mkuu wa Chuo kwa kipindi chote, tunajua nani walikuwa Makamu Mkuu wa Chuo miaka hiyo kuanzia Mkataba umesainiwa mpaka leo. Walikuwa ni sehemu ya bodi kwa maana ni *Board Members,* ukianza na Profesa Luhanga, Rwekaza Mkandala sasa hivi baada ya Rwekaza kuondoka ameingia Profesa mwingine wote hao ni Maprofesa. Profesa Muhanga, Profesa Mfinanga ameingia sasa hivi ndiyo *Board Member* amem-*replace* Mkandala, ana miezi kama miwili au mitatu, walikuwa wanaingia kwenye Bodi ya Mlimani *City Holding*. Kwa maana hiyo walikuwa ni sehemu ya maamuzi ya Mlimani *City Holdings*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huwa najiuliza, hivi hawa Maprofesa wetu, macho yao yalikuwa yameingia michanga au ni nini, mpaka wanaangalia haya maamuzi ambayo hayana tija kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajabu namba sita...

**MJUMBE FULANI:** Tema mtoto tema.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ajabu namba sita, ni *going concern* ya hii Kampuni ya Milimani *City* au kuendelea kuwepo kwenye kwa biashara kwa hii Kampuni kwa miezi 12 ijayo au mwaka mzima. *Going concern* au kuendelea kuwepo kwa biashara kwa Mlimani *City Holding* kunategemea na ipo kwenye ripoti, ipo kwenye *financial statement* za Mlimani *City Holding,* inategemea na uwezo wa *shareholders* kuendelea kuweka pesa. *Willingness* ya *Shareholders* kuweka pesa kwenye huo mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mkubwa kama huu unategemea jinsi gani mwanahisa atajisikia kuweka pesa kwenye mradi. Kwa hiyo, akiamka hajisikii ina maana huo

mradi utakufa, kwa hiyo, *we are not sure* hatuna uhakika wa kuwepo kwa hii Kampuni ya Mlimani *City* kwa miezi 12 ijayo hilo ni ajabu lingine la sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajabu la saba na la mwisho, yapo mengi lakini nimechukua haya makuu ambayo naomba Serikali mkayafanyie kazi.

**MJUMBE FULANI:** Endelea, endelea!

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ajabu la saba, ni huyu mwekezaji ambaye ni Mbotswana, mwenye asili ya Kihindi anaishi Afrika Kusini. Mwekezaji huyu tangu ameanza huu mradi hajawahi kuonekana *in physical.* Sasa sijui ni mzimu au huyu mwekezaji sijui ni nini, yaani unawekeza pesa zote hizo, unakopesha *almost 100 billion* maana 49 milioni *dollars* ni zaidi ya bilioni 100, lakini huoni umuhimu wa kuja *in physical* kufanya *negotiation* unawatuma wawakilishi, hajawahi kuonekana. Hilo ni ajabu la saba, *it can only happening in Tanzania*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naona Serikali ya CCM ime-*fail* kusimamia miradi, tunaanzisha miradi mizuri lakini tunashindwa kusimamia. Imeshindwa kufanya *oversight* na *monitoring* na mwisho wa siku tumeishia kuvunja Mikataba na kupata hasara kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe Serikali badala ya tukishasaini tu mnaiacha Mikataba, mnaiacha hamuangalii *implementation,* ni bora tuache kusaini hii mikataba kuliko kuendelea kupoteza pesa za umma, pesa za walipa kodi maskini na kuacha pesa hizi zinapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili ningependa kuchangia kuhusu Dege, mradi wa Dege *Eco Village*, mradi huu una utata mkubwa. Mradi wa Dege nilipata fursa ya kwenda kuangalia niliumwa tumbo la uzazi, kwa sababu ni Mwanachama wa *NSSF* nimekua nikichangia zaidi ya miaka 10, kwa hiyo, nina *interest* kwenye huo mradi wa Dege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu unautata kuanzia jinsi ulivyoanzishwa kwa maana jinsi gani ardhi ilipatikana mpaka *implementation* ya huo mradi. Tunaambiwa na Mkaguzi CAG anasema eka moja ilinunuliwa kwa milioni 800 Kigamboni. Sijui kwenye ile sehemu kuna *gold, I don't know* labda hawa watu waende wakaangalie inawezekana kuna *gold*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba sitaki kuongea maneno mengi naomba tu niishauri Serikali. Kwa vile mradi huu ni pesa za Wanachama wa *NSSF* na nikiwemo, naitaka Serikali na iazimie kwamba Mradi huu, pesa za *NSSF* zisiendelee kuingizwa kwenye mradi huu kwa sababu mpaka sasa hivi *NSSF* wameshaingiza bilioni 219 na ule mradi ni mfu mpaka itakapofanyika *independent actuarial valuation,* kuona kama pesa zilizoingizwa pale zina-*reflect investment cost* ya huu mradi sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba, kila siku gharama zinaongezeka lakini pia *depreciation* inatokea kwenye yale majengo na hizi gharama zitakuja kulipwa na Wanachama wenyewe. *(Makofi/vigelele)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimwa Ruge, muda wako umemalizika. Tunaendelea na Mheshimiwa Abdallah Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nami niungane na wenzangu kuwapongeza Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati hizi mbili kwa kazi nzuri walioifanya wale wa *PAC* na wale wa *LAAC*. Pia nichukue nafasi hii vilevile nimpongeze CAG kwa kazi nzuri anayoifanya, kwa sababu Kamati hizi mbili zinategemea na taarifa ambazo zinawasilishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa kazi nzuri hizi amewezesha Kamati hii kufanya kazi yake kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niipongeze Serikali kwa kuwezesha Ofisi ya *CAG* kwa sababu kwa mwaka huu wa Fedha *CAG* ameripoti kwamba amepewa fedha kwa kadiri alivyohitaji na ndiyo maana amewezesha kufanya ukaguzi wake kwa wakati na kaleta taarifa kwa wakati. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kusikiliza kilio cha Ofisi ya *CAG*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango yangu itajikita sana sana kwenye taarifa ya ya Hesabu za Serikali za Mitaa *LAAC*. Nianze na lile la ukaimu wa Wakuu wa Idara, nami niungane na Wajumbe waliosema kwamba imefika hatua sasa Serikali ichukue hatua mapema na kama ni sababu ya mchakato mrefu basi irahisishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu ya *LAAC* tulipoenda Korogwe, tumekuta kwenye Wakuu wa Idara 16 kuna *proper* Wakuu wa Idara watano tu; 11 ni Makaimu. Kwa hiyo utaangalia ni jinsi gani Ofisi hii au Halmashauri hii ya Korogwe haitaweza kutekeleza majukumu yake kwa umakini kwa sababu kuna Makaimu wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kaimu anapokaa ofisini kwanza anakosa kujiamini, anakosa ubunifu kwa sababu muda wote anafikiri kwamba Mkuu wa Idara anaingia. Kwa hiyo, naomba Serikali iharakishe na ili kuisaidia Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe naomba Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ichukue hatua za haraka. Kwa sababu kwenye Wakuu wa Idara 16 kuna *Proper Head of Departments* watano hapo kuna athari kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ninaomba kuliongelea ni suala la Kitengo cha Wakaguzi wa Ndani. Kitengo hiki ni muhimu sana na Kitengo hiki ni msaada mkubwa sana kwa Maafisa Masuuli. Hata hivyo, kama taarifa yetu inavyoonesha kwamba Kitengo hiki kuna upungufu wa rasilimali watu na upungufu wa rasilimali fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kama tulivyopendekeza kwenye taarifa ya mwaka jana, mwaka huu tumerudia kuwe na mkakati maalum wa kuongeza

Watumishi katika Kitengo hiki cha Ukaguzi wa Ndani kwa sababu Halmashauri nyingi ambazo zinakuja mbele ya Kamati kuna Mkaguzi mmoja au wawili na wakati Ikama inatakiwa kila Halmashauri iwe na Wakaguzi wa Ndani watano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba jitihada za makusudi zifanywe ili kuongeza Wakaguzi wa Ndani ili kurahisisha Wakurugenzi kufanya kazi zao kwa umakini. Hili ni jicho la karibu sana kwa Mkurugenzi au Afisa Masuuli kuonesha ni nini kinafanyika katika Taasisi. Kwa hiyo, kuwe na jitihada za makusudi za kuajiri Wakaguzi wa Ndani ili Kitengo hiki kiweze kufanya kazi yake kwa umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kwanza niipongeze Serikali kwa kuanzisha miradi mingi ya maendeleo na kama tulivyopitisha kwenye bajeti kwamba fedha nyingi zimeenda kwenye miradi ya maendeleo. Hata hivyo, hapa kuna changamoto mbili; changamoto ya kwanza kama tulivyosema fedha nyingi hazipelekwi kwa wakati, lakini fedha zinazopelekwa kuna maelekezo mengine ambayo yanachelewesha utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa wazo kwamba *TBA* na na SUMA JKT wapewe kazi, lakini miradi mingi ambayo imekaguliwa hivi karibuni imeonesha Taasisi hizi mbili zimeshindwa kutekeleza ile miradi ambayo imepewa kwenye halmashauri nyingi. Kwenye Halmashauri mpya *TBA* na SUMA JKT walipewa kujenga majengo ya Ofisi za Wakurugenzi, lakini ukaguzi ambao unafanywa sasa hivi wa kutembelea miradi hii bado *TBA* na SUMA JKT wameshindwa kuitekeleza miradi hii kwa wakati, wamepewa fedha lakini inaelekea wameelemewa na miradi mingi. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie upya uamuzi huu ili kuharakisha utekelezaji wa miradi katika mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Ofisi ya Rais, TAMISEMI juzi juzi walienda kwa Mkuu wa Mkoa wa Mara

wamechukua uamuzi wa haraka wa kuvunja Mkataba na *TBA*. Kwa hiyo, naiomba Ofisi ya Rais, TAMISEMI itembelee miradi mingine hasa ya ujenzi wa Ofisi za Wakurugenzi katika Halmashauri mpya 17. Ujenzi bado ni wakusuasua na bado hakuna kasi ambayo inaonesha kwamba miradi hii itakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua wakifika kule watajionea wenyewe na inawezekana ikachukuliwa hatua kama ilivyochukuliwa kwa mradi ule wa Musoma, ambao Naibu Waziri Mheshimiwa Kandege aliamua kuvunja Mkataba kwa niaba ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwa hiyo nakupongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nichangie kuhusu miradi ya maji kama ulivyosema katika taarifa yetu kuna utekelezaji wa kusuasua katika miradi ya maji na hapa kuna changamoto kubwa sana. Changamoto kubwa iliyopo, kuna utofauti sana wa utekelezaji wa miradi kati ya halmashauri na halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulienda Mkoa wa Tanga tukakuta Halmashauri ya Korogwe kuna changamoto kubwa sana ya utekelezaji wa miradi ya maji, inaanzia kwenye usanifu. Kuna miradi mingine wananchi wamekataa kutoa maji kwa sababu kwenye chanzo pale cha maji wananchi hawapewi *water point.* Mradi unatoa maji Kijiji X wananchi wa Kijiji X hawapewi maji wanapeleka Kijiji Y, wanachi wa eneo husika wanasema haiwezekani. Sasa huu ni udhaifu wakati wa usanifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeona miradi inachelewa kutekelezwa, mradi mmoja ulikuwa unatekelezwa kwa milioni 900, lakini kwa sababu ya kuchelewesha sasa hivi gharama yake ni bilioni nne, kwa hiyo, hizo ni hasara kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili hata huo usimamizi wa miradi yenyewe ya maji ni changamoto kubwa. Tulienda

kwenye mradi mmoja ambapo limetengenezwa hozi ya kunyweshea mifugo wakifika ng'ombe au mbuzi hawawezi kunywa maji na Mhandisi wa Maji yupo na Mhandisi wa Ujenzi yupo lakini wameshindwa kushirikisha wananchi wakatengeneza hozi ambayo ingetumika katika mazingira yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo miradi ya maji ina changamoto kubwa sana katika mamlaka ya Serikali za Mitaa na ndiyo maana ndiyo maana Kamati yetu tukaja na wazo basi uundwe Kamati maalum ya kufuatilia miradi hii ili tujue chanzo na sababu yake ni nini. Pengine tutoe mapendekezo ambayo yataisaidia Serikali katika utekelezaji wa miradi ya maji. Kwa hiyo, naomba Wabunge tuungane katika wazo hili ili Mheshimiwa Spika aunde Kamati Teule ifanye shughuli hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa hoja ya ucheleweshaji wa fedha za maendeleo. Kama nilivyosema kuna miradi mingi fedha zinakwenda kwa kusuasua na zinapofika kunakuwa na maelekezo tofauti lakini mbaya zaidi kwamba fedha hizi sasa zingine zinaletwa mwezi Juni, mwezi ambao kwa taratibu za manunuzi huwezi kufanya chochote. Kwa hiyo, naomba Hazina waharakishe utoaji wa fedha hizi ili mamlaka za Serikali za Mitaa zisiwe na bakaa na kusababisha hoja nyingi za ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdallah Chikota. Waheshimiwa Wabunge kwa vile shughuli zetu zimefikia mwisho kwa *session* hii ya asubuhi na muda umemalizika, kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Tunaendelea na majadiliano, tutaanza na Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Mussa Mbarouk na baadaye ataendelea Mheshimiwa Edward Mwalongo. Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie kwenye hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo ningependa nichangie ni kwamba kwenye hoja hii mwaka jana tulizungumza sana kuhusu uwezo wa baadhi ya Wakurugenzi wa Halmashauri zetu. Tuliishauri Serikali kwa makusudi kabisa ijitahidi kufanya semina, warsha na mafunzo kwa ajili ya kuwajengea uwezo baadhi ya Wakurugenzi ambao wameingia katika kazi hii kutoka kwenye shughuli nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya utendaji wao umesababisha migogoro kati yao na baadhi ya Watendaji wa Halmashauri. Wakurugenzi wakifikiria kwamba kule kuwa wasimamizi wa Halmashauri basi wao ndiyo kila kitu, umesababisha migogoro kati yao na Madiwani na baadhi ya Halmashauri migogoro hii inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokwenda kwenye Halmashauri na kukuta Mkurugenzi hayupo katika maelewano mazuri na Watendaji pamoja na Madiwani, kwa vyovyote vile Halmashauri haiendi. Ikumbukwe kwamba, hizi Halmashauri ni za wananchi, kwa hiyo Mkurugenzi hawezi kusimama kwenye Halmashauri kana kwamba yeye ndiyo mwenye kujua kila kitu, yeye ndiye mamlaka ya kila kitu, akikataa ushauri na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa kwanza kabisa naiomba Serikali iendelee kupitia uwezo wa

Wakurugenzi wake na isaidie kuwapa uwezo ili waweze kusimamia shughuli za Halmashauri vizuri, vinginevyo tutapata shida, kazi hazitaenda sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sambamba na hilo tumetembelea baadhi ya Halmashauri, miradi ya maendeleo haisimamiwi sawasawa. Unakuta kuna ile Idara ya Mipango ya Halmashauri ni kana kwamba inajiweka pembeni mambo yanakwenda yenyewe kwenye maeneo mbalimbali ya miradi, lakini unapohoji zile Idara utasikia kwamba ohoo, hili halikupitia kwetu na kadhalika. Ndio maana nasema kama Mkurugenzi yuko vizuri na Wakuu wake wa Idara mambo kama haya yasingeweza kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano tu wa Idara ya Elimu, hivi majuzi Mheshimiwa Rais kwa nia nzuri kabisa ametoa maagizo kwamba michango mbalimbali katika shule ambayo haina tija iondolewe, hiki ni kilio cha Watanzania, lakini sasa kutokana na uwezo mdogo wa Wakurugenzi lazima niseme na hili nawaomba Rais alisikie, uwezo mdogo wa Wakurugenzi umewafanya wakatafsiri lile agizo la Rais vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu zipo Halmashauri, zipo Wilaya ambazo wazazi katika kila shule walishakubaliana utaratibu wao wa namna watoto wao, kwa mfano wanavyopata chakula mashuleni, utaratibu huo hauhusiani na Mkuu wa Shule, hauhusiani na Mkurugenzi, wazazi wana chama chao, wana bajeti zao, wao ndiyo wanaopanga watoto wale nini, wao ndiyo wanaopanga bajeti iwe namna gani, kuni zipatikane wapi, chakula kipatikane wapi, kwa hiyo watoto wamekuwa wakila shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa upo uhusiano mkubwa kabisa kati ya tumbo na kichwa. Mtoto ambaye hajashiba hawezi hata siku moja akazingatia yale ambayo anaelekezwa shuleni. Sasa Wakurugenzi hawa baadhi yao wamekuwa kama *robot,* wamekwenda wametengeneza majedwali, wameandika barua, wamekwenda kuzuia wale

wazazi ambao kwa nia nzuri kabisa walikuwa wanachanga chakula kwa ajili ya watoto wao. Sasa nashangaa hapa tunaisaidia nchi au tunaibomoa, mtoto anaamka saa 11 alfajiri nyumbani, hajanywa uji, hajanywa chai, anakwenda shuleni hakuna chochote, halafu unasema kwamba tunakuza elimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Wakurugenzi walimtafsiri Rais vibaya, yako maeneo, kwa mfano katika Jimbo langu, tulikuwa hatuna tatizo kabisa lakini baada ya tangazo lile wamekwenda wale wazazi wamegawana chakula ambacho tayari walikuwa wamenunua, wamegawana kuni ambazo tayari zilikuwa shuleni, wamegawana pesa ambazo zilikuwa tayari zimeshakusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa sababu Waziri wa Elimu yupo hapa, atusaidie hawa Wakurugenzi waweze kuelewa vizuri agizo la Serikali lilikuwa nini kwa sababu sisi hatuna shida. Rombo kwa mfano, shule zote za Sekondari na za Msingi watoto wanakula shule na huhitaji kabisa kauli ya Mkuu wa Shule wala Mkurugenzi wala nini, wazazi wana vyama vyao, wanaitana wanajichangisha wenyewe, wanatengeneza bajeti wenyewe, wanaajiri mpishi wenyewe, wananunua kuni wenyewe. Sasa leo Mkurugenzi ukifikia mahali ukasema Rais kasema, matokeo yake hata Rais atachukiwa! Kwa sababu Wazazi kule tafsiri ni kwamba anachokula mtoto mchana nyumbani ndicho hicho tunaamishia shuleni, kwa hiyo hakuna tatizo lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo narudia kusema la kwangu ni hilo kubwa kwamba, baadhi ya Wakurugenzi wasiwe wanapokea maagizo ya Serikali halafu wanakuwa kama *robot,* sijui wametiwa hofu ya namna gani! Bila hata maelezo bila hata nini wanaingia katika utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulisema, hapa tunafanya bajeti, kila Halmashauri inajua kwamba bajeti ya maendeleo katika Halmashauri ni kiasi fulani. Kinachotokea ni kwamba,

Halmashauri nyingi ambazo tumezitembelea fedha za maendeleo hazifiki kwa wakati au hazifiki kabisa, matokeo yake ni kama vile Halmashauri zimefungwa mikono na miguu halafu zinaambiwa kimbia, haziwezi kukimbia haziwezi kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba fedha za miradi ya maendeleo katika Halmashauri ziende kwa wakati na kama hazijaenda basi utaratibu uelekezwe ili wajue watafanya nini, vinginevyo ziko Halmashauri ambazo zitaendelea kuachwa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ningependa kuchangia kwa sababu Mheshimiwa Gekul ameniomba dakika tano na nataka nimpatie ni kwamba Serikali imejitahidi sana kupeleka watumishi, lakini bado kuna Halmashauri ambazo Ikama haijakaa vizuri, bado kuna Halmashauri ambazo watumishi wengi wanakaimu. Mtu anayekaimu hana hakika na ile nafasi hawezi akatoa maamuzi, kwa hiyo bado tunasisitiza na tunaiomba Serikali kwamba, Wakuu wa Idara katika Halmashauri zetu ifanyike jitihada wale wanaokaimu waweze kuthibitishwa ili waweze kufanya kazi yao kwa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti ni hayo, naomba muda wangu uliobaki amalizie Mheshimiwa Gekul.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru kwa namna ya pekee Mheshimiwa Selasini Mbunge wa Rombo, kunipa dakika chache nami niseme machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza naunga mkono aliyoyasema kuhusu elimu sitaki kuyarudia ilikuwa niyasemee, lakini ni vizuri hiyo kauli ikatolewa ikaeleweka kwa sababu kama kuna kosa tutalifanya kama Taifa ni kuwafanya watoto wetu washinde kuanzia asubuhi mpaka jioni wasile chochote, kwa hiyo tunahitaji kauli ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ni suala la asilimia 10 ya vijana na akinamama. Nashukuru Wizara ya TAMISEMI Naibu Mawaziri walifanya ziara katika Jimbo langu la Babati Mjini lakini mkatoa mwongozo, kwamba sasa asilimia mbili ni kwa walemavu, halafu zile asilimia nane zigawanywe kwa akinamama na vijana. Naiomba Serikali ni vizuri mkatenga asilimia zingine mbili kwa ajili ya wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna timu kubwa sana ya wazee ambayo hainufaiki na hizi asilimia 10. Kama mliona busara kutenga asilimia mbili kwa ajili ya walemavu, sasa niiombe Serikali au niitake Serikali ione hitaji la wazee la muda mrefu ambalo wamekuwa wakiiomba Serikali iwatengee angalau kiasi fulani kwa kila mwezi wapewe. Sasa hizi asilimia 10 ukiwapatia vijana, akinamama na walemavu na hawa wazee muwakumbuke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni vizuri watu wengine wanapofanya kazi nzuri waweze kukumbukwa katika Serikali hii. Naishukuru sana timu ya wataalam katika Halmashauri yetu ya Mji wa Babati na Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba kama kuna miongoni mwa Halmashauri zinafanya vizuri kuhusu asilimia 10 ni pamoja na Halmashauri ya Babati Mjini. Ni vizuri wakawa-*promote* wale wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao wataalam ambao wanatusaidia zile fedha zinakuwa *revolving fund*, lakini Halmashauri zingine zile fedha zikiingia zinaingia kwenye *consumption* ya kawaida ya *OC* badala ya kurudi kwenye ule mfuko. Sisi kwa nini tumefanikiwa katika kutoa hiyo mikopo kwa asilimia 100 hiyo asilimia 10, ni kwa sababu tulikuwa na Mwanasheria mzuri sana, wale ambao hawalipi wanapelekwa Mahakamani, imesaidia watu kurejesha kwa sababu wanajua zile fedha lazima zirudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukawa na timu ya Maendeleo ya Jamii pamoja na Mkuu wao wa Idara ambao zile fedha zikiingia wanaiweka kwenye *account* ambayo inakuwa *revolving.* Naomba vitu vingine hata kama vinafanywa na watu wengine ambao hamuwapendi sana

kama ni vizuri basi mviige, njooni muone Babati tunafanya nini na tumefanikiwa kwa kiasi gani na nipongeze timu ya Babati Mkurugenzi na timu yake kwa sababu wanafanya kazi nzuri sana katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine ninaotaka kuutoa ni kuhusu *Pride* Tanzania. Nimeona kwenye ripoti kwamba Kamati imeshauri Serikali iangalie kwa sababu hii *Pride* ilianzishwa kwa fedha za Serikali kipindi hicho. Naiomba Serikali pamoja na kwenda kuiangalia na kuibinafsisha irudi kwenye mfumo wa Serikali hii *Micro Finance* ni vizuri wale vijana wetu wasiathirike ajira yao na shirika likaendelea, kwa sababu kama kuna taasisi au kama *Micro Finance* ambayo imeajiri vijana wengi wa Kitanzania ni pamoja na *Pride* Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pamoja na kwamba huko nyuma mliuzianauziana kinyemela, lakini mwangalie pia ajira za Watanzania hata kama mnakwenda kuibinafsisha, lakini ni miongoni mwa *Micro Finance* ambazo zimetoa ajira nyingi kwa Watanzania na imefika katika vijiji na katika *remote areas*. Kwa hiyo, nitoe ushauri wangu kwamba msikimbilie kubinafsisha tu, sawa mtaangalia mtafanya *audit* ya kutosha, lakini mwisho wa siku muone jinsi gani ambavyo vijana wetu hawapotezi ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la *OC*, hebu niombe Serikali tunafanya bajeti, lakini bajeti hii hakuna sababu ya kukaa miezi mitatu au miwili hapa, tuka- *budget* fedha za maendeleo fedha za *OC* lakini mwisho wa siku Mheshimiwa Waziri wa Fedha, fedha zikawa haziji kabisa. Mmechukua vyanzo vikubwa vya Halmashauri zetu lakini hivyo vyanzo pia mvifanyie *review,* mfano nitoe chanzo kimojawapo, mmefuta ushuru wa machinjio katika machinjio zetu, pale Babati Mjini tumetengeneza machinjio mazuri, zaidi ya milioni 50 tumekarabati. Mmefuta ule ushuru *at the same time* mnamwachia Mkurugenzi alipe bili ya maji, bili ya umeme wakati kuna watu ambao wanachinja ng'ombe wao pale, mmefuta ule ushuru, angalieni...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzunguzaji kwisha)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Hiyo ni kengele ya kwanza Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul zote zilikuwa pamoja ya kwanza ya Mheshimiwa Selasini hiyo ya kwako.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Ndiyo ya kwanza inalia hiyo, kengele ya pili bado.

**MWENYEKITI:** Tayari muda umemalizika Mheshimiwa.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante, namkaribisha Mheshimiwa Mussa Mbarouk, hayupo, tunaendelea na Mheshimiwa Edward Mwalongo.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hoja zetu mbili zilizopo hapa mezani, hoja ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Kamati Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niwapongeze sana Wenyeviti wetu, niwapongeze Wajumbe wa Kamati wote wa Kamati zote mbili, lakini nisiwe nimepungukiwa fadhira niishukuru sana Ofisi ya *CAG* kwa jinsi inavyotusaidia Wajumbe wa Kamati hizi mbili kutuwezesha kiutaalam lakini kutusaidia kutuongoza namna gani tunaweza kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kuchangia hoja ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Halmashauri mbalimbali zimekaguliwa nasi tumejaribu kuwahoji Maafisa Masuuli kama taarifa zetu zinavyoonesha, tumetembelea baadhi ya Halmashauri, lakini jambo kubwa ambalo

ningependa nilizungumzie zaidi hapa ni tatizo kubwa la maji. Kwanza kabisa naomba mtambue ndugu zangu, Wabunge wenzangu pamoja na Serikali kwamba kimsingi maji hayana mbadala, panapotakiwa maji lazima yapatikane maji, tatizo kubwa la nchi yetu mpaka sasa hivi tuna shida kubwa sana ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha ajabu kuliko yote maji ndiyo kitu ambacho kina teknolojia rahisi, sasa najiuliza tatizo liko wapi! Kama maji hata kwa asili tu watu walichimba visima, walitengeneza mifereji wakapata maji wakatumia, leo hii pamoja na maendeleo tunayosema tunayo tunashindwa kupata maji katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika Halmashauri unakutana na shida mbili kubwa, shida ya kwanza unakutana na matatizo ya usanifu wa miradi ya maji, shida ya pili unakuta kwamba mwenye mfuko wa pesa yuko Wizarani Halmashauri imekaa tu pale, mradi unapotekelezwa yuko mtu hapa katikati anaitwa Mhandisi Mshauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mhandishi Mshauri anaajiriwa na Halmashauri, lakini mradi unapoharibika Halmashauri hana cha kusema, ukiwauliza wataalam wa Halmashauri wanasema Mhandisi Mshauri alishauri hivyo na alisimamia hivyo. Sasa unajiuliza kwa mfano, tumeenda mradi mmoja kule Tanga unaitwa Changarikwa, mabomba mita 300 yanapasuka siyo hiyo tu, hata katika Halmashauri yangu ya Mji Njombe mradi wa maji wa Utengule mabomba yanapasuka. Ukiwauliza wataalam wa Halmashauri wanasema Mhandisi Mshauri ndio aliyesimamia huu mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tujiulize sasa kama Mhandisi Mshauri kimekuwa ni kichaka tutafute njia nyingine ya kufanya. Kama Mkoani kuna Injinia wa maji, Halmashauri yenyewe ina Injinia ya maji kwa nini miradi wasisimamie wenyewe, teknolojia ya maji ni ndogo sana. Tunagawa fedha hizi kidogo kuwapa Wahandisi Washauri wakati tumeajiri Wahandisi ndani ya Halmashauri wapo na miradi inakwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye upande wa ubunifu wa hii miradi, unakwenda mahala unakutana na mradi umebuniwa ni *borehole* wamechimba kisima, lakini umefungwa mashine ya *diesel* ifue umeme halafu ule umeme uingie kwenye *submersible pump* uendeshe ile *pump* ya maji. Mwananchi wa kawaida hawezi kulipa maji hayo, hawezi kulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeenda kutembelea mradi wa Mkonze hapa Dodoma tumeona hali hiyo, kwamba imefikia mahali wananchi kisima wanacho, miundombinu ipo lakini wanashindwa kuuhudumia ule mfumo wakaamua kumpa mtu tu aendeshe. Mtu yule amevuta umeme zaidi ya kilometa mbili. Sasa unajiuliza Serikali imeshindwaje kuvuta umeme ukaingia kwenye ile pampu ya maji mpaka mtu binafsi amefanya?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi ya maji inaharibika kwa sababu wabunifu wa miradi au mafungu yanayoletwa yanakuja na maelekezo kwamba huyu ndio Mhandisi Mwelekezi, atasimamia mradi huo ama atawabunia huo mradi. Nitoe ushauri kwa Serikali, tufanye haraka tuanzishe Wakala wa Maji Vijijini ili kusudi jambo la Maji lishughulikiwe na Wizara. Kama ni Wizara ishughulikie Wizara, kuanzia mwanzo ubunifu, usimamizi, utekelezaji, ulipaji na kila kitu. Kusiwe na kusigana kwamba Halmashauri mara Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii *certificate* nyingi za maji hazijalipwa. Wapi zimekwama? Haijulikani! Wakandarasi wamefanya kazi hawalipwi. Miradi ya maji inaharibika kwa sababu Mkandarasi anakuwa amefanya kazi lakini hajalipwa. Matokeo yake muda unakwenda mrefu halafu gharama zinaongezeka za mradi Mkandarasi anakuwa hayuko tayari kuendelea kutengeneza ule mradi. Kwa hiyo naiomba sana Serikali harakisheni huo mchakato wa kuunda Wakala wa Maji ambao mwaka jana tumelalamika sana hapa Bungeni, nina imani Serikali ni sikivu italifanya hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Idara ya

Uhandisi, unatembelea miradi ya ujenzi wa majengo mbalimbali ya Serikali unashindwa kuelewa kwamba hivi huyu ni Mhandisi kweli ambaye anastahili kuitwa Mhandisi? Kwa mfano, tulienda Tanga kutembelea Shule moja ya Msingi unakwenda kuangalia limejengwa jengo la msalani kwa ajili ya wanafunzi, lakini wote tunajua msala wa wanafunzi unatakiwa uweje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unamuuliza Mhandisi anasema aah! mchoro uliletwa hivyo. Sasa unajiuliza wewe Mhandisi ulishindwaje kushauri? Kwa hiyo, tuna shida kubwa sana hata kwa hawa Wahandisi wetu wa Halmashauri, fedha nyingi inakwenda lakini uwezo wao wa kusimamia hiyo fedha ya kusimamia miradi ni mdogo sana.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo linaleta shida kwenye Halmashauri zetu ni uchache wa wataalam hasa Wakuu wa Idara. Halmashauri nyingi ambazo tumepitia mahesabu yake kuna upungufu mkubwa sana wa Wakuu wa Idara. Kwa hiyo, inapokuwa kwamba Halmashauri haina Mkuu wa Idara au Idara fulani Mkuu wake anakaimu, matokeo yake ni kwamba hata maamuzi yake yanakuwa na sura hiyo ya kukaimu kaimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza anakuwa hajiamini, anashindwa kutoa maamuzi, anashindwa kufikiria kwamba idara yangu hii iendeje na niipangeje. Naomba kama TAMISEMI tunataka tuende vizuri, hawa wataalam wetu basi tuwathibitishe mapema. Tutoe maelekezo kwa Wakurugenzi kwamba ikiwa kuna mazingira ya kukaimu yanatakiwa yawepo, basi wawepo Wataalam ambao wana sifa ndio wakaimu hizo nafasi halafu muda ukifika wathibitishwe ili kuondoa hiyo nafasi ambayo inakuja kuleta ombwe hapo baadaye kwamba maamuzi hayafanyiki, shughuli zinachelewa ni kwa sababu tu kwamba mtu hajathibitishwa, lakini tukumbuke kwamba wananchi wanakosa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ukiangalia ushirikishaji wa kiidara. Idara ya ujenzi inapokuwa inatekeleza

mradi kwa mfano tunataka kutekeleza mradi wa afya, watu wa afya hawashirikishwi. Tumekwenda Tanga tumekuta Idara ya Maji inatekeleza mradi kwa ajili ya wananchi, lakini wakati huohuo kuna sehemu ya kunyweshea ng'ombe wanaita hozi, hozi za kunyweshea ng'ombe mtu wa mifugo hajui kabisa. Imejengwa hozi, ng'ombe hawezi kunywa yale maji. Sasa unajiuliza, hili hozi alikuwa anajengewa nani? Kwa hiyo hapo kuna tatizo la ushirikishwaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda mahali tumekuta kituo cha afya kimejengwa kizuri sana, lakini ukiangalia mahali lilipowekwa jengo la upasuaji inaonekana kwamba kwenye mpango wa ujenzi kulikuwa hakuna ushirikishwaji. Wamejenga lakini hakuna miundombinu sasa inayoweza kuunganisha kati ya jengo la upasuaji na majengo mengine ya kile kituo cha afya, matokeo yake jengo hilo la upasuaji halitumiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niseme kwenye mipango yetu ya wataalam wetu wa Halmashauri pamoja na wataalam elekezi wanaanzisha miradi lakini matokeo yake mradi unafika mwishoni, mradi ni wa maji unafika mwishoni wanapotaka kuwasha pampu za maji zianze kufanya kazi unaambiwa hapa pana *low voltage*. Sasa unajiuliza jamani hivi kuna maana gani ya kumweka mtu msomi hapa? Kama hakuweza kuliona hilo kabla akaona kwamba hapa pana *low voltage*, naleta pampu za maji zenye uwezo huu, niwasiliane na wanaohusika na maji ili wajue kabisa kwamba pampu za maji zinazoletwa hapa zina uwezo, zinaweza zikatumia umeme huu. Mradi umekamilika lakini wanashindwa kwenda kwa sababu tu pampu za maji hazifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ni pale ambapo Wataalam wa Halmashauri pamoja na hawa Wahandisi Wasimamizi wanafikia mahala kuwalipa Wakandarasi kazi hazijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wa Halmashauri

wanathibitisha kazi ya Mkandarasi wakati kazi haijakamilika. Nitatoa mifano hii ya Tanga kwa sababu ndiko ambako tumefanya ziara. Unakwenda pale unamuuliza Mhandisi wewe hapa kwenye tenki lenu umesema kuna *level indicator* iko wapi hapa kwenye tenki? Yule akiamini kwamba sisi ni Wanasiasa hatujui *level indicator* anatuambia *level indicator* ipo kwenye *DP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimuuliza wewe *level indicator* inakaa kwenye *DP*? Ukimbana kidogo na kumtikisa ndiyo anakiri kwamba aah! Mkandarasi hakuweka, lakini ameshalipwa na alishakwenda na muda wa matazamio ulishapita. Kwa hiyo ni jambo la kusikitisha sana unapokuwa na wataalam ambao wanathibitisha na Serikali inatoa fedha halafu kazi inakuwa haijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningelipenda nilisemee ni kama walivyosema wenzangu. Baadhi ya Halmashauri kweli Wakurugenzi wake hawatilii maanani sana wajibu wao kama Wakurugenzi, wakipewa hoja za Kamati hawajibu. Hii inaleta shida sana wamebuni utaratibu wanajua kabisa kwamba Kamati inakaa miaka miwili na nusu baada ya hapo Kamati itamaliza muda wake itaingia Kamati nyingine. Wanajua kabisa kwamba hoja kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali huwa inakwenda kwa muda maalum, muda huo ukipita hiyo hoja inakuwa hoja mfu hakuna atakayekuja kuibua tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naiomba Serikali iangalie ni kwa namna gani sasa iweke utaratibu pamoja na kwamba hizi hoja zingine zinakuwa hazijajibiwa, lakini uwepo utaratibu wa kusema kwamba hoja hizi zinafuatiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nisisitize tu kwamba maoni ya Kamati naomba yazingatiwe hasa lile ambalo tunasema kwamba tunaomba Bunge liazimie kwamba sasa iundwe Kamati Maalum, ifuatilie matatizo ya miradi ya maji katika nchi yetu, kwa sababu maji hayana mbadala. Bila maji nafikiri hamna ambaye leo angeweza

kutokea humu ndani. Kama wote tungekosa maji tusingetokea ndani ya Bunge leo kwa sababu tumekosa maji. Kwa sababu maji hayana mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiunda Kamati hii ndiyo itasaidia kuieleza Serikali na kuionesha Serikali upungufu ulipo na kuona kwamba nini sasa kifanyike. Kwa sababu hakuna mahali ambapo tuna mradi wa maji mzuri wa mfano kusema kwamba mradi huu kwa kweli umetekelezwa bila matatizo. Mradi utaona umetekelezwa lakini mabomba yanapasuka, mradi umekamilika maji hayatoki, mradi umekamilika wananchi hawawezi kuundesha ule mradi kwa sababu ya gharama zake. Limejengwa bwawa la umwagiliaji hakuna wakulima wanaohusika na kilimo, limejengwa bwawa la umwagiliaji bwawa limepasuka. Kwa hiyo ni matatizo mwanzo mpaka mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana mapendekezo ya Kamati Bunge hili liridhie na yawe ni maazimio ili kusudi yaweze kusaidia kutatua tatizo la maji. Tatizo la maji katika nchi yetu ndio tatizo kubwa na linamgusa kila mwanachi, tukitatua tatizo la maji tutakuwa tumetatua matatizo mengi sana, magonjwa yote ya matumbo yatakuwa yamekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuangalie bajeti ya dawa za matumbo ni kiasi gani, matumbo wananchi wanaumwa kwa sababu tu ya kukosa maji, lakini wakipata maji safi maana yake tumeokoa hiyo fedha wananchi wote watakuwa na afya tutaendelea na miradi mingine. Kwa hiyo, niombe sana hilo lizingatiwe tutatue tatizo la maji kwa wananchi ili kusudi wananchi wetu wawe na maji na waweze kufanya maendeleo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwalongo. Tunaendelea na Mheshimiwa Mussa Mbarouk na baadaye atafuatia Mheshimiwa Jamal Kassim.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuweza kusimama hapa na kuchangia katika taarifa za Kamati hizi mbili. Labda niseme tu kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *PAC*, vilevile nilikuwa kwenye Kamati Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kuchangia kuhusu Serikali za Mitaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya *LAAC* kuna maeneo ambayo yamezungumzia kuhusiana na kukaimu kwa Wakuu wa Vitengo au Wakuu wa Idara kwa muda mrefu. Naungana na wale wanaosema kwamba hili ni tatizo, kwa sababu unakuta Mkuu wa Idara anakaimu nafasi zaidi ya miezi sita inafika mpaka miaka mitatu wakati mwingine. Hii inapunguza uwezo wa kujiamini kwa Mkuu wa Idara pia anakuwa hana mamlaka kamili ya kusimamia au kutoa amri na maelekezo katika baadhi ya mambo. Kwa hiyo, naishauri Serikali katika hili baadhi ya taratibu zifuatwe ili wanaokaimu wasikaimu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu wapo watu wengi ambao wanazo sifa za kuwa Watumishi au Wakuu wa Idara kamili lakini kwa muda mrefu wanakaimu, hivyo hilo naomba lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kulizungumzia ni ucheleweshwaji wa ruzuku kutoka Serikali Kuu. Nashauri kwamba hakuna haja ya kuchelewesha ruzuku kwa sababu Halmashauri hasa ukizingatia baada ya kunyang'anywa baadhi ya vyanzo vya mapato zimekuwa hazina fedha, Kwa hiyo ruzuku inayotoka Serikali Kuu ndiyo inayofanyiwa kazi na Halmashauri zetu hivyo isicheleweshwe ili Halmashauri zikamilishe miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kulizungumzia ni unyang'anywaji wa *property tax* na

mabango ya biashara kwa Halmashauri zetu. Kwanza napenda niseme tu kwamba Serikali za Mitaa nazo ni Serikali, kwa sababu kwa ufahamu wangu najua kuna *Central Government* na *Local Government*, sasa hizi Serikali za Mitaa zina majukumu ya kutoa huduma na kutimiza wajibu wa kutoa huduma kwa wananchi, sasa tumezinyang'anya *property tax* pia tumechukua na mabango ya biashara, yote yamekwenda *TRA.* Nashauri kwamba turudishe *property tax*, turudishe mabango ya biashara katika Halmashauri zetu ili ziweze kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi mingi ya maendeleo kama vile vituo vya afya, kuna zahanati pia kuna miradi ya madarasa na mambo mengine kadha wa kadha ambayo kama tutazirudisha *property tax* na mabango ya biashara Serikali za Mitaa zitaweza kufanya kazi kwa ukamilifu na kuwapa huduma bora wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni matumizi mabaya ya fedha za umma ambapo katika Halmashauri inabidi zisimamiwe kikamilifu. Pamoja na kupeleka fedha bila ya kuzisimamia ipasavyo itakuwa ni sawa na kazi bure. Kama wataalam wanavyosema *the power without control is nothing*. Kwa hiyo, lazima tunavyopeleka pesa tuzisimamie. Tuhakikishe kwamba zinafanyiwa ukaguzi na wale ambao wanapata hati chafu na hati zenye mashaka nao wajieleze kwa nini wanapata hati hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kuzungumzia katika Serikali za Mitaa ni mikataba ya upimaji wa viwanja. Mara nyingi upimaji wa viwanja umekuwa unatumia fedha nyingi lakini haukamiliki kwa wakati. Sasa tutoe maelekezo kwa Wizara kwamba wahakikishe pale ambapo Halmashauri inataka kupima viwanja, viwanja vipimwe kwa wakati na wananchi wauziwe bei nafuu ili kila mmoja aweze kupata kiwanja na ajenge nyumba bora ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihamie sasa katika Kamati

ya *PAC*. Katika Kamati ya *PAC* kuna taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo imeishia tarehe 30 Juni 2016, taarifa hii imeeleza upungufu mwingi. Miongoni mwa upungufu uliojitokeza ni utekelezaji wa miradi iliyofanyika bila ya tija na kusababisha hasara kwa Serikali. Pia kuna dosari zilizojitokeza katika usimamizi wa miradi, kutokuwepo kwa nyaraka za malipo kwa baadhi ya taasisi na Wizara na Mashirika ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna upungufu wa kutokuzingatiwa kwa Sheria za Manunuzi ipasavyo, dosari katika usimamizi wa mikataba na ufanisi mdogo wa mabenki ya umma ukilinganisha na mabenki binafsi pia kuna kutokuzingatiwa kwa Sheria ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalotaka kulizungumzia ni taarifa ya kwamba hadi Juni 30, 2015 kuna Maazimio nane tu ambayo ni sawa na asilimia 64.2 kati ya maazimio 14 ambayo ndio yametekelezwa, lakini kuna mengine Sita ambayo ni sawa na asilimia 35.8 haya bado hayajatekelezwa. Nafikiri ipo haja Serikali kuhakikisha maazimio haya yanatekelezwa yale ambayo yamebaki ili kuweza kuisimamia Serikali, Bunge linapotoa maelekezo kutokana na maelezo ya taarifa za Kamati, basi maelekezo yale yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ipo taarifa kwamba Serikali kutokulipa kwa wakati madeni ambayo imechukua au imekopa kutoka katika Mifuko ya Jamii. *LAPF* wanaidai Serikali shilingi bilioni 243.43, *WCF* inaidai Serikali shilingi bilioni 26.6, *PPF* inaidai Serikali shilingi bilioni 139.5, *PSPF* inaidai Serikali bilioni 623. 93, *NSSF* inaidai Serikali bilioni 519.05, *NHIF* inaidai Serikali bilioni 43.8 jumla ya madeni haya yote ni takribani trilioni 1.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa Mifuko ya Kijamii ambayo jana tu tumepitisha sheria hapa kwamba iunganishwe kwa pamoja, lakini sasa kama fedha hizi hazitalipwa au zitakaa kama deni kwa Serikali kwa muda mrefu, hii Mifuko itajiendeshaje? Matokeo yake ndio

tunaposababisha watumishi wanapostaafu kukaa kwa muda mrefu wakisubiri mafao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niishauri Serikali katika hili, haraka iwezekanavyo ilipe madeni haya ya Mifuko ya Jamii, au kupitia kikao hiki Serikali ituambie baada ya jana kupitisha sheria ya kuunganisha Mifuko hii ya kijamii hadi lini Serikali itakuwa imelipa deni hili la shilingi trilioni 1.59. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naliona ni kutoanzishwa kwa Mfuko wa Uwekezaji wa Umma *(Public Investment Fund)* nao pia Serikali ituambie, kwa sababu hii ilikuwa ni katika mapendekezo na maazimio ya Bunge letu ni lini Serikali itaanzisha hii *Public Investment Fund*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni hali ya kifedha ya Mfuko wa *PSPF* kutoimarika ipasavyo. Hii nafikiri kwa upeo wangu ni ile kutokana na kuikopesha Serikali na Serikali kutolipa kwa wakati. Kwa hiyo nashauri Serikali ilipe madeni haya kwa wakati. Kingine pia ni usimamizi duni wa mikataba katika Wizara na Mashirika ya Umma. Mikataba yetu imekuwa na matatizo mengi na yote hii ni kwamba tuonawapa mamlaka na tunaowapa dhamana wanaona labda kwa sababu si mali yao, siyo taasisi zao binafsi ndiyo maana hawasimamii ipasavyo. Naishauri Serikali pale mtu anapofanya uzembe katika Idara yake au katika Wizara yake kama kuna mkataba mbovu mtu huyo awajibishwe moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ninalotaka kulizungumzia ni kutokukamilika kwa uzingatiaji wa Mfumo wa Kihasibu *(IPSAS) accrual basis*, hili ni tatizo, kwa sababu kama tunashindwa kusimamia mifumo na kuikamilisha tutasababisha ufisadi mwingi katika Halmashauri zetu. Ni bora hii mifumo tuisimamie lakini mifumo hii pia tuhakikishe inakamilika kwa wakati kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kulizungumzia ni baadhi ya Taasisi za Umma kutofuata Sheria za Manunuzi, ndiyo maana katika taasisi zetu za umma

kumekuwa na ubadhirifu mkubwa wa fedha za Serikali. Kwa mfano hata katika ununuzi wa samani tu kwa sababu hatusimamii vizuri, kwa sababu hatufuati Sheria za Manunuzi matokeo yake imekuwa kila mwaka tunabadilisha samani au kila mwaka rasilimali au vyombo vya Serikali vimekuwa havina ubora unaostahili na tunaagiza vyombo vipya, tukijua ni matumizi makubwa na matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kulizungumzia ni dosari katika mkataba wa Mlimani *City* na *Mlimani Holdings Limited*. Katika taarifa iliyosomwa hapa na Mwenyekiti wetu Mama Naghenjwa Livingstone Kaboyoka ameeleza upungufu mwingi sana katika Mkataba huu. Nami niungane na mchangiaji aliyesema kwamba, takribani miaka 17 sasa imepita, ubadhirifu unaendelea, miradi haikamiliki lakini watu walikuwa wako kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kama inafika mahali wanaingia mkataba mbovu kama huu, tutegemee nini? Kwa sababu katika Vyuo ndiko wanapotoka wasomi ambao ndiyo wanaokuwa Makatibu Wakuu wa Wizara, wanakuwa Makamishna, lakini leo hapohapo ndipo pana ubadhirifu na kumeingiwa mkataba mbovu. Sijawahi kuona katika mradi kama huu mkubwa kwamba eti Mwekezaji anatakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 inatakiwa Mwekezaji aoneshe mtaji wa namna gani anaweza kuendesha ule mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mradi wa Mlimani *City* Mwekezaji ameonesha Dola za Kimarekani 75 ambazo ni sawasawa na shilingi 150,000 lakini mkataba huo ukaingiwa. Sasa huu siyo wizi wa mchana kweupe? Bahati mbaya haya yametokea Serikali iko kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *PAC* kama nilivyosema, tumeanza kupigia kelele haya tangu mwaka jana na tukawaita baadhi ya Maafisa wa Chuo Kikuu vilevile tukatoa taarifa kwamba mkataba wa Mlimani *City* una upungufu, tulikitegemea tangu

kipindi hicho angalau wangefanya marekebisho. Hadi leo hii nazungumza hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali kwamba katika mradi au mkataba wa Mlimani *City* pamoja na Mlimani *Holdings* bado Serikali inatakiwa kufanya kazi kubwa katika hili na kupitia Bunge hili tutoe maelekezo kwamba waliohusika na mkataba ule Serikali iwachukulie hatua za kisheria haraka na mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kuzungumza ni ukiukwaji wa malipo ya *land rent* ambapo *UDSM* ilitakiwa ipate asilimia 10 ya pango kwa mapato ghafi, badala yake *UDSM* inalipwa baada ya kutoa gharama, wao wanalipwa asilimia 10 wakati walitakiwa walipwe kabla ya kutoa gharama. Kwa hiyo, ukiuangalia kwa undani mkataba huu wa Mlimani *City* na Mlimani *Holdings* pana uchafu mkubwa umejificha hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza *CAG* kwa kuibua uchafu na ubadhirifu katika mkataba ule, lakini kama *CAG* ndio jicho letu Wabunge anatuletea taarifa na Serikali haichukui hatua, itafika mahali tutamchosha *CAG*. Serikali imwezeshe kwa kumpa bajeti anayotaka kwa asilimia 100 lakini yale anayotuletea tusioneane haya, Waswahili wanasema ukicheka na nyani utavuna mabua. Kupitia Bunge hili nataka waliohusika wote katika mkataba ule wachukuliwe hatua kali za kisheria ili iwe ni funzo na fundisho kwa wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika mradi wa *Dege* Kigamboni au *Dege Eco Village,* kuna taarifa kwa kweli zinatia kichefuchefu, kuambiwa kwamba kuna kiwanja Kigamboni kinachoweza kufikia milioni 800 cha makazi ya kawaida. Hili naona halitakiwi kufumbiwa macho. Katika hili kwa kutokana na muda ni kwamba mkataba wa *NSSF* wana asilimia 45 ya hisa na hawa *AHER* au *Azimio Holdings...*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha, naomba umalizie sentensi yako.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Nimalizie kwa kusema kwamba mkataba wa *Dege Eco* unatakiwa ufanyiwe kazi lakini vilevile pia kupitia Bunge hili, taarifa ya mabaya yote yaliyoibuliwa katika taarifa ya *PAC* na *LAAC* Bunge lako lichukue hatua za kinidhamu na lichukue hatua za kisheria. Ahsante*. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbarouk, tunaendelea na Mheshimiwa Jamal atagawana muda wake na Mheshimiwa Leah Komanya.

Mheshimiwa Jamal karibu.

**MHE. JAMAL KASSIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Kamati ya *PAC.* Nianze moja kwa moja nami kujielekeza katika masuala manne kama muda utatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza ambalo nimekusudia kulichangia leo hii jioni ni suala la *NSSF.* Bahati nzuri Kamati yetu ya *PAC* tulibahatika kuonana na uongozi wa *NSSF,* tukabahatika kukagua hesabu zilizokaguliwa za *NSSF*. Kumekuwa na hoja potofu ambayo baadhi wa Wajumbe wamezungumza na imekuwa inazungumzwa. Nimewanukuu Mheshimiwa Mussa Mbarouk, nimemnukuu Mheshimiwa Catherine Ruge katika michango yao wamesema kwamba kwenye suala la mradi wa *Dege, NSSF* imenunua ardhi heka moja kwa thamani ya Sh.800,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwape *challenge,* nimepitia hesabu na wao tumepitia pamoja, ukipitia taarifa ya ukaguzi ya *CAG,* kile kitabu kina kurasa karibia 200 na kitu, hakuna hata sentensi moja iliyoandika kwamba *NSSF* wamenunua ardhi kwa shilingi milioni 800. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia taarifa za hesabu za *NSSF*, ukiangalia *financial statements* zake, hakuna sehemu yoyote ambayo *NSSF* wameripoti au kurekodi kwamba kuna pesa au miamala ambayo wamefanya ya ununuzi wa ardhi kwa hekari moja shilingi milioni 800. Kwa hiyo, nawaomba

wasipotoshe, kama wana ushahidi waulete na nipo tayari hata kujiuzulu Ubunge wangu katika hili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge waelewe nini hasa kinachoendelea katika mradi wa *Dege*. Mradi wa *Dege* ni miongoni mwa miradi ambayo inaendeshwa kwa mfumo wa *land for equity* na mradi huu sio umeingiwa mara ya kwanza na *NSSF*, miradi hii imefanywa na *National Housing* na taasisi mbalimbali za umma na za binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la *Dege*, mradi wa *Dege* ni mradi wa ubia baina ya *NSSF* na Kampuni ya Azimio *Limited* ambayo imesajiliwa Tanzania. Hawa wawili ndio wabia wa mradi huo. Katika *modality* ya miradi hii, katika soko yule ambaye anakuja na ardhi kawaida ana-*carry an interest of* 20 *percent* ya ule mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge wajue, ukienda Arusha kuna *Palace Hotel*, ile *property* ardhi ni ya *National Housing* waliingia ubia na mwekezaji *Palace Hotel Limited, National Housing* ina asilimia 20 na *Palace Hotel Limited* ina asilimia 80. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe ukienda Morogoro leo kuna *stand* kuu ya mabasi eneo lile ni la Manispaa ya Morogoro, *NSSF* wamewekeza pale, Manispaa ya Morogoro kwa vile ardhi ni yao wame-*carry an interest* ya ule mradi ya asilimia 23 na *NSSF* wamebakizwa asilimia 77. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wajue, hiyo hoja ni hoja potofu na sijui waliokuja nayo wana malengo gani. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Safii.

**MHE. JAMAL KASSIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile hili suala lilianza kwenye taarifa ya *CAG* ya mwaka 2014/2015 ambayo bahati nzuri mwaka jana tuliichambua na tukabahatika kutoa mapendekezo, niwapongeze Serikali kwa hatua mbalimbali ambazo wamezichukua, lakini kubwa

niwaombe mradi ule *NSSF* imeingiza takribani bilioni 219, pesa hizi ni pesa za wanachama wananchi wa Tanzania ambao Serikali yetu hii ndiyo *trustee.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana mradi ule ukiendelea kukaa vile ulivyo, hauna tija kwa Taifa letu. Tumewekeza pesa nyingi, ipo haja sasa ya ule mradi kuhakikisha unatoka pale na unaenda kwenye *level* nyingine ambayo tumekusudia*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naitaka Serikali ikae na mbia ambaye Azimio *Housing Limited* kuhakikisha yale makubaliano ambayo yameanza basi yanafikia tamati mapema na ule mradi unaendelea na kuleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulivyoenda *NSSF Dege* bahati nzuri wenzetu *Management team* ya *NSSF* walitueleza mipango mizuri kabisa juu ya huu mradi. Kwanza, walituambia zile nyumba kwa bei ya mwanzo kabisa zitauzwa kwa takribani dola 120,000 na wametoa fursa kwamba Watanzania na mwananchi yeyote anaweza kununua nyumba ile kwa muda wa miaka 15 bila kupitia benki. Kwa hiyo, hii ni fursa pekee ambayo makampuni yote yanayo-*deal* na *property business* hakuna hata moja inayofanya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Jamal.

**MHE. JAMAL KASSIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kidogo nichangie eneo lingine la pili eneo la Mlimani *City.* Kwa upande wa Mlimani *City* nami niungane na maelezo ya Kamati na mapendekezo..

**MBUNGE FULANI:** Muda!

**MHE. JAMAL KASSIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja mkataba wa Mlimani *City* ukapitiwa upya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Jamal, tunaomba tuendelee sasa na Mheshimiwa Leah Komanya na baadae

Mheshimiwa Conshester Rwamlaza ajiandae atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

**MHE. ALLY M. KEISSY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *Dege* ni ufisadi mkubwa sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia katika hoja zilizoletwa na Kamati hizi mbili. Napenda nizipongeze kwa taarifa nzuri za Kamati zote hizi mbili. Kwa kuanza naomba nijikite katika taarifa ya hesabu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu ilijikita kufanya mahojiano na Halmashauri pamoja na kutembelea miradi ya maendeleo. Katika kufanya mahojiano na Halmashauri, hoja nyingi zilizojitokeza ni Halmashauri kutokujibu hoja za ukaguzi hususani katika hoja za miaka ya nyuma. Halmashauri zinafanya uzembe na mazingira yanaonesha kwamba hawataki kujibu hoja hizo kwa sababu siyo sehemu ya ku-*form opinion.* Nitoe ushauri kwa Serikali kuchukua hatua ya ziada ili hoja hizo ziweze kupatiwa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkaguzi wa Hesabu aliendelea kuibua hoja za ukaguzi ambazo nyingi zilisababishwa na upungufu uliopo katika kutumia mfumo wa kihasibu wa *EPICAR.* Kama Serikali haitachukua hatua ya ziada kuweza kutatua tatizo katika mfumo wa hesabu *(EPICAR version 9.05)* hoja nyingi zitaendelea kuibuliwa kutokana na mapungufu yaliyopo katika mfumo wa kihasibu wa *EPICAR.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu ulianza Julai 2012 leo ni miaka sita mfumo hauna *asset modal* ambayo inasababisha madeni kutokuripotiwa katika hesabu za mwisho ama Mkurugenzi kuamua kufunga hesabu kwa namna anavyotaka zionekane mwenyewe. Haina ubishi kwamba Mkurugenzi inamlazimu aichukue *trial balance*

afanye *export* akafanye kwenye *excel.* Kwa hiyo, hii moja kwa moja anaweza akafanya udanganyifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu unatumia *cash basis* na tunajua Halmashauri zinatakiwa zifungwe hesabu kwa matakwa ya *IPSAS* na *full adoption* ya *IPSAS* kwa Tanzania katika Halmashauri ilikuwa ni mwaka 2013 lakini mpaka sasa hivi mfumo huu hauna *accrual basis.* Halmashauri zimeendelea kuandika *LPO* nje ya mfumo kwa sababu mfumo hau-*support accrual basis.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama una-*support cash basis* ni changamoto kwa Halmashauri kununua vifaa kwa kutumia *cash.* Ni dhahiri kwamba siyo muda wote Halmashauri itakuwa na fedha taslimu. Kwa hiyo, inazilazimu Halmashauri ziandike *LPO* nje ya mfumo na hivyo kujikuta madeni mengine hayatolewi ripoti katika hesabu za mwisho. Kwa hiyo, ile hoja ya kulipa madeni ambayo hayakuwa kwenye hesabu za Halmashauri, hoja hii itaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ilifanya ziara katika Mkoa wa Tanga na mikoa mingine, naomba nijikite katika hoja kubwa ambayo ilijitokeza katika miradi, hoja ya upungufu katika miradi ya maji. Tunao mradi wa *RWSSP* ambao unatekeleza miradi ya maji vijijini. Changamoto mojawapo iliyopo kwanza katika *RWSSP* kuna *component* ya *sanitation* lakini *component* hiyo imekuwa haifanyiwi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeenda kukagua miradi ya Tanga ya maji, sikuwahi kuona mahali popote kwamba kuna miradi ya usafi wa mazingira. Tulienda Iringa kukagua miradi, miradi mingine ya maji imekamilika lakini ile *component* ya *sanitation* fedha zake amepewa Mkandarasi lakini miradi haijatekelezwa. Kwa hiyo, Serikali pia iangalie kipengele cha *sanitation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi iliyokamilika ina jukumu…

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Leah Komanya

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Conchesta atagawana muda wake na Mheshimiwa Heche, Baadaye Mheshimiwa Stanslaus Mabula na Mheshimiwa Kigua wajiandae.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kidogo katika hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nagawana muda Mheshimiwa Heche basi nitachangia *point* moja tu kuhusu Mfuko wa Wanawake na Vijana wa asilimia 10 ambayo inapaswa kukatwa katika mapato ya *own source* ya Halamashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya *LAAC* tumeona kwamba huu Mfuko una umuhimu wake na kwa ujumla wake unaweza ukachochea maendeleo ya vijana na wanawake pale ambapo ukitumika kwa hali inayostahili ili hawa vijana na wanawake waweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinazotoka *own sources* ya Halmashauri ni kodi za wananchi. Utaratibu wa kuzitoa kama mikopo kwa vijana na wanawake haueleweki, walengwa ambao wanastahili kupata mikopo hii wengine hawapati kwa sababu gani. Hii ni kwa sababu tumegundua kwamba hata vikundi vingine ambavyo vinapewa hiyo pesa vinakuwa ni vikundi hewa, lakini katika Halmashauri nyingi hakuna hata zile Kamati ambazo zinapaswa kukaa na kutoa pesa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kushangaza kuna baadhi ya Halmashauri hata Wakurugenzi wengine hawajui *component* ni watu gani ambao wanapaswa kuwa kwenye Kamati hiyo. Kuna Mkugenzi mmoja alisema kwamba Mbunge ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo ilhali Wakurugenzi ndio Wajumbe, kwa hiyo mnaweza kuona ni namna gani mifuko

hii inavyotekelezwa bila hata Wakurugenzi kujali kinachoendelea katika Halmashauri zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia utaratibu wa kusimamia urejeshwaji wa pesa hiyo, hizi pesa tumekuwa tukisimamia kwa karibu Kamati zote, Kamati ya TAMISEMI na Kamati ya *LAAC* tunasimamia kuhakikisha Halmashauri wanapeleka pesa ya asilimia tano kwa wanawake na asilimia tano kwa vijana katika akaunti zao ili waweze kukopeshwa. Ninachotaka kusema ni kwamba pesa hizi hazirejeshwi, huu mfuko unakwenda kisiasa kabisa, ni kama upo upo tu basi, watu wanapata pesa wanajiondokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirejea maoni na ushauri au alichokiona *CAG* katika hesabu zake za mwaka wa fedha 2015/2016 kuna pesa zaidi ya bilioni nne zinadaiwa zipo nje, zipo katika vikundi na hizi pesa ni nyingi. Hata hivyo, ni kwamba hizi pesa ambazo zipo zinatolewa na Halmashauri hazina ukomo. Tunaona kwamba hizi pesa zitolewe halafu hii mifuko iwe na kiwango fulani na pia iwe na ukomo, iwe ni *rotation fund* yaani tukisema Halmashauri moja inajiwekea malengo kwamba sasa tunakusanya ama tunakopesha mpaka tunafikisha bilioni mbili au tatu basi tunaweka ukomo na pesa zingine zinaendelea kufanya maendeleo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu nasema kwamba mfuko huu wa kisiasa tu, pamoja na kwamba ni mzuri lakini malengo yake hayatekelezwi. Sioni sababu mfuko huu kuendelea lakini pesa za wananchi zikapotea ina maana Serikali inataka kutuambia nini. Katika ripoti ya mwaka jana, Kamati ya *LAAC* tulitoa ushauri kwamba itengenezwe sheria maalum ambayo itaweza kuonesha mfumo thabiti wa kuweza kukusanya hizo pesa, kukopesha na baadaye kuzirejesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haikutoa majibu na wala haikutengeneza sheria hii. Hata mwaka huu tumerudia tena maoni hayo kwamba itengenezwe sheria ili kuwezesha mfuko huu kuwa endelevu na kuweza kusaidia wanawake na vijana kwa malengo ambayo yanastahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na mapendekezo aliyoleta Mheshimiwa Zitto hapa hata kama ni mapema kwa sababu ilikuwa kwenye mchango wangu, kwamba ingekuwa vema basi kama Serikali ikiona haitaweza kuweka utaratibu mzuri basi ianzishe Benki ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa ili kuwezesha Halmashauri kuchangia ndani ya benki hiyo na benki ikakopesha vijana na wanawake ili hizi pesa zionekane zina manufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoona kule tunapokwenda kukagua ni kwamba vijana wanachukua pesa, wanawake wanachukua pesa basi imeishia hapo, huu mfuko umekuwa shamba la bibi. Kuna baadhi ya Halmashauri wameamua kuziweka kwenye *SACCOS* lakini ukifuatilia kuona hata wale walioweka kwenye *SACCOS* hizi pesa wanaopewa siyo walengwa wenyewe. Ukipeleka kwenye *SACCOS* wanakopa wale wenye uwezo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano tumekwenda kwenye Jiji la Dar es Salaam wamepeleka zaidi ya bilioni moja kwenye *SACCOS* yao, sijui kwenye Benki huko ya Dar es Salaam, lakini hizo pesa hazijarejeshwa mpaka leo, kwa hiyo unaweza kuona kwamba hata Halmashauri zenyewe hazina usimamizi mzuri.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa John Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli anaingia madarakani miongoni mwa miradi ambayo aliwatangazia Watanzania na dunia kwamba ni miradi ya kifisadi ni mradi wa *NIDA,* mradi wa vitambulisho vya Taifa wa *NIDA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unakumbuka wakati

akina Dickson Mwaimu wanawajibishwa, Rais Dkt. Magufuli alisema kwamba kitambulisho cha kupigia kura ambacho kilikuwa na ubora kuliko kitambulisho cha *NIDA* kilitengenezwa kwa Sh.3,000 na akasema kwamba vitambulisho milioni 23.5 vya kupigia kura vilitengenezwa kwa bilioni 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akawa anashangaa inawezekana vipi kitambulisho cha kupigia kura ambacho kina ubora kuliko wa *NIDA* kikatengenezwa kwa bei ya chini huku kitambulisho cha *NIDA* kikitengenezwa kwa Sh.17,000 na akina Dickson Mwaimu wakachukuliwa hatua sitaki kwenda huko. Akampeleka pale mtu anaitwa Ndugu Kipilimba, kukaimu nafasi ya Ndugu Dickson Mwaimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitambulisho kile ambacho kilikuwa Sh.17,000 kikapanda kwa kampuni ile ya kwanza iliyotuhumiwa kupewa tenda kuongezewa muda, kampuni iliyotuhumiwa kutengeneza kitambulisho kwa bei ya juu na watu wakachukuliwa hatua, ikatengenezwa *addendum* ikaongezewa muda kisanii na kitambulisho hiki kikapanda kutoka Sh.17,000 mpaka Sh.26,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitaji maelezo ya Serikali na Mwenyekiti wa Kamati atuambie ilikuwaje taarifa hii ikaondolewa? Huu ni ufisadi na siku zote tumesema kwamba Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi inalea ufisadi na inajaribu kufunga watu midomo wasiseme ufisadi unaotokea wakati huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili jana…

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilinde niendelee na mambo ya nchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche, taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa kaka yangu Mheshimiwa Heche, anasema Serikali hii imewafunga watu midomo wasiongee, nataka nimpe taarifa kuwa yeye hapo anatumia nini kuongea? *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche, naomba uendelee.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea mambo mazito sana sitaki kufanya *comedy* hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nahitaji maelezo, siku zote na Watanzania wajue kabisa kwamba kuna mambo mengi tu yanafanyika kwenye Serikali hii ambayo yana ufisadi kuliko hata Serikali zilizopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kitu ambacho kimezinduliwa jana kinaitwa *E-Passport,* huko nyuma uliwahi kufanyika utafiti wa jinsi ya kuleta kitu kinaitwa *E-Migration, E-Migration* ilikuwana zaidi ya *components* sita, ilikuwa na *E-Passport, E-Visa, E-Border* na *E-Visa* kitu kikubwa kilichokuwa mle ni kwamba mtu anapokata *visa* akiwa hata Marekani vituo vyetu vya *immigration* hapa nchini watu waweze kusoma na wakajua ili kudhibiti mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana imezinduliwa *E-Passport* na ule mradi mzima uliokuwa na *components* sita ulikuwa ni wa dola milioni 180, jana imezinduliwa kitu kinaitwa *E-Passport* ambacho kina *component* moja tu kwa dola milioni 50, tenda yake hatujui imetangazwa lini, nani na nani walioshindanishwa. Hii nchi ina sheria na taratibu, tunaruhusu vipi nchi yetu hii miradi ya kifisadi inatokea kila leo, kila kesho na Serikali hii inayojinasibu kwamba inashughulikia ufisadi watu wachache wanatengwa wengine wanaruhusiwa kuendelea kupiga ufisadi kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Serikali za Mitaa.

Amezungumza hapa Mheshimiwa Bobali kwamba Serikali za Mitaa Wakurugenzi waliowekwa ni Wakurugenzi ambao ni dhaifu na wengi ni walioshindwa uchaguzi katika kura za maoni za CCM. Mimi sitaki kulizungumzia hili, nataka tu nimwambie rafiki yangu, Mheshimiwa Bobali, haya ni makusudi ya Serikali hii kuua Serikali za Mitaa, imekusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana hata wakati watu wanazungumza hapa kuhusu Wakurugenzi na matatizo ya Wakurugenzi, amezungumza hapa Mheshimiwa Mzee Selasini, hakukuwa na Waziri hata mmoja hapa anayeshughulika na hilo, kwa sababu nia yao ni kuua hizi Serikali za Mitaa. Ndiyo maana hata mapato ya Serikali za Mitaa yametolewa na hayarudishwi. Mapato ya mabango, kodi za nyumba zilizokuwa zinakusanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nam-*challenge* kaka yangu pale atuambie, mkitoa pesa mnazochukua kwenye mabango ninyi mapato yenu ni kiasi gani, mtuambie ni shilingi ngapi mnazopata. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Kigua baadaye atafuata Mheshimiwa Stanslaus.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa jioni ya leo niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita zaidi kwenye ripoti hii ya *PAC* kwa sababu mimi ni Mjumbe kwenye Kamati hiyo. Yamezungumzwa mengi na kuna dosari nyingi sana lakini yote yameainishwa katika ripoti nisingependa kuyarejea. Kikubwa ambacho nataka nikizungumze ni juu ya ushauri kuhakikisha kwamba yale maoni ambayo yametolewa na Kamati yetu ya *PAC* yanafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa mengi juu ya dosari katika Mkataba wa Mlimani *City,* Mkataba wa *Dege* Kigamboni. Nadhani Serikali imefanya jambo kubwa na imeshaanza kuchukua maamuzi, niipongeze sana Serikali kwa sababu baadhi ya viongozi walishasimamishwa na hii ni kuonesha kwa dhati kabisa kwamba tayari Serikali ilishaona upungufu na imechukua uamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nina ushauri mdogo, katika ripoti ya *CAG* imezungumza juu ya upungufu wa Benki ya Kilimo. Benki hii bado haijapewa nguvu, pesa au mtaji ambao Benki yetu ya Kilimo imepewa ni ndogo sana. Nashauri Wizara ya Fedha pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo wakae chini waone namna ambavyo wanaweza wakaiongezea mtaji kwa sababu sehemu kubwa ya maisha ya Watanzania yanategemea kilimo na nina imani kwamba uanzishaji wa benki hii ulikuwa na lengo la kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo liko sambamba na hilo ni juu ya suala la Mkaguzi wa Mahesabu *(CAG),* yote haya tunayoyaona kwenye Kamati za *PAC* na *LAAC* yametokana na ripoti ya *CAG* ambayo ndiyo jicho la Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lazima tukubali kwamba *CAG* anafanya kazi kubwa sana, lakini anakwama kwa sababu hawezeshwi pesa nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano tu kwamba, katika kazi yake ya *auditing* (ukaguzi) *performance auditing* ndiyo kazi ambayo inaonesha mapungufu mengi sana, lakini ukikaa na *CAG* anakwambia pesa anayopewa ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu unaojionesha katika miradi mingi ya maji, miradi ya barabara ambayo inatokea katika Halmashauri zetu inaonekana kutokana na ripoti ya *CAG.* Nadhani muda umefika sasa wa kuhakikisha kwamba tunamsaidia *CAG* ili aweze kuwa na nguvu na ili aweze kutoa ripoti nzuri.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya maji, nimepitia taarifa hapa ya *LAAC* imeonekana miradi mingi ya maji haiko vizuri. Lakini nina ushauri mmoja kwa Serikali kwamba Wizara ya Maji na wenzetu wa TAMISEMI waweke utaratibu na kuunda kikosi kazi cha kuhakikisha na kuangalia kwamba miradi hii inafuatiwa na kukaguliwa ili kuangalia ile *value for money* inapatikana, vinginevyo malengo tunayokusudia malengo ambayo Serikali wanayokusudia hayatafikiwa kwa sababu maeneo mengi miradi hii iko chini ya kiwango. Mimi nashauri tuangalie namna ambavyo suala la ufuatiliaji wa miradi linakuwa ni suala muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nina ushauri juu ya makusanyo ya mapato katika Halmashauri zetu. Tumeona Serikali imeweka utaratibu wa kukusanya mapato kwa kutumia njia ya kielektroniki kwa maana TAMISEMI wanaona moja kwa moja Halmashauri fulani inakusanya kiasi gani, lakini bado utaratibu huu haujakaa vizuri, zipo baadhi ya Halmashauri ambazo bado mapato hayakusanywi sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri Waziri wa TAMISEMI aangalie namna ambavyo anaweza akaongeza udhibiti, au kwa kuongeza mafunzo kwa watumishi wetu wa TAMISEMI ili nia thabiti ya Serikali ya kukusanya mapato katika Halmashauri zetu ifikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kulizungumzia ni juu ya suala la Mlimani *City.* Mlimani *City* imezungumzwa sana juu ya mkataba ule. Ushauri ninaoutoa ni kwamba upungufu huu Serikali ichukue hatua haraka sana kwa sababu tunapoteza mapato mengi, hata taarifa hii nina uhakika haijamaliza mambo mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nataka kushauri kwamba taasisi ambayo ilikuwa inasimamia mkataba huu ni taasisi nyeti. Nina imani kwamba Serikali itachukua hatua za haraka sana kuhakikisha kwamba dosari zote ambazo zimejitokeza kwenye mikataba hii zinafanyiwa kazi haraka sana ili wananchi wa Tanzania wawe na imani kubwa na

Serikali yetu na nina imani kabisa kwamba maoni yetu na ushauri wetu utafanyiwa kazi haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kigua. Tunaendelea na Mheshimiwa Stanslaus Mabula na baadae Mheshimiwa Zitto Kabwe ajiandae.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia angalau kwa mambo machache ambayo nimeyapitia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii ya kusimama mbele ya Bunge leo kuchangia nikiwa kama mmoja wa Wajumbe wa Kamati zilizowasilisha ripoti zake leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na namna ambavyo *CAG* ametuonesha matumizi mabaya ya Ofisi ya *ALAT.* Ni ukweli usiopingika kwamba chombo cha *ALAT* kinachounganishwa na Halmashauri zote nchini, kinapokusanya fedha zake kinakusanya fedha kwa lengo la kuendesha chombo hiki na kila Halmashauri nchini inachanga fedha kwa ajili ya chombo hiki kuendeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka michache iliyopita *ALAT* ilikusudia kujenga jengo kwenye Mji wa Dodoma lakini kama *CAG* alivyotuonesha, kwenye milioni 523 kati ya fedha hizo milioni 367 hazionekani wapi zimekwenda. Kamati ya *PAC* imeliona hili na kulileta kwenye Bunge lako ili Bunge lako liweze kushauri vinginevyo lakini kuchukua hatua stahiki juu ya fedha za wananchi kutoka kwenye Halmashauri zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende haraka haraka kidogo kwa sababu najua muda wangu ni mchache. Lipo suala la urejeshaji wa fedha kutoka *TRA* kwenda kwenye taasisi mbalimbali za Serikali, tulitamani sana kama ambavyo makubaliano na mujibu unavyotaka fedha zote

zinazokusanywa kutoka Halmashauri, kutoka wapi, inapofika wakati kwa mujibu wa sheria na misingi ile ya kuendana na bajeti zilizopangwa, fedha hizi ziende kule kwenye halmashauri zikafanye kazi yake sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa kidogo, hawa Wakurugenzi wanaopigwa mawe hii tabia ya kuzungumza unaenda mbele unarudi nyuma, ndugu yangu, Mheshimiwa Heche amesahau kidogo, dakika chache zilizopita Mheshimiwa Gekul hapa ametupa mfano bora watu tukajifunze Babati kwamba pale kuna Mkurugenzi makini anayefanya kazi yake sawasawa. Sasa matatizo ya mtu mmoja hayawezi kujumlisha Wakurugenzi zaidi ya 168, ni lazima tukubali na twende na kauli hiyo, itatusaidia kujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa *PAC* Mheshimiwa Heche amezungumza hapa habari za *NIDA,* habari za vitambulisho na kadhalika. Kamati ya *PAC* ilipokuwa inapitia taarifa zake mbalimbali, zipo taarifa zitakuja kwa wakati mahsusi na yapo mambo kama hayajakamilika hayana sababu ya kuja kwenye Bunge hili! Hii ni sambamba na taarifa ya mradi wa *Dege,* Kamati imeunda Kamati ndogo imetengeneza taarifa zake vizuri imepeleka kwa Spika zimeanza kufanyiwa kazi, Bunge tusubiri taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni lazima tukubali. Umezungumzwa hapa mradi wa Mlimani *City,* umetajwa mradi wenye maajabu saba, ni kweli. Mradi wa Mlimani *City* leo una takribani miaka 11, mradi huu toka uanzishwe tunataka kusema pamoja na changamoto zake ambazo *CAG* ameziona, kama Kamati tumezielewa. Siyo hili tu la mradi mbovu, tunaongelea habari ya Chuo Kikuu cha Mlimani kinachotoa wataalam waliobobea, kinachotoa ma-Profesa, leo ametajwa humu Waziri wa Sheria, Mheshimiwa Profesa Kabudi pale na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo mimi niwaulize kwa makosa ya mtu mmoja kuingia mikataba mibovu, mnataka

kusema watu wote waliopita Chuo Kikuu cha Mlimani uwezo wao ni dhaifu? Kwa sababu ni lazima tukubali changamoto hizi zipo na kama changamoto hizi zipo, kwa mfano, mradi huu toka ulipoanzishwa sote tunafahamu zipo faida kubwa zimeonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulipojengwa mradi wa Mlimani *City* tunaamini eneo lile limeongezeka thamani, pamoja na matatizo ya Mlimani *City* sote tunafahamu miaka 11 iliyopita ukirudisha miaka minne nyuma, Chuo Kikuu cha Mlimani kimekuwa kikipata bilioni 16 na pointi kama gawio kutoka Chuo Kikuu, fedha hizi zinaiwezesha Mlimani *City* kujihudumia kwenye bajeti yake kwa asilimia 28. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifanya hesabu ya kawaida sote tunakubali Mlimani *City* ina matatizo ya kimkataba na waliohusika wapo na hatua zimeshaanza kuchukuliwa baada ya *CAG* kutoa ripoti hii. Tunachokisema sasa Serikali baada ya mradi huu tutulie twende polepole, tunaongea *facts* hapa, hatupigi kelele, tunaongea *facts* hapa! Serikali kila mwaka inapata kodi ya *VAT... (Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Serikali kila mwaka inapata kodi ya *VAT* bilioni 18 kutoka Mlimani *City* kwenye biashara zote zilizopo pale. Sote tunakubali *property tax* takribani milioni 150, lakini *tax levy* ya Manispaa ya Ubungo zaidi ya milioni 72. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema, Kamati imebaini matatizo kwenye Mkataba wa Mlimani *City...*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stanslaus.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Tunaiomba Serikali iangalie na ifanye kazi vizuri kuhakikisha mradi huu unakamilika kwa uhakika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stanslaus, naomba usubiri na ninyi tulieni.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba Bunge lako liweze kuunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mnafanya vurugu ndiyo maana hatusikilizani. Naomba tuendelee na Mheshimiwa Zitto Kabwe atakuwa mchangiaji wa mwisho kwa upande wa Wabunge.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya naomba ukae, tunaendelea na Mheshimiwa Zitto.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utende haki.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana nami kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwapongeza Wajumbe wote wa Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)* na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* kwa kazi kubwa ambayo wameifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wafahamu ya kwamba Kamati hizi mbili ndizo ambazo zinafanya kazi ya *oversight* kwa niaba ya Bunge letu, kwa hiyo ni Kamati ambazo taarifa zake ambazo tunazijadili mara moja kwa mwaka na bahati mbaya sana siku hizi kwa siku

moja, ni taarifa ambazo ni nyeti mno kiasi kwamba zinahitaji tutulize akili zetu tujadiliane na tuweze kuwa na maamuzi ambayo yatawezesha tuweze kwenda vizuri kwa sababu kazi hizi ni kazi za Bunge, sio kazi za Serikali, kwa hiyo ni lazima Wabunge tuweze kufanya kazi hizi kwa ufanisi na kuweza kufanikisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo ndiyo taarifa zake *PAC* na *LAAC* wameleta hapa ilizungumzia mambo mengi sana, miongoni mwa mambo ambayo yalizungumzwa ni suala la Deni la Taifa. Bahati mbaya sana na nadhani hii ni kwa mara ya kwanza tangu *PAC* itoe taarifa zake kwenye Bunge hii ni mara ya kwanza hatuoni *chapter* inayohusu Deni la Taifa. *Chapter* hii ni *chapter* muhimu ni *chapter* ya lazima Mama Mwenyekiti mwakani kosa hili lisirudiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukitazama aliyosema *CAG* kuhusu Deni la Taifa inaonesha kwamba ndani ya kipindi kifupi sana Deni la Taifa limeongezeka kwa asilimia 168, lakini baya zaidi deni ambalo linatokana na masharti ya biashara limeongezeka kwa asilimia 17 ndani ya mwaka mmoja, madeni yanayotokana na masharti ya biashara, gharama zake ni kubwa sana na inawezekana uwezo wetu wa kuwalipa ukawa na matatizo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya taarifa hii ya *CAG* inaonesha kwamba taarifa ambayo Serikali ilitoa kuhusu Deni la Taifa, deni la jumla ya shilingi trilioni 3.2 halikuwamo katika taarifa ya Deni la Taifa. Tulitarajia kwamba leo tungepata maelezo ni kwa nini trilioni 3.2 hazikuhusishwa katika taarifa ya pamoja ya Deni la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, kwa mujibu wa taarifa ya *CAG* uwiano asilimia 31 ya deni letu la nje ni *commercial loans* ni madeni ya kibiashara ambapo kama nilivyoeleza hapo mwanzo gharama ni kubwa mno na sasa

hivi mwaka jana walikuja Waziri Mheshimiwa Philip Mpango na mwenzake Naibu wake wakaja Bungeni wakaomba ruhusa ya Bunge kukopa dola milioni 700 kwenye bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilikuwa taarifa ya Wizara ya Fedha kuhusiana na tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Taarifa inasema katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imepanga kukopa dola za Kimarekani milioni mia saba zile walizoruhusiwa na Bunge. Taarifa hiyo inaendelea, Serikali imekamilisha majadiliano na Taasisi za kifedha kwa lengo la kukopa kiasi cha dola za Kimarekani bilioni 1.5 maana yake ni bilioni 1.46. Kwa ajili ya kugharamia mradi wa ujenzi ya reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge* kutoka Morogoro hadi Makutupora (Makofi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Serikali inakamilisha taratibu za kusaini mikataba. Waziri Mpango ruhusa uliyopewa na Bunge dola za Kimarekani milioni mia saba. Ni wapi ulipata ruhusa ya kwenda kujadiliana kukopa ziada ya 1.5 bilioni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wote ninyi ni mashahidi, kila siku tunaambiwa tunajenga *standard gauge* kwa fedha zetu za ndani. Leo Serikali inasema tunakopa kwa nini tunawalaghai wananchi, kwa nini hatuwaelezi wananchi ukweli kwamba hatuna uwezo wa kujenga kwa fedha za ndani, lakini tunakopa kuna ubaya gani? Maana yake kukopa siyo dhambi hamna mtu ambaye hana mikopo hapa, kwa nini tusiwaambie wananchi ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunamuacha Rais anasema kwamba tunajenga kwa fedha zetu za ndani halafu tunakuja humu Bungeni taarifa za Serikali zinasema tunakopa mnamuaibisha Rais. Kwa hiyo, kuna haja ya kupata maelezo ya Serikali kuhusu masuala haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili Taasisi ya Kupambana na Rushwa *PCCB* imeundwa kwa mujibu wa sheria. Sheria Sura Na. 329, kifungu cha 47(2) cha sheria ile,

kinaitaka *PCCB* kila mwaka ifunge mahesabu yake yakaguliwe na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, yapitiwe na *PAC* yaletwe Bungeni. Toka mwaka 2016 *PCCB* haijafunga mahesabu yake ya mwaka, haijakaguliwa, hawa ndiyo watu ambao wanapambana na rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi wamemshtaki Mhasibu wao kwa wizi wamejuaje ameiba wakati hawana *audited accounts? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji maelezo ya Serikali, Taasisi hii ni *special* kiasi gani. Jeshi linakaguliwa, Mwamunyange alikuwa anakuja kwenye Kamati ya *PAC* na Makamanda wenzake wote kuelezea mahesabu ya Jeshi, kwa nini *PCCB* haikaguliwi? Naomba tupate maelezo ya kina kabisa ya Serikali kuhusiana na jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu Mama yangu Conchesta amelizungumza, *LAAC* wametoa taarifa nzuri sana ambayo inaelezea tatizo la asilimia 10. Waheshimiwa Wabunge tusidanganyane humu ndani, sote humu tumekuwa Wabunge wale ambao wamekuwa Wabunge sasa wana miaka kadhaa, wale ambao wamekuwa Wabunge muda mrefu wanajua, asilimia 10 kwa mazingira ya sasa hivi haitekelezeki. Waheshimiwa Wabunge fedha hizi za asilimia 10 siyo ndogo ni fedha nyingi ukiangalia bajeti ya ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ambayo tumepitisha hapa ndani ya Bunge hii inayotumika sasa, jumla ya fedha ambazo Halmashauri zetu zinakusanya kwa mwaka ni bilioni mia sita themanini na saba (bil. 687), asilimia 10 yake ni bilioni sitini na nane, 10 *percent* hizi kama alivyosema mama yangu Mheshimiwa Conchesta tuzibadilishe. Tuanzishe benki na Halmashauri ziingize hizi fedha kwenye ile benki vijana na wanawake wakachukua mikopo kwenye ile benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika fedha hizi kwanza zitapelekwa kwa sababu wale mameneja wa matawi ya benki watahakikisha zinapelekwa lakini pili

wananaochukua watalipa. Tutaokoa fedha nyingi sana na tutaweza kuleta maendeleo makubwa sana katika Nchi (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa tumepewa amri au maelekezo ya kwamba tuweke viwanda 100 kila Halmashauri kila Mkoa sijui kila Halmashauri au kila Mkoa. Serikali Kuu haina ardhi, ardhi ni ya Serikali za Mitaa, kosa kubwa tutakalolifanya ni kwenda kunyang'anya watu wetu ardhi walipwe fidia kidogo watu waje waweke viwanda, watu wale watapata hela kwa muda mfupi watazitumia zitakwisha. Hebu tubadilisheni kifikra, ardhi ya mwananchi inayotolewa kwa ajili ya uwekezaji iwe *land for equity*. Wananchi wapate hisa itawalipa ile kwa muda mrefu zaidi na itakuwa na mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo wamefanya, Mkoa wa Kigoma tumefanya Mji wa Ujiji *City* tumeingia mkataba na kampuni kutoka China 20 *percent*. Mradi mmoja wa hospitali utatupa *five billion* mapato ya ndani kwa mwaka mmoja. Sasa hivi mapato yetu ya ndani ni bilioni moja tu. Kwa hiyo napenda nishauri tulitazame hili, Waziri wa TAMISEMI aangalie namna ambavyo atalileta kisheria ili tulinde watu wetu tusiwafanye waje kuwa manamba wa wawekezaji bali wafaidike kutokana na uwekezaji ambao utakuwa unafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono taarifa zote hizi mbili na nina maazimio ya marekebisho kidogo kwenye taarifa moja ya *LAAC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zitto Kabwe.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia upande wa Waheshimiwa Mawaziri nitaanza na Mheshimiwa Waziri Isack Kamwelwe na baadaye Dkt. Philip Mpango na Mheshimiwa Joyce Ndalichako wajiandae, dakika tano, tano.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hizi Kamati mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kusema kwamba mwanadamu ameumbwa kufikiria mambo mengi sana kila baada ya dakika moja na fikra hizi anaziwekea mipango matakwa na haraka anaweza akaamua kutekeleza. Sisi Wabunge tena ambao hatuzidi hata 400 tuna kazi ya *digest* fikra za Watanzania zaidi ya milioni hamsini kuziwekea mipango, bajeti na kusimamia Serikali katika utekelezaji na tunaisimamia Serikali humu Bungeni pia tunaisimamia Serikali tukiwa katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Wizara ya Maji baada ya bajeti ni kutoa miongozo ya utekelezaji wa miradi ya maji kwenye Halmashauri. Moja ya miongozo ambayo imetolewa ni kwamba Serikali haiwezi kupeleka fedha katika Halmashauri lazima kwanza kazi zitekelezwe, kazi ifanyike katika viwango vinavyotakiwa. Kama kazi yetu sisi Wabunge basi ni kusimamia utekelezaji katika Halmashauri, kama kazi yetu tungeitekeleza vizuri kwenye Halmashauri hata hoja za kuisimamia Serikali ndani ya Bunge kwa vyovyote vile zingepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelizungumza hili kwa sababu nazunguka katika Halmashauri mbalimbali, nakutana na changamoto nyingi kama ambavyo zimeainishwa na *CAG* katika taarifa zake. Waheshimiwa Wabunge wametoa michango,

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lubeleje amezungumzia visima vimechimbwa sita tangu mwaka 2002 lakini havijawekewa pampu. Miongozo ipo nimpongeze sana Mheshimiwa Lubeleje ni kweli amekuwa kila wakati nikikutana naye ananiomba niende kwenye Jimbo lake nikaangalie hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Gerson Lwenge akiwa Waziri aliwahi kwenda kule lakini juzi

nimemtuma Naibu Waziri wangu na nimwahidi Mheshimiwa Lubeleje baada ya Bunge nitaenda nae tena kule, nimeshatoa miongozo kwamba kama umechimba kisima na maji yapo tengeneza *quotation, lete* tukupe fedha ili uweze kununua hiyo pampu ili wananchi wapate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bobali nikushukuru umeongea vizuri miradi mingi inakamilika bila kuwa na viwango vya thamani ya fedha inayotakiwa. Kama nilivyosema wasimamiaji ni sisi wenyewe kwenye Halmashauri. Sisi ndiyo tunaosimamia Serikali Bungeni na tunasimamia Serikali kwenye Halmashauri. Sheria tumezitunga wenyewe inabidi tuzisimamie na Serikali yetu kwa sasa wenyewe ni mashahidi mtu akifanya ufisadi ni moja kwa moja hatua zinachukuliwa hapohapo. Hili halina mashaka kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Abdallah Chikota umetoa mfano wa mradi wa Korogwe kwa Mheshimiwa Maji marefu ule mradi ulisanifiwa ukaanza kutekelezwa hadi maeneo ya Mlembule lakini ikaja kuonekana kwamba mradi ule unatoa maji kutoka Vuga, watu wa Vuga hawakupewa yale maji, tulipokuja ku-*review* ule mradi wataalam wetu waliweka hela nyingi sasa hivi tunarudia tena ili uweze kutekelezwa. Ninachoomba tu Waheshimiwa Wabunge tusaidiane katika maeneo yetu ili mambo yaweze kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia mtiririko wa fedha kama nilivyozungumza, kwanza niwashukuru sana kuweka Mfuko wa Maji. Mfuko wa Maji kila mwezi unatoa fedha hadi Desemba katika bajeti iliyopangwa ya bilioni 158 tayari Hazina imeshatoa bilioni themanini na kila mwezi kila anayezalisha *certificate* tunamlipa. Kwa hiyo, suala la mtiririko wa fedha ili uwe mzuri ni sisi Waheshimiwa Madiwani maana yake Wabunge lakini tukirudi kwenye Halmashauri tunakuwa Madiwani, tusimamie utekelezaji wa miradi wazalishe walete hati ili tuweze kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwalongo ni kweli nilitembelea Njombe. Hii miradi yote aliyoizungumza

Utengule na Changalikwa tuliitembelea, tukakuta changamoto utekelezaji haukuwa mzuri, tayari tumeunda Tume iende ikachunguze na kitu chochote kitakachopatikana ambacho ni kibaya, basi sheria itachukua mkondo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni dakika tano nimeweka mambo kidogo, nilikuwa na mambo mengi nafikiri haya yanatosheleza. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Isack Kamwele. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango kwa dakika 10.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naomba nianze kwa kweli kwa kuwapongeza Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati hizi sababu wamegusa maeneo muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu na hususani wote kwa pamoja ni lazima tupambane na ubadhirifu dhidi ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Serikali Kuu pia katika Serikali za Mitaa. Wamefanya kazi nzuri sana wanastahili pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maeneo ambayo ningependa nitoe ufafanuzi kidogo

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na suala la Benki ya Azania, ni kweli Benki ya Azania pale tuna tatizo na tatizo lenyewe ni la kisheria. Benki hii ilisajiliwa kwa Sheria ya Makampuni Sura 212. Kwa hiyo, kwa usajili huo inakuwa ni kampuni binafsi na *CAG* hawezi kui-*audit* hata kama inamilikiwa kwa takribani asilimia 92 ya hisa zinashikiwa na mifuko yetu. Kwa hiyo, huo ndiyo utata ulipo ingawa benki hii imekuwa inakaguliwa pia na makampuni ambayo *CAG* kwa nyakati tofauti anayatumia pia kukagua taasisi mbalimbali kwa niaba yake na wanawasilisha taarifa kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamewahi kukaguliwa *KPMG*, *PWC* na hivi sasa wanakaguliwa na *Ernst and Young*. Kwa hiyo, jambo kubwa hapa ninachofikiri ni kwamba *CAG* wakati utata huu wa kisheria unafanyiwa kazi ni vema angeanza kuzitazama hizi *audit report* ambazo zinakaguliwa na *Ernst and Young*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *Pride* sijui naweza nikalisema kiasi gani, kwa kifupi ni kwamba hili shauri limepelekwa Mahakamani, liko Mahakama ya biashara na limepangiwa kusikilizwa mwezi Machi tarehe za mwanzoni. Mengine yanayosemwa pengine ni magumu hayapendezi sana labda niyaache kwa sababu ni shauri ambalo liko Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulisemea ni kuhusu fedha za maendeleo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Fedha hizi tumejitahidi kutoa kulingana na makusanyo ambayo yamepatikana katika kipindi cha miezi sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha za ndani mpaka kufikia mwezi Desemba tulikuwa tumetoa shilingi bilioni 165.96 ikilinganishwa na lengo la miezi sita la kutoa bilioni 264.8. Maana yake kwa nchi nzima tayari tumekwisha kutoa takribani asilimia 63 ya lengo la nusu mwaka.

Kwa upande wa fedha za nje tulitoa bilioni 205.93 ukilinganisha na lengo la bilioni 174.5, hiyo ni asilimia 118 ya lengo. Nadhani ni vizuri hizi takwimu zikafahamika Mzee wangu Mheshimiwa Lubeleje nikitoa mfano wa Mpwapwa fedha za ndani, Mpwapwa *DC* walipatiwa shilingi milioni 884.1 wakati lengo ilikuwa ni bilioni 1.48 hii ni asilimia 60. Fedha za nje walipatiwa milioni 606.2 wakati lengo lilikuwa ni milioni 469 hii ni asilimia 129, naweza nikaendelea kutoa mifano mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano *OC* ya Babati tumetoa milioni 394 kati ya lengo la milioni 465.9 hii ni asilimia 85 kwa Babati *TC.* Kwa upande wa *DC* tumetoa mlioni 808 wakati lengo lilikuwa ni milioni 901.9, na hii ni asilimia 90 kwa ajili ya Babati *DC* kwa *OC.* Kwa hiyo siyo kweli kwamba hatujatoa fedha, tumetoa fedha. Fedha zinakwenda lakini kwa *quarter* ya kwanza nakiri kuna tatizo la upatikanaji wa fedha na hapo ndiyo kuna *slow down* lakini sasa zimeanza kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja imesema kwamba *CAG* hapewi fedha; nadhani ni vizuri tuwe tunajiridhisha na takwimu. Kwa upande wa *OC Vote 45* kwa miezi sita tumempatia bilioni 17.8 kati ya lengo la bilioni 22.2, kwa hiyo kwa miezi sita amepatiwa asilimia 80 ya lengo. Upande wa *development* ni kweli tumechelewa lakini fedha za nje tayari amepatiwa asilimia 41 ya lengo la *development* katika kipindi hicho. Kwa hiyo ni vizuri nadhani tuwe tunaziangalia hizi namba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Heche alini-*challenge* na mimi ngoja nim-*challenge* kidogo. Kwa miezi sita upande wa *property tax* tumekusanya shilingi bilioni 16.6. Sasa makusanyo ya *TRA* peke yake kwa mwezi mmoja ni wastani wa trilioni 1.2 kwa hiyo hesabu iko wazi kabisa siyo kwamba hiki chanzo ndicho *the major source* ya mapato ya Serikali hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kodi ya majengo, sisi tunaongozwa na kifungu cha 65(b) cha Sheria ya Fedha ambayo Bunge hili lilitunga mwaka jana na kinaelekeza kwamba fedha hizi zikusanywe na *TRA* moja na kuhifadhiwa kwenye Mfuko Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni kwamba mgawanyo wa utoaji wa fedha uendane na bajeti ya Halmashauri husika. Na takwimu nilizoanza kuzitoa kwa maana ya fedha ambazo tumepeleka kwenye Halmashauri zinafuata utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme pia kuhusu utendaji wa Benki ya Kilimo Tanzania. Ni kweli hili lina matatizo na Serikali imeliona na imeanza kulifanyia kazi. Tayari tumekwisha kutafuta *management* mpya kwa utaratibu wa *search* na tayari wamefanyiwa *interview* na kwa hiyo, baada ya muda mfupi kwanza tunabadilisha *management.* Na kwa upande wa mtaji ni kweli mwaka 2014 ndipo Serikali ilitoa shilingi bilioni 60 kama mtaji, lakini baada ya hapo tulitoa shilingi bilioni 206 ambazo ulikuwa ni mkopo nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika. Kwa hiyo, suala la mtaji kwa ajili ya Benki yetu hiyo ambayo ni muhimu...

**TAARIFA**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri; kwenye Taarifa ya Kamati wanasema kwamba tatizo moja wapo kwamba *CAG* anapewa pesa kidogo na yeye ameleta taarifa kwamba ameshampa kwa *quarter* hii asilimia 90. Hili tatizo lilianzia tangu kwenye bajeti, kinachosemwa hapa ni kwamba *CAG* anatengewa pesa kidogo hata kama amepewa hiyo asilimia 90 bado ni kiodgo kwenye kazi zake ndicho kilichoongelewa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na vilevile hapa anaposema, anapotoa takwimu kwamba utoaji wa pesa umeshafika asilimia 90, inawezekana utoaji huu usiwe mgao wa sawasawa kwa sababu kama kuna Mbunge analalamika kwenye halmashauri yake hajapata pesa na yeye anasema kwamba kuna asilimia 90 ameshatoa basi mgawanyo siyo sawasawa, kwa hiyo nilitaka kumpa hiyo taarifa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hayo mengine asubiri kesho, Serikali inatoa fedha kuendana na bajeti. Kama Bunge hili lilipitisha kiasi fulani kwa ajili ya Ofisi ya *CAG* ndizo hizo tunafanyakazi tukishakusanya tutampa hizo na siyo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naeleza juu ya *TADB* (Benki ya Kilimo) kwa hiyo mbali ya zile bilioni 60 ambazo tulitoa mwaka 2014, tulitoa pia bilioni mia mbili na sita ambazo tulipata mkopo nafuu kutoka *African Development Bank.* Baada ya kuimarisha utendaji katika Benki hii hapo ndiyo tutaendela kushughulikia suala hili la mtaji maana hatutaki pia tuendelee kupeleka mtaji ukazame kama kwenye shimo na kupoteza fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nitapenda kulisema ni fedha ambazo *TRA* inakusanya kwa ajili ya taasisi mbalimbali. Tunakusanya fedha kwa mfano, *wharfage* kwa ajili ya *TPA* lakini pia ziko fedha kwa ajili ya *REA, Road Fund,* maji; hizi kwa ujumla hazina matatizo. Hazina matatizo kwa sababu marejesho yake yako kwenye bajeti ya matumizi *(Appropriation Bill),* na hizi zinatolewa kuendana na utaratibu wetu wa mgao wa kila mwezi. Shida inapoonekana sanasana ni kwenye maeneo mawili; kuna *bed night levy* kwenye utalii na *cashewnut levy* kwa upande wa korosho asilimia 35. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa fedha zote hizi zinaingizwa kwenye mfuko mkuu wa hazina. Sisi tunachosisitiza ni kwamba ni muhimu sana tujiridhishe na matumizi ya fedha hizi. Fedha hizi mnajua, mifano ni mingi *boards* zilizokuwa zinakaa nje ya nchi mnafahamu, Kamati ya *PAC* imetoa mfano wa fedha za *ALAT* ambazo zimekuwa *misused.*

Kwa hiyo, ni muhimu sana kwamba fedha hizi zionekane kwenye bajeti ya matumizi na kwahiyo ziombewe na kugawiwa kama utaratibu mwingine unavyofanya. Kwa hiyo hili nadhani shida iko hapa lakini tumelimaliza kwa uoande wa korosho tayari Serikali imeshawapatia shilingi bilioni 10 na kwahioyo pale watakapoleta matumizi mengine yakachambuliwa watapewa fedha wka utaratibu wa kawaida maana wameshaingizwa kwenye mfumo rasmi wa matumizi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

**MWENYEKITI:** Tunaendeleana Mheshimiwa Joyce Ndalichako, Waziri wa Elimu kwa dakika tano.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia dakika tano nina mambo mengi lakini nitajitahidi kuongea kwa muda niliopatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuishukuru Kamati kwa taarifa lakini pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia na hususani maeneo ambayo yanahusu sekta ya elimu. Kwa hiyo, nitaanza moja kwa moja kuzungumzia suala la *Mlimani City* ambalo limezungumzwa sana kwenye Kamati lakini pia limechangiwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba Serikali inatambua kwamba katika utekelezaji wa mkataba huu wa *Mlimani City* yapo maeneo ambayo kuna ukakasi katika utekelezaji, na tayari Serikali ilikwishaanza kuchukua hatua. Kama ambavyo Kamati imeeleza kwamba imekuwa hairidhishwi na mazungumzo kati ya mwekezaji na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ni kweli kulikuwa na ugumu hata wa hawa watu kukaa mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tarai Serikali imekwishamlazimisha yule mwekezaji kufanya mazungumzo na mwekezaji amekiwshakubali na sasa hivi Serikali inaangalia ni nani awe kwenye timu ya majadiliano ili kuangalia vipengele vya mkataba ambavyo havitekelezwi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilihakikishie Bunge kwamba Serikali ya Awamu ya Tano ina dhamira ya dhati ya kulinda rasilimali na ndiyo maana tulileta hapa Bungeni Sheria ya kulinda rasilimali yetu. Kwa hiyo, hili halina mjadala lazima

Watanzania wanufaike na rasilimali yao, pale mwekezaji amechukua ardhi, kwa hiyo, lazima Serikali ihakikishe tunanufaika kama ambavyo imekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kwamba miaka 13 sasa mradi wa hoteli ya nyota tatu bado haujaanza. Ni kweli kwamba bado haijaanza kujengwa, lakini niseme kwamba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam bado kinamkomalia mwekezaji na kwa sababu muda wa kumaliza uwekezaji ni Disemba, 2019. Tutahakikisha kwamba hilo suala tunaendelea kulisimamia kama ambavyo liko kwenye mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme tu kwamba baadhi ya wachangiaji wamekuwa wakionesha kwamba huu mradi hauna manufaa kabisa. Naomba tu kwa ajili ya kuweka *records* vizuri; niseme tu kwamba hwa wa Mlimani *city* wamekuwa wakikilipa Chuo Kikuu cha Dar es salaam takribani bilioni mbili kwa mwezi na hata zile samani zilizowekwa katika hosteli mpya za Chuo Kikuu cha Dar es salaam zimenunuliwa kwa kutumia fedha ambazo zinalipwa na mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile pia huu mradi umeweza kutengeneza ajira kwa Watanzania zaidi ya 1,600 ajira za moja kwa moja na ajira ambazo tunasema ni *indirect employment.* Pia hili eneo limekuwa sehemu ambayo watu wengi wamekuwa wakienda pale kupumzika na kupata burudani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa nataka kusema kwamba si kwamba hakuna manufaa kabisa, lakini kuna vipengele vya mkataba ambavyo havitekelezwi vizuri na hivyo Serikali tayari imeshamlazimisha yule mwekezaji ambaye alikuwa na ugumu wa kuzungumza na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikuhakikishie kwamba chini ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano hakuna mtu yoyote ambaye anataka kuhujumu rasilimali yetu atakaebaki salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala ambalo kaka yangu Paroko Selasini alizungumzia kuhusiana na utekelezaji wa elimu bila malipo. Kwanza nimshukuru sana kwa sababu naona anaelewa vizuri waraka huu ambao ndio unatoa mwongozo wa namna ya kutekeleza elimu bila malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda niseme tu suala ambalo amelizungumzia ambalo limeleta ukakasi. Baada ya sisi kukemea wale ambao walikuwa wanatoa michango ambayo ni kinyume na maelekezo hayo; sasa kuna watu wengine wanataka kupotosha, wanasema kwamba hata vyakula kwa wanafunzi wa kutwa hawaruhusiwi kuchangia hii si kweli, huu waraka umebainisha bayana majukumu ya wadau mbalimbali; na kwa ridhaa yako na kwasababu hili jambo ni muhimu kwa Taifa naomba uniruhusu nitolee ufafanuzi ili mkanganyiko unaondelea usiendelee kujitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waraka unasema wazi kabisa, wajibu wa Mkuu wa Shule ni kuwapa maelekezo wazazi kuhusu aina na vifaa vinavyohitajika. mfano rangi ya kitambaa cha sare ya shule, idadi ya madaftari, vitabu na kadhalika. Kilichokuwa kinajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tafadhali dakika mbili tu.

**MWENYEKITI:** Malizia kidogo.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Kilichokuwa kinajitokeza baadhi ya walimu walikuwa wanalazimisha wazazi kununua sare shuleni kwa bei ambayo ilikuwa ni kubwa ukilinganisha na vile ambavyo mzazi angeweza kununua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye suala la chakula ambalo limeleta sintofahamu; huu waraka unasema

wazi kabisa kwamba ni jukumu la mkuu wa shule kushirikiana na jamii katika kuweka utaratibu wa kutoa huduma ya chakula cha mchana kwa wanafunzi wa kutwa au kutoa chakula na husuma nyingine kwa wanafunzi wa bweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye Kamati ya Shule pia inasema ni jukumu la Kamati ya Shule kushirikiana na jamii katika kuweka utaratibu wa kutoa huduma ya chakula kwa wanafunzi wa bweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu ka kusema kwamba, hakuna mahali ambapo ama Serikali kwa kupitia waraka ama ufafanuzi wowote ambao umetolewa na viongozi umekataza wazazi kwa hiari yao kuweka utaratibu wa chakula na michango mingine shuleni. Kwa hiyo niwatake wakurugenzi na watu wote ambao wanasimamia utaratibu huu kuhakikisha kwamba wanazingatia huu waraka kama ambavyo umeainishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndalichako.

**MBUNGE FULANI:** Utugawie waraka huo.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Jafo kwa dakika 10 na baadae tutamalizia na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwa dakika 10.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawagawia waraka kama walivyoomba, samahani. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza awali ya yote napenda sana kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha mwaka huu wa 2018 na hili ni Bunge letu Tukufu tumekutana Bunge la Wabunge wenyewe kwa sababu ndiyo Kamati za Bunge zinawasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kupongeza Kamati zote mbili na nipende kuwapongeza kwa dhati ya moyo wangi Wenyeviti wa Kamati na Wajumbe wao wote. Mimi nashukuru sana Kamati ya *LAAC* tumekaa muda mrefu sana tukijadiliana, kwa kweli imetupa mwongozo mkubwa sana wa nini tunatakiwa tufanye katika kuhakikisha kwamba tunazisimamia vizuri Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mgheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika kamati ya *LAAC* nimekuta hoja hii ya fedha za *ALAT* ambazo zimetumika kinyume na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli chombo kile huko nyuma kilikuwa hakiendi vizuri na ndiyo maana hivi sasa kuna timu imeundwa na leo hii Kamati Tendaji ya *ALAT* Taifa iko hapa Dodoma kwa ajili ya kupitia repoti ya ukaguzi maalum iliyofanywa. Lengo lake ni kwamba yale yatakayobainika hatua mbalimbali ziweze kuchukuliwa. Kwa hiyo, ni jukumu la Serikali kwamba inapopata repoti kuhakikisha inafanyakazi vya kutosha kuhakikisha kuondoa machafu yote. Sisi tumejipambanua, ajenda yetu ni kuhakikisha kwamba pale kwenye maovu ya aina yoyote tuweze kuyafanyia kazi kwa mustakabali mpana wa rasilimali za nchi yetu ziweze kukaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli taarifa ya Mkaguzi Mkuu imeeleza suala zima la manunuzi yasiyozingatia Sheria na utaratibu na kweli hili lilitokea huku nyuma. Kamati ilizibainisha wazi, na halmashauri mbalimbali zilizoitwa pale kuna maelekezo mengi yalitolewa. Hata hivyo jukumu letu sisi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika hilo, tuliweza kuchukua hatua mbalimbali kwa wale wote ambao walikiuka taratibu. Tumechukua hatua takribani kwa watumishi wapatao 434, kati ya hao tisa wamefukuzwa kazi, 210 wamepewa maonyo mbalimbali, watumishi 15 wapo katika vyombo vya dola, lakini 28 wamesimamishwa kazi kwa ajili ya uchunguzi, wapatao 64 wako katika hatua ya uchunguzi mbalimbali za kiupelelezi, 13 wametakiwa kulipa fidia hasara waliyoisababisha katika maeneo yao hali kadhalika watumishi wanne wameshushwa vyeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kubwa la hili ni kutekeleza yale ambayo yamebainishwa katika repoti mbalimbali. Hili ni jukumu letu, lazoma tuweke nidhamu katika nchi yetu. Kwa sababu Halmashauri zetu; kwa mfano tukichukua bajeti ya mwaka huu ya trilioni 31.7 karibu trilioni 6.58, asilimia 20.7 ya *total budget* iko katika halmashauri zetu. Kwa hiyo tusiposimamia vyema tutaliangusha taifa hili. Kwahiyo naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati, na maagizo mbalimbali tunaendelea kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajenda nyingine ni kuhusu ukusanyaji wa mapayo. Ni kweli Halmashauri zetu huko nyuma tulikuwa tunakusanya watu wanasema kwa zile *receipt* za ngalawa. Sasa kuna maelekezo mbalimbali ya jinsi ya kutumia mifumo ya *electronic* katika Halmashauri zetu. Katika jambo hili tumefanya hatua mbalimbali na hasa kuzihimiza Halmashauri zijirekebishe katika ukusanyaji wa mapto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru tunapozungumza Halmashauri zote 184 zimeshaingia katika mifumo huo wa ukusanyaji wa mapato. Kwa hiyo hii ofisi yetu imehakikisha kwamba inetekeleza agizo hili, vilevile Kamati wanafaham. Katika hatua mbalimbali Kamati ya TAMISEMI na Kamati ya *LAAC* tumeendelea ku-*report* kwamba tumeweza kutekeleza katika yale ambayo maeneo hapo awali yalikuwa na mapungufu makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo naomba niwaombe Wabunge wenzangu, sisi tukiwa kama Madiwani katika Halmashauri zetu, hata hii mifumo ikiwepo bado kuna watu wengine wana-*divert* kutoka katika mifumo hii. Badala ya watu kuhakikisha tunasimamia lakini kuna watu wengine wanatumia mifumo mingine kwa sababu wameshazoea ubadhirifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana mifumo hii sasa ipo, tusisitize katika Halmashauri zetu na kuhakikisha wale ma-*accounting officers* katika Halmashauri zetu na wasimamizi wao wote wa chini wahakikishe fedha

zinakusanywa, zinaingia katika mfuko ili hatimaye tuweze kupata mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nyinyi mnafahamu, hata katika sekta ya afya kwa kutumia mifumo leo hii tumepata faida kubwa sana. Hospitali zilikuwa zinakusanya wastani wa shilingi 150,000 mpaka 200,000 kwa siku lakini leo hii wanakusanya kuanzia milioni moja mpaka milioni 1.5 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *variation*kubwa sana, ukiangalia hospitali nyingine kwa mwezi wanakusanya takriban wastani wa shilingi milioni nne sasa wanakusanya milioni ishirini na sita mpaka milioni arobaini. Kwa hiyo mfumo wa ukusanyaji wa mapato; na mimi niwashukuru sana Kamati zote, Kamati ya *LAAC* kwa ajili ya kubainisha hili na kutoa maelekezo na Kamati ya TAMISEMI inayotusimamia katika jambo hili. Tumepata mafankio makubwa; na mimi nina imani tutaendelea kuweka msingi mzuri wa ukusanyaji wa mapato katika maeneo mbalimbali

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajenda nyingine iliyobainishwa ni suala la mikataba. Kwamba kuna usimamizi mbovu wa mikataba; na ndiyo maana naomba niwaambie kwamba sisi ofisi yetu baada ya kuona hili sasa tumejikita katika kusimamia mikataba. Naomba niwaambie kwamba tumeshaanza kuchukua hatua mbalimbali na ninyi wenyewe nio mashahidi. Hata mwaka huu kama mlivyoona kwamba suala la mikataba inayokiuka utaratibu, hasa kule Nkasi tumemsimamisha Mkurugenzi kwa ajenda tu hii ya usimamaizi wa mikataba; pamoja na maeneo mbalimbali. Mmesikia maeneo hata Butiama juzi tumemsimamisha Mkurugenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo sasa hivi tunawafanyia *vetting* Wakurugenzi ambao wanashindwa *commitment* zao za kazi. Ndiyo maana hata ndugu yangu pale Nape ameshika shavu hapa ananisikiliza, niwaambie tu kwamba nafanya kazi kweli kweli tunahakikisha kwamba tutafanya *vetting,* na Mheshimiwa Rais ameteuwa hawa Wakurugenzi wana uwezo mkubwa. Hata hivyo lakini wale

watakaobainika baada ya kuona kwamba mambo mengine hayaendi vizuri si jukumu la Serikali hii kuvumilia watu ambao wanashindwa kutimiza wajibu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la miradi ya maji. Ni kweli, na bahati nzuri kaka yangu *Engineer* Kamwelwe amelizungumza hapa; tutalisimamia. Waheshimiwa Wabunge mnafahamu huko tulikopita kuna maeneo mengine wakandarasi wengine tumewatoa katika miradi hii ya kazi. Lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba tunapata wakandarasi ambao wako *competent. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na tatizo lingine la wasimamizi, wakandarasi na washauri. Wakati mwingine kulikuwa na *negosiation* inafanyika kuhusiana na miradi hii ndiyo maana ilikuwa inaenda vibaya. Mnakumbuka tulivyokuwa Korogwe kule nilimuomba Mheshimiwa Rais atupatie fursa ya ku-*blacklist* wakandarasi wote wa miradi ya maji, hali kadhalika miradi ya barabara ambao wanakwamisha. Naomba niwaambie hili zoezi sasa hivi linaendelea na si muda mrefu mtaona watu mbalimbali wakili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba niwasihi Wabunge. Kuna wakandarasi wengine ni marafiki zetu. Wakati tunawashughulikia naomba mtuache tuwashughulikie kwa nidhamu ya nchi hii, kwa sababu hatuwezi kukubali fedha ambazo zinaenda kwa wananchi kuna watu wengine wanazifanyia mambo ya hovyo ambayo hayakubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili suala zima la asilimia tano. Ni kweli kwamba historia ya huko tulikotoka hii asilimia tano ilikuwa haiendi vizuri. Wale walio katika Kamati ya TAMISEMI wanafahamu kwamba tuliitengeneza bajeti *guideline,* kwamba lazima kila Halmashauri itenge asilimia tano kwa vijana na asilimia tano kwa akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha uliopita takribani shilingi bilioni 19 kwa mara ya kwanza ziweze kufika katika Halmashauri zetu. Mwaka huu tuna zaidi ya shilingi bilioni sitini na moja kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017, 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zitto amezungumza hoja hapa, leo hii tuna Bodi yetu ya Serikali za Mitaa; nimewaambia wataalamu wetu, kwamba fedha hizi kwa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa tunaweza tukatengenezea utaratibu na tukaweka mfumo mzuri ili Halmashauri zetu zipeleke huko moja kwa moja kwa utaratibu mzuri ili watu waweze kukopa na hatimaye *compliance* ya ulipaji wa madeni iweze kuwa vizuri. Watu wanaona hizi fedha zinatolewa kama sadaka, hapana hizi fedha zimelengwa ni kwaajili ya kuwasaidia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nishukuru sana, katika mwaka huu wa fedha Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wamesimama hapa kushuhudia yaliyotokea leo hii katika Halmashauri nyingi. Hii ni tofauti na yaliyotokea nyuma ambayo ripoti hii leo tunaijadili. Kwa kiwango kikubwa maeneo mengi watu wameendelea kufanya vizuri. Katika hili niwasihi Waheshimiwa Wabunge fedha hizi siku zote nasema zinabaki katika Halmashauri zetu kule kule hazifiki kwa Dkt. Mpango, hizi ni Kamati ya Fedha kila mwezi tunakusanya mapato yetu. Naomba tusaidiane katika kuhakikisha kwamba tunasimamia fedha hizi ili vijana wetu na akina mama katika maeneo hayo waweze kupata fursa ya mikopo ambayo itawasaidia katika uwekezeji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndiyo maana ile ajenda yangu ya kusema viwanda vidogo 100 katika kila mkoa; tena nilisema viwanda vidogo vidogo na maana yangu ni kwamba kiwanda kidogo *unit price* ya kiwanda kidogo kina *range* kati ya shillingi milioni tano mpaka milioni kumi. Ukija katika bajeti yetu ya takriban shilingi bilioni sitini *plus.* Ukizungumza *unit price* ya kiwanda cha wastani cha milioni 10 unazungumza viwanda takribani 6000 hata nusu ya pesa

hiyo ikitoka karibuni bilioni 30 unazungumza karibuni viwanda 3000 tume- *outstand expectation* ya viwanda 2600 kwa mikoa yote. Kwa hiyo, nilizungumza *target* ile ili viongozi tuweke *leadership* ya kuhakikisha tunawahamasisha watu wetu, ambao wengine ni wadogo wadogo wanataka kusaidiwa. Hii ni sehemu ya *employment* kwake la kumuwezesha kufuka katika suala zima la kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuhakikisha maagizo ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali zinafuatiliwa, jambo hili tumelichukulia hatua kali sana. Tumewaagiza Wakurugenzi wote kwamba tutawapima kwa utekelezaji wa maagizo ya *CAG.* Jambo hili nimeripoti mpaka katika Kamati na tuko *firm* katika hili; na naomba niwaambie mtaona kundi kubwa la Wakurugenzi tutawaondoa katika nafasi zao, wale wataoshindwa ku-*meet target* ambayo tumewaelekeza; kwa sababu nikijua hapa hii ndiyo sehemu ambayo inaenda kujibu matatizo ya wananchi wetu ili hatimaye waone kwamba maeneo mbalimbali wananchi wanapata fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa fursa hii, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Jafo. Tunamalizia na Mheshimiw Mwigulu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi niweze kusema machache kwenye hoja zilizojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimejitokeza hoja takribani tatu ambazo zinahitaji kutolewa ufafanuzi, na mimi nitaenda moja baada ya nyingine. Nikianza na hoja iliyojitokeza kuhusu ununuzi wa magari ya polisi.

Kwanza nishukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kusema hoja hiyo lakini nitoe majibu ya Serikali kwamba jambo hili Serikali inalijua na limeshafanyiwa kazi kwa kiwango kikubwa sana. Niwakumbushie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba kabla jambo hili hata halijatoka kwenye

ripoti hii Mheshimiwa Rais ameshafanya ziara bandarini alishatoa maelekezo na baadhi ya vyombo vinaenedelea kufanyia kazi, kila chombo na nafasi yake ya utaalamu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna timu zinazofanyia kazi upande mmoja tu wa ubora wa magari na hilo ni jambo ambalo na Waheshimiwa Wabunge wamelisemea, hakuna gari bovu litakalopokelewa. Kuna timu inayofanyia kazi kuhusu ubora wa magari, lakini kuna timu ambazo zinafanyia kazi kuhusu masuala ya kiujumla ya kimkataba. Nimpongeze pia Mheshimiwa Naibu wangu *Engineer* Masauni baada ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwenye Wizara na yeye alishaenda akiwa na Katibu Mkuu pamoja na *IGP.* Kuna timu ambayo inaundwa na watu wa kutoka ofisi tofauti tofauti ambao nao wanafanyia kazi jambo hili hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna vyombo vingine ambavyo vinafanyia kazi upande wa kimaadili kama kuna maeneo kama ambavyo Kamati iliweza kusema yanayohusisha mambo ya kimaadili, kuanzia mchakato wa kwanza mpaka ukamilishwaji wake. Jambo moja tu ambalo Kamati ilisema kwamba magari yamelipiwa *cash,* si *cash.* Utaratibu unaotumika wa *credit export guarantee* ni kwamba nchi na nchi zinaingia mkataba, zikishaingia mkataba malipo yanakuwa yanafanywa na yule aliye *guarantee* mkopo ule, pale ambapo *recipient* atakuwa amepokea na kukiri kupokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo baada ya *units* za kwanza kuwa zilipokelewa, mnakumbuka yalikuwa magari takribani 77, ndipo malipo yakafanyika kwa zile *units* ambazo zilikuwa zimepokelewa. Kwa hiyo si kwamba fedha zote zimelipwa kabla ya magari kupokelewa, si hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kwa ujumla wake kwa hoja zilizojitokeza yale yote ambayo yana makandokando yanafanyiwa kazi na Serikali kwa hatua ya mbele kabisa kabisa katika kuhakikisha hatua hizo zinachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wabunge mimi niwaombe muendelee kuiamini Serikali, muendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Rais na hakuna kitu ambacho kina ukakasi kitakachofanyika, Serikali iko macho na iko mbele ya matukio kuhakikisha kwamba hatua zinachukuliwa haraka iwezekanavyo pale ambapo panatokea kuna jambo lisilo la kimaadili limefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili limesemwa ni hili la upande wa mkataba wa Vitambulisho vya Taifa, amelisemea babu yangu Mheshimiwa Heche. Niseme tu kwamba taarifa alizozisema si sahihi na kile ambacho kimefanyika. Moja, amesema kwamba mkataba ulibadilishwa na bei ya kitambulisho ikabadilishwa.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lilofanyika liko namna hii; ni kweli Serikali ilikuwa na mkataba na kampuni ile ya kutengeneza vitambulisho vya uraia na kulikuwepo na makubaliano ya kimkataba ya malipo pamoja na urefu wa mkataba. Hata hivyo kwa kuwa kuna baadhi ya vitu vilikuwa bado havijakamilika havikukamilika vyote kwa mfano mambo kama ya *connectivity* mambo ya *server*, mambo ya *integration* mmeona mengine yamekuja kuanza kukamilika wakati *printing* zikiwa zimeshaanza kufanyika, yakiwemo na mambo ya malipo pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kilichofanyika muda wa utekelezaji wa mkataba ulikuwa unafika, mwisho muda wa utekelezaji ulikuwa unafika mwisho. Mathalani tukienda kwa uhalisia wenyewe ulikuwa unatakiwa uishie Septemba 2016. Sasa mwaka 2016 imefika *server* hazijakamilika zile *ID* zenyewe *raw card* hazijakamilika, malipo hayajakamilika. Kilichotakiwa na ambacho kimefanyika ilikuwa ni kuwapa ruhusa ya kuendelea kufanya kazi lakini kwa fedha ile ile kwa makubaliano yale yale kwa gharama zilezile hakukwepo na makubaliano mapya ya bei za vitambulisho wala fedha zingine zaidi ya zile ambazo zilitakiwa zifanyike katika mkataba huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, kama ambavyo nimesema tangu mwanzo na namjua babu yangu Mheshimiwa Heche, tangu akiwa kwenye BAVICHA kule haka kawimbo ka ufisadi kalikuwa kananoga sana majukwaani. Hata hivyo nikuhakikishie tu si kwa awamu hii, Serikali iko macho na inachukua hatua mara panapokuwepo na jambo lenye harufu za aina hiyo na kama kuna mtu anadhani haya ninayosema siyo atasubiri sana. Mimi niwahakikishie Serikali iko macho na wala hairuhusu harufu za aina hiyo ziweze kujitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la mwisho lililoongelewa lilikuwa la *passport.* Hili na lenyewe taarifa alizozisema sio hizo na mimi niwaaambie kwamba mwanzo upembuzi uliokuwa unafanyika na hatua ambazo zinachukuliwa kabla ya Serikali haijaingilia kati, ukubwa wa mradi ni ule ule na fedha zilizokuwa zinatarajiwa kutumika ilikuwa dola takribani milioni 192; ukiweka na *VAT* zilikuwa zinaenda kwenye mia mbili *plus*. *Component* zile kama ulizosema zilikuwa zile nne.

Sasa hivi tunachotofautisha sasa babu yangu anasema imekuja kufanyika *component* moja kwa dola milioni 50 si hivyo *component* ni zilezile nne na kinachofanyika na kilichofanyika jana ni kwamba tunaanza na *component* ya kwanza, lakini mkataba ambao umesainiwa una *component* zote nne na ni sharti uanze na kimojawapo ambacho kina uharaka ni dola milioni 57.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatumika kwa *component* zote. Tunaanza na *e-passport* tutaenda *e-gates,* tutaenda *e-permit* na tutaenda la mwisho ambalo kwa mfululizo ambao sio huu niliioutaja tunatoka *e-passport*, tunaenda *e-visa*, tunaenda *e-gates*, tunaenda *e-permit* ni dola milioni 57.8. Hii ndiyo tumeshaanza na hicho ndicho kitakachofanyika. Sasa mimi ninayesema ndio Waziri wa Wizara ninyi kama mna *retire imprest* hapa rudisheni hizo taarifa hizo mnazozitoa si sahihi, hizi ninazosema ndio taarifa sahihi za jambo linaloenda kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Waheshimiwa Wabunge wengine ambao mnajua kazi inayofanyika nitoe wito kwamba sasa mnaweza mkafanya *application online* mkapata *e-passport* mtakapoenda Dar es Salaam mtaenda kupiga picha. Hapo hapo unapomaliza kupiga picha ukimaliza kupanda juu unaenda kuchuka *passport* yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tuko *online* hapa ulipo unaweza ukaingia kwenye mtandao ukafanya *application,* ukatuma picha halafu utakapozungukia Dar es Salaam ukapate *passport.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wabunge na kwa Mtanzania yeyote ambaye anataka apate *passport* ya kisasa ambayo inatumika duniani si lazima kusubiri kwanza kile kitabu kingine kiishe hata sasa unaweza ukapata hiyo nyingine na ukaendelea kuitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limefanyika kwa uangalifu mkubwa. Mimi nimpongeze na nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutoa fedha pia kwa kutoa dira nzuri sana ambayo imetuweka kwenye historia nzuri, na jambo hili limezingatia matumizi bora ya fedha za walipa kodi watanzania na si vinginevyo kama ambavyo ndugu yangu alitaka kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge kwenye hizi hoja zilizojitokeza niwahakikishie kwamba hatua thabiti zitachukuliwa pale ambapo Serikali imeshaona kuna jambo la kuchukua hatua, lakini kwa hizi zingine Serikali imezingatia matumizi bora ya fedha za walipa kodi na miradi ambayo imetekelezwa inatekelezwa kwa umakini mkubwa tena kwa ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *passport* yetu hii ambayo imeshatoka mtachukua hata nninyi na mtakayechukua Yule atakayesafiri aende aifananishe na ya Marekani, aende aifananishe na ya Uingereza, yetu itakuwa ya kisasa kuliko ya Uingereza naitakuwa ya kisasa kuliko ya Marekani ya sasa.

Ninaamini na wao watataka kufanya za kisasa baada ya kuwa tumeshaenda kwenye teknolojia ya kisasa zaidi na kampuni iliyofanya kazi hii ilishashinda kwenye *European union* ilikuwa na *passport* za kisasa kuliko zote kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni kitu ambacho nakisema na ni kitu ambacho ni cha uhakika nakushukuru sana na naunga mkono maelezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Mawaziri katika hoja zingine zote, Serikali iko macho, iko macho, iko macho kupindukia na imebeba dhamana ya kuhakikisha kwamba inawafikisha Watanzania kwenye matarajio yao nakushukuru sana asante sana kwa kunipa fursa hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, sasa nampa nafasi Mheshimiwa Jesnista Mhagama kwa sakika tano.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani nitatumia dakika chache tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba kama ni kwa muktadha ya taarifa ya *PAC* ambayo tunayo hapa mezani leo na hasa katika suala la Mradi wa Dege; taarifa ya *PAC* imejipambanua wazi imesema ukienda ukurasa wa 18 kwamba *PAC* ilishafanya kazi yake na tarehe 13 Februari, 2017 imewasilisha taarifa ya kamati ndogo ilyoundwa ndani ya *PAC* kwa Mheshimiwa Spika ili utekelezaji wa yale yaliyopendekezwa na kamati kuhusu Mradi wa Dege yaweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda ukurasa wa 44 wa Taarifa ya *PAC* inasema unaiagiza na kuipendekeza kwa Serikali kwamba Serikali itekeleze mapendekezo ya kamati yanayohusu Mradi wa Dege mapema iwezekanavyo ili kuokoa fedha za umma zilizowekwa katika mradi huu. Ndiyo maana nimekwambia hapa mimi nasimama wala siwezi kutumia dakika nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali tunaagizwa kutekeleza maagizo ya kamati tunasubiri basi Bunge tuleteeni kwasababu bado hatujapokea taarifa hiyo ili sisi tuweze kutekelezwa hayo yaliyoagizwa na Kamati ya *PAC. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mara mtakapokuwa mmetuletea tutafanya wajibu wa kutekeleza lakini wakati huo tunaposubiri tumeshafanya kikao na bodi yetu ya *NSSF*, Bodi yetu ya *NSSF* tulicho waagiza ni kuhakikisha wana hakikisha ile fedha bilioni 219 ambazo ni fedha za wanachama, kama kuna mazungumzo, kama kuna jambo lolote, jambo la kwanza ni kuhakikisha bilioni 219 hazipotei ambazo ni fedha za wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuisema hapa ni kwamba *PAC* tunawapongeza, mnaendelea kufanya kazi zenu kwa utaratibu unaotakiwa. Kwa hiyo, mara mtakapotukamilishia, mkatuletea ripoti na mkaona ripoti hiyo inatakiwa ije Serikalini ili Serikali tutekeleze yale mliyoagiza sisi kama Serikali tuko tayari na tunawasubiri; tuleteeni tuweze kuchukua hatua mtakazozisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niendelee kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, jana tumetunga sheria ya kuunganisha mifuko na nilishawaambia kwamba kwenye suala la madeni ya Serikali kwenye mifuko na hasa fedha ambazo zinahusu michango ya wanachama Serikali tayari imeshalipa trilioni 1.3 ili kuhakikisha kwamba michango ya wanachama inakuwa salama. Masuala mengine tunamwachia Mheshimiwa Waziri wetu wa fedha ataendelea kuyafanyia kazi kwa utaratibu unaotakiwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niokoe dakika zako, kwa sababu haya ndiyo yaliyojiri kwenye sekta ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ninakushukuru kwa kunipa muda.

**MWENYEKITI**: Ahsante Mheshimiwa Jenista Mhagama. Waheshimiwa Wabunge tumemaliza michango ya Waheshimiwa Mawaziri, sasa namkaribisha Mwenyekiti wa

Kamati ya *PAC* aweze kuja kuhitimisha hoja yake ya taarifa kwa dakika 30.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii tena ya kuweza kufanya majumuisho ya taarifa ya *PAC* tuliyoileta asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kukushukuru tena wewe binafsi kwa kuongoza mjadala huu tangu asubuhi mpaka sasa hivi. Naomba pia niwashukuru wachangiaji wote waliochangia hoja hii; kwa kuwa wengi wanaunga mkono taarifa ya Kamati katika kusimamia matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahili kwamba Waheshimiwa Wabunge wanachukizwa na matumizi mabaya ya fedha za umma. Wachangiaji waliochangia ni wengi akiwemo Mheshimiwa Allan Kiula ambaye amezungumzia mradi wa *Mlimani City*, Suma JKT, Polisi na *TANESCO*. Mheshimiwa Munde pia ameongea kwa undani mambo ya *TANESCO* na *NSSF*, Mradi wa Dege pamoja na *Mlimani City,* Mheshimiwa Catherine amezungumzia *Mlimani city* na *NSSF.* Wote hawa pamoja na wachangiaji wenzangu wengine ambao si rahisi kila mmoja kusema eneo lake.

Lakini Mheshimiwa Gekul amezungumzia mambo ya *Pride,* Mheshimiwa Mussa Mbarouk amezungumzia mambo yote yaliyoko kwenye taarifa yetu, Mheshimiwa Kigua mambo ya *ALAT* na Mheshimiwa Mabula umesisitiza ripoti ya Kamati Ndogo ambayo mwisho iliridhiwa na Kamati yote kwa Spika na pia akazungumzia mambo ya *Mlimani City.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wenzetu wengine wamechangia kwa kuleta kwa maandishi ambao ni wengi na nafikiri majina yao ninayo. Walioleta ni pamoja na Mheshimiwa Rhoda Kunchela, Mheshimiwa Mary Muro ameleta pia, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Lucia Mlowe na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipende kutoa masikitiko yangu kwamba Kamati, *especially* hii yetu ya *PAC* na *LAAC* tunapewa muda mfupi sana wa kushughulikia hesabu hizi za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma pamoja na Serikali za Mitaa. Kwa uzoefu wenzetu wa Mabunge mengine hata ukienda Bunge la Uingereza unakuta kazi ya *PAC* ni ya kudumu, wana ofisi wanayofanyia kazi kwa muda kwa hiyo wanajipanga vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi muda tunaopewa ni mdogo sana. Wiki mbili uwe *field,* wiki moja uandae taarifa ulete hapa. Kwa hiyo, unakuta tija ni ndogo mno. Hatuwezi kuitendea haki kazi inayofanywa na *CAG* ya mashirika zaidi ya 200 halafu tukakaa hapa kwa nusu siku tunaongea taarifa za *CAG* za mashirika yote hayo pamoja na Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na ripoti zote na ripoti yoyote ambayo tumeileta na *reaction* za Waheshimiwa Wabunge na Mawaziri, niseme kwa kiwango kikubwa ripoti yetu imekubaliwa. Niwashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina machache tu ya kuongea. Mheshimiwa Waziri wa Fedha ame-*cover* mambo ya Benki ya Azania, *Pride* na amesema yanashughulikiwa. Nina maeneo mawili ambayo nataka kweli tuyazungumze kwa kina kuhusu hoja ya *Mlimani City* ambayo pia Waziri wa Elimu amejaribu kuyaeleza na kuelezea jinsi ambayo Chuo Kikuu kinafaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kusema kwamba tunakubali vitu vidogo vidogo sana. Ukipewa shilingi bilioni mbili mwenzio akichukua bilioni 20 unaona ni sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema tumedhulumiwa sana katika *project* hii ya *Mlimani City.* Hoteli ya nyota tatu yenye vyumba 100 ilitakiwa iwe imeisha tangu mwaka 2006. Hebu hesabu ni pesa ngapi tumepoteza tangu hapo mpaka leo,?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *botanical garden* ilitakiwa iishe mwaka 2006. Pesa kiasi gani tumepoteza ambazo kulikuwa kuwe na *tourism* pia mpaka leo bado tunasifu kwamba mwekezaji anatupa chochote, sisi tumekuwa watu wa chochote, inasikitisha sana. *(Makofi)*

Nipende kusema tuwe na uchungu wa nchi yetu. Huyu mwekezaji amesema kwamba wanamshinikiza aje akae waongee, hebu ona anashinikizwa! Mtu aliyekuja na dola 75 leo anashinikizwa ili aje aongee matatizo haya. Kama kweli ameweka pesa nyingi katika mradi huu kwa nini ashinikizwe? Tuna mambo mengi ya kujiuliza juu ya *Mlimani City.* Inawezekana hata huyo mwekezaji hayupo, ni watu wachache wamejichukulia jina akasema ni mzaliwa wa Botswana anaishi *South Africa,* lakini hata kwenye Kamati juzi hakuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mtu ameweka pesa yake nyingi hivi, *structure* zile asionekane kwa nini? Na bado tuichukulie juu juu. Mimi nasema kwa hili bado Kamati ilivyoshauri kwamba ufanyike ukaguzi wa kiuchunguzi, nasema Bunge lako liridhie ifanyike *forensic and performance audit.* Nasikitika na naona uchungu, naomba maji maana nasikitika jinsi ninavyoona Serikali inachukulia jambo hili kijuu juu, tunajaribu kuli-*water down.* Ardhi yote ile imechukuliwa, mikataba inaongezwa kidogo kidogo. Mkataba haujaisha umeongezwa, umesahihishwa na bado tunaongea, tunafurahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hata mtukufu Rais akisikia hili atasikitika sana na atasikitika jinsi ambavyo Watanzania tunatetea wawekezaji. Kamati tumejipinda bila *overtime* bila nini, tunafanya kazi. Hata tuliposema hatuna muda wa kutosha wa kufanyia kazi tukawaambia hapana leteni hivyo hivyo hiyo ripoti yenu. Bado tunakuja hapa Serikali inatetea kwamba mwekezaji anafanya vizuri katupa shilingi bilioni mbili, inatosha. Yeye akichukua hata shilingi bilioni 40, sisi tukipata shilingi bilioi mbili inatosha! Kweli katika awamu hii tunataka kwenda kwenye viwanja, tunataka kukusanya hela, tunaweza kutetea hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu angalia, nafikiri Waziri wa Viwanda na Biashara ataeleza jinsi ambavyo *CBE* imetoka mahali ambapo ilikuwa inapata ruzuku kutoka Serikalini sasa hivi inajitegemea na uangalie *university* mpaka sasa hivi inasaidiwa kujenga *hostel,* lakini tuna mradi ambao ungeweza ukajenga *hostel* hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu angalia wanafunzi wetu wanapelekwa Mabibo, wana-*cross* barabara wanaibiwa *computer,* wangetakiwa wafanye kazi mpaka usiku wakiwa kwenye *lecture rooms'* lakini wanashindwa wanaondoka mapema maana hapo Ubungo kupita mpaka Mabibo wanaibiwa. *Hostel* inajengwa nje ya chuo wakati nafasi kubwa ilikuwa pale, eneo kule lile. Lile eneo ungetegemea ndiyo zijengwe hizi *hostel* tukaona tuwekeze, leo tunakuja na neno la kwamba tunapata bilioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwaambie ukweli…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, endelea.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nielezee hivi; hii hela tunayoambiwa Chuo Kikuu wanapata bilioni mbili, naombeni mnisikilize. Chuo Kikuu wameshindwa kufunga mahesabu yao tangu 2014. Kamati imehangaika nao, ilikuwa ifikie hatua mbaya sana, lakini sisemi mengi.

**WABUNGE FULANI:** Sema.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mwaka 2014 hawajafunga hesabu, 2015/2016 hawajafunga hesabu na ni Chuo Kikuu Kikuu kinachofundisha wahasibu, Chuo Kikuu cha nchi chenye hadhi hiyo. Sasa hata hii hela

tunaambiwa inaingia huko kutoka *Mlimani City,* tuna uhakika nayo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba, tuna muda mfupi wa kuzungumzia mambo haya lakini *forensic audit* inavumbua mambo mengi sana. Tutataka wote waliosaini huu mkataba waonekane, wazungumze, huu mkataba waliousaini hivi ulikuwa na maana gani? Halafu ukisoma ule mkataba ulikuwa haufungamanishi ujenzi wa *Mlimani City* na barabara ya Sam Nujoma. *TIC* wanawaongezea kwamba barabara kweli ilichelewa, wakati ujenzi haukuwa na mahusiano yoyote na barabara ya Sam Nujoma. Kwa hiyo *TIC* nao wanaingia hapo, Serikali, inaingia kati inamuongezea huyu mwekezaji muda kila leo. Mkataba haujaisha, umeongezwa mwingine, hivi tuieleweje nchi hii? Kwa hiyo *TIC* wanahusika pia katika kuhujumu nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba imeongezwa kiaina aina, tena *correspondences* tunazoziona ni kwa *e-mails;* hebu fikiria mtu mwenye hela yake nyingi hivi, hapo *South Africa* anafanya kwa *e-mail.* Juzi tulimuita kwenye Kamati tunataka tumuone mwekezaji, hakuonekana! Katuma Meneja wake, tukimuuliza swali anasema ngoja nikapige simu nimuulize mwekezaji. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili tunadharauliwa vya kutosha. Hii Kamati imeundwa na ninyi, ni sehemu ya Bunge, *auditor* anafanya kazi kubwa, anaeleza matatizo halafu tuliokosa uzalendo tunakuja hapa tuna *water down,* hivi unatetea nini? Hivi kweli Rais Magufuli akiona hili atafurahi kweli kwamba tunatetea kitu hapa. Kwa kweli nasema *personal interest* tuziache. *(Makofi)*

Mimi nasema, hilo naomba, kuna mambo mengi sana Waheshimiwa Wabunge ambayo hatuna muda wa kuyaelezea kwenye hizi *documents* zote. Muda tunaopewa, napewa nusu saa kuelezea mambo yote yaliyofanyiwa *audit,* kwa nusu saa tu! Kweli naweza kufanya *justice* katika Idara hii? Hapo hapo mjue hatuna ofisi, kila mmoja anakaa na

*documents* zake nyumbani, ukitafuta hili unachambua siku nzima, hujapata unalitafuta! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba kusema kwamba naomba tuombe ufanyike uchunguzi wa kitaalam tangu uanzishwe mradi huu waliosaini akina Profesa Luhanga, nafikiri wako hai na *TIC* ilivyoingia hapo ndani mpaka hapa tulipofika.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uendelee. Mheshimiwa, naomba ukae.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utunze muda wangu maana hizi *interruptions* zina ni...

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, makinikia...

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ameeleza mambo kwa ufasaha najua *ALAT* unaifanyia kazi kwa hiyo tutangojea matokeo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuingie kwa Waziri wa Mambo ya Ndani. Waziri wa Mambo ya Ndani amekuja hapa ameeleza mambo ya magari haya na mikataba ya *NIDA,* mikataba ya *immigration.* Nikiongelea hili la magari tumehangaika nalo tangu mwaka wa jana tukiomba mikataba tunapigwa danadana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati tunaomba mkataba ambao unaruhusu pesa zitumike ambazo hata kama ni deni

nchi italipa! Tunapigwa dana dana. Kwa hiyo tunafanya kazi bila vitendea kazi vilivyokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kwa kwenda hapo bandarini hailizuii Bunge kuunda kamati ya uchunguzi ikafanye kazi yake. Ijulikane wazi kwamba kama Mheshimiwa Rais asingekwenda juzi ina maana wenzetu Wizara wangekuwa bado wanalifumbia macho. Hili tatizo hatukulileta jana au juzi, lililetwa tangu mwaka jana. Tumempa Afisa Masuuli nafasi mara tatu, akija anatupiga danadana mara apite huku, apite huku. Vile vitu tunavyomwambia, atuletee, *documents* hizi na hizi, hataki kuleta! Sasa hayo mambo yalikuwa wazi kwanini hakuleta ile mikataba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hatuzungumzii kwamba risasi ngapi ama bunduki ngapi ziliingizwa, tunazungumzia fedha za umma inakuwaje iwe ngumu kuleta taarifa kamili ili tulione hilo na kuangalia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri anaposema eti, wameunda Kamati zinachunguza, hivi kweli mtu anaweza kujichunguza mwenyewe? Kwani hayo magari yameletwa mwaka huu? Kwanini huo uchunguzi angoje mpaka Mheshimiwa Rais aende ndipo aunde uchunguzi? Kwa hiyo ni wazi kwamba Wizara ilikuwa imelifumbia macho na wanajua kilichokuwa kinatendeka. Sasa haya yote yanayozungumziwa hapa mimi nasema Bunge lako Tukufu liazimie kwamba ukaguzi wa kiuchunguzi ufanyike. Hatuwazuii wao kufanya kazi yao wanayotaka, wakitaka kufanya kazi yao waendelee, lakini Bunge lijiridhishe kama makinikia ilivyofanyika na hii ifanyike hivyo hivyo, ieleweke kwamba kuna nini hapa. Kwa vile kuna mambo mengi inaelekeza yamejificha, sasa sisi tutafanya *cosmetic,* lakini tunataka tuingie ndani ya mzizi huu wa tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa tunataka kuongea mambo ya *NIDA* tukaambiwa kwamba kesi iko Mahakamani. Kwa hiyo, hata mkataba hamuwezi kuletewa, zaidi ya hapo tukaambiwa hii iliyowekwa sasa hivi ni

*addendum,* hamuwezi kuongelea *addendum* kama hamkuingia kwenye mkataba wenyewe. Sasa ni kama *PAC* tumefungwa miguu na mikono. Kila ukitaka kuangalia hiki unaambiwa hapana. Mambo ya Ndani ukitaka kuangalia hiki unaambiwa hapana. Lakini mbona Jeshi la Wananchi wa Tanzania tukiwaambia leteni hiki wanaleta? Jeshi wanaleta, haya ya Mambo ya Ndani kwa nini yanakuwa mazito? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba Bunge lako Tukufu liridhie kwamba kuna mambo ambayo yamefichika ambayo kama tukiyachukua juu juu kwa maneno ya kisiasa tutakuwa hatumsaidii Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli. Tunataka uchunguzi ili Mheshimiwa Rais yawe mezani kwake! Bunge likishajua ajue kuna nini mbivu na mbichi zijulikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya *passport, immigration;* Kamati imezungumzia kwa undani jinsi pesa za *visa* zinavyopotea, kwamba mtu akikata *visa* Marekani au Ufaransa au Dubai au wapi haijulikani na upotevu wa pesa nyingi uko katika *visa.* Sasa leo tukiongelea tu *passport,* hata zikarembwa kiasi gani, zikawa nzuri kiasi gani wakati hakuna jinsi ya kujua kwamba pesa ya *visa* imeingia kiasi gani, tunafanya kazi gani?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kunywa maji!

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mmh, mambo mazito haya lazima ninywe maji.

Kwa hiyo tunaomba kwamba tuyaangalie haya mambo kwa undani. Nia ya kwenda kwenye uchumi wa viwanda inataka tuwe na hela. Kama tunataka kuwa na hela lazima tuangalie kule kote ambako pesa yetu inapotea. Sasa kama hatuingii kuangalia *visa* zinalipwaje, je, wale wanaoingilia *airport* pale wanalipa kiasi gani, zinawekwa wapi na zinawekwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna *data* ya kuonesha kwamba kuna kusomeka mtu akichukua *visa* akiwa *South* Africa au akiwa Uarabuni wakikaa ofisini pale wanaona watu wangapi leo wameingia Tanzania na wamelipa kiasi gani. kwa hiyo tusirembeerembe mambo hapa kwamba *passport* nzuri sana, hata gauni yangu hii nzuri. *(Makofi/kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama hatuzungumzii mambo ya msingi tukizungumzia vitu vidogo vidogo kwamba hiki kizuri, hii hata kama ingekuwa nzuri kiasi gani mbona hata Marekani wanaweza kukakatalia usiingie kule kwenye nchi yao, hata kama ingekuwa nzuri kiasi gani. *(Makofi)*

Kwa hiyo tuangalie mambo kwa undani, tunafanya kwa awamu, awamu ingeanzia basi kwenye *immigration* ili tujue pesa imeingia kiasi gani. Ili tujue basi tutengeneze *passport* nzuri maana tuna hela, tunaanza *vice versa* kwa nini? Ninaomba tuangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongea kwa juu juu sana mambo mengi maana tukisema tuingie ndani kwa muda ulionipa nitakuwa siwezi kumaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie tu utata ambao ulitokea kati ya Wajumbe wangu wa Kamati ambayo mmoja anasema heka moja ilinunuliwa milioni 800 mwingine anasema sio hivyo. Ni kwamba wanaweza hawa watu wakawa wanaongea kitu kimoja isipokuwa mmoja anaongea *land for equity* mwingine anaongelea *cash money.* Hili jambo ukitaka kulieleza sasa hivi sitaweza kulizungumzia maana la kihasibu zaidi, lakini itoshe kusema kwamba...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kaboyoka tafadhali kidogo naongeza dakika 30 kwa mujibu wa Kanuni ya 28(5) endelea.

**MHE. NEGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti,ahsante sana. Hapo awali huu mradi wa mradi wa dege ulikuwa mwekezaji alisema ana

hekari 20,000 ambazo ndio alikuwa ameweka katika mradi. Baada ya *auditor* kufanya kazi akaonekana ana heka 300 tu. Kwa hiyo si hekari 20,000 ana heka 300; kwa hiyo pungufu ya hekari 19,700. Sasa hawa watu wawili ni wahasibu, mmoja kachukua hesabu za mwekezaji alisema nini mmoja akachukua *land for equity* kwamba ile *land* ilipewa thamani ya kiasi gani, lakini wote walikuwa wanaongelea jambo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu itoshe tu kusema mradi huu umekuwa na utata, mradi huu ripoti yake Kamati Ndogo walienda kuungalia kwa undani, ukaletwa ripoti kwenye Kamati nzima ya *PAC* tukaupitia. Uliangaliwa kwa kina na ukatengenezwa mapendekezo yake na kama alivyosema Mheshimiwa Mhagama ripoti ikapelekwa kwa Mheshimiwa Spika. Ripoti ilipelekwa tangu Februari, 2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme kwamba hii ripoti imezungumzia mambo mengi ambayo siwezi kuyasema kwa muda huu mfupi na ndio maana Kamati ikasema, Mheshimiwa Spika ailete ile ripoti iangaliwe ili Bunge liweze kutoa maazimio. Kwa mantiki hiyo na tunajua kwamba Mheshimiwa Spika hayuko nchini, kwa hiyo tukashindwa kwamba turudie tena mapendekezo yale yale na ina maana tunge-*rewrite* ile ile ambayo tayari iko kule kwake tukaona kwamba Kamati tutakuwa tunajichanganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nawaombeni Waheshimiwa Wabunge tuvute subira, Mheshimiwa Spika atarudi, hii ripoti itaangaliwa kwamba inasemaje. Kwa hiyo, tumeshindwa sasa hivi tusemeje isipokuwa tumesisitiza tu kwamba yale mapendekezo kamati iliyotoa kwenye ripoti ile yafanyiwe kazi na hapo yatakapoletwa Waheshimiwa Wabunge tutaweza wote kuiangalia na ku-*debate.*

Kwa hiyo niseme kwa kifupi kwamba kwa muda ulionipa niliogopa nisichanganyikiwe kama asubuhi ambayo nilikuwa na mengi ya kuongea na sikuweza kuhitimisha sasa nitajipeleka kwenye kidogo ili niweze kuzungumza yale

machache ambayo ningeweza kuzungumza pamoja na kwamba kuna mengi ambayo ningeweza kuzungumza lakini itoshe na naona umeshanipigia kengele nikushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Wabunge wengine waliochangia ambao kwa kweli haikuwa rahisi kuwataja wote kwa sababu ya muda nashukuru kwamba mmenisikiliza Waheshimiwa Wabunge hivyo basi Kamati inashauri Bunge lako kukubaliana na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali kauwa maazimio ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ameshatoa hoja.

**MHE. NEGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mnataka nirudie au?

**MJUMBE FULANI:** Eeeh rudia.

**MHE. NEGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivyo basi Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kukubaliana na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuwa Maazimio ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. KHAFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya *PAC* hoja imeungwa mkono na …*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge sasa nitalihoji Bunge kuhusu taarifa, maoni na mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya *PAC. (Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2017 ilipitishwa na Bunge Zima)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, walioafiki wameshinda. Waheshimiwa Wabunge sasa namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Serikali za Mitaa aweze kuhitimisha hoja yake. *(Makofi)*

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nichukue fursa hii kuwaashukuru wachangiaji wote waliochangia katika taarifa ya Kamati yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya usimamizi wa Hesabu za Serikali za Mitaa imechangiwa na jumla ya wachangiaji 22; kati yao saba walichangia kwa maandishi na 15 walichangia kwa maelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Bobali alieleza kuhusiana na aina ya Wakurugenzi waliopo na kama wana uwezo wa kusimamia shughuli za maendeleo. Alieleza pia kwamba Wakurugenzi waliopo hawakupatikana katika mfumo wa watumishi wa umma. Pia alieleza kwamba kuna tatizo katika ukusanyaji wa mapato na hili linatokana na kushuka kwa bei ya mazao ya wakulima. Kamati imepokea ushauri huo na Kamati ilitoa mapendekezo katika taarifa ya mwaka jana kwamba Serikali inatakiwa semina kwa Wakurugenzi ili waweze kufanya kazi ipasavyo. Pia Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kila Halmashauri inakuwa na mfumo wa kieletroniki ili basi iweze kuongeza mapato ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bobali pia ameeleza pia kuhusu tatizo la mradi wa maji. Ameeleza kwamba kuna mradi wa vijiji kumi ambao umeonyesha kutofanikiwa kabisa. Kamati imechukua ushauri huo, Kamati imeliona hilo na katika taarifa yake imeeleza na kutoa mapendekezo kwa Bunge kuazimia kuunda kamati teule ya Bunge kuchunguza matatizo ya maji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lubeleje ameishauri Kamati kupewa fedha nyingi zaidi ili kuweza kukagua miradi mingi ya maendeleo na hivyo kuona thamani halisi ya fedha zinazotumika. Tunashukuru kwa ushauri huo na katika taarifa yetu tulieleza kwamba tusingeona vizuri kufanya tu kazi ya mezani, ni vizuri tukatembelea miradi ya maendeleo ili kuona thamani halisi ya matumizi ya fedha za Serikali. Pia alieleza suala la watumishi kukaimu kwa muda mrefu bila kuthibitishwa. Kamati nalo katika taarifa yake imeliona hilo na imeitaka Serikali kuhakikisha kwamba watumishi wasikaimu zaidi ya miezi sita, wathibitishwe ili kuleta tija katika utendaji katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chikota ameeleza kuhusu tatizo la kukaimu kwa Wakuu wa Idara na ametolea mfano halmashauri ya Korogwe ambayo kuna wakuu wa idara 11 wanaendelea kukaimu mpaka sasa, lakini pia ameeleza tatizo la miradi ya maji, ameelezea pia kucheleweshwa kupelekwa kwa fedha za miradi ya maendeleo. Taarifa ya Kamati imezingatia hayo yote na tunashukuru Mheshimiwa Chikota kwa ushauri wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Selasini ameelezea uwezo wa baadhi ya Wakurugenzi wa Halmashauri zetu, hali ambayo inaleta matatizo na migongano na baadhi ya watumishi.

Suala hili limekuwa likijirudia mara kwa mara na ni kweli Wakurugenzi wengi tulionao sasa hawatokani na mfumo wa utumishi wa umma na hii imeleta tatizo kubwa katika utendaji wa kazi na usimamizi wa shughuli za maendeleo katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Gekul yeye alielezea kuhusiana na suala la asilimia 10 ya mfuko wa maendeleo ya vijana na akina mama na alishauri pia hii ihusishe pia wazee. Alieleza pia tukajifunze kutoka Halmashauri ya Babati ambayo imefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kuchangia fedha hizi. Nichukue nafasi hii kuitaka Serikali iende ikajifunze katika Halmashauri ya Babati tuone namna gani wameweza kuchangia pesa za mfuko huu kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Edward Mwalongo alieleza kuhusiana na tatizo la maji, ameeleza kuna tatizo la wakandarasi washauri na miradi mingi ya maji inaharibika mara tu baada ya kuanza kutumika. Tatizo hili sisi kama Kamati tumelieleza kwa kina na kama tulivyoelekeza tunalitaka Bunge liunde Kamati Teule ya Bunge ili kuchunguza matatizo yote ya maji kwa maana kuna tatizo la miradi ya maji karibu nchi nzima. Katika kila miradi tuliokuwa tumetembelea miradi mingi bado haijafanya kazi vizuri. Kuna tatizo kubwa la usanifu wa miradi hiyo kwa hiyo tumeelekeza Bunge liunde Kamati Teule ya Kibunge kuchunguza matatizo ya miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Musa Mbarouk naye pia alieleza tatizo la kukaimu kwa Wakuu wa Idara na Vitengo kwa zaidi ya miezi sita na ucheleweshaji wa pesa za miradi ya maendeleo. Hili nalo tumelieleza vizuri kwenye maazimio ya Kamati yetu na tunaitaka Serikali itekeleze hilo haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Leah Komanya alieleza kuhusiana na kutojibu hoja za ukaguzi na matumizi ya mfumo wa kihasibu wa *EPICOR.* Mfumo huu hauna *asset model,* wakurugenzi wanaweza wakajifanyia mahesabu kwa kadiri wanavyotaka; mfumo huu una *cash basis,* lakini hauna *a clause basis* na hii kuleta tatizo katika suala zima la mahesabu. Lakini upo uwezekano pia wa kufanya mahesabu nje ya mfumo. Kamati imeshauri Serikali ihakikishe mfumo wa *EPICOR* unafanyiwa marekebisho, bado kuna tatizo

kubwa la mfumo wa *EPICOR* ambao tunautegemea kwa kufanya mahesabu katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza ameeleza kuhusiana na mfuko wa maendeleo ya wanawake na vijana akasema mfuko huu ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi lakini utaratibu unaotumika hauko sawa sawa, vikundi vingine vinavyolipwa pesa za mfuko huu ni vikundi hewa. Pia alieleza kwamba mfuko huu unatumika kisiasa; lakini pia alikubaliana na wazo la Mheshimiwa Zitto. Tumepokea ushauri huu na sisi Kamati tumeitaka Serikali ilete muswada wa sheria kwa ajili ya mwongozo wa matumizi ya mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kigua ameeleza kuhusiana na miradi ya maji, lakini ameeleza tatizo la makusanyo ya mapato ya Halmashauri. Kamati imeeleza kwa kina matatizo ya miradi na maji na pia Kamati imeitaka Serikali ihakikishe kila halmashauri inatumia mfumo wa kieletroniki ili kuhakikisha kwamba inaongeza mapato ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zitto Kabwe alileta nyongeza ya kuiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuunda Benki ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa kwa kutumia asilimia 10 ya mapato ya ndani ambayo itatekeleza wajibu wa kutoa mikopo kwa vikundi vya vijana na wanawake. Vilevile Serikali itafiti uwezekano wa kuanzisha *scheme* ya hifadhi za jamii kwenye Serikali za Mitaa ili kusimamia mikopo ya vijana na wanawake. Ongezeko hili Kamati tumelikubali lakini pia kamati tulisisitiza kwamba haya yote yataweza tu kufanyika kama Serikali italeta Sheria ya Mwongozo wa Uendeshaji wa Mfuko huu wa Wanawake na Vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Isack Kamwelwe yeye alielezea kuhusiana na matatizo ya maji katika Wizara, akaeleza kwamba Wizara inatoa pesa tu pale ambapo kazi itakuwa imefanyika na Serikali itahakikisha kwamba huduma za maji zinapatikana. Mheshimiwa Waziri nichukue nafasi hii kukueleza kwamba katika ukaguzi

tulioufanya tumegundua miradi mingi ya maji haitekelezwi ipasavyo na tatizo kubwa ni kwamba wakandarasi wanavyo-*raise certificate* Wizara inachukua muda mrefu kutoa pesa hizo na inasemekana ni lazima ukauze sura Wizarani ndipo *certificate* hizo ziweze kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri inatakiwa hili ulifanyie kazi ili kuhakikisha miradi ya maji inatekelezwa ipasavyo. Kamati pia imeliona hilo na kutaka kuundwa kwa kamati teule ya Bunge ambayo itaangalia nini kiini cha matatizo katika utoaji wa huduma ya utekelezaji wa miradi ya maji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mpango ameeleza kwamba Serikali inapeleka pesa za miradi ya maendeleo tofauti na tulivyoeleza Kamati. Mheshimiwa Waziri nieleze tu kwamba unasema kwamba Serikali inapeleka fedha za miradi ya maendeleo ipasavyo, lakini fedha hizo hazifiki katika Halmashauri na ndio maana miradi mingi ya maendeleo inashindwa kutekelezeka. Kama fedha hizo zingekuwa zinafika kwa wakati miradi ingekuwa inatekeleza bila matatizo na kusingekuwa na malalamiko yoyote kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ndalichako ameeleza utekelezaji wa elimu bure na ameeleze ufafanuzi uliotolewa na waraka, kwa mfano suala la chakula kwa wanafunzi. Mheshimiwa Waziri nieleze tu kwamba kauli iliyotolewa na Mheshimiwa Rais ikikuagiza wewe pamoja na Waziri wa TAMISEMI kwamba kuanzia sasa ikipiga marufuku michango yoyote kwa ajili ya uchangiaji katika suala zima la elimu imeleta mkanganyiko mkubwa. Ipo haja ya kutoa tafsiri sahihi ya agizo la Rais na wakati mwingine inashindwa kueleweka kama je, tufate Waraka au agizo la Mheshimiwa Rais. Sasa ninavyoongea kuna shule nyingi huko zimefungwa na watendaji wa Serikali, wakuu wa shule wanapata shida kubwa ya nini kifanyike katika agizo hilo la Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, nitoe wito kwa Serikali kutoa ufafanuzi wa agizo hili la Rais ili kuepusha mkanganyiko unaoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jafo ameelezea kuhusiana na hatua zilizochukuliwa kwa Wakurugenzi ambao wameeonyesha kutokuwa na utendaji mzuri, lakini ameelezea suala zima la ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na pia ameeleza kuna baadhi ya watendaji wamelazimika kulipia hasara walizosababisha na ameeleza pia wako katika *vetting* kuangalia utendaji wa baadhi ya Wakurugenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kufanya *vetting,* la kuangalia utendaji wa baadhi ya Wakurugenzi tunaliomba lifanyike kwa haraka kwa sababu wananchi wetu na Halmashauri zetu zinapata shida. Wapo Wakurugenzi ambao mpaka sasa utendaji wao haueleweki na hivyo kurudisha nyuma maendeleo katika Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo naomba kuchukua fursa hii sasa kueleza azimio kubwa la Kamati ambalo lingependa lifanyiwe kazi kwa haraka ni kuhusu kuundwa kwa Kamati Maalum ya Kibunge itakayochunguza sababu za chanzo la tatizo la miradi ya maji kutekelezwa chini ya kiwango au kutotekelezwa kabisa.

Pia nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Spika, Job Ndugai kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai, kwa ushirikiano waliouonyesha pamoja na shukrani za dhati kwa Ndugu Athuman Hussein - Mkurugenzi wa Kamati za Bunge, Waziri wa TAMISEMI - Mheshimiwa Jafo na Manaibu wake, Makatibu wa Kamati, Ndugu Dismas Myanjwa, Ndugu Godfrey Kassanga, Ndugu Victor Mhagama pamoja na watumishi wengine wote wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa namna ya kipekee nichukue nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza kwa namna wanavyotoa ushirikiano Wajumbe wote wa Kamati ya *LAAC* kwa kufanya kazi bila kuchoka kuhakikisha kwamba taarifa hii inakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Vedustus Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa taarifa na hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge kabla sijalihoji Bunge namkaribisha Mheshimiwa Zitto Kabwe aweze kuwasilisha jedwali la mabadiliko yake.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kama nilivyoeleza wakati nachangia nimeleta jedwali la mabadiliko ambalo linaongeza kifungu (c) katika maazimio ambayo Kamati imeyaleta na tayari Mwenyekiti wa Kamati ameridhia kwa hiyo nilikuwa naomba Mwenyekiti uwahoji Wabunge ili iwe pamoja na mabadiliko yake, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi kama Serikali tumeliona hili jedwali la marekebisho. Kwa kuwa jedwali lenyewe kadri lilivyoandikwa na Mheshimiwa Zitto, kwa mfano anasema Serikali iangalie uwezekano wa kuunda Benki ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa kwa kutumia asilimia 10 ya mapato ya ndani ambayo itatekeleza wajibu wa kutoa mikopo kwa vikundi vya vijana. Sasa ndiyo nataka kulisema hilo, sina shida na Pendekezo lake, na kwa kuwa amesema tuangalie uwezekano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuliarifu Bunge lako Tukufu ni kwamba Mheshimiwa Zitto anakwenda sambamba na yale ambayo sasa yanaendelea ndani ya Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, Tunakumbuka mwaka 2015 tulitunga sheria ya kuunda Baraza la Taifa la Vijana na linasimamiwa na sera ya vijana. Tamko la kisera kifungu cha

tatu maelezo katika eneo la 16 limeagiza kuundwa kwa Benki ya Vijana na chanzo kingine cha fedha kwa ajili ya Benki hiyo ya vijana ni pamoja na hizi fedha za kwenye halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndiyo maana nasema kwa sababu Mheshimiwa Zitto anaelekea kwenye ajenda hiyo hiyo na kwa kuwa hapa eneo alililoliweka tuone uwezekano kwa hiyo tunakubaliana naye. Hata hivyo tunakwenda kuangalia lile jambo ambalo limekwisha kuanzishwa na Serikali tunaweza tukaliimarisha namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la pili Mheshimiwa Zitto pia amependekeza vilevile kwamba Serikali itafiti uwezekano wa kuanzisha *scheme* za hifadhi ya jamii kwenye Serikali za Mitaa ili kusimamia mikopo kwa ajili ya vijana na wanawake. Mwaka 2008 tulianzisha sheria ya Mdhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii Nchini, mwaka 2012 tukafanya marekebisho ya sheria hiyo kifungu cha 6 na 5 cha Sheria hiyo ya Mdhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii ambapo sasa kinaweka majukumu ya mdhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya mdhibiti ni pamoja na hili analotuagiza Mheshimiwa Zitto, kwamba tuone namna ya kufanya tafiti za kuanzisha *schemes* mbalimbali katika sekta mbalimbali ndani ya nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo kwa sababu tayari jukumu hili limeshaanza kufanywa, na Mheshimiwa Zitto anajua hata katika eneo lake kuna *scheme* ambayo anafikiria kuianzisha kwenye halmashauri, lakini vilevile sisi kama Serikali kwa kutumia kifungu hicho cha sheria nilichokisema tutakuwa na wajibu wa kushughulikia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka kuyaweka tu yote sawa kwamba ni mapendekezo ya Mheshimiwa Zitto lakini na ndani ya Serikali yanafanyiwa kazi. Vile vile maneno aliyoyatumia sisi kama Serikali tutakuwa *flexible* kuyatazama na kutekeleza yale maudhui mazuri ya kuwaletea maendeleo wanayoyahitaji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jenista kwa maelezo ya ziada kuhusiana na hiyo *issue* ya Mheshimiwa Zitto. Sasa tutalihoji kwanza Bunge kuhusiana na jedwali la mabadiliko lililoletwa na Mheshimiwa Zitto .

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Jedwali la Mabadiliko la Mhe. Zitto Z. R. Kabwe lilikubaliwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Baada ya hapo sasa nitalihoji Bunge kwa ujumla pamoja na taarifa hiyo kuingia katika Taarifa ya Kamati ya *LAAC*, wanaoafiki taarifa, maoni na mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa iweze kupitishwa na kuwa maazimio ya Bunge .

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2017 Ilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge taarifa za kamati zote mbili *PAC* na *LAAC* zimepitishwa kuwa maazimio ya Bunge hili nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza sana wale wote ambao wamefanya kazi hii hadi kufikia leo kukamilisha, lakini niwapongeze sana Kamati ya *PAC* ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Kaboyoka pamoja na Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Aeshi.

Pia Kamati ya *LAAC* ambayo inaongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Ngombale na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Chikota. Kwa hiyo, niwatakieni Baraka zote kwa kazi nzuri mliyoifanya na hasa kwa namna ambavyo taarifa mmeandika kwa lugha ya heshima ya Kibunge naamini kabisa Serikali itaipokea kwa heshima hiyo hiyo na itaifanyia kazi inavyostahili. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge kwa vile shughuli zetu za leo zimekamilika nalihairisha Bunge hadi kesho tarehe 2 Februari, 2018 saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.08 Usiku Bunge lilihairishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 2 Februari, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*